Kantor Dakwah Sulay
Telp. 2414488 – 2410615, fax: 232,

# NGUZO ZA UISLAMU MUKHTASARI WA MAELEZO YA

5

SHAHADA

S A L A T

Z A K A T

S A W M

H A J J

KIMETUNGWA AN: MWANAFUNZI
KIMEPITIWA NA: SHEIKH ABDULLAH BIN ABDUR RAHMAN AL-JABRIN
Mfasiri : Uthman M.Ali,

5302001

www.islamnewlife.com

كتب الجاليات
١
١٨٨

السلي

مكتب الدعوة بالسلي
هاتف ٠١٢٤١٠٦١٥ ، تحويله ٥٥٥ - ٠١٢٤١٤٤٨٨ ، ناسوخ ٢٣٢

# مختصر
# أركان الإسلام

5

الشهادتان
الصلاة
صوم رمضان
الزكاة
الحج

تقديم / الشيخ عبد الله بن عبد الرحمن الجبرين

ترجمه إلى السواحلية / عثمان محمد على

السواحلية

الحساب الموحد بمصرف الراجحي SA 2280000296608010070509

www.islamnewlife.com

1

# KIDOKEZO

Namshukuru ALLAH kwa idadi ya viumbe Vyake. Rehma na Amani zimwendee Mjumbe Wake na Wafuasi wake.

Ama baada ya haya;

Ni kama ionekanavyo, kitabu hiki kilichofukizwa uturi wa kupendeza, kwa moshi wa kupuliza, ni tafsiri ya kitabu kiitwacho **'Mukhtasari Sharh Arkaanul-Islaam'.** Asili ya kitabu chenyewe kimeandikwa katika Lugha ya Kiarabu, nami nikakifasiri tu, wala sikutia langu neno.

Katika kuifanya kazi hii, nimefwata njia zifwatazo:

* Hadithi zote zilizomo humu, ni baina ya Swahih na Hassan, wala hakuna dhaif hata moja. Kwa hivyo sikuona haja ya kuandika **"Hadithi hii ni Swahih"** au **"Hadithi hii ni Hassan"**, kama alivyofanya mwandishi wa asili ya kitabu hiki.

* Dua zilizomo humu kwa Lugha ya Kiarabu sikuziandika kwa Kilatini, bali nimezifasiri kwa Kiswahili tu. Kwa sababu ni imani yangu kuwa, kujua kusoma ni wajibu wa kila Muislamu, mume na mke.

Ni mimi msi daraja, Fahari na mengineyo,
Kama mtu ana haja, Kutengeza nisemayo,
Hatakosa yake tija, Siku hiyo ya mgawo,
Ya kutuzwa kila mja, Kwa tuzo na kwa jazuo.

رَبِّ أَوْزِعْنِيٓ أَنْ أَشْكُرَ نِعْمَتَكَ ٱلَّتِيٓ أَنْعَمْتَ عَلَيَّ وَعَلَىٰ وَٰلِدَيَّ وَأَنْ أَعْمَلَ صَٰلِحًا تَرْضَىٰهُ وَأَدْخِلْنِي بِرَحْمَتِكَ فِي عِبَادِكَ ٱلصَّٰلِحِينَ ١٩

**"Ewe Mola wangu! Nipe nguvu nishukuru neema yako uliyonineemesha mimi na wazazi wangu, na nipate kufanya vitendo vizuri uvipendavyo, na uniingize - kwa Rehma yako - katika waja wako wema."** (27:19).

**'Uthman M. 'Ali**

Imepokewa kutoka kwa 'Abdallah bin 'Umar bin Al-khattab (R.A.) akisema: Nilimsikia Mtume (S.A.W.) akisema: "Uislamu umejengwa kwa nguzo tano: Kushuhudia kuwa hapana Mola anaestahiki kuabudiwa kwa haki ela ni ALLAH, na kuwa Muhammad ni Mtume wa ALLAH, na kusimamisha Swala, na kutoa Zaka, na kuhiji Al-ka'ba, na kufunga mwezi wa Ramadhani."

Muttafaq

Namhimidi ALLAH, namshukuru, namuomba msamaha, namuomba atugawie shukurani za neema zake na atuondolee maangamivu yake. Nashuhudia kuwa yeye ndiye Mola wa haki, hapana Mola asiekua yeye wala hakuna muabudiwa wa haki ela ni yeye. Na nashuhudia kuwa Muhammad ametumilizwa kutoka kwa Mola wake, na kwamba amefikilizisha ujumbe, akaitekeleza amana. Nashuhudia kuwa Makhalifa wake waongofu wenye kuongoza na Maswahaba wake ni katika wakweli, mashahidi na walio wema. Na kwamba wao waliibeba sheria yake, wakaifanyia amali na wakawafikilizishia walio baada yao. Rehma, amani na baraka za ALLAH zimfikie Mtume wake Muhammad. ALLAH awaelee radhi Maswahaba wake wote na wanaowafuata kwa wema mpaka siku ya Qiyama.

Ama baada ya haya, nimeisoma risala tukufu iliyoandikwa na mwenye kutafuta elimu kuhusu sherehe (maelezo) ya nguzo tano za Uislamu nazo ni: Shahada mbili, Swala, Saumu na Hajji, amefupiliza kwa kuzitaja nguzo hizo pasina kutaja hukumu nyenginezo. Hakufanya hivyo ila ni kwa sababu ya umuhimu wa nguzo hizi, na kwa kuwa ni matendo ya dhahiri katika ulimi, mwili na mali. Anatakiwa kila aliye mukallaf kuzitekeleza. Na (pia amefanya hivyo) kwa sababu ya kuhitajika mno mtu kuzijua, kutojulikaniwa sana, kukosea katika kuzifanya katika nchi nyingi zinazojiita kuwa ni nchi za Kiislamu pasina kutekeleza taaluma zake na kuzifanyia amali nguzo zake, kwa sababu ya kuwa mbali na elimu sahihi na kuadimika mwenye kuwaongoza au kuwatanabahisha, pamoja na kuwa na taksiri na kuyashughulikia yenye kupumbaza. Hapana shaka kuwa Muislamu atakapozisimamisha nguzo hizi katika hali timamu na kuyafanya yanayomlazimu katika yenye kukamilisha (nguzo hizi), basi jambo hilo litamsukuma kwenda kuyafanya mafundisho mengine ya Dini yake, atajihimu katika 'Aqida (Imani) atafanya pupa kutafuta halali, atajiepusha na maasi na ataadabika kwa adabu za Kiislamu na tabia zake. Kwa yakini katika risala hii ameyaandika yalio muhimu katika elimu za nguzo za Uislamu pamoja na kufupiliza na ibara iliyo wazi kwa watu wote. Mwandishi amefupiliza juu ya kauli moja yenye nguvu kwetu, ingawaje kuna anaechagua kauli nyingine, lakini kutaja hitilafu na kauli nyingi huwaingiza watu wa kawaida katika udangamanifu. Basi watakapojua hukumu (ya jambo)

na wakaifanyia amali kufuatana na kauli moja pamoja na kutaja dalili na kuwa na niya ya kweli watapata thawabu na wataepukana na madhambi ya kudharau. Hivyo basi twawahimiza wafanyaji kheri kuzisambaza risala za aina hii pande zote za miji ya Kiislamu ili watu wawe macho katika Dini yao. Na mwenye kujulisha kheri atapata ujira wa mwenye kuifanya, na mwenye kulingania katika uongofu atapata ujira wa atakaemfuata pasina (hao wenya kufuata) kupunguziwa chochote katika ujira wao. ALLAH amjazi - aliyeandika na kuisambaza risala hii - majazi mema. Rehma na amani zimwendee Muhammad, Aali zake na maswahaba wake.

23-1-1415H.

**'Abdullah bin 'Abdurrahman bin 'Abdullah bin Jabrin'**

# UTANGULIZI

Hakika jinsi ya shukrani zote ni zenye kumthubutukia ALLAH, twamhimidi, twamuomba msaada na twamtaka msamaha. Twajilinda kwa ALLAH kutokana na shari za nafsi zetu na uovu wa matendo yetu. Anayeongozwa na ALLAH hakuna wa kumpoteza, na anaepotezwa (na ALLAH) hakuna wa kumuongoza. Twashuhudia kuwa hapana Mola anaestahiki kuabudiwa kwa haki isipokua ni ALLAH peke yake, hana mshirika, na twashuhudia kuwa Muhammad ni mja wake na ni mjumbe wake, Rehma, amani na baraka za ALLAH zimwendee yeye, Aali zake na maswahaba wake walio wazuri na wanaowafuata kwa wema mpaksiku ya malipo.

Ama baada ya haya, hiki ni kitabu mukhtasari kuhusu sherehe ya nguzo tano za Uislamu: Kushuhudia kuwa hapana Mola anaestahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa ni ALLAH na kuwa Muhammad ni Mtume wa ALLAH, kusimamisha Swala, kutoa Zaka, kufunga Ramadhani na kuhijji nyumba tukufu ya ALLAH. Tumekusudia kufupiliza na kuzitaja hukumu kwa dalili zake kutoka katika kitabu cha ALLAH au Sunna toharifu zilizo swahihi au ijimai (muafaka wa Ulamaa). Pamoja na kuziashiria Aya za Qur'aani katika sura zake katika Msahafu mtukufu na Hadithi za Mtume katika machimbuko yake kutoka asili ya vitabu vya Hadithi vilivyo mashuhuri.

Tumechunga katika kitabu hiki kuzidisha anuwani muhimu na nukta za pambizoni zitakazomsahilishia msomaji na kumsaidia kufikia makala anayoyataka. Tumezikusanya mada zake za kiilimu kutoka katika asili ya vitabu mashuhuri, vya zamani na vya sasa. Na tumekipangilia mpangilio sahali unaonasibiana na kuchukuana na viwango mbali mbali vya wasomaji.

Katika chapa hii tumeongeza baadhi ya vifungu muhimu ili kuitimiza faida. Vifungu vyenyewe ni kama vinavyofuata:

1 - Sharuti za shahada mbili.

2 - Namna ya utwahara wa mgonjwa.

3 - Sunna za Swala za ratiba na witri.

4 - Namna ya Swala ya mgonjwa.

Na ni ALLAH pekee ndiye tunayemuomba awanufaishe Waislamu kwa kitabu hiki, kwani yeye ni mpaji aliye karimu.

Mwisho wa maombi yetu ni kusema: Kila jinsi ya sifa njema ni yenye kumthubutukia ALLAH Mola wa viumbe v y o t e .

# NGUZO YA KWANZA

Kukiri kwa moyo na kubaini kwa ulimi kuwa hapana Mola anayestahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa ALLAH na kuwa Muhammad ni mjumbe wa ALLAH.

# KUSHUHUDIA KUWA HAPANA MOLA ANAYESTAHIKI KUABUDIWA KWA HAKI ISIPOKUWA ALLAH NA KUWA MUHAMMAD NI MJUMBE WA ALLAH.

Hakika kushuhudia kuwa hapana Mola anayestahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa ALLAH, ni nguzo ya kwanza katika nguzo za Uislamu (na inaingia katika nguzo hiyo kushuhudia kuwa Muhammad (S.A.W.) ni mjumbe wa ALLAH. Ijapokuwa mara nyingine haitajwi katika kilma hicho). Na jambo hili linajulikana katika dini kuwa ni dharura na hapana hitilafu ndani yake baina ya Waislamu wote.

Na tutaizungumzia nguzo hii kubwa katika vifungu hivi:

Kwanza, majina yake: kilma cha shahada لا إله إلا الله

Kina majina mengi miongoni mwayo: **"Kilma cha Tawhid"**, **"Kilma cha Ikhlas"**, **"Kilma cha shahada"**, **"shahada ya ukweli"**.

Pili, nguzo zake: kilma cha Tawhid kina nguzo mbili kubwa nazo ni:

a. Kukanusha, na makusudio yake ni لا إله

Hapana Mola.

b. Kuthibitisha, nako ni إلا الله

isipokuwa ALLAH.

Basi kilma hiki kina kanusha kuwepo - katika vinavyopatikaniwa - mwenye kuabudiwa wa haki, **"isipokuwa ALLAH"**, inathubutisha kuwa yeye ni mmoja hana mshirika. Na hizi nguzo mbili zilizokusanywa katika Aya nyingi zenye kubainisha maana ya shahada, miongoni mwazo ni:

1. Kauli yake Mwenyezi Mungu aliyetukuka:

﴿ لَا إِكْرَاهَ فِي الدِّينِ قَدْ تَبَيَّنَ الرُّشْدُ مِنَ الْغَيِّ فَمَنْ يَكْفُرْ بِالطَّاغُوتِ وَيُؤْمِنْ بِاللَّهِ فَقَدِ اسْتَمْسَكَ بِالْعُرْوَةِ الْوُثْقَىٰ لَا انْفِصَامَ لَهَا وَاللَّهُ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴾(١) .

**"Hakuna kulazimishwa mtu (kuingia) katika dini. Uongofu umekwisha pambanuka na upotofu. Basi anayemkataa Twaghut na akamwamini ALLAH, bila shaka yeye ameshika kishiko chenye nguvu kisichokuwa na kuvunjika. Na ALLAH ni mwenye kusikia mwenye kujua."** (Q 2:256).

Na kishiko chenye nguvu ni

**"Hapana Mola anayestahiki kuabudiwa kwa haki isipokua ALLAH"**, kama alivyotafsiri hivyo Ibnu Abbas, Said bin Jubair, Adhahak na Sufyan.

Na Twaghut: Ni kila ambacho binadamu amekipitishia mpaka kutokana na chenye kuabidiwa au kufuatwa au mwenye kutiiwa (naye akawa yuko radhi katika jambo hilo, ikiwa ni katika wanadamu).

Basi aya hii imejulisha nguzo mbili nazo ni: Kumkufuru Twaghut na Kumuamini ALLAH, na hii ndiyo maana halisi ya

شهادة أن لا إله إلا الله .

2. Kauli yake Mweny-ezi Mungu aliyetukuka:

﴿ وَلَقَدْ بَعَثْنَا فِي كُلِّ أُمَّةٍ رَسُولاً أَنِ اعْبُدُوا اللَّهَ
وَاجْتَنِبُوا الطَّاغُوتَ فَمِنْهُمْ مَنْ هَدَى اللَّهُ وَمِنْهُمْ مَنْ حَقَّتْ عَلَيْهِ
الضَّلَالَةُ فَسِيرُوا فِي الْأَرْضِ فَانْظُرُوا كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الْمُكَذِّبِينَ ﴾

**"Na bila shaka tulimpeleka Mtume katika kila umma ya kwamba "mwabuduni ALLAH na muepukeni (Ibilis) muovu". Basi wako miongoni mwao ambao ALLAH amewaongoa, na wako miongoni mwao ambao upotofu, (upotevu) umethubutu juu yao. Basi tembeeni katika ardhi na muangalie ilikuaje mwisho wa wale waliokadhibisha".** (Q 16: 36).

Aya hii ni kama iliyotangulia.

3. Kauli yake ALLAH alietukuka, kuwaelezea watu wa 'Adi:

﴿ قَالُوا أَجِئْتَنَا لِنَعْبُدَ اللَّهَ وَحْدَهُ وَنَذَرَ
مَا كَانَ يَعْبُدُ آبَاؤُنَا فَأْتِنَا بِمَا تَعِدُنَا إِنْ كُنْتَ مِنَ الصَّادِقِينَ ﴾

**"Wakasema " Je! Umetujia ili tumuabudu ALLAH peke yake na tuyaache waliyokuwa wakiyaabudu baba zetu? Basi tuletee unayo - tuahidi ukiwa ni miongoni mwa wasemao kweli".** (7:70). Hilo ni jawabu lao kumjibu Nabii Hud (A.S.) alipowaambia:

**"Enyi kaumu yangu! Mwabuduni Allah, nyinyi hamna Mungu ila yeye. Basi hamuogopi?"** (7:65). Jawabu hilo ndiyo maana ya

kama ilivyo katika kauli yake:

﴿ وَمَا أَرْسَلْنَا مِن قَبْلِكَ مِن رَّسُولٍ إِلَّا نُوحِي إِلَيْهِ أَنَّهُ لَا إِلَٰهَ إِلَّا أَنَا فَاعْبُدُونِ ﴾[1]

**"Na hatukumtuma kabla yako Mtume yoyote ila tulimfunulia ya kwamba hakuna aabudiwaye ila mimi, basi niabuduni".** (21:25)

Basi aliwalingania katika kushuhudia kuwa hapana Mola anaestahiki kuabudiwa kwa haki ila ALLAH, na wakaiifahamu hilo. Kuwa alikuwa akiwalingania katika mambo mawili:

KWANZA: Kauli yao inayosema: **"ili tumwabudu ALLAH peke yake"**. Na hii ninguzo ya kuthibitisha (kuwepo kwa ALLAH).

PILI: Kauli yao inayosema: **"tuyaache waliyokuwa wakiyaabudu baba zetu"**. Na ni nguzo ya kukanusha (shirki).

4. Katika Swahihi Muslim, Mtume S.A.W. amesema:

« من قال لا إله إلا الله وكفر بما يعبد من دون الله حرم ماله ودمه، وحسابه على الله عز وجل »[1] . وفي رواية الإمام أحمد : « من وحد الله وكفر بما يعبد من دونه حرم ماله ودمه » إلخ

**"Atakaesema "Hapana Mola anaestahiki kuabudiwa kwa haki ila ALLAH", na akavikufuru vinavyoabudiwa badala ya ALLAH, ni haramu mali yake na damu yake, na hisabu yake iko kwa ALLAH aliyeshinda na kutukuka".** Na katika riwaya ya Imam Ahmad: **"Mwenye kumpwekesha ALLAH na akavikufuru vinavyoabudiwa badala ya ALLAH ni haramu mali na damu yake"**, mpaka mwisho wa Hadithi. Na katika Hadithi hii inasisitizwa nguzo ya pili.

TATU: Hakika na maana yake:

Kilma cha shahada kimekusanya hakika na maana mengi yenye

kulazimiana, tutayaeleza ili kuweka wazi zaidi, maana muhimu zaidi ni:

A. Kumpwekesha ALLAH - aliyetukuka - kwa ibada: (taarifa yake itakuja).

Nako (kumpwekesha huko) ni kujikurubisha kwake peke yake na kumuomba yeye pekee. Na katika jambo hili muna dalili nyingi, miongoni mwazo:

1. Kauli yake ALLAH: قُلْ إِنَّمَا أَدْعُوا رَبِّي وَلَا أُشْرِكُ بِهِ أَحَدًا

**"Sema: "Ninamuabudu Mola wangu tu wala simshirikishi na yoyote."** (72:20).

2. Kauli yake ALLAH:

﴿ قُلْ لَوْ كَانَ مَعَهُ آلِهَةٌ كَمَا يَقُولُونَ إِذًا لَابْتَغَوْا إِلَىٰ ذِي الْعَرْشِ سَبِيلًا ﴾

**"Sema: "Lau wangalikuwa pamoja naye (ALLAH) waungu (wengine) kama wasemavyo, basi wangalitafuta njia ya kufikia kwa ALLAH (kupigana naye)."** (17:42).

3. Kauli yake ALLAH:

﴿ أُولَٰئِكَ الَّذِينَ يَدْعُونَ يَبْتَغُونَ إِلَىٰ رَبِّهِمُ الْوَسِيلَةَ أَيُّهُمْ أَقْرَبُ وَيَرْجُونَ رَحْمَتَهُ وَيَخَافُونَ عَذَابَهُ إِنَّ عَذَابَ رَبِّكَ كَانَ مَحْذُورًا ﴾

**"Hao wanaowaomba, (wenyewe) wanatafuta ukaribiano na Mola wao, (hata) walio karibu sana miongoni mwao (na ALLAH, kama Malaika, wao wanafanya yaya haya) wanatumai rehema zake na wanaogopa adhabu Yake. Hakika adhabu ya Mola wako ni ya kuogopwa."** (17:57).

4. Kauli yake ALLAH:

﴿ وَمِنْ آيَاتِهِ اللَّيْلُ وَالنَّهَارُ وَالشَّمْسُ وَالْقَمَرُ لَا تَسْجُدُوا لِلشَّمْسِ وَلَا لِلْقَمَرِ وَاسْجُدُوا لِلَّهِ الَّذِي خَلَقَهُنَّ إِنْ كُنْتُمْ إِيَّاهُ تَعْبُدُونَ ﴾

**"Na katika alama zake (za Uungu wake ALLAH) ni (huku kupatikana) usiku na mchana na jua na mwezi, basi msilisujudie jua wala mwezi, bali msujudieni ALLAH aliyeviumba, ikiwa nyinyi mnamuabudu yeye (basi fanyeni hivi)."** (41:37).

5. Kauli yake ALLAH:

﴿ قُلْ إِنَّ صَلاَتِي وَنُسُكِي وَمَحْيَايَ وَمَمَاتِي لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴾

**"Sema: "Hakika Swala yangu, na ibada zangu (zote nyingine) na uzima wangu, na kufa kwangu, (zote) ni kwa ALLAH, mwumba wa walimwengu wote".** (6:162).

6. Kauli yake ALLAH

﴿ وَمَنْ يُسْلِمْ وَجْهَهُ إِلَى اللَّهِ وَهُوَ مُحْسِنٌ فَقَدْ اسْتَمْسَكَ بِالْعُرْوَةِ الْوُثْقَى وَإِلَى اللَّهِ عَاقِبَةُ الأُمُورِ ﴾

**"Na ajisalimishae uso wake kwa ALLAH, na hali ya kuwa anawafanyia mema (viumbe wenziwe), bila shaka amekwisha kamata fundo lililo madhubuti, na mwisho wa mambo yote ni kwa ALLAH."** (31:22).

B. Kuiyepuka shirki na watu wake: Mja asimfanye yeyote badala ya ALLAH kuwa ndiye mwenye kumnusuru, na asiwatawalishe maadui wa ALLAH. Na jambo hili lina dalili katika Aya nyingi, miongoni mwazo ni:

﴿ وَإِذْ قَالَ إِبْرَاهِيمُ لِأَبِيهِ وَقَوْمِهِ إِنَّنِي بَرَاءٌ مِمَّا تَعْبُدُونَ إِلاَّ الَّذِي فَطَرَنِي فَإِنَّهُ سَيَهْدِينِ ، وَجَعَلَهَا كَلِمَةً بَاقِيَةً فِي عَقِبِهِ لَعَلَّهُمْ يَرْجِعُونَ ﴾

1. **"Na (wakumbushe) Ibrahimu alipomwambia baba yake na watu wake: Bila shaka mimi ninajitenga na hayo mnayoyaabudu. Isipokuwa yule aliyeniumba, kwa yakini yeye ataniongoa. Na akalifanya (neno) hili ni neno lenye kubaki katika kizazi chake ili warejee (katika tamko hili)."** (43:26-28).

2. Kauli yake ALLAH kumweleza Nabii Ibrahim:

﴿ قَالَ أَفَرَأَيْتُم مَّا كُنتُمْ تَعْبُدُونَ
أَنتُمْ وَآبَاؤُكُمُ الْأَقْدَمُونَ ، فَإِنَّهُمْ عَدُوٌّ لِّي إِلَّا رَبَّ الْعَالَمِينَ ﴾

**"Akasema: "Je mumewaona hawa mnaowaabudu nyinyi na wazee wenu waliotangulia. Bila shaka hao ni adui zangu (basi nitawadhuru, mimi simwabudu) ila Mola wa walimwengu wote".** (Q26: 75-77)

3.

قُلْ يَا أَيُّهَا الْكَافِرُونَ ، لَا أَعْبُدُ مَا تَعْبُدُونَ ، وَلَا أَنتُمْ عَابِدُونَ مَا أَعْبُدُ ، وَلَا أَنَا عَابِدٌ مَّا عَبَدتُّمْ ، وَلَا أَنتُمْ عَابِدُونَ مَا أَعْبُدُ ، لَكُمْ دِينُكُمْ وَلِيَ دِينِ

**"Sema: Enyi makafiri siabudu mnachoabudu wala nyinyi hamuabudu ninaye muabudu, wala sitaabudu mnachoabudu. Wala nyinyi hamtaabudu ninayemwabudu. Nyinyi mna dini yenu nami nina dini yangu".** (Q 109:1-6).

4.

﴿ لَا تَجِدُ قَوْمًا يُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ يُوَادُّونَ مَنْ حَادَّ اللَّهَ وَرَسُولَهُ وَلَوْ كَانُوا آبَاءَهُمْ أَوْ أَبْنَاءَهُمْ أَوْ إِخْوَانَهُمْ أَوْ عَشِيرَتَهُمْ أُولَٰئِكَ كَتَبَ فِي قُلُوبِهِمُ الْإِيمَانَ وَأَيَّدَهُم بِرُوحٍ مِّنْهُ وَيُدْخِلُهُمْ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِن تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمْ وَرَضُوا عَنْهُ أُولَٰئِكَ حِزْبُ اللَّهِ أَلَا إِنَّ حِزْبَ اللَّهِ هُمُ الْمُفْلِحُونَ ﴾

**"Huwapati (huwaoni) watu wanaomwamini ALLAH na siku ya mwisho, kuwa wanawapenda wale wanaopinga ALLAH na Mtume wake, hata wakiwa ni baba zao au watoto wao au ndugu zao au jamaa zao. Hao ndio ambao (ALLAH) ameandika, (amethibitisha kweli kweli) nyoyoni mwao imani na akawatia nguvu kwa Roho itokayo kwake, na atawaingiza katika mabustani yapitayo mito mbele yake, humo watakaa daima. ALLAH amekuwa radhi nao, na wao wamekua radhi naye. Hao ndio kundi la ALLAH. Sikilizeni! Hakika kundi la ALLAH ndilo linalofaulu."** (Q 58:22).

5.

﴿ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تَتَّخِذُوا الْكَافِرِينَ أَوْلِيَاءَ مِن

﴿ دُونِ الْمُؤْمِنِينَ أَتُرِيدُونَ أَنْ تَجْعَلُوا لِلَّهِ عَلَيْكُمْ سُلْطَانًا مُبِينًا ﴾

**"Enyi mlioamini! Msiwafanye makafiri kuwa marafiki badala ya Waislamu. Mnataka awe nayo (Mtume wa) ALLAH hoja dhahiri juu yenu (ya kuwa nyinyi wabaya?"** (4:144).

6.

﴿ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تَتَّخِذُوا الْيَهُودَ وَالنَّصَارَىٰ أَوْلِيَاءَ بَعْضُهُمْ أَوْلِيَاءُ بَعْضٍ وَمَنْ يَتَوَلَّهُمْ مِنْكُمْ فَإِنَّهُ مِنْهُمْ إِنَّ اللَّهَ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الظَّالِمِينَ ﴾

**"Enyi mlioamini! Msiwafanye Mayahudi na Wakristo kuwa marafiki (wakuwapa siri zenu), woa kwa wao ni marafiki. Na miongoni mwenu atakayefanya urafiki huo nao, basi huyo atakuwa pamoja nao. Hakika ALLAH hawaongozi (njia ya kheri) watu madhalimu"** (Q 5:51).

C. Mtu asimfanye badala yake (ALLAH) hakimu atakayemhukumu: na akawa yuwapokea hukumu za halali na haramu kutoka kwake. Halali ni aliyoihalalisha ALLAH, haramu ni alioiharamisha ALLAH na dini ni aliyoiweka ALLAH, ima katika kitabu chake au kwa ulimi wa Mtume wake (S.A.W.). Na dalili juu ya jambo hili ni nyingi:

1. ﴿ أَفَغَيْرَ اللَّهِ أَبْتَغِي حَكَمًا وَهُوَ الَّذِي أَنْزَلَ إِلَيْكُمُ الْكِتَابَ مُفَصَّلًا وَالَّذِينَ آتَيْنَاهُمُ الْكِتَابَ يَعْلَمُونَ أَنَّهُ مُنَزَّلٌ مِنْ رَبِّكَ بِالْحَقِّ فَلَا تَكُونَنَّ مِنَ الْمُمْتَرِينَ ﴾

**"(Sema): Je, nimtafute hakimu asiyekuwa ALLAH (wa kunihukumu baina yangu na nyinyi), hali yeye (ALLAH) ndiye aliyewateremshia kitabu (hiki) kielezacho (kila kitu) waziwazi? (Na kishasema kuwa mimi nimo katika haki). Na wale tuliowapa kitabu wanajuwa ya**

**kwamba kimeteremshwa na Mola wako kwa haki (ila wanapinga kwa inadi tu na uhasidi). Basi usiwe miongoni mwa wanaotia shaka."** (6:114).

2.

﴿ اتَّخَذُوا أَحْبَارَهُمْ وَرُهْبَانَهُمْ أَرْبَابًا مِنْ دُونِ اللَّهِ وَالْمَسِيحَ ابْنَ مَرْيَمَ وَمَا أُمِرُوا إِلَّا لِيَعْبُدُوا إِلَٰهًا وَاحِدًا لَا إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ سُبْحَانَهُ عَمَّا يُشْرِكُونَ ﴾

**"Wamewafanya wanavyuona wao na watawa wao kuwa ni Miungu badala ya ALLAH, na (wamemfanya) masihi mwana wa Maryamu (pia Mungu), hali hawakuamrishwa isipokuwa kumwabudu Mungu mmoja, hakuna anayestahiki kuabudiwa ila yeye. Ametakasika na yale wanayomshirikisha nao."** (9:31)

3.

﴿ أَمْ لَهُمْ شُرَكَاءُ شَرَعُوا لَهُمْ مِنَ الدِّينِ مَا لَمْ يَأْذَنْ بِهِ اللَّهُ وَلَوْلَا كَلِمَةُ الْفَصْلِ لَقُضِيَ بَيْنَهُمْ وَإِنَّ الظَّالِمِينَ لَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴾

**"Oh! Wana washirika (wa ALLAH) waliowawekea dini asiyoitolea ALLAH ruhusa (yake)? Na kama kisingelikuwako neno la (kuwa iko siku ya) kupambanua hukumu (huko Kiyama), basi hukumu ingelikatwa baina yao (sasa hivi), na kwa yakini itakuwa kwa madhalimu adhabu iumizayo."** (42:21).

4.

﴿ أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ يَزْعُمُونَ أَنَّهُمْ آمَنُوا بِمَا أُنْزِلَ إِلَيْكَ وَمَا أُنْزِلَ مِنْ قَبْلِكَ يُرِيدُونَ أَنْ يَتَحَاكَمُوا إِلَى الطَّاغُوتِ وَقَدْ أُمِرُوا أَنْ يَكْفُرُوا بِهِ وَيُرِيدُ الشَّيْطَانُ أَنْ يُضِلَّهُمْ ضَلَالًا بَعِيدًا ، وَإِذَا قِيلَ لَهُمْ تَعَالَوْا إِلَىٰ مَا أَنْزَلَ اللَّهُ وَإِلَى الرَّسُولِ رَأَيْتَ الْمُنَافِقِينَ يَصُدُّونَ عَنْكَ صُدُودًا ، فَكَيْفَ إِذَا أَصَابَتْهُمْ مُصِيبَةٌ بِمَا قَدَّمَتْ أَيْدِيهِمْ ثُمَّ جَاءُوكَ يَحْلِفُونَ بِاللَّهِ إِنْ أَرَدْنَا إِلَّا إِحْسَانًا وَتَوْفِيقًا ، أُولَٰئِكَ الَّذِينَ يَعْلَمُ اللَّهُ مَا فِي قُلُوبِهِمْ فَأَعْرِضْ عَنْهُمْ وَعِظْهُمْ وَقُلْ

لَهُمْ فِي أَنْفُسِهِمْ قَوْلاً بَلِيغاً ، وَمَا أَرْسَلْنَا مِنْ رَسُولٍ إِلاَّ لِيُطَاعَ
بِإِذْنِ اللَّهِ ، وَلَوْ أَنَّهُمْ إِذْ ظَلَمُوا أَنْفُسَهُمْ جَاءُوكَ فَاسْتَغْفَرُوا اللَّهَ
وَاسْتَغْفَرَ لَهُمُ الرَّسُولُ لَوَجَدُوا اللَّهَ تَوَّاباً رَحِيماً ، فَلاَ وَرَبِّكَ لاَ
يُؤْمِنُونَ حَتَّىٰ يُحَكِّمُوكَ فِيمَا شَجَرَ بَيْنَهُمْ ثُمَّ لاَ يَجِدُوا فِي أَنْفُسِهِمْ
حَرَجاً مِمَّا قَضَيْتَ وَيُسَلِّمُوا تَسْلِيماً ﴾

**"Huwaoni wale wanaodai kwamba wameamini yale yaliyoteremshwa kwako na yalioteremshwa kabla yako? Nao wanataka wahukumiwe kwa njia isiyowafiki sharia, na hali wameamrishwa kukataa njia hiyo. Na shetani anataka kuwapoteza upotofu (upotevu) ulio mbali (na haki). Na wanapoambiwa "Njooni katika yale aliyoyateremsha ALLAH, na (njooni) kwa Mtume", utawaona wanafiki wanaojiweka mbali nawe kabisa. Basi itakuwaje itakapowafika msiba kwa sababu ya yale iliotanguliza mikono yao? Kisha wakakujia wakiapa "Wallahi! Hatukutaka ila wema na mapatano."** Hao ndio wale ambao ALLAH anayajua yaliyomo nyoyoni mwao. **"Basi waachilie mbali, (lakini uwape mawaidha na uwaambie maneno yenye taathira yatakayoingia katika nafsi (nyoyo) zao. Na hatukuleta Mtume yeyote ila atiiwe kwa amri ya ALLAH. Na lau wangelikuja walipojidhulumu nafsi zao (kwa kwenda kuhukumiwa kwa njia isiyokuwa ya sharia) wakaomba msamaha kwa ALLAH, na (yeye) Mtume pia akawaombea msamaha, bila shaka wangemkuta ALLAH ni mwenye kupokea toba (na) mwenye kurehemu. Naapa kwa (haki ya) Mola wako. Wao hawawi wenye kuamini (kweli kweli) mpaka wakufanye (wewe ndiye) hakimu (mwamuzi) katika yale wanayohitalifiana, kisha wasione uzito**

**nyoyoni mwao juu ya hukumu aliotoa, na wanyenyekee kabisa".** (4:60-65).

5. ﴿ إِنَّا أَنْزَلْنَا التَّوْرَاةَ فِيهَا هُدًى وَنُورٌ يَحْكُمُ بِهَا النَّبِيُّونَ الَّذِينَ أَسْلَمُوا لِلَّذِينَ هَادُوا وَالرَّبَّانِيُّونَ وَالأَحْبَارُ بِمَا اسْتُحْفِظُوا مِنْ كِتَابِ اللَّهِ وَكَانُوا عَلَيْهِ شُهَدَاءَ فَلاَ تَخْشَوُا النَّاسَ وَاخْشَوْنِ وَلاَ تَشْتَرُوا بِآيَاتِي ثَمَنًا قَلِيلاً وَمَنْ لَمْ يَحْكُمْ بِمَا أَنْزَلَ اللَّهُ فَأُولَئِكَ هُمُ الْكَافِرُونَ ﴾

**"Hakika tuliteremsha Taurat yenye uongozi na nuru, ambayo kwa manabii waliojisalimisha (kwa ALLAH) waliwahukumu Mayahudi, na Watawa na Maulamaa pia (walihukumu kwa hiyo Taurati), kwa sababu walitakiwa kuhifadhi kitabu (hicho) cha ALLAH, nao walikuwa mashahidi juu yake. Basi (nyinyi waislamu) msiwaogope watu bali niogopeni mimi, wala msibadilishe Aya zangu kwa thamani chache (ya dunia). Na wasiohukumu kwa yale aliyoteremsha ALLAH, basi hao ndio makafiri".** (5:44).

NNE: Sharuti zake:
Kilma cha shahada

kina sharuti (zake), yapasa juu ya kila Muislamu kujifundisha kilma hicho na kukifanyia amali. Na sharuti hizi zimechukuliwa kutoka katika Qur'aan na Hadithi, nazo ni kama zinazofuatia:

1. Elimu na dalili yake ni kauli ya (ALLAH):

فاعلم أنه لا إله إلا الله

**"Jua ya kwamba hakuna Abudiwae kwa haki ila ALLAH".** (47:19).
Imam muslim amepokea kutoka kwa Uthman (R.A) Amesema:

قال رسول الله ﷺ : « من مات وهو يعلم أن لا إله إلا الله دخل الجنة »

**"Amesema Mtume (S.A.W.): "Atakaye kufa ilhali yeye yuwajua**

**kuwa hapana Mola anayestahiki kuabudiwa kwa haki isipokua ALLAH. Ataingia Peponi". (Muslim). Na muradi ni ilmu ya hakika juu ya maana ya shahada mbili na yanayo lazimu kila moja wapo kutokana na amali, na kinyume cha ilimu ni ujinga nao, (ujinga huo) ndio uliowatia mushrikina katika umma huu katika kuyahalifu maana yake kwani wame ingia katika ujinga kutomfahamu ALLAH. Na maana ya kukanusha na kuthibitisha, na hawakujua kuwa makusudio ya kilma hiki ni kufahamu maana yake na hiyo ndiyo** walioikhalifu mushrikina, wanaojua maana iliyojulishwa na kilma hicho, waliposema:

﴿ أَجَعَلَ الْآلِهَةَ إِلَٰهًا وَاحِدًا ﴾

**"Oh! Amewafanya Miungu (wote) kuwa Mungu mmoja tu"!** (38:5).

Na wakasema:

﴿ أَنِ امْشُوا وَاصْبِرُوا عَلَىٰ آلِهَتِكُمْ ﴾

**"Nendeni (zenu), (msimsikilize huyo) na dumuni na miungu yenu"**. (38:6).

2. Yakini: Kinyume chake ni shaka na kusita au dhana na shaka. Na maana yake ni kuwa mwenye kutamka shahada mbili hapana budi kuyakinisha moyoni kwake na kuitakidi usahihi wa anayoyasema hutokana na uhaki wa ALLAH kuwa ndiye mwenye kustahiki kuabudiwa, na kuswihi Utume wa Nabii Muhammad (S.A.W.) na kubatilika uungu wa asiyekuwa ALLAH kwa sampuli yeyote atakavyodai Uungu na kubatilika kauli ya kila anaedai Utume baada ya Muhammad (S.A.W.). Basi mtu atakapotia shaka katika kuswihi maana ya kilma hicho au akasita kubatilisha ibada ya asiyekuwa ALLAH basi shahada hizo mbili hazitamfalia kitu. Na dalili ya sharti hii ni kama alivyopokea Imamu Muslim kutoka kwa Abu Hureira (R.A.A.) kutoka kwa Mtume (S.A.W.) akisema kuhusu shahada mbili:

« لا يلقى الله بهما عبد غير شاك فيهما إلا دخل الجنة ».

**"Hakuna mja yeyote atakayemkuta ALLAH kwa vilma hivyo ilhali ya kutovitilia shaka ila ataingia Peponi."** (Muslim). Na katika Swahihi imepokewa tena kutoka kwa Abu Hureira kuwa Mtume (S.A.W.) alimwambia:

« من لقيت من وراء هذا الحائط يشهد أن لا إله إلا الله مستيقنا بها قلبه فبشره بالجنة »

**"Utakayemkuta aliye nyuma ya ukuta huu akawa yuwashuhudia kuwa hakuna Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa ALLAH, ilhali moyo wake umeyakinisha kilma hicho basi mbashirie pepo."** (Muslim).

ALLAH aliyetukuka amewasifu waumini kwa kauli yake:

﴿ إِنَّمَا الْمُؤْمِنُونَ الَّذِينَ آمَنُوا بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ ثُمَّ لَمْ يَرْتَابُوا ﴾

**"Wenye kuamini kweli kweli ni wale waliomwamini ALLAH na Mtume wake, kisha wakawa si wenye shaka."** (49:15).

Na akawashutumu wanafiki kwa kauli yake:

﴿ وَارْتَابَتْ قُلُوبُهُمْ فَهُمْ فِي رَيْبِهِمْ يَتَرَدَّدُونَ ﴾

**"Na nyoyo zao zina shaka, kwa hivyo wanasitasita kwa ajili ya shaka yao."** (9:45).

Na imepokewa kutoka kwa Ibnu Mas'ud (R.A.) akisema:

« الصبر نصف الإيمان واليقين الإيمان كله »

**"Subira ni nusu ya imani na yakini ni imani yote."** (Fathul Bari: 1:45).

Na hapana shaka kuwa mwenye kuyakinisha maana ya shahada mbili viungo vyake vitavundumka (vitataharaki) katika kumwabudu ALLAH peke yake na kumtii Mtume (S.A.W.).

3. Kukubali bila ya kupinga:

Hakika muna anayejua maana ya shahada mbili na kuyakinisha maana yake lakini akawa azipinga kwa sababu ya kiburi na uhasidi. Na hii ndio hali ya wanavyuoni wa Kiyahudi na Wakinaswara, kwani wameshuhudia Uungu wa ALLAH peke yake na wakamjua Muhammad (S.A.W.) kama wanavyowajua watoto wao lakini pamoja na hivyo hawakumkubali.

﴿ حَسَدًا مِّنْ عِندِ أَنفُسِهِم مِّن بَعْدِ مَا تَبَيَّنَ لَهُمُ الْحَقُّ ﴾

**"Kwa sababu ya husuda iliyomo nyoyoni mwao, (iliyowapata baada ya kuwapambanukia haki)."** (2:109).

Na hivi ndivyo walivyokuwa mushrikina wakijua maana ya

لا إله إلا الله

**"Hapana Mola anayestahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa ALLAH"**, na wakiujua ukweli wa Muhammad (S.A.W.) lakini wakafanya kiburi kutomfuata, kama alivyosema ALLAH:

﴿ إِنَّهُمْ كَانُوا إِذَا قِيلَ لَهُمْ لَا إِلَٰهَ إِلَّا اللَّهُ يَسْتَكْبِرُونَ ﴾

**"Wao, walikua wakiambiwa "hakuna aabudiwae kwa haki isipokuwa ALLAH", walikuwa wakikataa (wakifanya kiburi)."** (37:35). ALLAH amesema:

﴿ فَإِنَّهُمْ لَا يُكَذِّبُونَكَ وَلَٰكِنَّ الظَّالِمِينَ بِآيَاتِ اللَّهِ يَجْحَدُونَ ﴾

**"Basi wao hawakukadhibishi wewe, lakini madhalimu hao wanakanusha hoja za ALLAH."** (6:33).

4. Kufuata.

Pengine tofauti baina yake na baina ya kukubali ni kuwa kufuata ni kuandama kwa vitendo na kukubali ni kudhihirisha Usahihi wa maana ya hayo kwa maneno, na yalazimu katika yote, hayo

mawili kuandama, lakini kufuata ni kujisalimisha na kudhihirisha na kutoingilia chochote katika hukumu za ALLAH.

ALLAH amesema:

﴿ وَأَنِيبُوا إِلَىٰ رَبِّكُمْ وَأَسْلِمُوا لَهُ ﴾

**"Na rejeeni kwa Mola wenu na mnyenyekee kwake."** (39:54).

ALLAH amesema:

﴿ وَمَنْ أَحْسَنُ دِينًا مِّمَّنْ أَسْلَمَ وَجْهَهُ لِلَّهِ وَهُوَ مُحْسِنٌ ﴾

**"Na ninani aliye bora kwa dini kuliko yule ambae ameuelekeza uso wake kwa ALLAH, naye nimwema."** (4:125).

ALLAH amesema:

﴿ وَمَن يُسْلِمْ وَجْهَهُ إِلَى اللَّهِ وَهُوَ مُحْسِنٌ فَقَدِ اسْتَمْسَكَ بِالْعُرْوَةِ الْوُثْقَىٰ ﴾

**"Na ajisalimishae uso wake kwa ALLAH, na hali ya kuwa anawafanyia wema (viumbe wenzie), bila shaka amekwisha kamata fundo lililomadhubuti".** (31:22).

Basi huku ndiko kumfuata ALLAH aliyetukuka kwa kumwabudu peke yake. Ama kumfuata Mtume (S.A.W.) kwa kuzikubali Sunna zake na kuyafuata aliyokuja nayo na kuiridhia hukumu yake kumeshatajwa na ALLAH kwa kauli yake:

﴿ فَلَا وَرَبِّكَ لَا يُؤْمِنُونَ حَتَّىٰ يُحَكِّمُوكَ
فِيمَا شَجَرَ بَيْنَهُمْ ثُمَّ لَا يَجِدُوا فِي أَنفُسِهِمْ حَرَجًا مِّمَّا قَضَيْتَ
وَيُسَلِّمُوا تَسْلِيمًا ﴾

**"Naapa kwa (haki ya) Mola wako wao hawawi wenye kuamini (kweli kweli) mpaka wakufanye wewe ndie hakimu (mwamuzi) katika yale wanayohitalifiana, kisha wasione uzito nyoyoni mwao juu ya hukumu uliyotoa na wanyenyekee kabisa".** (4:65).

Basi akashurutisha katika kusihi imani yao ni wainyenyekee kabisa hukumu yake. Yaani wafuate na wadhihirishe aliyokuja nayoMtume kutoka kwa Mola wake.

5. Ukweli, na kinyume chake ni uongo. Sharti hiyo imekuja katika Hadithi iliyo swahihi kutoka kwake Mtume (S.A.W.):

« من قال لا إلـه إلا الله صادقاً من قلبـه دخـل الجنـة »¹

"Atakayesema"

لا إله إلا الله

**"Hakuna Mola anayestahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa ALLAH", ilhali ya kusadikisha moyoni mwake ataingia Peponi."** (Musnad Ahmad: 4:16). Ama mwenye kukisema kilma hicho kwa ulimi wake, akayakanusha maana yake kwa moyo wake basi hakitamwokoa. Kama anavyotolea hikaya ALLAH kuhusu wanafiki waliposema: ﴿ نَشْهَدُ إِنَّكَ لَرَسُولُ اللَّهِ ﴾ ، فقال تعالى :

﴿ والله يعلم إنك لرسوله والله يشهد إن المنافقين لكاذبون ﴾

**"Tunashuhudia ya kuwa kwa yakini wewe ni Mtume wa ALLAH."** ALLAH akasema : **"Na ALLAH anajua kuwa wewe ni Mtume wake na ALLAH anashuhudia ya kuwa hakika wanafiki ni waongo, (wanasema wasiyoyasadiki)."** (63:1).

Na hivyo hivyo ALLAH amewakadhibisha kwa kauli yake:

﴿ وَمِنَ النَّاسِ مَنْ يَقُولُ آمَنَّا
بِاللَّهِ وَبِالْيَوْمِ الآخِرِ وَمَا هُمْ بِمُؤْمِنِينَ ﴾

**"Na katika watu, wako (wanafiki) wasemao: "Tumemwamini ALLAH na siku ya mwisho", na hali ya kuwa wao si wenye kuamini."** (2:8).

6. Ikhlas na kinyume chake ni shirk. ALLAH anasema:

﴿ فَاعْبُدِ اللَّهَ مُخْلِصاً لَهُ الدِّينَ . أَلاَ لِلَّهِ الدِّينُ الْخَالِصُ ﴾

**"Basi mwabudu ALLAH kwa kumfanya Mola yeye tu. Wa kuitakidiwa Mola ni ALLAH tu."** Na akasema tena:

﴿ قُلْ إِنِّي أُمِرْتُ أَنْ أَعْبُدَ اللَّهَ مُخْلِصاً لَهُ الدِّينَ ﴾

**"Sema:"Hakika nimeamrishwa nimuabudu ALLAH kwa kumuitakidi kuwa Mola ni yeye tu."** (39:14).

Akasema tena:

﴿ قُلِ اللَّهَ أَعْبُدُ مُخْلِصاً لَّهُ دِينِي ﴾

**"Sema : "Na mwabudu ALLAH kwa kumuitakidi kuwa yeye tu ndiye ALLAH."** (39:15).

Katika Swahihil - Bukhari muna Hadithi iliyopokewa kutoka kwa Abu Hureira, naye kutoka kwa Mtume (S.A.W.) akisema:

« أسعد الناس بشفاعتي من قال لا إله إلا الله خالصاً من قلبه »

**"Atakaefaulu kuipata shafaa yangu (siku ya Qiyama) ni aliesema**

لا إله إلا الله

**"Hapana Mola anaestahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa ALLAH" ilhali ya kutakasa moyoni mwake".** (Bukhari na wengineo). Nayo ndio maana ya kauli yake Mtume (S.A.W.) katika Hadithi ya 'Itbaani:

« فإن الله حرم على النار من

قال لا إله إلا الله يبتغي بذلك وجه الله »

**"Hakika ALLAH ameharamisha kumuingiza motoni aliesema**

لا إله إلا الله

**akawa yuwataka Radhi za ALLAH kwa sababu ya neno hilo."** (Bukhari na Muslim). Kwa hivyo Ikhlaas (maana yake) ni kuwa ibada ifanywe kwa ajili ya ALLAH peke yake,pasina kumwelekezea yeyote - asiekuwa Yeye - sehemu katika ibada hiyo, si Malaika aliekaribu na ALLAH wala Nabii alietumilizwa. Vile vile kufanya Ikhlaas katika kumfuata Nabii Muhammad (S.A.W.) kwa kutosheka juu ya sunna zake na alivyohukumu, na kuacha bid'a na yanayokhalifiana (na Sunna). Vile vile kuacha kuhukumu kwa sheria na kanuni walizoziweka binadamu, sheria walizozizua zinazopingana na sheria za Uislamu, basi atakaeziridhia au akahukumu kwa sheria hizo hatakuwa miongoni mwa wenye Ikhlasi.

7. Mapenzi yasiokuwa na kinyume cha uchukivu: Yapasa

juu ya mja kumpenda ALLAH, kumpenda Mtume wake (S.A.W.) na kulipenda kila analolipenda (Mtume) kutokana na amali na kauli, na kuwapenda mawalii wake (ALLAH) na wenye kumtii. Basi mapenzi ya aina hii popote yatakapokuwa ni swahihi, athari yake hudhihiri juu ya mwili, utamwona mja wa kweli yuwamtii ALLAH, yuwamfuata Mtume wake (S.A.W.), yuwamwabudu ALLAH kikweli kweli, yuwaona ladha katika kumtii ALLAH, yuwakimbilia kutenda kila analolipenda Mola wake katika jumla ya vitendo na maneno, utamwona yuwatahadhari na maaswia akijiepusha nayo na akiwachukia wenye kuyafanya hayo maaswia, ingawa maaswia hayo yanapendekeza katika nafsi, yote hayo anayafanya kwa kujua kwake kuwa moto umezungukwa kwa matamanio na pepo imezungukwa kwa machukio, basi popote atakapokuwa hivyo yeye ni mwenye mapenzi ya kweli kwa (ALLAH). Kwa ajili hii Dhun-nun al Misri (Rahimahu Allahu) alipoulizwa: **"Wakati gani nitakuwa nimempenda Mola wangu?"** Akajibu: **"Litakapokuwa linalomuudhi ni uchungu kwako kuliko subili."** (Al-Hulya, 9:363).

Baadhi yao wamesema: " **anaedai mapenzi ya ALLAH wala asimuafiki (kwa vitendo vyake) basi madai yake ni batili."**

ALLAH ameshurutisha, katika alama ya mapenzi yake ni kufuata suna za Nabii Muhammad (S.A.W.), aliposema:

﴿ قُلْ إِنْ كُنْتُمْ تُحِبُّونَ اللَّهَ فَاتَّبِعُونِي يُحْبِبْكُمُ اللَّهُ وَيَغْفِرْ لَكُمْ ذُنُوبَكُمْ ﴾

**"Sema: "Ikiwa nyinyi mnampenda ALLAH, basi nifwateni, (hapo) ALLAH atawapenda na atawaghufiria madhambi yenu."** (3:31).

8. Kuvikufuru vinavyoabudiwa badala ya ALLAH, sharti hii imechukuliwa kutoka katika kauli yake Mtume (S.A.W.):

« من قال لا إله إلا الله ، وكفر بما يعبد من دون الله حرم ماله ودمه »

**"Atakayesema**

لا إله إلا الله

**na akavikufuru vinavyoabudiwa badala ya ALLAH, ni haramu (kuchukuliwa) mali yake na damu yake."** (Muslim).

Tano: Ni jambo gani linalotangua shahada?

Linalotangua shahada ya

لا إله إلا الله

ni kumkufuru ALLAH na kumshirikisha. Na kuna sura nyingi, miongoni mwazo ni:

Ya kwanza: Kudai kuwa kuna yeyote asiyekuwa ALLAH, yuwaumba au yuwaruzuku au yuwahuisha au yuwafisha au yuwapeleka mambo au ana washirika katika jambo hilo pamoja na ALLAH. Dalili ya hayo ni kauli yake ALLAH aliyetukuka:

1. ﴿ قُلِ ادْعُوا الَّذِينَ زَعَمْتُمْ مِنْ دُونِ اللَّهِ لاَ يَمْلِكُونَ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ فِي السَّمَوَاتِ وَلاَ فِي الأَرْضِ وَمَا لَهُمْ فِيهِمَا مِنْ شِرْكٍ وَمَا لَهُ مِنْهُم مِنْ ظَهِيرٍ ﴾

**"Sema: "Waiteni mnaowadaia uungu kinyume cha ALLAH, (wawasaidie, hawawezi kuwasaidia kitu), hawamiliki (hata) uzito wa mdudu chungu mbinguni wala ardhini, wala hawana ushirika (na ALLAH) katika hizo (mbingu wala ardhi), wala yeye hana msaidizi miongoni mwao."** (34:22).

2. ﴿ الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالأَرْضَ وَجَعَلَ الظُّلُمَاتِ وَالنُّورَ ثُمَّ الَّذِينَ كَفَرُوا بِرَبِّهِمْ يَعْدِلُونَ ﴾

**"Sifa zote njema zinamthubutukia ALLAH aliyeumba mbingu na ardhi na akafanya giza na nuru. Na juu ya haya wale waliokufuru wanamsawazisha Mola wao (na vijiungu vya uongo)".** (6:1).

3. ﴿ قل من رب السموات والأرض قل الله قل أَفَتَّخَذْتُمْ مِنْ دُونِهِ أَوْلِيَاءَ لاَ يَمْلِكُونَ لأَنْفُسِهِمْ نَفْعاً وَلاَ ضَرّاً قُلْ هَلْ يَسْتَوِي الأَعْمَىٰ وَالْبَصِيرُ أَمْ هَلْ تَسْتَوِي الظُّلُمَاتُ وَالنُّورُ أَمْ

جعلوا لله شركاء خلقوا كخلقه فتشابه الخلق عليهم قل الله خالق كل شيء وهو الواحد القهار ﴾

**"Sema: "Ni nani Mola wa mbingu na ardhi?"** Sema: **"Ni ALLAH"** Sema: **"Je mnafanya waola wengine badala yake, ambao hawamiliki kwa ajili ya nafsi yao (kujivutia) nafuu wala (kujiondolea) dhara", "Sema: "Je wanaweza kuwa sawa kipofu na aonae? Au vinaweza kuwa sawa giza na nuru? Au wamemfanyia ALLAH washirika ambao wameumba kama alivyoumba ALLAH, kwa hivyo viumbe (vya pande mbili hizo) vimewadanganikia?" "Sema: "ALLAH ndie muumbaji wa kila kitu na ni mmoja tu, anayepitisha anayoyataka".** (13:16).

Na hili ndilo lililokuwa wakilikiri umma wengi, miongoni mwao ni washrikina wa Kiarabu ambao wametumiliziwa Mtume (S.A.W.). ALLAH amesema:

﴿ قُلْ مَنْ يَرْزُقُكُمْ مِنَ السَّمَاءِ وَالأَرْضِ أَمَّنْ يَمْلِكُ السَّمْعَ وَالأَبْصَارَ وَمَنْ يُخْرِجُ الْحَيَّ مِنَ الْمَيِّتِ وَيُخْرِجُ الْمَيِّتَ مِنَ الْحَيِّ وَمَنْ يُدَبِّرُ الأَمْرَ فَسَيَقُولُونَ اللَّهُ فَقُلْ أَفَلاَ تَتَّقُونَ ﴾

**"Sema: "Ni nani anayeruzuku kutoka mbinguni (kwa kuleta mvua) na katika ardhi (kwa kuotesha mimea)? Au ni nani anayemiliki masikio (yenu) na macho (yenu)? Na nani amtoae mzima katika mfu na kumtoa mfu katika mzima? Na nani atengezae mambo yote?" "Watasema ni ALLAH" Basi sema Je! Hamuongopi? (mnawaabudu wengine pamoja nae)!"** (10:31).

Lakini wao hawakushudia kuwa hapana Mola anayestahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa ALLAH, bali walikuwa kama alivyosema ALLAH:

﴿ إِنَّهُمْ كَانُوا إِذَا قِيلَ لَهُمْ لاَ إِلَهَ إِلاَّ اللَّهُ يَسْتَكْبِرُونَ ، وَيَقُولُونَ أَئِنَّا لَتَارِكُوا آلِهَتِنَا لِشَاعِرٍ مَجْنُونٍ ﴾

**"Wao walipokuwa wakiambiwa, "hakuna aabudiwae kwa haki isipokuwa ALLAH"** walikuwa wakikataa. Na husema: **"Oh! Tuiache Miungu yetu kwa ajili ya (huyu) mtunga mashairi mwenda**

**wazimu?"** (37: 35-36).

Na wakasema, kama alivyotaja ALLAH kuhusu wao:

﴿ أَجَعَلَ الْآلِهَةَ إِلَٰهًا وَاحِدًا إِنَّ هَٰذَا لَشَيْءٌ عُجَابٌ ﴾

**"Oh! Amewafanya miungu (wote) kuwa Mungu mmoja tu! Bila shaka hili ni jambo la ajabu."** (38:5).

Basi kukubali kwao kwa sampuli hii hakukuwanufaisha wac kwa yule asiyemkubali ALLAH kabisa!

Pili, kumfanyia asiyekuwa ALLAH sampuli yeyote ya ibada. Ibada ni jina lililokusanya kila alipendalo ALLAH na kuliridhia kutokana na kauli na amali za nje na ndani ambazo hazifai kumfanyia yeyote asiyekuwa yeye. Mfano wake ni kama kuchinja, kuweka nadhiri, kusujudu, khofu, matarajio, mapenzi, kutaka msaada na kujilinda. Dalili zake ni nyingi miongoni mwazo ni kauli yake ALLAH aliyetukuka (kutuelimisha namna ya kumuomba):

1.

﴿ إِيَّاكَ نَعْبُدُ وَإِيَّاكَ نَسْتَعِينُ ﴾

**"Wewe tu ndiye tunayekuabudu, na wewe tu ndie tunaekuomba msaada."** (1:5).

2.

﴿ يَا أَيُّهَا النَّاسُ اعْبُدُوا رَبَّكُمُ الَّذِي خَلَقَكُمْ وَالَّذِينَ
مِنْ قَبْلِكُمْ لَعَلَّكُمْ تَتَّقُونَ ﴾

**"Enyi watu, mwabudini Mola wenu ambae amewaumba nyinyi na wale wa kabla yenu, ili mpate kuokoka."** (2:21).

3.

﴿ وَاعْبُدُوا اللَّهَ وَلَا تُشْرِكُوا بِهِ شَيْئًا وَبِالْوَالِدَيْنِ
إِحْسَانًا وَبِذِي الْقُرْبَىٰ وَالْيَتَامَىٰ وَالْمَسَاكِينِ وَالْجَارِ ذِي الْقُرْبَىٰ
وَالْجَارِ الْجُنُبِ وَالصَّاحِبِ بِالْجَنْبِ وَابْنِ السَّبِيلِ وَمَا مَلَكَتْ
أَيْمَانُكُمْ إِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ مَنْ كَانَ مُخْتَالًا فَخُورًا ﴾

**"Mwabuduni ALLAH aliyetukuka wala msimshirikishe na kitu chochote. Na wafanyieni ihsani wazazi wawili, na jamaa na**

**mayatima na masikini na jirani waliokaribu na jirani walio mbali, na marafiki walio ubavuni (mwenu) na msafiri aliyeharibikiwa na wale iliyowamiliki mikono yenu ya kulia (kuume). Bila shaka ALLAH hawapendi wenye kiburi wajivunao".** (4:37).

4. ﴿ وَمَنْ أَضَلُّ مِمَّنْ يَدْعُوا مِنْ دُونِ اللَّهِ مَنْ لَا يَسْتَجِيبُ لَهُ إِلَىٰ يَوْمِ الْقِيَامَةِ وَهُمْ عَنْ دُعَائِهِمْ غَافِلُونَ ، وَإِذَا حُشِرَ النَّاسُ كَانُوا لَهُمْ أَعْدَاءً وَكَانُوا بِعِبَادَتِهِمْ كَافِرِينَ ﴾

**"Na wapotofu (wapotevu) wakubwa, ni nani kuliko wale wanaowaomba asiyekuwa ALLAH ambao hawatawajibu mpaka siku ya Qiyama, na hawatambui dua zao. Na (ambao) watakapokusanywa watu watakuwa maadui zao na wataikataa ibada yao."** (46: 5-6)

5. ALLAH anasema - kuyanakili maneno ya majini

﴿ وَأَنَّهُ كَانَ رِجَالٌ مِنَ الْإِنْسِ يَعُوذُونَ بِرِجَالٍ مِنَ الْجِنِّ فَزَادُوهُمْ رَهَقًا ﴾

**"Na hakika kulikuwa na wanaume miongoni mwa wanadamu wakijikinga kwa wanaume miongoni mwa majini, kwa hivyo wakawazidishia taklifu, (kama hivi wenye pepo wakataka hao mapepo kuchezewa ngoma na kuchinjiwa wanyama)."** (22:6).

6. ﴿ فَصَلِّ لِرَبِّكَ وَانْحَرْ ﴾

**"Basi swali kwa ajili ya Mola wako na uchinje (kwa ajili ya Mola wako)."** (108:2).

Tatu, (katika yanayotangua shahada) ni kufanya sawa baina ya ALLAH aliyetukuka na baina ya yeyote katika viumbe vyake katika mapenzi, taadhima, na kutukuza. Na dalili zake ni kama zinazofuata katika maneno ya ALLAH (S.W.T.):

1. ﴿ قُلْ هَلُمَّ شُهَدَاءَكُمُ الَّذِينَ يَشْهَدُونَ أَنَّ اللَّهَ حَرَّمَ هَٰذَا فَإِنْ شَهِدُوا فَلَا تَشْهَدْ مَعَهُمْ وَلَا تَتَّبِعْ أَهْوَاءَ الَّذِينَ كَذَّبُوا بِآيَاتِنَا وَالَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِالْآخِرَةِ وَهُمْ بِرَبِّهِمْ يَعْدِلُونَ ﴾

**"Sema: "Leteni mashahidi wenu wanaoweza kushuhudia kuwa ALLAH ameharamisha (wanyama) hawa (mnaosema kuwa ALLAH amewaharamisha). Basi wakitoa ushahidi (wa uwongo huo), wewe usishuhudie pamoja nao, wala usifuate matamanio ya wale waliokadhibisha aya zetu na wale wasioamini akhera na ambao wanawafanya (masanamu) sawa na Mola wao (ALLAH)."** (6:150).

2. ﴿ وَمِنَ النَّاسِ مَنْ يَتَّخِذُ مِنْ دُونِ اللَّهِ أَنْدَادًا يُحِبُّونَهُمْ كَحُبِّ اللَّهِ وَالَّذِينَ آمَنُوا أَشَدُّ حُبًّا لِلَّهِ وَلَوْ يَرَى الَّذِينَ ظَلَمُوا إِذْ يَرَوْنَ الْعَذَابَ أَنَّ الْقُوَّةَ لِلَّهِ جَمِيعًا وَأَنَّ اللَّهَ شَدِيدُ الْعَذَابِ ﴾

**"Na katika watu kuna wanaofanya waungu wasiyokuwa ALLAH. Wanawapenda kama kumpenda ALLAH. Lakini walioamini wanampenda ALLAH zaidi sana. Na laiti waliodhulumu nafsi zao wanaijua (balaa itakayowapata) watakapoiona adhabu (siku hiyo ya Qiyama), kwa kuwa nguvu zote ni za ALLAH (siku hiyo - hakuna masanamu wa kuwashufaia wala mengineyo) na kuwa ALLAH ni mkali wa kuadhibu".** (2:165).

3. ALLAH anasema, kuwanukuu mushrikina watakaokuwa motoni: ﴿ تَاللَّهِ إِنْ كُنَّا لَفِي ضَلَالٍ مُبِينٍ إِذْ نُسَوِّيكُمْ بِرَبِّ الْعَالَمِينَ ﴾

**"Wallahi, kwa yakini tulikuwa katika upotofu uliodhahiri. Tulipokuwa tukiwafanya sawa na (ALLAH) Mola wa walimwengu wote."** (26: 97-98).

4. Mtume (S.A.W.) amesema,

« من حلف بغير الله فقد كفر أو أشرك »

**"Atakayeapa kwa asiyekuwa ALLAH - amekufuru au ameshirikisha."** (Hakim na wengineo).

Nne (katika yanayotangua shahada) ni kudai wasila au wasitwa baina ya ALLAH na viumbe vyake, watu wamkurubie wasila huyo ilhali ya kudhania kuwa ndie anayewakurubisha kwa ALLAH au kuwaombea. Dalili ya hayo ni maneno ya ALLAH yanayofwatia:

1. ﴿أَلَا لِلَّهِ الدِّينُ الْخَالِصُ وَالَّذِينَ اتَّخَذُوا مِنْ دُونِهِ أَوْلِيَاءَ مَا نَعْبُدُهُمْ إِلَّا لِيُقَرِّبُونَا إِلَى اللَّهِ زُلْفَى إِنَّ اللَّهَ يَحْكُمُ بَيْنَهُمْ فِي مَا هُمْ فِيهِ يَخْتَلِفُونَ إِنَّ اللَّهَ لَا يَهْدِي مَنْ هُوَ كَاذِبٌ كَفَّارٌ﴾

**"Wakuitakidiwa Mola ni ALLAH tu, lakini wale wanaofanya wengine kuwa waungu badala yake (husema:) "sisi hatuwaabudu hawa ila wapate kutufikisha karibu kabisa na ALLAH". Hakika ALLAH atahukumu baina yao katika yale wanayokhitalifiana. Bila shaka ALLAH hamuongoi aliye muongo, aliye kafiri."** (39:3).

2. وَيَعْبُدُونَ مِن دُونِ اللَّهِ مَا لَا يَضُرُّهُمْ وَلَا يَنفَعُهُمْ وَيَقُولُونَ هَٰؤُلَاءِ شُفَعَاؤُنَا عِندَ اللَّهِ قُلْ أَتُنَبِّئُونَ اللَّهَ بِمَا لَا يَعْلَمُ فِي السَّمَاوَاتِ وَلَا فِي الْأَرْضِ سُبْحَانَهُ وَتَعَالَىٰ عَمَّا يُشْرِكُونَ ⑱ وَمَا كَانَ

**"Nao wanaabudu (waungu) - wasiokuwa ALLAH - wasioweza kuwadhuru (wanapowacha) kuwaabudu wala kuwanufaisha (wakiwaabudu). Na wanasema: "Hao (waungu wadogo washirika wake tunaowaabudu) ndio waombezi wetu mbele ya ALLAH. "Sema: "Je! Mnamwambia ALLAH asiyoyajua katika mbingu wala katika ardhi? "Ameepukana na upungufu (wa kutaka mshirika), na ametukuka na hao wanaowashirikisha naye."** (10:18).

Tano, kuhukumu kwa sheria isiyokuwa ya ALLAH. Dalili yake ni maneno ya ALLAH yasemayo:

1. ﴿أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ يَزْعُمُونَ أَنَّهُمْ آمَنُوا بِمَا أُنْزِلَ إِلَيْكَ وَمَا أُنْزِلَ مِنْ قَبْلِكَ يُرِيدُونَ أَنْ يَتَحَاكَمُوا إِلَى الطَّاغُوتِ وَقَدْ أُمِرُوا أَنْ يَكْفُرُوا بِهِ وَيُرِيدُ الشَّيْطَانُ أَنْ يُضِلَّهُمْ ضَلَالًا بَعِيدًا﴾

**"Wao ni wale wanaodai kwamba wameamini yale yaliyoteremshwa kwako na yaliyoteremshwa kabla yako? Nao wanataka wakahukumiwe kwa njia isiowafiki sharia, na hali wameamrishwa kukataa njia hiyo. Na shetani anataka kuwapoteza upotofu (upotevu) ulio mbali (na haki)."** (4:60).

2. ﴿ وَأَنِ احْكُم بَيْنَهُم بِمَا أَنزَلَ اللَّهُ وَلَا تَتَّبِعْ أَهْوَاءَهُمْ وَاحْذَرْهُمْ أَن يَفْتِنُوكَ عَن بَعْضِ مَا أَنزَلَ اللَّهُ إِلَيْكَ فَإِن تَوَلَّوْا فَاعْلَمْ أَنَّمَا يُرِيدُ اللَّهُ أَن يُصِيبَهُم بِبَعْضِ ذُنُوبِهِمْ وَإِنَّ كَثِيرًا مِّنَ النَّاسِ لَفَاسِقُونَ أَفَحُكْمَ الْجَاهِلِيَّةِ يَبْغُونَ وَمَنْ أَحْسَنُ مِنَ اللَّهِ حُكْمًا لِّقَوْمٍ يُوقِنُونَ ﴾

**"Na wahukumu baina yao kwa yale aliyoyateremsha ALLAH, wala usifwate matamanio yao nawe jihadhari nao kukugeuza na baadhi ya yale aliyokuteremshia ALLAH. Na kama wakikugeuka, basi jua kwamba hakika ALLAH anataka kuwafikishia (adhabu) kwa baadhi ya dhambi zao. Na bila shaka wengi katika watu ni maasi. Je, wao wanataka hukumu za kijahili (ya zile siku za ujinga kabla ya kuletwa Mtume)? Na nani aliye mwema zaidi katika hukumu kuliko ALLAH, (yanafanyika hayo) kwa watu wenye yakini."** (5: 49-50).

Na sampuli hizi huenda zika jumuika katika baadhi ya watu na huenda pia zikapatikana moja moja kwa watu wengine. Basi kushuhudia kuwa **"hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa ALLAH"** ni jambo kubwa walilokuwa wakililingania Mitume wote na wakikariri kuwaambia watu wao:

**"Mwabuduni ALLAH. Nyinyi hamna Mungu ila yeye".** (7:59), na mfano wa maneno kama hayo yaliotajwa katika sehemu nyingi za Qur'aan. ALLAH alipomtumiliza Mtume Muhammad (S.A.W.) neno hilo ndilo lililokuwa kubwa zaidi akililingania na akapigana jihadi katika njia yake, seira yote ya Mtume Muhammad (S.A.W.) yathibitisha jambo hilo, kama alivyosema Mtume Muhammad (S.A.W.):

« بعثت بالسيف بين يدي الساعة حتى يعبد الله وحده لا شريك له وجُعِلَ رزقي تحت ظل رمحي وَجُعِلَ الذلة والصغار على من خالف أمري »

**"Nimetumilizwa kwa upanga karibu na Qiyama ili aabudiwe ALLAH peke yake hana mshirika, imejaaliwa riziki yangu kuwa chini ya kivuli cha mshale na umejaaliwa unyonge na udhalilifu juu ya atakaye ikhalifu amri yangu".** (Ahmad na wengineo) Akasema tena

**"Nimeamrishwa kupigana na watu hata washuhudie kuwa hapana Mola anayestahiki kuabudiwa isipokuwa ALLAH na kwamba Muhammad ni Mtume wa ALLAH, wasimamishe Swala na watoe Zaka na watakapofanya hivyo zitahifadhika kutokana na mimi, damu zao na mali yao isipokuwa kwa haki yake na hisabu yao iko kwa ALLAH aliyetukuka."** (Bukhari na Muslim). Mtume (S.A.W.) alikuwa akituma wajumbe na barua kwa ajili ya kuwalingania watu jambo hilo, kama ilivyokuja katika kisa cha Mu'adh, kuwa Mtume (S.A.W.) alimwambia - alipomtumiliza kuenda Yemen:

« إنك تأتي قوماً من أهل الكتاب فادعهم إلى شهادة أن لا إلـه إلا الله وأني رسول الله . فإن هم أطاعوك لذلك فأعلمهم أن الله افترض عليهم خمس صلوات في كل يوم وليلة ، فإن هم أطاعوك لذلك فأعلمهم أن الله افترض عليهم صدقة تؤخذ من أغنيائهم فترد في فقرائهم ، فإن هم أطاعوك لذلك ، فإياك وكرائم أموالهم . واتق دعوة المظلوم فإنه ليس بينها وبين الله حجاب »

**"Hakika unawaendea watu ambao ni Ahlu-kitab, basi walinganie katika kushuhudia kuwa hapana Mola anaestahili kuabudiwa kwa haki isipokua ALLAH, na kwamba mimi ni Mtume wa ALLAH. Wakikutwii katika jambo hilo, waelimishe kuwa ALLAH amewafaradhia swala tano kila mchana na usiku. Wakikutwii katika jambo hilo, waelimishe kuwa ALLAH amewafaradhia Zaka, huchukuliwa kutoka kwa matajiri wao zikarejeshewa mafukara wao. Wakikutwii katika jambo hilo jitahadhari na ziada ya mali yao. Na uiyogope dua ya aliedhulumiwa, kwani haina hijabu (pazia) baina baina yake na baina ya ALLAH."** (Bukhari na Muslim).

Kushuhudia kuwa hapana Mola anaestahiki kuabudiwa kwa

haki isipokuwa ALLAH, ni jambo la kwanza la wajibu juu ya waja wote na ni jambo la mwisho analolinganiwa mja, kama ilivyokuja katika Hadithi:

« لقنوا موتاكم شهادة أن لا إله إلا الله »

**"Wafundisheni watu wenu wanaofikiwa na mauti kutamka Shahada ya** لا إله إلا الله

(Muslim). Na Hadithi (Isemayo:)

« من كان آخر كلامه لا إله إلا الله دخل الجنة »

**"Ambae maneno yake ya mwisho yatakuwa ni**

لا إله إلا الله

**ataingia Peponi."** (Abudaud na Hakim katika **'Al-Mustadrak').** Na kwa ajili ya kilma hicho cha Shahada, ALLAH ameweka Sharia ya Jihad, ulinganizi, kuamrisha mema na kukataza mabaya. Na kwa ajili ya kilma hicho watu wamekuwa makundi mawili: watu wa Imani, nao ndio watu wa peponi, na watu wa kufri (ukafiri) nao ndio watu wa motoni.

Basi atakayekithibitisha kilma hicho kwa nje na ndani na akazitekeleza hukumu zake na haki zake atakuwa na amani iliyotimia na uongofu uliokamilika duniani na Akhera kama alivyosema ALLAH aliyetukuka:

﴿ الَّذِينَ آمَنُوا وَلَمْ يَلْبِسُوا إِيمَانَهُمْ بِظُلْمٍ أُولَٰئِكَ لَهُمُ الْأَمْنُ وَهُمْ مُهْتَدُونَ ﴾

**"(Hapana shaka kuwa) wale walioamini na hawakuchanganya imani yao na ushirikina kuwa hao ndio watakaopataamani, na ndio waliyoongoka."** (6:82). Na kama ilivyo katika kauli yake Mtume

« إن الله حرم على النار من قال لا إله إلا الله يبتغي بذلك وجه الله »

(S.A.W.), **"Hakika ALLAH ameharamisha kuingia motoni kwa atakayesema**

لا إله إلا الله

**ilhali yuwatafuta radhi za Mwenyezi Mungu kwa neno hilo."** (Bukhari na Muslim). Basi kilma hicho ni sharti ya kuokoka duniani na Akhera nacho kilma hicho ni dhikr iliyo bora na ni wasila kubwa.

Twamuomba ALLAH (S.W.) atujaalie sisi na ndugu zetu Waislamu ni wenye kujua hakika yake (kilma hicho) wakakifanyia amali kwa muktadha wake na wakafanya Ikhlas katika kukitamka, hakika ya yeye ni mwenye kusikia na ni mwenye kujibu.

* * * * * * * *

# UKAMILISHO KUHUSU KUSHUHUDIA KUWA MUHAMMAD (S.A.W.) NI MTUME WA ALLAH:

Imetangulia kuashiria kuwa kushuhudia kwamba Muhammad (S.A.W.) ni Mtume wa ALLAH (S.W.T.) huingia katika shahada ya

لا إله إلا الله

kwa uhakika na mafhum. Kila kilichotangulia kuhusiana na shahada hukusanya jumla mbili japo haikutajwa ila jumla ya Kwanza - shahada ya

لا إله إلا الله

Isipokuwa shahada ya

محمداً رسول الله ﷺ

(Muhammad ni Mtume wa ALLAH) imelinganishwa kwa kilma cha shahada kwa sababu ya hikma kubwa na maana tukufu yanayojulisha juu yake, miongoni mwayo:

1. Kumpenda Mtume (S.A.W.) nayo ndiyo msingi mkubwa katika misingi ya imani. Mtu hawezi kuwa mu'mini ila kwa mapenzi hayo, wala haifikii imani ila baada ya kukamilisha mapenzi hayo. Mtume S.A.W. amesema:

« والذي

نفسي بيده لا يؤمن أحدكم حتى أكون أحب إليه من ولده ووالده

والناس أجمعين »

**"Naapa kwa ambaye nafsi yangu iko mkononi mwake, haamini mmoja wenu mpaka niwe napendeza zaidi kwake yeye kuliko mtoto wake, mzazi wake na watu wote".** (Bukhari na Muslim).

2. Kumfuata na kumtii Mtume (S.A.W.). Jambo hili ndilo jambo kubwa zaidi katika mambo yanayolazimu kumpenda yeye na kumwamini. ALLAH amesema:

﴿ قُلْ إِنْ كُنْتُمْ تُحِبُّونَ اللَّهَ فَاتَّبِعُونِي يُحْبِبْكُمُ اللَّهُ وَيَغْفِرْ

لَكُمْ ذُنُوبَكُمْ وَاللَّهُ غَفُورٌ رَحِيمٌ قُلْ أَطِيعُوا اللَّهَ وَالرَّسُولَ فَإِنْ تَوَلَّوْا فَإِنَّ اللَّهَ لا يُحِبُّ الْكَافِرِينَ ﴾

**"Sema: "Ikiwa nyinyi mnampenda ALLAH, basi nifuateni, (hapo) ALLAH atawapenda na atawaghufiria madhambi yenu. Na ALLAH ni mwenye maghfira (na) mwenye Rehema. "Sema: "Mtiini ALLAH na Mtume (wake). Na kama mkikengeuka, (ALLAH) atawatia adabu, kwani ALLAH hawapendi makafiri".** (3:31-32).

Basi atakeitakidi kuwa kuna yeyote anaeweza kutoka katika twaa yake (Mtume-S.A.W.) au kufika kwa ALLAH pasina kufwata njia yake, atakuwa amekufuru. ALLAH amesema:

﴿ وَمَا أَرْسَلْنَا مِنْ رَسُولٍ إِلاَّ لِيُطَاعَ بِإِذْنِ اللَّهِ ﴾

**"Na hatukumleta Mtume yeyote ila atiiwe kwa amri ya ALLAH".** (4:64).

3. Kumsadikisha katika yote aliyoyatolea khabari. Atakaerudisha jambo alilokuja nalo na akamkadhibisha katika jambo hilo, basi mtu huyo ni kafiri. Ni sawa tu, awe amelirudisha jambo hilo kwa kufwata matamanio, au kufwata sharia ilokwishafutwa, au kufwata falsafa ya kurithiwa, au kuifwata elimu iliyoekewa na wanaadamu. ALLAH amesema:

﴿ وَالَّذِي جَاءَ بِالصِّدْقِ وَصَدَّقَ بِهِ أُولَئِكَ هُمُ الْمُتَّقُونَ ﴾

**"Na aliyeleta ukweli na aliyeusadikisha - hao ndio wamchao ALLAH".** (39:33). Akasema tena ALLAH:

﴿ فَآمِنُوا بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ وَالنُّورِ الَّذِي أَنْزَلْنَا ﴾

**"Basi muaminini ALLAH na Mtume wake na nuru tuliyoiteremsha, (Qur'aan)".** (64:8). Na akasema tena ALLAH:

﴿ وَمَا يَنْطِقُ عَنِ الْهَوَى إِنْ هُوَ إِلاَّ وَحْيٌ يُوحَى ﴾

**"Wala hasemi kwa matamanio (ya nafsi yake). Hayakuwa haya (anayosema) ila ni wahyi (ufunuo), uliofunuliwa (kwake)".** (53:3-4).

Mtume (S.A.W.) amesema:

« والذي نفسي بيده لا يسمع بي يهودي ولا نصراني ثم لا يؤمن بي إلا كان من أهل النار»

**"Naapa kwa ambae nafsi yangu i mikononi mwake, hatonisikia Myahudi wala mnasara kisha asiniamini ila atakuwa ni mtu wa Motoni".** (Muslim).

Basi jambo hili limethubutu kwa Ah-lul-kitab na kwa wasiokuwa wao ni aula zaidi.

4. Kumfanya Mtume (S.A.W.) kuwa ni Hakimu katika kilajambo, asiitangulie kauli wala hukmu yake kwa kauli na hukmu ya mwingine, wala rai ya yeyote, awe awavyo.

ALLAH amesema:

﴿ فَلَا وَرَبِّكَ لَا يُؤْمِنُونَ حَتَّىٰ يُحَكِّمُوكَ فِيمَا شَجَرَ بَيْنَهُمْ ثُمَّ لَا يَجِدُوا فِي أَنفُسِهِمْ حَرَجًا مِّمَّا قَضَيْتَ وَيُسَلِّمُوا تَسْلِيمًا ﴾

**"Naapa kwa (haki ya) Mola wako. Wao hawawi wenye kuamini (kweli kweli) mpaka wakufanye (wewe ndiye) hakimu (mwamuzi) katika yale wanayokhitilafiana, kisha wasione uzito nyoyoni mwao juu ya hukumu uliyotoa, na wanyenyekee kabisa."** (4:65).

ALLAH amesema:

﴿ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تُقَدِّمُوا بَيْنَ يَدَيِ اللَّهِ وَرَسُولِهِ ﴾

**"Enyi mlioamini! Msitangulize (kusema lenu) mbele ya (neno la) ALLAH na Mtume wake."** (49:1).

Akasema tena ALLAH:

﴿ وَمَا كَانَ لِمُؤْمِنٍ وَلَا مُؤْمِنَةٍ إِذَا قَضَى اللَّهُ وَرَسُولُهُ أَمْرًا أَن يَكُونَ لَهُمُ الْخِيَرَةُ مِنْ أَمْرِهِمْ ﴾

**"Haiwi kwa mwanamume aliyeamini wala kwa mwanamke aliyeamini, ALLAH na Mtume wake wanapokata shauri, wawe na hiari katika shauri lao."** (33:36).

Basi kwa ajili hii, kila anaehukumu kwa kanuni zilizoekwa na watu na kwa maoni ya kijahilia atakua ameshaitanguwa shahada ya

محمداً رسول الله

**"Muhammad ni Mtume wa ALLAH."**

5. Asiabudiwe ALLAH ila kwa sharia aliyoiweka, nayo ni kushikamana na sunna zake (Mtume) na kujilazimu uongofu wake katika mambo yote na kuacha aliyokataza katika bid'a na kuzua katika Dini, hata kama mtu atadhania kuwa bid'a hiyo inamkurubisha kwa ALLAH. Na kumuiga Mtume (S.A.W.) katika kila ambalo ni la kufuatwa na kuigwa. ALLAH amesema.

﴿ لَقَدْ كَانَ لَكُمْ فِي رَسُولِ اللَّهِ أُسْوَةٌ حَسَنَةٌ لِمَنْ كَانَ يَرْجُو اللَّهَ وَالْيَوْمَ الآخِرَ وَذَكَرَ اللَّهَ كَثِيرًا ﴾

**"Bila shaka mnao mfano mwema (ruwaza nzuri) kwa Mtume wa ALLAH, kwa mwenye kumuogopa ALLAH na siku ya mwisho, na kumtaja ALLAH sana."** (33:21) Akasema tena ALLAH:

﴿ وَمَنْ يُشَاقِقِ الرَّسُولَ مِنْ بَعْدِ مَا تَبَيَّنَ لَهُ الْهُدَى وَيَتَّبِعْ غَيْرَ سَبِيلِ الْمُؤْمِنِينَ نُوَلِّهِ مَا تَوَلَّى وَنُصْلِهِ جَهَنَّمَ وَسَاءَتْ مَصِيرًا ﴾

**"Na atakayemwasi Mtume baada ya kumdhihirikia uwongofu na akafwata njia isiyokuwa ya Waislamu, tutamgeuza alikogeukia mwenyewe na tutamuingiza katika Jahannam, hapo ni pahali pabaya kabisa pa mtu kurudia."** (4:115). Mtume (S.A.W.) amesema:

« من عمل عملاً ليس عليه أمرنا فهو رد »

**"Atakayefanya amali ambayo si katika jambo letu basi amali hiyo ni yenye kurudishwa."** (Bukhari na Muslim). Na katika riwaya (Mapokezi) nyingine yasema:

« من أحدث في أمرنا هذا ما ليس منه فهو رد »

**"Atakaezua katika jambo letu hili ambalo halitokani nalo, basi jambo hilo ni lenye kurudishwa."** (Riwaya ya Muslim). Akasema tena:

« لقد تركتكم على مثل البيضاء(٦) ليلها كنهارها لا يزيغ عنها إلا هالك »

**"Hakika nimewaacha juu ya mfano wa jua, usiku wake ni kama mchana wake, hakuna atakaegeuka ila mwenye kuangamia."** (IBNU ABI 'AASIM, katika kitabu cha '**Assunnah**').

(Mpaka hapa tulipofika) Rehma na Amani zimwendee (Nabii Muhammad), Aali zake, Maswahaba wake na kila atakaeufwata mwendo wake hadi siku ya malipo........................Aamin.

# NGUZO YA PILI

# SWALA

# UTANGULIZI WA UTWAHARA

## TAARIFA YA UTWAHARA NA HUKUMU YAKE:

Utwahara ni kujinadhifisha na kujiepusha na uchafu na najisi. Nao huo (utwahara) ni waajib juu ya Muislamu. Kwa dalili ya kauli yake ALLAH:

﴿ وَثِيَابَكَ فَطَهِّرْ ﴾

**"Na nguo zako uzisafishe."** (74:4). Na kauli yake nyingine:

﴿ وَإِنْ كُنْتُمْ جُنُبًا فَاطَّهَّرُوا ﴾

**"Na mkiwa na janaba basi ogeni."** (5:6). Na kauli ya Mtume (S.A.W.):

« لاتقبل صلاة بغير طهور »

**"Haikubaliwi Swala pasina utwahara".** (MUSLIM). Na kauli yake:

« الطهور شطر الإيمان »

**"Kujitwahirisha ni nusu ya Imani".** (MUSLIM).

## SAMPULI ZA UTWAHARA:

Twahara ni sampuli mbili: utwahara wa ndani na utwahara wa nje.

1. Utwahara wa ndani: ni kuutwahirisha moyo kutokana na uchafu wa shirki, shaka (katika Dini), shubha na maafa (mengine) kwa sampuli na maumbile yake. Hayo hupatikaniwa kwa kumfanyia ALLAH Ikhlaas na kumwelekea ki-kweli kweli na kumfwata Mtume wake (S.A.W.) na kuitwahirisha nafsi kutokana na athari za maasia, madhambi na kukhalifu, nayo hupatikaniwa kwa toba ya kweli bila kuyarudia tena madhambi.

2. Utwahara wa nje nao ni kuutwahirisha uchafu na utwahara wa hadathi.

a. Kuutwaharisha uchafu: huwa kwa kuziondosha najisi-kwa maji yalotwahara - katika mwili, nguo, ardhi na sehemu nyingine.

b. Utwahara wa hadathi: nao ni udhu, kuoga na kutayamamu.

## UTWAHARA UNAFANYIKA KWA KITU GANI?

Utwahara huwa kwa mambo mawili:

1. Maji mutlaq.

Nayo ni yaliyo katika asili ya maumbile yake kwa namna ambayo hayakutangamana na kitu kinachokua mbali nacho aghalabu, kitu hicho kiwe ni najisi au ni twahara, kama maji ya mvua, kisimani, chemchem, jangwa, mito, theluji zilizoyayuka na bahari ya chumvi. ALLAH (S.W.T.) amesema:

﴿ وَأَنزَلْنَا مِنَ السَّمَاءِ مَاءً طَهُورًا ﴾

**"Na tunayateremsha kutoka mawinguni maji safi (kabisa)".** (25:48). Na Mtume (S.A.W.) amesema, **"maji ni twahara hayanajisiwi na kitu"**, (Ahmad, Abu Dawud na wengineo).

2. Mchanga Twahara - nao ni ulio juu ya ardhi iliyo twahara kutokana na mchanga au changarawe au mawe, kwa dalili ya kauli yake Mtume S.A.W.

« وجُعِلَتْ لِي الأرض طهـوراً ومسـجداً »

**"Na imejaaliwa kwangu mimi ardhi ni twahara na ni mahali pa kuswalia."** (Muslim). Na yatakiwa mchanga uwe Twahara katika hali ya kukosekaniwa maji au kushindwa kuyatumia maji hayo kwa sababu ya ugonjwa na mfano wake, kwa dalili ya kauli yake ALLAH (S.W.T.):

﴿ فَلَمْ تَجِدُوا مَاءً فَتَيَمَّمُوا صَعِيدًا ﴾

**"Na kama mukiwa wagonjwa (mmekatazwa kutumia maji) au mmo safarini au mmoja wenu ametoka msalani (chooni) au mmewagusa wanawake - na msipate maji - basi ukusudieni (tayamamuni) udongo safi".** (4:43). Na kauli ya Mtume yasema,

« إن الصعيد الطيب طهور المسلم وإن لم يجد الماء عشر سنين
فإذا وجد الماء فليمسه بشرته »

**"Hakika mchanga mzuri ni utwahara wa Mwislamu, hata asipopata maji miaka kumi. Atakapoyapata maji na ayagusishe ngozi yake".** (Ahmad, Tirmidhi na wengineo).

## FAIDA: VIGAWANYO VYA MAJI.

1. Maji Mutlaq.

Tumeshayataja mbeleni, na hukumu yake ni kuwa maji hayo ni Twahur, yaani hayo yenyewe ni Twahara na ni yenye kutwahirisha vitu vingine, na tumeshataja sampuli zake pia.

2. Maji yaliyotumiwa

Nayo ni maji yaliyokuwa yameshatumiwa katika viungo vya mwenye kutawadha na mwenye kuoga. Hukumu yake ni Twahur kama maji Mutlaq, kwa kuzingatia asili yalipokuwa ni twahara. Kwani imethubutu kuwa Mtume S.A.W.: **"Alipukusa kichwa chake kwa maji yaliyobakia katika mkono wake".** (Ahamad na Abu Dawud).

3. Maji yaliyotangamana na kitu Twahara kama sabuni na vyenginevyo katika vitu ambavyo huwa mbali na maji hayo na hukumu yake ni Twahur maadamu yamehifadhika kuwa ni maji Mutlaq. Yakitoka katika sifa yake hiyo kwa namna ya kutoitwa tena maji Mutlaq basi yatakuwa hayo yenyewe ni Twahara lakini hayawezi kutwahirisha kitu kingine.

4. Maji yaliyokutana na najisi, yana hali mbili:

Kwanza: Ile najisi ibadilishe tamu (ladha) ya maji hayo au rangi yake au harufu yake. Basi katika hali hii haifai kujitwahirisha kwa maji hayo kwa itifaki ya wanazuoni wote. ALLAH awarehemu.

Pili: Yabakie maji juu ya sifa yake, kwa kutobadilika mojawapo ya sifa zake tatu. Hukumu yake katika hali hii itakuwa ni hayo yenyewe ni twahara na yanaweza kutwahirisha kitu kingine, yawe kidogo au mengi. Kwa dalili yake Mtume (S.A.W.):
**"Maji ni twahara hayanajisiwi na kitu".** (Ahmad, Abudawud na wengineo).

## SAMPULI ZA NAJISI:

Najisi ni: chenye kutoka katika uchi wa Binadamu kutokana na kishonde, au mikojo au madhy, au wadii, vilevile na mikojo na choo cha kila hayawani ambaye nyama yake si halali kuliwa, vilevile damu, matapishi na usaha. Kadhalika sampuli mbali mbali za mfu na viungo vyake, ila ngozi inapodabighiwa, kwani kutwahirika kwakeni kwa kuidabighi. Kwa dalili ya kauli ya Mtume (S.A.W.):

« أيما إهاب دبغ فقد طهر »

**"Ngozi yoyote iwayo ikidabighiwa imeshatwahirika".** (Muslim).

## ADABU ZA KUKIDHI HAJA:

Kwa mwenye kukidhi haja ana adabu anazotakiwa kuzifanya. Nazo ni:

1. Atafute mahali pasipokuwa na watu, pawe mbali na macho yao. Kama ilivyothubutu kuwa, Mtume (S.A.W.):

« كان إذا أراد (البراز) انطلق حتى لا يراه أحد »

**"Alikuwa anapotaka kwenda haja (kubwa) huondoka ili asionekane na yeyote".** (ABUDAUD NA TIRMIDHY).

2. Asisuhubiane na kitu chenye jina la ALLAH. Isipokuwa atakapochelea kupotea.

3. Asizungumze katika hali ya haja.

4. Kukitukuza Qibla, asikielekee wala asikipe mgongo katika hali ya kuenda haja kubwa au haja ndogo. Kwa dalili ya kauli yake Mtume (S.A.W.):

« لا تستقبلوا القبلة ولا تستدبروها بغائط أو بول »

**"Msikielekee Quibla wala msikipe mgongo katika hali ya kwenda haja kubwa au ndogo".** (BUKHARI NA MUSLIM).

5. Kujiepusha vivuli wanavyoketi watu, njia wanazopita, mabaraza yao, maji wanayochota na miti yenye matunda, (ajiepushe

sehemu hizo) katika hali ya kuenda haja kubwa au ndogo. Kwa dalili ya kauli yake Mtume (S.A.W.):

« اتقوا اللاعِنَيْنِ

قالـوا : ومـا اللاعنان يا رسول الله ؟ قال : « الذي يتخلى في طريق الناس أو ظلهم »[1]

**"Jiepusheni na yaletayo laana".** Wakauliza: **"Ni yapi hayoyaletayo laana ewe Mtume wa ALLAH?"** Akajibu: **"Ni anaekidhi haja katika njia wanazozipita watu au katika vivuli vyao (wanavyoketi)."** (MUSLIM).

6. Autangulize mguu wake wakushoto wakati wa kuingia, atakapotoka atautanguliza mguu wake wa kulia, kinyume na Msikitini. Sababu ya kufanya hivyo ni kuzipambanua sehemu zenye utwahara na sehemu zenye najisi.

7. Aseme kabla ya kuingia:

« بسم الله » ، « اللهم إني أعوذ بك من الخبث[3] والخبائث »[1]

**"Kwa jina la ALLAH ewe Mola hakika mimi najilinda kwako kutokakana na mashetani wachafu wanaume na wanawake."** (Bukhari na Muslim). Na kupiga Bismi Ilahi kabla ya kuingia kwa dalili ya kauli yake Mtume (S.A.W.): **"Sitara baina ya majini na uchi wa binaadamu anapoingia chooni mmoja wao aseme:**

بسم الله

(Ahamad, Tirmidhi na Ibnu Maja). Na imepokewa katika riwaya nyengine kujumuisha baina ya kupiga Bismi Ilahi na kuomba dua iliyotajwa. (Said bin Mansur katika kitabu chake cha Sunan).

8. Asiiyenuwe nguo yake mpaka akurubie katika ardhi, ili kuisitiri tupu yake, kama ilivyoamrishwa ki-sharia.

9. Baada ya kukidhi haja na kutoka, aseme:

« غفرانك »

**"Msamaha ni wako ewe Mola."**

## ADABU ZA KUTAMBA NA ISTIJMARI (1)

1. Asitambe wala asifanye istijmari kwa mfupa au choo cha mnyama. Kwa dalili ya kauli yake Mtume (S.A.W.):

« لا تستنجوا بالروث ولا بالعظام فإنه زاد إخوانكم من الجن »

**"Msitambe kwa choo (cha mnyama au ndege) wala kwa mifupa kwani ni vyakula vya ndugu zenu majini:"** (Tirmidhy na wengineo Asili ya Hadithi hii imo katika Swahihi Muslim).

2. Kadhalika asifanye istijmari kwa kitu chenye manufaa, wala kwa kitu kinachohishimiwa, kama vile chakula.

3. Asipanguse au kutamba kwa mkono wake wa kulia, au kuigusa dhakari yake kwa mkono huo. Kwa dalili ya kauli yake Mtume (S.A.W.):

« لا يمس أحدكم ذكره بيمينه وهو يبول ولا يتمسح من الخلاء بيمينه »

**"Asiiguse mmoja wenu dhakari yake kwa mkono wa kulia ilhali yuwakojoa. Wala asijipanguse chooni kwa mkono wake wa kulia."** (Bukhari na Muslim).

4. Afanye istijmari kwa witri. Kama kufanya istijmari kwa mawe matatu, ikiwa hayakusafisha afanye kwa mawe matano, namna hiyo, kwa dalili ya kauli ya Salman (R.A.):

« نهانا رسول الله ﷺ أن نستقبل القبلة بغائط أو بول أو أن نستنجي باليمين ، أو أن نستنجي بأقل من ثلاثة أحجار أو أن نستنجي برجيع(٤) أو عظم »

---

(1) ISTIJMARI: ni kutamba kwa mawe au kitu kingine, bila kutumia maji.

**"Mtume (S.A.W.) ametukataza kuelekea Qibla wakati wa kuenda haja kubwa au ndogo, au kutamba kwa mkono wa kulia, au kutamba kwa uchache wa mawe matatu, au kutamba kwa choo (cha mnyama) au mfupa."** (Muslim).

5. Akijumuisha baina ya kutamba kwa maji na mawe, atatanguliza mawe kwanza halafu maji. Na akitumia kimojawapo kitamtosha. Isipokuwa tu, maji ni usafi na ni utwahara zaidi.

## U D H U

### DALILI YA KUFANYWA KUWA NI SHARIA:

Imethubutu udhu kuwa ni sharia, kwa dalili tatu:

- Dalili ya kwanza: Ni katika Qur'aan Tukufu. ALLAH amesema:

﴿ يَاأَيُّهَا الَّذِينَ
آمَنُوا إِذَا قُمْتُمْ إِلَى الصَّلاَةِ فَاغْسِلُوا وُجُوهَكُمْ وَأَيْدِيَكُمْ إِلَى
الْمَرَافِقِ وَامْسَحُوا بِرُؤُسِكُمْ وَأَرْجُلَكُمْ إِلَى الْكَعْبَيْنِ ﴾

**"Enyi mlioamini! Mnaposimama ili mkasali, basi osheni nyuso zenu na mikono yenu mpaka vifundoni, na vichwa vyenu, na (osheni) miguu yenu mpaka vifundoni."** (5:6).

- Dalili ya pili: Ni katika Sunna Toharifu. Mtume (S.A.W.) amesema:

« لا يقبل الله صلاة أحدكم إذا أحدث حتى يتوضأ »

**"ALLAH haikubali swala ya mmoja wenu - anapopatwa na hadathi - mpaka atawadhe."** (Bukhari na Muslim).

- Dalili ya tatu: Ijmai Waislamu wote wameafikiana kuwa udhu ni sharia, tangu zama za Mtume (S.A.W.) mpaka siku hii ya leo. Basi ikajulikana katika dini jambo hili kuwa ni dharura.

**FADHILA ZA UDHU:**

Zimepokewa Hadithi nyingi kuhusiana na fadhila za udhu. Tutazitaja baadhi tu: Mtume (S.A.W.) amesema:

« ألا أدلكم على ما يمحو الله به الخطايا ويرفع به الدرجات ؟ قالوا : بلى يا رسول الله ، قال : « إسباغ الوضوء على المكاره وكثرة الخطا إلى المساجد وانتظار الصلاة بعد الصلاة ، فذلكم الرباط(٣) فذلكم الرباط ، فذلكم الرباط

**"Je, nisiwajulishe jambo ambalo, ALLAH hufuta dhambi kwa sababu yake na yuwainua daraja kwa sababu yake?"** Wakasema: **"Tufundishe."** Akasema: **"Kueneza udhu wakati wa kuona karaha, kuenda hatua nyingi hadi Msikitini na kuingojea swala baada ya Swala. Basi (kufanya hayo) ndio kujifunga katika njia ya ALLAH, kufanya hayo ndio kujifunga, kufanya hayo ndio kujifunga".** (Muslim).

- Mtume (S.A.W.) amesema:

« إذا توضأ العبد المسلم أو المؤمن فغسل وجهه خرجت من وجهه كل خطيئة نظر إليها مع الماء أو مع آخر قطر الماء ، فإذا غسل يديه خرجت كل خطيئة بطشتها يداه مع الماء أو مع آخر قطر الماء ، فإذا غسل رجليه خرجت كل خطيئة مشتها رجلاه مع الماء أو مع آخر قطر الماء حتى يخرج نقياً من الذنوب »

**"Mja Muislamu au Muumini anapotawadha akaosha uso wake, litatoka - katika uso wake - kila dhambi alilolitazama pamoja na maji au pamoja na tone la mwisho la maji. Atakapoyaosha mikono yake, litatoka kila dhambi alililoliendea kwa miguu yake pamoja na**

**yake litatoka kila dhambi alilolishika kwa mkono wake pamoja na maji au pamoja na tone la mwisho la maji. Atakapoyaosha miguu yake pamoja na maji au pamoja na tone la mwisho la maji, mpaka atoke hali ya kuwa ni safi kutokana na madhambi."** (Muslim).

**FARADHI ZA UDHU:**

1. Ni kutia niya: nayo (hiyo niya) ni moyo kuazimia juu ya kitendo cha udhu, ilihali ya kufwata Amri ya ALLAH aliyetukuka na kutafuta Radhi zake. Kwa dalili ya kauli yake Mtume (S.A.W.): **"Hakika kuswihi kwa amali huzingatiwa niya."** (Muttafaq).

2. Kuosha uso mara moja. Kuanzia juu ya kipaji hadi mwisho wa kidevu, na kutoka kigingi cha sikio hadi kigingi cha sikio lingine. Kwa dalili ya kauli yake ALLAH:

﴿ فَاغْسِلُوا وُجُوهَكُمْ ﴾

**"Osheni nyuso zenu."**

3. Kuosha mikono hadi katika viwi. Kwa dalili ya kauli yake ALLAH.

﴿وَأَيْدِيَكُمْ إِلَى الْمَرَافِقِ﴾

**"........Na mikono yenu hadi katika viwi."**

4. Kupukusa kichwa kuanzia mwisho wa kipaji hadi kishogoni. Kwa dalili ya kauli yake ALLAH:

﴿ وَامْسَحُوا بِرُؤُسِكُمْ ﴾

**"Na mmpanguse vichwa vyenu."**

5. Kuiyosha miguu hadi vifundoni kwa dalili ya kauli yake ALLAH:

﴿ وَأَرْجُلَكُمْ إِلَى الْكَعْبَيْنِ ﴾

**"Na (muiyoshe) miguu yenu hadi katika vifundo vya miguu."**

6. Kutungamanisha baina ya viungo vyenye kuoshwa. Nako ni kuosha uso kwanza, kisha mikono, halafu apukuse kichwa na hatimae aoshe miguu. Kwa sababu utaratibu huo ndivyo ulivyokuja katika Aya Tukufu ya Qur'aan.

7. Kufwatanisha. Nako ni kuifanya amali ya udhu katika wakati mmoja bila ya kupambanua katika zama, kwa sababu imekatazwa kukata Ibada baada ya kuingia. ALLAH amesema:

﴿ وَلَا تُبْطِلُوا أَعْمَالَكُمْ ﴾

**"Wala msiviharibu vitendo vyenu."** (47:33). Ispokuwa kipambanuzi kidogo husamehewa.

## SUNNA ZA UDHU:

1. Ni kusema wakati wa kuanza kutawadha:

بسم الله

**"Kwa Jina la ALLAH."** Kwa kuwa imepokewa kutoka kwa Mtume (S.A.W.):

« لا وضوء لمن لم يذكر اسم الله عليه »

**"Hapana udhu kwa asielitaja jina la ALLAH juu ya udhu ule."** (Ahamad na Abu Daud).

2. Kupiga msuwaki: Kwa dalili ya kauli yake Mtume (S.A.W.):

« لولا أن أشق على أمتي لأمرتهم بالسواك مع كل وضوء »

**"Lau nisingaliona uzito juu ya umma wangu, ningaliwaamrisha kupiga mswaki wakati wa kila kutawadha."** (Muttafaq).

3. Kuosha vitengele (viganja) mara tatu mwanzo wa kutawadha. Kama ilivyopokewa kuwa Sayyidna 'Uthman bin 'Affan (R.A.) alitawadha, akimimina maji juu ya vitengele vyake mara tatu, akaviosha na akasema mwisho wa kutawadha: **"Nilimwona Mtume (S.A.W.) akitawadha mfano wa udhu wangu huu."** (Muttafaq).

4. Kusukutuwa: Nako ni kuyataharakisha maji yaliyo ndani ya mdomo kisha kuyatema, kwa dalili ya kauli yake Mtume (S.A.W.):

« إذا توضأت فمضمض »

**"Unapotawadha sukutuwa."** (Abu Daud).

5. Kupandisha maji puwani na kuyatoa, kwa dalili ya kauli

yake Mtume (S.A.W.):

« وبالغ في الاستنشاق إلا أن تكون صائماً »

**"....naupandishe zaidi maji puwani, ila utakapokuwa umefunga."** (Ahmad Abu Daud, Tirmidhy na wengineo).

6. Kuzisugua ndevu zilizoshindamana:

Kwa dalili ya kauli ya 'Ammar bin Yasir - alipostaajabiwa alipoonekana akizisugua ndevu zake -: **"Na ni kipi kitakachonizuwia ilihali nimemwona Mtume (S.A.W.) akizisugua ndevu zake."** (Ahmad na Tirmidhy).

7. Kuvisugua vidole vya mikono na miguu kwa dalili ya kauli ya Mtume (S.A.W.):

« إذا توضأت فخلل أصابع يديك ورجليك »

**"Unapotawadha sugua vidole vya mikono yako na miguu yako."** (Tirmidhi).

8. Kupukusa masikio nje na ndani kama Mtume (S.A.W.) alivyofanya hivyo.

9. Kuosha mara tatu-tatu kwani faradhi ni kuosha mara moja. Kuosha mara tatu ni sunnah.

10. Kuanzia upande wa kulia katika kuosha mikono na miguu. Kwa dalili ya kauli ya Mtume (S.A.W.):

« إذا لبستم وإذا توضأتم فابدءوا بأيامنكم

**"Mnapovaa na mnapotawadha anzeni kwa upande wenu wa kulia."** (Ahmad na Abu Dawud). Na kauli ya Bibi Aisha (R.A.): **"Alikuwa Mtume (S.A.W.) akipenda kuanza upande wa kulia katika kuvaa kwake viatu, kuchana kwake, kujitwahirisha kwake na katika mambo yake yote."** (Mattafaq).

11. Kurefusha sehemu zote za uso na mikono, ama kurefusha uso ni kuosha sehemu kuanzia mwanzo wa kichwa au kupita uso zaidi ya sehemu ambayo ni wajib katika kuosha. Ama kuosha mikono ni kuosha juu ya viwi na vifundo vya miguu. Kwa dalili ya kauli yake Mtume (S.A.W.):

« إن أمتي يأتون يوم القيامة غراً محجلين من آثار الوضوء فمن استطاع منكم أن يطيل غرته فليفعل »

**"Hakika umma wangu watakuja siku ya Qiyama hali ya kuwa ni weupe wa nyuso na mikono kutokana na athari za udhu. Basi anayeweza miongoni mwenu kurefusha uso wake na afanye."** (Muttafaq) (1)

12. Aseme baada ya kutawadha,

أشهد أن لا إله إلا الله وحده لا شريك له وأشهد أن محمداً عبده ورسوله ، اللهم اجعلني من التوابين واجعلني من المتطهرين ،

**"Nashuhudia kwamba hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa ALLAH peke yake hana mshirika na nashuhudia kwamba Muhammad (S.A.W.) ni mja wake na ni Mtume wake. Ewe Mola nijaalie mimi niwe miongoni mwa wenye kutubia na unijaalie miongoni mwa wenye kujitwahirisha."** Kwa dalili ya kauli yake Mtume S.A.W.:

« ما منكم من أحد يتوضأ فيسبغ الوضوء ثم يقول : أشهد أن لا إله إلا الله وحده لا شريك له ، وأشهد أن محمداً عبده ورسوله إلا فتحت له أبواب الجنة الثمانية يدخل من أيها شاء »

**"Hakuna yeyote miongoni mwenu atakayetawadha, akaueneza udhu wake sawa sawa kisha akasema. "Nashuhudia kuwa hakuna Mola anayestahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa ALLAH peke yake hana mshirika na nashuhudia kuwa Muhammad ni mja wake na ni Mtume wake, isipokuwa atafunguliwa milango minane ya peponi aingie katika mlango wowote anaotaka".** (Muslim na Tirmidhi).

---

1. Yaani nuru itawaenea nyusoni, mikononi na miguuni mwao siku ya Qiyama. Mambo hayo ni makhsus katika umma huu.

## MAKRUHU YA UDHU:

1. Kuacha sunna moja au zaidi miongoni mwa sunna za udhu. Kwa sababu jambo hilo hupelekea kupunguza amali na kukosa ujira.

2. Kutawadha pahali penye najisi kwa sababu huogopewa zile najisi zisije zikamrukia.

3. Kufanya Israfu katika maji. Kwani Mtume (S.A.W.): "**Alitawadha kwa kibaba.**" (Muslim). Na israfu imekatazwa katika kila jambo.

4. Kuzidisha zaidi ya mara tatu. Kwa dalili ya Hadithi kuwa Mtume (S.A.W.): "**Alitawadha mara tatu-tatu na akasema: "Huu ndio udhu atakayezidisha zaidi ya hivi, hakika atakuwa amefanya vibaya, ameruka mpaka na amedhulumu.**" (Ahmad, Nasai, Ibnu Majah na wengineo).

5. Kupigapiga makofi uso wake kwa maji ya kuosha, kwani jambo hilo lapingana na adabu ya kutawadha na pia huwa ni kujishabihisha kwa anayejipiga makofi matavuni mwake kwa sababu ya kujutia juu ya kukosa kitu chenye thamani.

### NAMNA YA KUTAWADHA:

Anayetaka kutawadha atafanya yanayofuata:
Atataja Jina la ALLAH (kusema:

بسم الله

Atamimina maji juu ya vitengele vyake hali ya kunuwia udhu, ataviosha mara tatu kisha atasukutua na kupandisha maji puwani kwa teko moja, atafanya hivyo mara tatu ikiwa ni Sahali, na ndio bora zaidi. Ikiwa hawezi atapambanuwa baina ya kusukutuwa na kupandisha maji puwani - mara tatu - kwa kila moja wapo. Kisha ataosha uso wake mameleo ya nywele za kichwa chake hadi mwisho wa ndevu zake, huo ndio urefu. Na kutoka kigingi cha sikio hadi kigingi cha sikio lingine, atafanya hivyo mara tatu. Halafu ataosha mkono wake wa kulia hadi kwenye kisukusuku, mara tatu, hali ya kuvisugua vidole vyake, na visukusuku pia vinaingia katika kupasa kuoshwa. Kisha atauwosha mkono wake

wa kushoto vivyo hivyo. Kisha atakipukusa kichwa chake mara moja, ataanzia mwanzo wa kichwa chake, aipitishe mikono yake hali ya kupukusa hadi kishogoni, halafu airudishe pale alipoanzia. Halafu atayapukusa masikio yake nje na ndani kwa maji yaliyobakia mikononi mwake, au ikiwa maji hayakubakia atapukusa kwa maji mingine. Kisha ataosha mguu wake wa kulia pamoja na kifundo (cha mguu), mara tatu. Halafu ataosha mguu wake wa kushoto vivyo hivyo. Hatimaye atasema:

أشهد أن لا إله إلا الله وحده لا شريك له ، وأشهد أن محمداً

عبده ورسوله ، اللهم اجعلني من التوابين واجعلني من المتطهرين .

Nashuhudia kuwa hakuna Mola anaestahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa ALLAH peke yake hana mshirika. Na nashuhudia kuwa Muhammad ni mja wake na ni Mtume wake. Ewe Mola, nijaalie niwe miongoni mwa wenye kutubia na unijaalie miongoni mwa wenye kujitwahirisha.

## YENYE KUTANGUA UDHU:

1. Chenye kutoka kwa njia mbili, uchi wa mbele na wa nyuma, kiwe ni kidogo au kingi, na ni sawa tu uwe ni mkojo au choo au madhii au wadii (1) au kushuta au kutokwa upepo na vitu hivi viwili vya mwisho huitwa hadathi na ndio makusudio katika kauli yake Mtume (S.A.W.): « لا يقبل الله صلاة أحدكم إذا أحدث حتى يتوضأ »

**"ALLAH haikubali swala ya mmoja wenu anapotokwa na hadathi mpaka atawadhe."** (Bukhari).

2. Usingizi mzito ambao aliyelala hahisi chochote, pamoja na kutomakinika makalio juu ya ardhi kwa dalili ya kauli yake Mtume (S.A.W):

« العين وكاء السه فمن نام فليتوضأ »

**"Jicho ni hifadhi ya tupu atakayelala atawadhe."** (Abu Dawud na

---

1. Wadii: Ni maji meupe mazito yanayotoka mwisho wa kukojoa au mwisho wa kazi ngumu. Lakini ujuwe manii yakitoka hupasisha kuoga).

Ibnu Majah).

3. Kugusa Dhakari kwa matumbo ya kitengele cha mkono na vidole pasi na kizuizi, kwa kauli yake Mtume (S.A.W):

« من مس ذكره فليتوضأ »

**"Atakayegusa dhakari yake atawadhe."** (Abu Dawud , Tirmidhi na wengineo).

4. Kuondokewa na akili na kupotewa na hisia, iwe ni kwa sababu ya wazimu au kulewa au kupewa dawa au kutumia chenye kulevya. Na ni sawa tu iwe ni kidogo au kingi na pia ni sawa tu iwe makalio yamejimakini juu ya ardhi au la. Kwa sababu kuondokewa na akili katika sababu hizi ni kuzito zaidi kuliko kulala kwenyewe, na Mwislamu hajui linalompata katika hali kama hizo kutokana na kutanguka na udhu mfano wa kushuta na mengineo. Maulamaa wameafikiana juu ya kupasa kutawadha kwa mtu aliyeondokewa na akili.

5. Kumgusa mwanamke kwa matamanio, kwani kuyakusudia matamanio ni kama kuwepo kwa hivyo hutangua udhu. Kwa dalili ya mtu anayeishika dhakari huamriwa atawadhe, kwa sababu kuishika dhakari huharakisha shahwa (matamanio). Na linalotilia nguvu madhehebu haya ni ile kauli ya 'Abdullah bin'Umar (R.A.):
**"Mtu kumbusu mkewe na kumgusa kwa mkono wake ni katika "kugusana".** (1) (Imam Malik katika Muwatta).

6. Kuritadi (kutoka katika Uislamu) - ALLAH atulinde nako. Nako ni kufanya jambo linalomtoa mtu katika Uislamu, kwa kutamka au itikadi au kutia shaka. Basi anayefanya mojawapo ya mambo hayo udhu wake utabatilika na amali zake zote za ibada zitabatilika. Basi

---

1. Anashiria katika Aya isemayo: **"Na kama mkiwa wagonjwa (mumekatazwa kutumia maji) au mumo safarini au mmoja wenu ametoka msalani (chooni) au mnapogusana na wanawake - na msipate maji - basi ukusudieni (tayamamuni) udongo safi."** (4:43). Pia tazama Suratul-Maidah Aya 6. **"Anakusudia kuwa, huko ni katika kugusana kunakopasisha kutawadha."**

atakapourudia Uislamu hatoswali mpaka atawadhe. Kwa dalili ya kauli yake ALLAH:

﴿ وَمَنْ يَكْفُرْ بِالإِيمَانِ فَقَدْ حَبِطَ عَمَلُهُ ﴾

**"Na anayekataa kuamini bila shaka amali zake zimepotea."** (5:5). Na kauli yake ALLAH:

﴿ لَئِنْ أَشْرَكْتَ لَيَحْبَطَنَّ عَمَلُكَ ﴾

**"Kama ukimshirikisha (ALLAH) bila shaka amali zako zitaruka patupu."** (39:65).

7. Kula nyama ya ngamia. Kwa dalili ya lile Swala la swahabakumwuliza Mtume (S.A.W.): **"Je, tutawadhe tunapokula nyama ya mbuzi?"** Mtume (S.A.W.) akajibu: **"ukitaka utatawadha na ukitaka usitawadhe."** Yule mtu akauliza: **"Je, tutawadhe tunapokula nyama ya ngamia?"** Mtume (S.A.W.) akajibu: **"Ndio, tawadha kwa kula nyama ya ngamia."** (Muslim).

Imam Nawawy amesema: **"Madhehebu haya ndio yenye dalili yenye nguvu zaidi, japokua Wanavyuoni wengi wamo kinyume chake."**

Lakini ujue kuwa Wanavyuoni wote wa ki-swahaba Waki-Taabiina na waliokuja baada yao - wakiongozwa na Makhalifa wanne (R.A) - hawaoni kupasa kutawadha kwa kula nyama ya ngamia. Hoja yao ni kuwa Hadithi hii - iliotajwa mbeleni - ni **'Mansukh'** (imefutwa).

## YANAYOPASISHA KUTAWADHA:

Yapasa kutawadha kwa sababu ya mambo matatu:

KWANZA: Kuswali Swala yoyote, ya faradhi au sunna japo ni swala ya jeneza, kwa dalili ya kauli ya ALLAH:

﴿ يَاأَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا إِذَا قُمْتُمْ إِلَى الصَّلَاةِ فَاغْسِلُوا وُجُوهَكُمْ وَأَيْدِيَكُمْ إِلَى الْمَرَافِقِ وَامْسَحُوا بِرُءُوسِكُمْ وَأَرْجُلَكُمْ إِلَى الْكَعْبَيْنِ ﴾

**"Enyi mlioamini! Mnaposimama ili mkaswali, basi osheni nyuso zenu na mikono yenu mpaka vifundoni, na mpaka vichwa vyenu,**

**na (osheni) miguu yenu mpaka vifundoni."** (5:6). Yaani mnapotaka kusimama kuenda kuswali nanyi muna hadathi, basi osheni nyuso zenu............................mpaka mwisho.

Mtume (S.A.W.) amesema:

«لا يقبل الله صلاة بغير طهور ولا صدقة من غلول»(٢)

**"ALLAH haikubali Swala bila ya udhu, wala haikubali sadaka inayotokana na kuiba."** (Muslim).

PILI: Kutufu Alkaaba. Kwa dalili ya kauli yake Mtume (S.A.W.):

« الطواف بالبيت صلاة إلا أن الله تعالى أباح فيه الكلام »

**"Kuitufu Al-kaaba ni kuswali, isipokuwa ALLAH aliyetukuka amehalalisha ndani yake kuzungumza."** (Tirmidhy, Haakim na wengineo).

TATU: Kuugusa Msahafu. Kwa dalili ya kauli yake Mtume (S.A.W.):

«لا يمس القرآن إلا طاهر»

**"Asiiguse Qur'aan ila mwenye udhu."** (Daaraqutany, Haakim na wengineo). Na hii ndio ijimai (maafikiano) ya Maimamu wanne walio Ma-Faqihi (wajuzi wa ilimu ya Sharia), (R.A.) na wengineo. Haijuzu kwa mwenye hadathi kuugusa msahafu, yapasa atawadhe anaopotaka kuugusa. Ama kusoma Qur'aan kwa mwenye hadathi asiye na udhu pasina kuugusa msahafu inafaa kwa itifaki ya Wanavyuoni wote. Vile vile inafaa kwa mwenye hadathi kubeba msahafu kwa kuishika kamba iliyofungwa katika msahafu huo na kuugusa juu ya kizuizi.

## UDHU WA MWENYE UDHURU:

Mwenye udhuru ni anayetokwa na hadathi yenye kutangua udhu, katika nyakati zake nyingi, kama anayeghilibiwa kutokwa na mkojo au kuponyokwa na upepo, au kama vile mwanamke anayetokwa na damu siku ambazo si za hedhi wala nifaas. Basi watu hawa na walio katika hukumu yao yapendekeza kwao wao - pamoja na kufanya dawa kiasi wanavyoweza - kutawadha katika kila swala, na Swala yao

ni swahihi pamoja na kuwa wana udhuru kama huo. Dalili yake ni kauli yake Mtume (S.A.W.) kumwambia Fatma binti Abi Hubeish aliyekuwa akitokwa na damu nyingi (ya ugonjwa). "..........**kisha utatawadha katika kila Swala.**" (Abu Dawud, Tirmidhi, Nasai na wengineo), Na wengineo wenye nyudhuru kama hizo watakisiwa juu yake.

## NAMNA YA UTWAHARA WA MGONJWA.

1. Yapasa juu ya mgonjwa kujitwahirisha na maji atatawadha kutokana na hadathi ndogo na ataoga kutokana na hadathi kubwa.

2. Atakapokuwa hawezi kujitwahirisha na maji kwa sababu ya kushindwa kwake au kuhofia ugonjwa usije ukazidi au kuwa atachelewa kupoa basi atatayamamu.

3. Namna ya kutayamamu: Ataipiga mikono yake juu ya ardhi iliyo twahara pigo moja, ataupukusa uso wake kwa mikono hiyo kisha atavipukusa vitengele vyake baadhi yake kwa baadhi nyingine. Atakapokuwa hawezi kutayammam yeye mwenyewe, atatayamumishwana mtu mwingine, mtu huyo ataipiga ardhi iliyo twahara kwa mikono yake hiyo na vitengele vyake, kama ambavyo asipoweza kutawadha yeye mwenyewe atatawadhishwa na mtu mwingine.

4. Yafaa kutayamamu katika ukuta au katika kitu kingine ambacho ni twahara na chenye vumbi. Utakapokuwa ukuta umepakwa kitu kisichotokana na jinsi ya ardhi kama kupakwa rangi basi hatotayamamu kwa kitu hicho ila kiwe na vumbi.

5. Utakapokuwa ukuta au kitu kingine hakina vumbi basi hapana ubaya kuweka mchanga juu ya kitambara au chombo na atayamam kutokana na kitambara hicho au chombo hicho.

6. Atakapotayamam kwa ajili ya Swala na akabaki juu ya utwahara wake mpaka wakati wa swala nyingine basi ataiswali swala hiyo kwa tayamam ile ile ya kwanza wala hatatayamam tena mara nyingine kwa sababu yeye yu katika utwahara wake wala hakikupatikaniwa chenye kubatilisha utwahara huo. Na ni mustahabu (imependekezwa) kutayamam katika kila Swala.

7. Yapasa kwa kila mgonjwa kuutwahirisha mwili wake kutokana na najisi. Atakapokuwa hawezi ataswali juu ya hali yake ile ile na swala yake ni swahihi wala hatoirudisha.

8. Yapasa juu ya mgonjwa kuzitwahirisha nguo zake kutokana na najisi au azivue na avae nguo zilizotwahara. Atakapokuwa hawezi ataswali katika hali yake ile ile na swala yake ni swahihi wala hatairudisha.

9. Yapasa juu ya mgonjwa aswali juu ya kitu kilicho twahara itakapokuwa juu ya kitanda kuna najisi ataiosha au atakibadilisha kitanda hicho kwa kitanda kingine kilichotwahara au atatandika juu yake kitu kilichotwahara. Atakapokuwa hawezi ataswali katika hali aliyo na swala yake ni swahihi wala hatairudisha.

# KUOGA

Kuoga maana yake ni: Kuyaeneza maji katika mwili mzima kwa niya ya kuondosha hadathi kubwa ili kuhalalisha - kilichozuiwa na hadathi hiyo - kutokana na ibada.

## KUEKWA SHARIA YA KUOGA:

Ni sharia kuoga kwa mujibu wa Qur'aan. Tukufu na Sunna Takatifu. ALLAH amesema:

﴿ وَإِنْ كُنْتُمْ جُنُبًا فَاطَّهَّرُوا ﴾

**"Na mkiwa na janaba basi ogeni."** (5:6). Na ALLAH amesema:

﴿ وَلَا جُنُبًا إِلَّا عَابِرِي سَبِيلٍ حَتَّىٰ تَغْتَسِلُوا ﴾

**"Wala mwenye janaba (hafai kukaribia Swala) - Isipokuwa mmo safarini - mpaka mkoge."** (4:43). Mtume (S.A.W.) amesema:

« إذا تجاوز الختان الختان وجب الغسل »

**"Tupu itakapopita katika tupu nyingine yapasa kuoga."** (Muslim).

## YENYE KUPASISHA KUOGA:

Yapasa kuoga kwa sababu zinazofwata:

1. Janaba, vile vile kushusha, nako ni kutokwa na manii kwamatamanio katika usingizi au macho, mwanamke au mwanamume. Vile vile kujimai, nako ni kukutana tupu mbili japo bila ya kuteremsha (manii). ALLAH amesema:

﴿ وَإِنْ كُنْتُمْ جُنُبًا فَاطَّهَّرُوا ﴾

**"Na mkiwa na janaba basi ogeni."** Mtume (S.A.W.) amesema:

« إذا التقى الختانان فقد وجب الغسل »

**"Zinapokutana tupu mbili imeshapasa kuoga."**

2. Kukatika damu ya hedhi na nifasi. Kwa dalili ya kauli yake ALLAH:

﴿ فَاعْتَزِلُوا النِّسَاءَ فِي الْمَحِيضِ وَلَا تَقْرَبُوهُنَّ حَتَّى يَطْهُرْنَ فَإِذَا تَطَهَّرْنَ فَأْتُوهُنَّ مِنْ حَيْثُ أَمَرَكُمُ اللَّهُ ﴾

**".........Basi jitengeni na wanawake wakati wa hedhi (zao). Wala msiwakaribie mpaka watwahirike". Wakishatwahirika basi waendeeni katika pale alipowaamrisha ALLAH."** (2:222). Na kwa dalili ya kauli yake Mtume (S.A.W.) kumwambia Fatima binti Abi Hubaish (R.A): **"Itakapokuja hedhi acha kuswali, na itakapoondoka oga na uswali."** (Bukhari). Na damu ya nifasi ni kama ya hedhi kwa ijimai ya Ma-Swahaba (R.A.).

3. Kufa. Muislamu anapokufa yapasa kumwosha, kwa amri ya Mtume (S.A.W.) katika jambo hilo. Aliamrisha binti yake Zainab (R.A.) aoshwe wakati alipokufa, kama ilivyopokewa katika Swahihi Bukhari na Swahihi Muslim.

4. Kafiri aliyesilimu. Yeyote katika makafiri akiingia katika Uislamu yapasa aoge, kwa sababu Mtume (S.A.W.) alimwamrisha Qays bin 'Aaswim aoge aliposlimu. (Abu Daud, Nasai na wengineo). Kadhalika Thumamah Al-hanafy. (Ahmad, Buyhaqy na Abdurrazzaq). Asli yake i katika Swahihi mbili).

## MAMBO AMBAYO NI MUSTAHABU KUOGA KWA AJILI YAKE:

Ni mustahabu kuoga kwa sababu ya mambo yanayofwatia:

1. Ijumaa: Kwa dalili ya kauli ya Mtume (S.A.W.):

« غسل الجمعة واجب على كل محتلم »

**"Kuoga Ijumaa ni wajibu kwa kila aliyebaleghe."** (Muttafaq).

2. Kwa aliyemwosha maiti: Kwa dalili ya kauli yake Mtume (S.A.W.):

« من غسل ميتاً فليغتسل ومن حمله فليتوضأ »

**"Anayemwosha maiti aoge na anayembeba atawadhe."** (Abu Daud, Tirmidhy, Ibnu Maajah na wengine).

3. Kuhirimia: Ni sunna kuoga kwa anaetaka kuhirimia 'Umra au Hijja, kwa kuwa Mtume (S.A.W.) alifanya hivyo. Zaid bin Thabit amesema kuwa yeye **"Alimwona Mtume (S.A.W.) alipohirimia na akaoga."** (Tirmidhy, Darimy na Daraqutany).

4. Kuingia Makkah na kusimama Arafat kwa kuwa Mtume (S.A.W.) alifanya hivyo. Ama kuingia Makkah ni kwa athari ya Ibnu Umar: **"Alikuwa haingii Makkah ila hulala hapo Dhi-Tuwa mpaka kupambazuke akioga na kiingia mchana."** Na yasemekana kuwa Mtume (S.A.W.) alifanya hivyo. (Muslim). Ama kusimamaArafat ni kwa athari ya Ibnu Umar (R.A): **"Alikuwa akioga kwa ajili ya Ihram yake kabla ya kuhirimia, na kwa ajili ya kuingia makkah na kusimama kwake jioni ya Arafat."** (Malik katika Muwatta. Na asili yake iko katika Bukhari na Muslim).

5. Kuoga Idi Mbili. Wanavyuoni wamependekezesha kuoga siku za Idi mbili, wala haikuja hadithi sahihi katika jambo hilo. Katika

kitabu Al-Badrul Muniir imeelezwa kuwa: **"Hadithi za kuoga siku za Idi mbili ni dhaifu." Na muna athari nzuri kutoka kwa maswahaba."**

## FARADHI ZA KUOGA

1. Kutia nia: Nayo hiyo nia ni moyo kuazimia juu ya kuondosha hadathi kubwa kwa kuoga kwa dalili ya kauli yake Mtume S.A.W.:

« إنما الأعمال بالنيات وإنما لكل امرىء ما نوى »

**"Hakika kuswihi kwa amali yazingatiwa nia, na kila mtu atapata malipo ya alilolinuiliya."** (Bukhari na Muslim).

2. Kueneza maji katika mwili wote kwa kusugua sehemu zinazomkinika kuzisugua na kumimina maji juu ya sehemu ambazo ni vigumu kuzisugua, mpaka ighilibu juu ya dhana kuwa maji yameenea mwili mzima.

3. Kuzisugua nywele: Nywele za kichwa na sehemu nyingine.

## SUNNA ZA KUOGA

1. Kupiga Bismillah, kwani ni sheria katika kila jambo muhimu.
2. Kuviosha vitengele hali ya kuanza, mara tatu.
3. Kuanza kuosha uchi na kuondoa uchafu.
4. Kutawadha - kabla ya kuoga - udhu ulio kamili kama udhu wa Swala. Na mwenye kuoga anaweza kucheleweshа kuiosha miguu yake mpaka atakapomaliza kuoga. Na asili ya yote hayo imepokewa kutoka kwa Bibi Aisha (R.A.) kuwa: **"Mtume S.A.W. alikuwa anapooga kutokana na janaba akianza kwa kuosha mikono yake kisha akiyamimina maji kwa mkono wake wa kulia juu ya mkono wake wa kushoto, akiuosha uchi wake kisha akitawadha udhu wake wa swala"**. (Bukhari na Muslim).

## MAKRUHU KATIKA KUOGA

1. Kufanya Israfu katika maji. Kwani Mtume (S.A.W.) alioga kwa pishi, nayo ni vibaba vinne.

2. Kuoga katika sehemu zilizo najisi kwa kuchelea kujipaka najisi.

3. Kuoga bila ya sitara ya ukuta au mfano wake. Kwa dalili ya kauli yake Mtume (S.A.W.):

« إن الله عز وجل حيي ستير يحب الحياء والستر، فإذا اغتسل أحدكم فليستتر »

**"Hakika ALLAH aliyeshinda na kutukuka ni mwenye haya, mwenye kusitiri yuwapenda haya na sitara. Basi atakapooga mmoja wenu na ajistiri."** (Abu Dawud na Nasai. Hadithi hii ni Swahih).

4. Kuoga katika maji yaliyotowama ambayo hayaendi. Kwa dalili ya kauli yake Mtume (S.A.W.):

« لا يغتسل أحدكم في الماء الدائم وهو جنب »

**"Asioge mmoja wenu katika maji yaliyotowama na ilhali ana janaba."** (Muslim).

## NAMNA YA KUOGA

Kwanza aseme

بسم الله

**"Bismillahi"** (kwa Jina la ALLAH) ilhali ya kunuwiya kuondosha hadathi kubwa kwakuoga kwake huko. Kisha ataviosha vitengele vyake mara tatu, halafu atatamba, atauwosha uchafu ulio katika tupu yake nana pambizoni mwake. Kisha atatawadha udhu kamili, na anaweza kuakhirisha miguu yake hadi atakapomaliza kuoga. Kisha atamimina maji kichwani mwake na a zisugue nywele zake.(1) Kisha ataosha

---

1. Mwanamume ndiye atakaefanya hivyo. Ama mwanamke, inamtosha kuteka mateko (makonde) matatu ayamimine kichwani mwake na asugue, wala hazifungui nywele zake. Kwa dalili ya Hadithi ya Ummu Salamah (R.A.) aliposema: **"Ewe Mtume wa ALLAH, mimi ni mwanamke ninaeifunga mikili ya nywele za kichwani mwangu. Je niifungue wakati wa kuoga janaba?"** Mtume (S.A.W.) akamwambia: **"Laa, inakutosha kuteka mateko matatu ya maji na umimine juu ya kichwa chako."** (Muslim).

kichwa chake pamoja na masikio mara tatu. Halafu atajimiminia maji upande wake wa kulia kuanzia juu mpaka chini, kisha upande wa kushoto vivyo hivyo, ilhali ya kufuatilia - wakati wa kuoga kwake - zile sehemu zilizojificha na kuingia ndani kama kitovuni, chini ya makapwa na mfano wake. Kwa dalili ya Hadithi ya Bibi 'Aisha (R.A.) aliponena: **"Mtume (S.A.W.) alikua anapotaka kuoga janaba akianza kuiosha mikono yake. Kisha akimimina maji kwa mkono wake wa kulia juu ya mkono wake wa kushoto akiuwosha uchi wake. Kisha akitawadha udhu wake wa kuswalia. Halafu akizilowesha maji nywele zake. Kisha akiteka mateko matatu, akimimina juu yake. Halafu akimimina maji juu ya mwili wake wote. Hatimaye akiiosha miguu yake."** (Bukhari na Muslim).

## AMBAYO NI HARAMU KWA MWENYE JANABA:

1. Kuswali Swala yoyote ya Faradhi au ya Sunnah. Kwa dalili ya kauli yake ALLAH aliyetukuka:

﴿ يَاأَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تَقْرَبُوا الصَّلَاةَ وَأَنْتُمْ سُكَارَىٰ حَتَّىٰ تَعْلَمُوا مَا تَقُولُونَ وَلَا جُنُبًا إِلَّا عَابِرِي سَبِيلٍ حَتَّىٰ تَغْتَسِلُوا ﴾

**"Enyi mlioamini! Msikaribie Swala hali mumelewa, mpaka muyajue mnayosema, wala hali mna janaba - isipokuwa mnin safarini mpaka mkoge."** (4:43).

2. Kuushika msahafu. Kwa dalili ya kauli yake Mtum (S.A.W.):

« لا يمس القرآن إلا طاهر »

**"Asiiguse Qur'aan ila aliye twahara."** (Dara Qutany, Haakim wengineo).

3. Kutufu katika Al-kaaba tukufu. Dalili yake imeshatang tazama katika **"Yanayopasisha mtu kutawadha."**

4. Kusoma Qur'aan. Kwa dalili ya kauli ya Imam Ali (R)

**"Alikuwa Mtume (S.A.W.) akitusomea Qur'aan katika hali zote maadam hana janaba."** (Imam Ahmad, Abu Daud na wengineo).

5. Kuketi Msikitini - isipokua kupita kwa aliyepatwa na dharura ya kufanya hivyo - kwa dalili ya kauli yake ALLAH aliyetukuka:

﴿ وَلاَ جُنُباً إِلاَّ عَابِرِي سَبِيلٍ حَتَّىٰ تَغْتَسِلُوا ﴾

**"........Wala hali mna janaba - isipokuwa mmo safarini - mpaka mkoge."** (4:43).

# SWALA

## HUKUMU YA SWALA:

Swala ni faradhi iliyo waajib juu ya kila muumini mwanamume na mwanamke. ALLAH (S.A.W.) ametuamuru kuisimamisha katika Aya nyingi za Qur'aan Tukufu, akasema:

﴿ فَأَقِيمُوا الصَّلَاةَ إِنَّ الصَّلَاةَ كَانَتْ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ كِتَابًا مَوْقُوتًا ﴾

**"Basi simamisheni Swala. Kwa hakika Swala kwa Waislamu ni faradhi iliyowekewa nyakati makhsusi."** (4:103). Akasema tena:

﴿ حَافِظُوا عَلَى الصَّلَوَاتِ وَالصَّلَاةِ الْوُسْطَى ﴾

**"Angalieni sana swala (zote kuziswali, khasa jamaa) na (khasa) ile Swala ya kati na kati."** (2:238).

Mtume (S.A.W.) amefanya Swala kuwa ni nguzo ya pili miongoni mwa nguzo tano za Uislamu, akasema:

« بني الإسلام على

خمس شهادة أن لا إله إلا الله وأن محمداً رسول الله وإقام الصلاة وإيتاء

الزكاة وحج البيت وصوم رمضان »

**"Uislamu umejengwa juu ya nguzo tano, kushuhudia kuwa hakuna Mola anayestahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa ALLAH, na kuwa Muhammad ni Mtume wake, kusimamisha Swala, kutoa Zaka, kuhiji Al-kaaba na kufunga mwezi wa Ramadhani."** (Muttafaq). Basi mwenye kuacha kuswali ni kafiri, anastahiki kuuwawa ki-sharia. Na mwenye kuidharau (Swala) ni fasiki moja kwa moja.

## FADHILA YA SWALA:

Fadhila za swala ni kubwa na ujira wake ni mkubwa. Hadithi zilizopokewa kuhusu jambo hilo, ni nyingi mno. Tutazitaja baadhi yake tu:

1. Mtume (S.A.W.) alipoulizwa: **"Amali gani ni bora?"** Alijibu: **"Kuswali kwa wakati wake".** (Muttafaq).

2. Kauli yake Mtume (S.A.W.):

« أرأيتم لو أن نهراً بباب أحدكم يغتسل منه كل يوم خمس مرات ، هل يبقى من درنه(٢) شيء ؟ » قالوا لا يبقى من درنه شيء ، قال : « فذلك مثل الصلوات الخمس يمحو الله بهن الخطايا »

**"Je, mwaonaje lau mto ukawa unapita mbele ya mlango wa mmoja wenu akawa yuwaoga katika mto huo mara tano kila siku, je, kitabakia kitu katika uchafu wake?"** Maswahaba wakasema: **"Hakibakii chochote katika uchafu wake."** (Mtume S.A.W.) akasema: **"Basi huo ni mfano wa Swala tano. ALLAH anayafuta madhambi kwa Swala hizo".** (Muttafaq).

3. Kauli yake Mtume (S.A.W.):

« ما من امرىء مسلم تحضره صلاة مكتوبة فيحسن وضوءها وخشوعها وركوعها إلا كانت كفارة لما قبلها من الذنوب ما لم تؤت كبيرة وذلك الدهر كله »

**"Hakuna mtu yeyote Muislamu atakayefikiwa na swala ya faradhi akatawadha vizuri, akatimiza khushui (kunyenyekea) yake na rukuu zake ila - Swala hiyo - itakuwa ni kafara ya madhambi aliyoyafanya kabla ya Swala hiyo, maadamu halijafanywa dhambi kubwa. Hali hiyo ni mwaka mzima (kila siku)".** (Muslim).

4. Kauli yake Mtume (S.A.W.):

« رأس الأمر الإسلام وعموده الصلاة وذروة سنامه الجهاد في سبيل الله »

**"Msingi wa jambo (ibada) ni Uislamu na nguzo yake ni swala na upeo wa utukufu wake ni Jihadi katika njia ya ALLAH."** (Ahmad, Tirmidhy na wengineo).

## KUTAHADHARI KUACHA SWALA:

Zimekuja Aya katika Qur'aan na Hadithi za Mtume (S.A.W.) zinazotahadharisha kuacha Swala na kuichelewesha katika wakati wake. Nazo ni kama kauli yake ALLAH (S.A.W.):

﴿ فَخَلَفَ مِنْ بَعْدِهِمْ خَلْفٌ أَضَاعُوا الصَّلَاةَ وَاتَّبَعُوا الشَّهَوَاتِ فَسَوْفَ يَلْقَوْنَ غَيًّا (٦) ﴾

**"Lakini wakaandama baada yao chipukizi mbaya (watoto wabaya). Wakapuuza Swala na wakafuata matamanio mabaya, kwa hivyo watakutana na adhabu kali."** (19:59).

- ALLAH amesema:

﴿ فَوَيْلٌ لِلْمُصَلِّينَ الَّذِينَ هُمْ عَنْ صَلَاتِهِمْ سَاهُونَ ﴾

**"Basi adhabu itawathubutukia wanaoswali. Ambao wanapuuza (maamrisho ya) Swala zao."** (107: 4-5)

- Mtume (S.A.W.) amesema:

« بين الرجل وبين الشرك والكفر ترك الصلاة »

**"Baina ya mtu na baina ya shirki na ukafiri ni: kuacha Swala."** (Muslim).

- Mtume (S.A.W.) amesema:

« العهد الذي بيننا وبينهم الصلاة فمن تركها فقد كفر »

**"Ahadi (mkataba) ulio baina yetu na wao (wanafiki) ni Swala.**

**Atakayeiwacha ameshakufuru."** (Ahmad, Tirmidhy na Nasai).

- Siku moja Mtume (S.A.W.) aliitaja swala, akasema:

« من حافظ عليها كانت
له نوراً وبرهاناً ونجاة يوم القيامة ، ومن لم يحافظ عليها لم يكن له
نور ولا برهان ولا نجاة وكان يوم القيامة مع قارون وفرعون وهامان
وأبي بن خلف »

**"Atakayeihifadhi (kwa kudumu nayo) itakuwa kwake yeye ni nuru, dalili na ni uokofu siku ya Qiyama. Na asiyeihifadhi hatokuwa na nuru, dalili wala uokofu, atakuwa siku ya Qiyama yu pamoja na Karuni, Firauni, Hamana na Ubayi bin Khalaf."** (Ahmad, Tabrany na Ibnu Hibban).

## SHARUTI ZA SWALA:

Nazo ni ambazo huwepo kabla ya swala, isipokuwa niya - sharuti ya nane - bora zaidi ni kuikutanisha na Takbira, yapasa kwa mwenye kuswali kuzileta sharuti hizo. Atakapoiacha sharuti (moja) miongoni mwa sharuti hizo swala itakua baatil. Sharuti zenyewe ni kama zinavyofwatia:

**SHARUTI YA KWANZA:** Uislamu,

Haikubaliwi swala ya kafiri wala haiswihi, vile vile matendo yake yote. ALLAH amesema:

﴿ مَا كَانَ لِلْمُشْرِكِينَ أَنْ يَعْمُرُوا
مَسَاجِدَ اللَّهِ شَاهِدِينَ عَلَىٰ أَنْفُسِهِمْ بِالْكُفْرِ أُولَٰئِكَ حَبِطَتْ أَعْمَالُهُمْ وَفِي
النَّارِ هُمْ خَالِدُونَ ﴾

**"Haiwi kwa makafiri (kuhisabika) wanaamirisha Misikiti ya ALLAH, hali wanajishuhudia kwa ukafiri. Hao (ndio ambao) vitendo vyao vyema vimeruka patupu, na katika moto watakaa daima".** (9:17).

**SHARUTI YA PILI:** Akili;

Haipasi swala kwa mwendawazimu, kwa dalili ya kauli yake Mtume (S.A.W.):

« رفع القلم عن ثلاثة عن النائم حتى يستيقظ ، وعن الصبي حتى يحتلم ، وعن المجنون حتى يعقل »

**"Kalamu imeinuliwa kwa watu watatu, kwa aliyelala mpaka atakapoamka, na kwa mtoto mpaka atakapobaleghe na kwa mwendawazimu mpaka awe na akili."** (Abu Daud na wengineo).

**SHARUTI YA TATU:** Kubalighi;

Swala haipasi kwa mtoto mdogo mpaka atakapobalighi kwa dalili ya Hadithi iliotangulia, isipokuwa tu, huamriwa kuswali tangu anapokua ana umri wa miaka saba, ataswàli kwa kupendekezwa. Kwa dalili ya kauli yake Mtume (S.A.W.):

« مروا الصبي بالصلاة إذا بلغ سبع سنين وإذا بلغ عشر سنين فاضربوه عليها »

**"Mwamrisheni mtoto kuswali afikiliapo umri wa miaka saba. Na atakapofikilia umri wa miaka kumi, mpigeni kwa kuiacha Swala hiyo."** (Abu Daud na wengineo).

**SHARUTI YA NNE:** Kutwahirika kutokana na Hadathi ndogo na kubwa, Hadathi ndogo ni kutokua na udhu. Hadathi kubwa ni kutooga janaba kwa dalili ya kauli yake ALLAH:

﴿ يَاأَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا إِذَا قُمْتُمْ إِلَى الصَّلَاةِ فَاغْسِلُوا وُجُوهَكُمْ وَأَيْدِيَكُمْ إِلَى الْمَرَافِقِ وَامْسَحُوا بِرُؤُسِكُمْ وَأَرْجُلَكُمْ إِلَى الْكَعْبَيْنِ وَإِنْ كُنْتُمْ جُنُباً فَاطَّهَّرُوا ﴾

**"Enyi mlioamini! Mnaposimama ili mkaswali, basi osheni nyuso zenu na mikono yenu mpaka vifundoni, na mpake vichwa vyenu, na (osheni) miguu yenu mpaka vifundoni. Na mkiwa na janaba basi ogeni."** (5:6).

Na kauli yake Mtume (S.A.W.):

« لا يقبل الله صلاة بغير طهور »

**"ALLAH haikubali swala yoyote bila ya udhu."** (Muslim).

**SHARUTI YA TANO:** Kutwahirika mwili, nguo na mahala,

Ama kutwahirika mwili ni kwa dalili ya kauli yake Mtume (S.A.W.) kumwambia yule aliekua akitokwa na damu ya ugonjwa: **"Iyoshe damu yako kisha uswali."** (Bukhari na Muslim).

Ama kutwahirika nguo, ni kwa dalili ya kauli yake ALLAH:

﴿ وَثِيَابَكَ فَطَهِّرْ ﴾

**"Na nguo zako uzitwahirishe."** (74:4).

Ama kutwahirika mahali pa kuswalia, ni kwa dalili ya Hadithi ya Abu Huraira (R.A.) aliposema:

« قام أعرابي فبال في المسجد فقام إليه الناس ليقعوا به فقال ﷺ : « دعوه وأريقوا على بوله سجلاً من ماء أو ذنوباً[1] ، من ماء فإنما بعثتم ميسرين ولم تبعثوا معسرين »

**"Alisimama mbedui akakojoa Msikitini, watu wakamsimamia kutaka kumpiga. Mtume (S.A.W.) akasema: "Mwacheni na mumimine - juu ya mkojo wake - ndoo ya maji, au dishi la maji. Hakika mumeletwa kuwa ni wenye kusahilisha wala hamkuletwa kufanya uzito."** (Bukhari).

**SHARUTI YA SITA:** Kuingia wakati ,

Haipasi swala ila unapoingia wakati wake. Wala haiswihi itakaposwaliwa kabla ya kuingia wakati wake, kwa dalili ya kauli yake ALLAH:

﴿ إِنَّ الصَّلَاةَ كَانَتْ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ كِتَابًا مَوْقُوتًا ﴾

**"Kwa hakika swala kwa Waislamu ni faradhi iliyowekewa nyakati makhsusi."** (4:103).

Yaani nyakati zilizoekewa mpaka maalumu. Na Jibril (A.S.) aliteremka akamfundisha Mtume (S.A.W.) nyakati za Swala. Akamswalisha mwanzo wa wakati na mwisho wake. Kisha akamwambia: **"Baina ya nyakati hizi muna wakati (wa kuswalia)."** (Tirmidhy, Nasai na wengineo).

**SHARUTI YA SABA:** Kuusitiri uchi,
Kwa dalili ya kauli yake ALLAH:

﴿ يَا بَنِي آدَمَ خُذُوا زِينَتَكُمْ عِنْدَ كُلِّ مَسْجِدٍ ﴾

**"Enyi wanaadamu! Chukueni mapambo yenu wakati wa kila Swala."** (7:31). **"Mapambo"** katika nguo ni yanayositiri uchi. Wenye Ilimu wote wamekata kauli moja kuwa kusitiri uchi ni sharuti katika kuswihi Swala. Anayeswali uchi ilhali yuwaweza kuusitiri uchi wake, basi Swala yake ni faasid (haifai).

**SHARUTI YA NANE:** Niya,
Kwa dalili ya kauli yake Mtume (S.A.W.):

« إنما الأعمال بالنيات وإنما لكل امرىء ما نوى »

**"Hakika kuswihi kwa amali huzingatiwa niya, na kila mtu ana malipo ya atakalolinuwilia."** (Bukhari na Muslim).

**SHARUTI YA TISA:** Kuelekea Qibla,
Kwa dalili ya kauli yake ALLAH:

قَدْ نَرَىٰ تَقَلُّبَ وَجْهِكَ فِي السَّمَاءِ فَلَنُوَلِّيَنَّكَ
قِبْلَةً تَرْضَاهَا فَوَلِّ وَجْهَكَ شَطْرَ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ وَحَيْثُ مَا كُنتُمْ فَوَلُّوا وُجُوهَكُمْ شَطْرَهُ

**"Kwa yakini tukiona unavyogeuzageuza uso wako mbinguni. Basi tutakugeuza katika Qibla ukipendacho. Basi geuza uso wako upande wa Msikiti Mtakatifu (Al-kaaba), na popote mnapokuwa zielekezeni nyuso zenu uliko (Msikiti huo)."** (2:144).

## NGUZO ZA SWALA:

Swala ina nguzo au faradhi. Lau nguzo moja itachelewa - katika nguzo zake - Swala itabatilika. Tazama ubainifu wake:

1. Niya: Nayo ni moyo kuazimia juu ya kutekeleza Swala maalum, kwa dalili ya kauli yake Mtume (S.A.W.): **"Hakika kuswihi kwa amali huzingatiwa nia."** Na hiyo nia inakutanishwa pamoja na Takbiratul Ihram na pamoja na kuinua mikono wala hapana ubaya ikitangulia kidogo mbele ya Takbiratul Ihram.

2. Takbiratul Ihram kwa lafdhi ya **"ALLAH AKBAR."** Kwa dalili ya kauli yake Mtume (S.A.W.)

« مفتاح الصلاة الطهور وتحريمها التكبير وتحليلها التسليم »

**"Ufunguo wa Swala ni udhu na tahrimu yake ni kupiga takbira na kujifungua kutoka katika swala ni kupiga salaam."** (Abu Dawud, Tirmidhi na wengineo).

3. Kusimama pamoja na kuweza katika swala ya faradhi kwa dalili ya kauli yake ALLAH:

﴿ حَافِظُوا عَلَى الصَّلَوَاتِ وَالصَّلَاةِ الْوُسْطَى وَقُومُوا لِلَّهِ قَانِتِينَ ﴾

**"Angalieni sana Swala (zote kuziswali, khasa jamaa) na (khasa) ile swala ya kati na kati. Na simameni kwa unyenyekevu katika kumwabudu ALLAH."** (2:38).

Na kwa dalili ya kauli yake Mtume (S.A.W.) kumwambia Imran bin Huswain:

« صل قائماً فإن لم تستطع فقاعداً فإن لم تستطع فعلى جنب »

**"Swali kwa kusimama ikiwa huwezi kwa kuketi na ikiwa huwezi basi swali kwa ubavu."** (Bukhari).

4. Kusoma Suratul Fatihah katika kila rakaa miongoni mwa rakaa za Swala za faradhi na sunna, kwa dalili ya kauli yake Mtume (S.A.W.):

« لا صلاة لمن لم يقرأ بفاتحة الكتاب »

**"Hapana Swala kwa asiyesoma Fatihatil kitaab (Al-Hamdu)."** (Bukhari).

5. Kurukuu. Nako ni faradhi kwa ijimai ya ulamaa wote, kwa dalili ya kauli ya ALLAH:

﴿ يَاأَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا ارْكَعُوا وَاسْجُدُوا وَاعْبُدُوا رَبَّكُمْ وَافْعَلُوا الْخَيْرَ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ ﴾

**"Enyi mlioamini! (Swalini) rukuuni na kusujudu na mwabudini Mola wenu na fanyeni mema, ili mpate kufaulu".** (22:77). Na kwa dalili ya kauli yake Mtume (S.A.W.) kumwambia aliyeswali vibaya:

« . . . ثم اركع حتى تطمئن راكعاً ».

**".... kisha rukuu mpaka utulie hali ya kuwa umerukuu".** (Bukhari na Muslim).

6. Kuinuka kutoka katika rukuu, kwa dalili ya kauli ya Mtume (S.A.W.) kumwambia aliyeswali vibaya:

« ثم ارفع حتى تعتدل قائماً ».

**"Kisha uinuke mpaka ulingane hali ya kuwa umesimama."** (Bukhari na Muslim).

7. Kuitadili hali ya kusimama wima, kwa dalili ya Hadithi iliyotangulia na kwa kauli yake Mtume (S.A.W.):

« لا ينظر الله إلى صلاة رجل لا يقيم صلبه بين ركوعه وسجوده ».

**"ALLAH hatazami swala ya mtu asiyeusimamisha uti wake wa mgongo baina ya kurukuu kwake na kusujudu kwake."** (Ahmad).

8. Kusujudu, kwa dalili ya Aya Tukufu iliyotangulia, na kauli yake Mtume (S.A.W.) kumwambia aliyeswali vibaya:

« ثم اسجد حتى تطمئن ساجداً ».

**"Kisha usujudu mpaka utulie hali ya kuwa umesujudu."** (Bukhari na Muslim).

9. Kuinuka kutoka katika sijda, kwa dalili ya kauli yake Mtume (S.A.W.) kumwambia aliyeswali vibaya:

« ثم ارفع حتى تطمئن جالساً »

**"Kisha uinuke (kutoka katika sijda) mpaka utulie ḥali ya kuwa umeketi."** (Bukhari na Muslim).

10. Kuketi baina ya Sijda mbili, kwa dalili ya kauli yake Mtume(S.A.W.):

« لا ينظر الله إلى صلاة رجل لا يقيم صلبه بين ركوعه وسجوده »

**"ALLAH haitazami Swala ya mtu asiyeusimamisha uti wake wa mgongo baina ya kurukuu kwake na kusujudu kwake."** (Ahmad).

11. Kujituliza katika kurukuu, kusujudu, kusimama na kuketi, kwa dalili ya kauli yake Mtume (S.A.W.) kumwambia aliyeswali vibaya: **".... mpaka utulie .....".** (Bukhari na Muslim). Alimtajia hivyo katika kurukuu, kusujudu na kuketi (baina ya sijda mbili). Na akamtajia kuitadili (kusimama wima) katika kisimamo.

Hakika ya kujituliza ni: Kujituliza kwa mwenye kurukuu, mwenye kusujudu na mwenye kuketi au mwenye kusimama baada ya kustakiri (kutulia) viungo vyake kwa kadiri ya muda wa kusema:

سبحـــان ربي العظيم

**"SUBHAANA RABBIYAL 'ADHWIIM"** mara moja, ikizidi fauka ya hapo ni sunna.

12. Tashahudi (Tahiyatu) ya mwisho na kitako chake: Ama Tashahudi ya mwisho ni kwa dalili ya kauli ya Ibni Mas'uud (R.A.): **"Tulikua tukisema katika swala - kabla ya kufaradhiwa Tashahudi":**

السلام على الله السلام على جبريل وميكائيل ،

**"Amani iwe juu ya ALLAH. Amani iwe juu ya Jibril na Mikail."** Mtume (S.A.W.) akasema:

« لا تقولوا هكذا فإن الله عز وجل هو السلام

ولكن قولوا : التحيات لله والصلوات والطيبات ، السلام عليك

أيها النبي ورحمة الله وبركاته ، السلام علينا وعلى عباد الله الصالحين ، أشهد أن لا إله إلا الله وأشهد أن محمداً عبده ورسوله »

**"Msiseme hivyo, kwani ALLAH yeye mwenyewe ni Amani."** Lakini semeni: **"Kila jinsi ya maamkuzi mema ni yenye kumthubutukia ALLAH na Rehma na mambo mema. Amani iwe juu yako ewe Mtume, Rehma za ALLAH na Baraka zake. Amani iwe juu yetu na juu ya waja wa ALLAH waliowema. Nashuhudia kuwa hakuna Mola anayestahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa ALLAH. Na nashuhudia kuwa Muhammad ni mja wake na ni Mtume wake."** (Nasai, Daraqutwany na Baihaqy).

Na kwa dalili ya kauli yake Mtume (S.A.W.): **"Atakapoketi mmoja wenu (katika Tahiyatu) basi aseme":**

التحيات لله والصلوات والطيبات »

(Abu Daud, Nasai na wengineo. Asili yake imo katika Bukhari na Muslim).

13. Kutoa salamu, kwa dalili ya kauli yake Mtume (S.A.W.):

« مفتاح الصلاة الطهور وتحريمها التكبير وتحليلها التسليم »

**"Ufunguo wa Swala ni udhu, na Tahrim yake ni kupiga Takbira na kujifungua kutoka katika swala ni kutoa salamu."** (Abu Daud, Tirmidhy na wengineo).

14. Kutungamanisha baina ya nguzo. Hawezi kuisoma Suratul Faatiha kabla ya Takbiratul-Ihram, wala hawezi kusujudu kabla ya kurukuu, kwa dalili ya kauli yake Mtume (S.A.W.):

« صلوا كما رأيتموني أصلي »

**"Swalini kama mnavyoniona ninavyoswali."** (Bukhari).

Basi atakapokhalifu katika kutungamanisha faradhi za Swala - kama ilivyohifadhiwa kutoka kwa Mtume (S.A.W.) - mithili ya kukitanguliza kinachoakhirishwa na kukiakhirisha kinachotangulizwa, Swala yake itabatilika.

# WAJIBATI* ZA SWALA:

Wajibati za Swala ni ambazo zimo ndani yake, swala hubatilika kwa kuacha mojawapo, kwa makusudi, na huanguka kwa kusahau, na atasujudu - kwa kusahau huko - sijdatussahwi (Sijda ya kusahau). Tazama ubainifu wake:

1. Takbira za kugura kila unaponyanyuka, kuinama, kusimama na kuketi - isipokuwa kunyanyuka kutoka katika rukuu - kwa dalili ya kauli ya "Abdullah bin Mas'uud (R.A.): **"Nilimwona Mtume (S.A.W.) akipiga Takbira katika kuinama, kunyanyuka, kisimamo na kuketi."** (Ahmad, Tirmidhy, Nasai na wengineo).

2. Kusema:

سبحان ربي العظيم

Mara moja katika rukuu, kwa dalili ya kauli ya Hudhaifa katika Hadithi yake: **"....akawa - yaani Mtume (S.A.W.) - akisema katika rukuu yake":**

سبحان ربي العظيم

na katika sijda yake:

سبحان ربي الأعلى »

(Ahmad, Abu Daud, Tirmidhy na wengineo).

3. Kusema:

« سبحـان ربي الأعلى

mara moja katika sijda, kwa dalili ya Hadithi ya Hudhaifa iliyotangulia.

4. Kusema:

« سمع الله لمن حمده »

kwa Imamu na anaeswali peke yake, kwa dalili ya kauli ya Abu Huraira (R.A.), kuwa Mtume (S.A.W.) alikua akisema:

سمع الله لمن حمده

---

***Wajibati: mambo ambayo ni wajibu/lazima.**

anapouwinua mgongo wake kutoka katika rukuu. Kisha akisema naye amesimama:

« ربنا ولك الحمد »

(Muttafaq).

5. Kusema:

« ربنا ولك الحمد »

Kwa Imamu, Maamuma na anaeswali pekee, kwa dalili ya hadithi iliyotangulia na kauli yake Mtume (S.A.W.): **"Imamu atakapo sema"**:

سمع الله لمن حمده

basi semeni.

« اللهم ربنا ولك الحمد »

(Muttafaq).

6. Kusoma dua baina ya sijda mbili, nayo ni:

« اللهم اغفر لي وارحمني وعافني واهدني وارزقني »

(Abu Daud na Tirmidhy). Au kusema:

« رب اغفر لي رب اغفر لي »

(Ibnu Maajah, Haakım na wengineo). Mtume (S.A.W.) alikisoma hivyo.

7. Tashahudi ya kwanza na

8. Kitako chake, kwa dalili ya kauli yake Mtume (S.A.W.) kumwambia Rifaa bin Raafi: **"Utakapokua umesimama katika Swala yako, piga Takbira kisha usome kichache ulichonacho kutokana na Qur'aan. Utakapoketi katikati ya Swala jitulize na ulilaze paja lako la kushoto kisha usome Tashahudi."** (Abu Daud na Baihaqy).

## SUNNA ZA SWALA:

Swala ina sunna nyingi ambazo zimependekezwa kwa

mukabala wa masikio katika hali zinazofuatia:

a. Wakati wa kupiga Takbiratul Ihram.

b. Wakati wa kurukuu.

c. Wakati wa kunyanyuka kutoka katika rukuu.

d. Wakati wa kusimama kutoka katika rakaa ya pili kwenda katika rakaa ya tatu, kwa dalili ya kauli ya Ibnu Umar (R.A) kuwa Mtume (S.A.W.) alikuwa anaposimama katika swala huinyanyua mikono yake hata yakawa mkabala wa mabega yake, kisha akipiga Takbira. Anapotaka ku-rukuu huinyanyua vilevile, na anapokinyanyua kichwa chake kutoka katika rukuu huinyanyua mikono yake kadhalika. (Muttafaq)

Ama wakati wa kusimama katika rakaa ya tatu, ni kwa kuwa Ibnu Umar alikuwa: **"Anaposimama kutoka katika rakaa ya pili huinyanyua mikono yake."** (Bukhari). Na tendo hilo akilinasibisha kwa Mtume (S.A.W.).

2. Kuweka mkono wa kulia juu ya mkono wa kushoto, juu ya kifua au chini ya kifua na ni juu ya kitovu. Kwa dalili ya kauli ya Sahl bin Sa'd (R.A.): **"Watu walikuwa wakiamrishwa, mtu aweke mkono wake wa kulia juu ya dhiraa yake ya kushoto katika Swala."** (Bukhari).

Imepokewa kutoka kwa Wail bin Hujr (R.A.) akisema: **"Niliswali pamoja na Mtume (S.A.W.) akauweka mkono wake wa kulia juu ya mkono wake wa kushoto, juu ya kifua chake."** (Ibnu khuzeima).

3. Kusoma Dua ya kufungulia Swala, nayo ni:

« سبحانك اللهم وبحمدك، وتبارك اسمك وتعالى جدك ولا إله غيرك »

**"Kutakasika ni kwako Ewe Mola, Himdi zote ni zako, limetukuka jina lako, umetukuka utukufu wako na hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa ni wewe."** (Muslim na wengineo).

4. Kupiga Audhubillah katika rakaa ya kwanza na kusoma Bismillah kwa siri katika kila rakaa, kwa dalili ya kauli yake ALLAH:

﴿ فَإِذَا قَرَأْتَ الْقُرْآنَ فَاسْتَعِذْ بِاللَّهِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ ﴾

**"Na ukitaka kusoma Qur'aan piga Audhu (kwanza, jikinge) kwa ALLAH (S.W.) (akulinde) na shetani aliyefukuzwa (katika rehema yake ALLAH)."** (16:98). 5. Kuleta **'Aamin'** baada ya kusoma Suratul Fatiha. Yasunniwa kufanya hivyo kwa kila mwenye kuswali, Imam, Maamuma au mwenye kuswali peke yake, kwa dalili ya kauli ya Mtume (S.A.W.): **"Imam atakaposema":**

« غير المغضوب عليهم ولا الضالين »

Semeni: **"Aamiin, kwani ambae kauli yake itaafikiana na kauli ya Malaika, atasamehewa dhambi zake zilizotangulia."** (Bukhari na Muslim ameipokea kwa maana hayo hayo). Mtume (S.A.W.) alikuwa anaposoma:

« غير المغضوب عليهم ولا الضالين »

akisema **'Aamiin'.** Akiivuta sauti yake kwa hiyo **'Aamiin'**. (Abu Daud na Tirmidhi kutoka katika riwaya ya Wail bin Hujr).

6. Kusoma-baada ya Suratul-Faatihah - kadiri ya sura au chochote kutokana na Qur'aan kama aya moja hivi au aya mbili baada ya kuisoma Suratul-Faatihah katika rakaa mbili za asubuhi na rakaa mbili za mwanzo za adhuhuri, alasiri, magharibi na isha. Kwa dalili iliopokewa kuwa Mtume (S.A.W.). **"Alikuwa akisoma katika (Swala ya) adhuhuri - katika rakaa mbili za mwanzo, na katika rakaa mbili za mwisho akisoma Suratul-Faatihah nawakati mwingine alikuwa akiwasikilizisha aya."** (Muttafaq).

7. Kudhihirisha kusoma katika swala ya jahariya, na kusoma kwa siri katika Swala ya kusiririsha. Atadhihirisha katika rakaa mbili za mwanzo katika Swala ya magharibi na isha na katika rakaa mbili za swala ya asubuhi. Na katika Swala zisizokuwa hizi atasoma kwa siri. Haya yote atayafanya katika Swala ya faradhi. Na yamethubutu na ni mashuhuri kutoka kwa Mtume (S.A.W.) kwa kauli na kwa feli.

Ama katika Swala ya nafla (Sunna), sunna ni kusoma kwa

siri ikiwa ni Swala ya mchana. Na kusoma kwa dhahiri ikiwa ni Swala ya usiku isipokuwa atakapochelea kumwuudhi mtu kwa kusoma kwake, hapo imependekezwa kusiririsha wakati huo.

8. Kurefusha kisomo katika Swala ya asubuhi na kusoma kwa wastani katika swala ya adhuhuri, alasiri na isha, na kufupisha katika Swala ya magharibi.

Sulaiman bin Yasar amepokea kutoka kwa Abuhureira (R.A.) akisema: **"Sijamwonapo mtu anaeswali Swala inayofanana zaidi na Swala ya Mtume (S.A.W.) kuliko fulani - ambae ni Imamu wa Madina".** Sulaiman akasema: **"Basi nikaswali nyuma yake (Imamu wa Madina), akawa anazirefusha rakaa mbili za mwanzo za (Swala ya) adhuhuri na akizikhafifisha rakaa nyenginezo. Na akiikhafifisha Swala ya alasiri. Na katika Swala ya magharibi akisoma - katika rakaa mbili za mwanzo - sura fupi fupi za Mufassal. Na akisoma - katika rakaa mbili za mwanzo za Swala ya isha - sura za wastani za Mufassal. Na katika Swala ya asubuhi akisoma sura ndefu ndefu za Mufassal."** (1)

9. Namna ya kuketi kulikothubutu kama ilivyopokewa kutoka kwa Mtume (S.A.W.). Nako ni kuketi kikao cha Iftirashi katika vikao vyote na katika tashahudi zote isipokuwa tashahudi ya mwisho iwapo katika swala muna tashahudi mbili - kwani ataketi kikao cha tawaruki. Kwa dalili ya kauli ya Abi Humaid As-saa'idy katika hadhara ya swahaba hali ya kuisifu swala ya Mtume (S.A.W.), akaeleza **"....Atakapoketi katika rakaa ya pili ataketi juu ya mguu wake wa kushoto na atausimamisha mguu wa kulia. Na atakapoketi katika rakaa ya mwisho, atautanguliza mguu wake wa kushoto na atausimamisha mguu mwingine na ataketi juu ya makalio yake."** (Bukhari)

Na katika maelezo hayo, yabainika kwa msomaji mtukufu maana ya **"Iftirashi"** na **"Tawaruki."**

---

(1). Mufassal inaanzia suratu Qaaf mpaka mwisho wa Msahafu. Sura ndefu za Mufassal zinaanzia suratu Qaaf mpaka 'Amma yatasaaalun. Na sura zake za wastani zinaanzia hapo ('Amma) mpaka Wad-dhuhaa. Na sura zake fupi fupi zinaanzia Wadh-dhuhaa mpaka mwisho wa Qur'aan.

Na Hadithi hiyo imepokewa na Imam Ahmad na Nasaai, nayo ni swahihi.

Iftirashi: ni kuketi juu ya matumbo ya mguu wa kushoto na kuusimamisha mguu wa kulia.

Tawaruki: ni kuyafanya matumbo ya mguu wa kushoto chini ya paja la mguu wa kulia, na tako lake atalieka juu ya ardhi na atausimamisha unyayo wake wa kulia.

**FAIDA:** Mtume (S.A.W.) alikuwa anapoketi katika tashahudi huuweka mkono wake wa kushoto juu ya goti lake la kushoto na akiuweka mkono wake wa kulia juu ya goti lake la kulia na akiashiria kwa kidole cha shahada (Muslim) na **"alikuwa, jicho lake halipiti ishara yake."** (Abu Daud).

10. Kuomba dua katika kusujudu, kwa dalili ya kauli yake Mtume (S.A.W.) « ألا وإني نهيت أن أقرأ القرآن

راكعاً أو ساجداً ، فأما الركوع فعظموا فيه الرب ، وأما السجود

فاجتهدوا في الدعاء فقمن(٣) أن يستجاب لكم »

**"Juweni kwamba, nimekatazwa kusoma Qur'aan hali ya kurukuu au kusujudu. Ama kurukuu mtukuzeni Mola ndani yake na ama kusujudu jitahidini katika dua, kwani ni hakika tu kuwa mtajibiwa."** (Muslim).

11. Kumswalia Mtume(S.A.W.) katika tashahudi ya mwisho. Baada ya kusoma tashahudi.

« التحيات لله . . . وأن محمداً عبده ورسوله »

atasema:

« اللهم

صل على محمد وعلى آل محمد كما صليت على إبراهيم وعلى آل

إبراهيم ، وبارك على محمد وعلى آل محمد كما باركت على إبراهيم

وعلى آل إبراهيم في العالمين إنك حميد مجيد »

(Muslim kadhalika imezidishwa kutoka katika riwaya nyingine zilizo

Swahihi).

12. Kuomba dua baada ya kumaliza tashahudi ya mwisho baada ya kumswalia Mtume (S.A.W.): **"Mmoja wenu atakapomaliza kuswali aombe mambo manne kisha aombe anachotaka."** (Ataomba:)

اللهم إني أعوذ

بك من عذاب جهنم ، وعذاب القبر ، وفتنة المحيا والممات وفتنة

المسيح الدجال »

(Baihaqy).

13. Kutoa salamu ya pili upande wa kushoto wa mwenye kuswali. Imethubutu **"Kuwa Mtume (S.A.W.) alikuwa akitoa salamu kuliani kwake na kushotoni mwake mpaka weupe wa taya yake ukionekana."** (Muslim).

14. Adhkaar na dua baada ya kutoa salamu.

Imepokewa kutoka kwa Mtume (S.A.W.) jumla ya adhkaar na dua baada ya salamu. Ni mustahabu kwa mwenye kuswali kuzileta. Nasi tumechagua baadhi, nazo ni:

a. Thauban (R.A.) amesema: **"Alikuwa Mtume (S.A.W.) anapomaliza Swala yake akiomba istighfaar mara tatu."** Na akisema:

« اللهم أنت السلام ومنك السلام تباركت يا ذا الجلال والإكرام »

**"Ewe Mola, wewe ni Amani. Kwako inatoka Amani, Umetukuka ewe Mwenye Utisho na Utukufu."** (Muslim).

b. Imepokewa kutoka kwa Mu'adh bin Jabal (R.A.) kuwa Mtume (S.A.W.) alimshika mkono wake - siku moja - kisha akasema: **"Ewe Mu'adh, mimi nakupenda. Nakuusia ewe Mu'adh, baada ya kila Swala usiache kunena":**

اللهم أعني على ذكرك وشكرك وحسن عبادتك »

**"Ewe Mola nisaidie juu ya kukutaja, kukushukuru na kufanya uzuri ibada zako."** (Imepokewa na Imam Ahmad, Abu Daud na Haakim).

c. Imepokewa kutoka kwa Mughira bin Shu'ba (R.A) kuwa Mtume (S.A.W.) alikuwa akisema baada ya kila Swala ya Faradhi:

« لا إله إلا الله وحده لا شريك له ، له الملك وله الحمد وهو على كل شيء قدير ، اللهم لا مانع لما أعطيت ، ولا معطي لما منعت ، ولا ينفع ذا الجد منك الجد »

(Bukhari na Muslim).

d. Imepokewa kutoka kwa Abuhureira (R.A) kuwa Mtume (S.A.W.) amesema:

« من سبح الله في دبر كل صلاة ثلاثاً وثلاثين وحمد الله ثلاثاً وثلاثين ، وكبر الله ثلاثاً وثلاثين ، فتلك تسعة وتسعون ، وقال تمام المائة ، لا إله إلا الله وحده لا شريك له ، له الملك وله الحمد وهو على كل شيء قدير ، غُفرت له خطاياه وإن كانت مثل زبد البحر »

**"Atakaemsabihi ALLAH baada ya kila swala mara thalathini na tatu (33), akamhimidi ALLAH mara thalathini na tatu (33) na akamkabiri ALLAH mara thalathini na tatu (33) - hizo ni mara tisaini na tisa (99) - na akasema kukamilisha mia (100):**

**Basi atasamehewa dhambi zake ingawa ni tamthili ya povu la bahari."** (Muslim).

e. Imepokewa kutoka kwa Abu Umama (R.A.) kuwa Mtume (S.A.W.) amesema:

« من قرأ آية الكرسي دبر كل صلاة لم يمنعه من دخول الجنة إلا أن يموت »

**"Atakaesoma Ayatul-kursy baada ya kila swala, hakuna kitakachomzuilia Peponi ela ni kufa."** (Imepokewa na Nasai, Ibnu hibban na Twabrany).

f. Sa'di bin Abi Waqqaas (R.A.) alikuwa akiwafunza wanawe maneno haya kama jinsi ya mwalimu awafundishavyo watoto namna ya kuandika, na akisema, hakika Mtume (S.A.W.) alikuwa akijilinda kwa maneno hayo (nayo ni):

« اللهم إني أعوذ بك
من البخل ، وأعوذ بك من الجبن ، وأعوذ بك أن أرد إلى أرذل
العمر ، وأعوذ بك من فتنة الدنيا ، وأعوذ بك من عذاب
القبر »

**"Ewe Mola, kwa yakini najilinda kwako kutokana na ubakhili. Na najilinda kwako kutokana na uwongo. Na najilinda kwako kurudishwa kwenye umri dhalili. Na najilinda kwako kutokana na fitina za ulimwengu. Na najilinda kwako kutokana na adhabu ya kaburini."** (Bukhari na Muslim).

## YANAYORUHUSIWA KATIKA SWALA:

Katika Swala yaruhusiwa kufanya baadhi ya mambo, miongoni mwayo ni:

1. Kumfungulia Imamu, anapoisahau Aya, maamuma atamkumbusha Aya hiyo.

Imepokewa kutoka kwa Ibni 'Umar (R.A.) kuwa Mtume (S.A.W.) aliswali swala, akachanganyikiwa. Alipomaliza alimwuliza baba yangu **"Je umeswali pamoja nasi?"** **Akajibu Ndio."** Akamwambia **"Ni kitu gani kilichokuzuwia usinifungulie?"** (Abu Daud, Hakim na Ibnu Hibban).

2. Kusabihi na kupiga kikofi linapotokea jambo, kama

kumkumbusha Imamu anaposahau, au kumwongoza kipofu na mfano wake.

Mtume (S.A.W.) amesema:

« من نابه شيء في صلاته فليسبح فإنما التصفيق للنساء »

**"Atakaepatwa na jambo katika Swala basi asabihi, kwani kupiga kikofi ni kwa wanawake."**

3. Kumwua nyoka, nge na mfano wake.

Mtume (S.A.W.) amesema:

« اقتلوا الأسودين في الصلاة الحية والعة »

**"Uweni vyeusi viwili katika Swala, nyoka na nge."** (Ahmad, Abu Daud, Tirmidhy na wengineo).

4. Kumzuwiya anaepita mbele ya anaeswali

Mtume (S.A.W.) amesema:

« إذا صلى أحدكم إلى شيء يستره من الناس فأراد أحد أن يجتاز بين يديه فليدفعه فإن أبى فليقاتله فإنما هو شيطان »

**"Atakaposwali mmoja wenu kukielekea kitu kinachomsitiri na watu, halafu mtu akataka kupita mbele yake, basi amzuwie. Akikataa apigane naye, hakika huyo atakua ni shetani."** (Muttafaq).

5. Kumrudishia kwa ishara anaemsalimia au anaemzungumzisha.

Imepokewa na Jabir bin 'Abdulla (R.A.) akisema: **"Mtume (S.A.W.) alinituma naye alikua akienda kwa Bani Mustalik. Nikamwendea naye yuwaswali juu ya mnyama wake. Nikamzungumzisha akaashiria hivi kwa mkono wake (akawa anaashiria). Kisha nikamzungumzisha akaashiria hivi, nami namsikia akisoma akiashiria kwa kichwa chake. Alipomaliza alisema: "Umefanya nini katika jambo nililokutuma? Kwani hakuna jambo lililonizuwia kuzungumza nawe ela tu nilikuwa katika Swala."** (Muslim).

Imepokewa kutoka kwa Ibnu 'Umar, nae kutoka kwa Suhaib (R.A.) akisema: **"Nilimpatia Mtume (S.A.W.) nae yuwaswali, nikamsalimia, akanirudishia kwa ishara. Sijui ela kuwa yeye aliashiria kwa kidole chake."** (Abu Daud, Tirmidhy, Nasai na Wengineo).

Kwa hivyo imejulikana - kutokana na Hadithi hizi - kuwa kuashiria huwa ni kwa mkono wote au kuashiria kwa kichwa au kidole.

6. Kumbeba mtoto na kuwa naye. Abu Qatada Al-Ansaary (R.A.) amesema: **"Nilimwona Mtume (S.A.W.) akiswalisha watu na Umama binti Abil'aas - binti ya Zainab Bint ya Mtume (S.A.W.) - yuko juu ya mabega yake. Anapo rukuu humweka na anapoinuka kutoka katika Sijda humrudisha (mabegani mwake)."** (Muslim).

7. Kuenda kidogo kiasi cha haja.

Bibi Aisha (R.A) amesema: **"Mtume (S.A.W.) alikua akiswali nyumbani na mlango umefungwa. Nikaja nikataka kufunguliwa, akatembea akinifungulia kisha akarudi mswalani mwake. - Mlango wenyewe ulikua upande wa Qibla."** (Ahmad, Abu Daud, Tirmidhy na wengineo).

8. Kufanya tendo dogo, kama kumtengeza alie katika safu kwa kumvutia mbele au nyuma, au kumzungusha anaemfwata Imamu kutoka kushotoni hadi kuliani, au kuitengeza nguo, kukohoa wakati wa haja, kujisugua mwili kwa mkono, kwenda mwayo na kuweka mkono juu ya mdomo.

Ibnu Abbas (R.A.) amesema: **"Nililala kwa khalati yangu Maimuna, Mtume (S.A.W.) akasimama kuswali Swala ya usiku, nami nikasimama kuswali pamoja naye upande wake wa kushoto, akakishika kichwa changu akanisimamisha kuliani mwake."** (Muttafaq).

## MAKRUHU KATIKA SWALA:

1. Kuinua macho mbinguni kwa dalili ya kauli yake Mtume (S.A.W.):

« ما بال أقوام يرفعون أبصارهم

إلى السماء في صلاتهم ؟ لينتهن عن ذلك أو لتخطفن أبصارهم »

**"Kwa nini watu wanayainua macho yao mbinguni katika swala zao? Watakoma kufanya hivyo au watapokonywa macho yao."** (Bukhari. Imam Muslim amepokea Hadithi yenye maana yayo hayo).

2. Kuweka mkono kiunoni kwa sababu Mtume (S.A.W.) alikataza **"Kuuweka mkono kiunoni katika Swala."** (Muttafaq).

3. Kugeuza kichwa au macho ela kwa haja, kwa dalili ya kauli ya 'Aisha (R.A.): Nilimwuliza Mtume (S.A.W.) kuhusu mtu kugeuka katika Swala. Akasema: **"Ni unyakuzi wa shetani anaomnyakulia mtu katika Swala ya mja."** (Bukhari na Abu Daud).

4. Kucheza na kila limshughulishalo mtu katika Swala likamwondolea khushui yake.

Mtume (S.A.W.) amesema: **"Tulieni katika Swala."** (Muslim).

5. Kuzizuwia nywele zilizoachilika au nguo yake au mkono wake wa kanzu.

Mtume (S.A.W.) amesema:

« أمرت أن أسجد على سبعة أعظم ولا أكف ثوباً ولا شعراً »

**"Nimeamrishwa kusujudu juu ya viungo saba, wala nisiizuwie nguo wala nywele."** (Muttafaq).

6. Kupangusa vijiwe na kuusawazisha mchanga zaidi ya mara moja mahala pa kusujudu.

Mu'ayqib amesema: Mtume (S.A.W.) alitaja kupangusa (vijiwe) Msikitini. Akasema: **"Ikiwa huna budi kufanya hivyo, basi fanya mara moja."** (Muslim).

Vile vile imepokewa kutoka kwa Mu'ayqib kuwa Mtume (S.A.W.) alisema kuhusu mtu anayeusawazisha mchanga pale anaposujudu. Akasema: **"Ikiwa ni mwenye kufanya, basi ni mara**

**moja."** (Muttafaq).

7. Kujifinika gubigubi na kuuziba mdomo.

Abu huraira (R.A.) amesema: **"Mtume (S.A.W.) amekataza mtu kujifunika gubigubi."(1). Katika Swala na mtu kuuziba (2) mdomo wake."** (Abu Daud, Tirmidhy na wengineo).

8. Kuswali wakati wa chakula kuwa tayari:

Mtume (S.A.W.) amesema:

« لا صلاة بحضرة الطعام »

**"Hakuna Swala wakati wa kuhudhuria chakula."** (Muslim).

9. Kuswali pamoja na kutaka kwenda haja kubwa au ndogo na mfanowe katika mambo yashughulishayo moyo.

Mtume (S.A.W.) amesema: **"Hapana kuswali chakula kinapokuwa kimehudhuria wala anapotaka mtu kukidhi haja kubwa au ndogo."** (Muslim).

10. Kuswali wa kuzidiwa na usingizi:

Mtume (S.A.W.) amesema:

« إذا نعس أحدكم وهو
يصلي فليرقد حتى يذهب عنه النوم ، فإن أحدكم إذا صلى وهو
ناعس لا يدري لعله يذهب يستغفر فيسب نفسه »

**"Anaposinzia mmoja wenu nae yuwaswali, basi alale mpaka usingizi umwishe. Kwani mmoja wenu anaposwali naye yuwasinzia, hajui pengine atataka kuomba maghfira halafu ajitukane."** (Muttafaq).

## YANAYOBATILISHA SWALA:

Swala hubatilika kwa kufanya moja wapo kati ya mambo yanayofwatia:

---

(1) Kujifunika gubigubi katika Swala ni mtu kujitatia nguo yake, aingize mikono yake kwa ndani, arukuu na kusujudu katika hali hiyo, kwani Mayahudi walikua wakifanya hivyo.

(2) Waarabu walikua na desturi ya kuvifunika vinywa vyao kwa vilemba. Wakakatazwa kufanya hivyo katika Swala. Lakini kwa anaekwenda mwayo aruhusiwa kuufunika mdomo wake, kwani imethubutu katika Hadithi

1. Kula na kunywa makusudi.

Mtume (S.A.W.) amesema: **"Hakika katika swala muna shughuli."** (Muttafaq). Na ijimai ya ulamaa wote imefungamana juu ya jambo hilo.

2. Kuzungumza kusudi pasina maslahi ya swala.

Zaid bin Arqam (R.A.) amesema: Tulikua tukizungumza katika Swala, mmoja kati yetu akimzungumzishá mwenziwe naye yu ubavuni mwake katika Swala. Hata ilipoteremka: **"Na simameni kwa unyenyekevu katika kumwabudu ALLAH."** (2: 238). **"Tukaamriwa kunyamaza na tukakatazwa kuzungumza."** (Muttafaq).

Mtume (S.A.W.) amesema:

« إن هذه الصلاة لا يصلح فيها شيء من كلام الناس »

**"Hakika hii Swala haifai ndani yake chochote katika maneno ya watu."** (Muslim).

Ama yawapo maneno ni kwa ajili ya kuitengeza Swala, hapana ubaya, kama vile Imamu anapohitajia kukumbushwa na Maamuma akamkumbusha, au Imamu atoe salamu kisha aulize kutimia Swala yake, atakapoambiwa kuwa Swala yake haikutimia ataitimiza.

Iliwahi kutokea hivyo kwa Mtume (S.A.W.), Dhul-yadain akamwambia: **"Je, umesahau au Swala imepunguzwa?"** Mtume (S.A.W.) akamwambia: **"Sikusahau wala haikupunguzwa."** Akasema: **"Bali umesahau ewe Mtume wa ALLAH."** Mtume (S.A.W.) akauliza: **"Ni kweli alivyosema Dhul-yadain?"** Wakasema: **"Ndio."** **"Akaswali rakaa mbili nyingine kisha akasujudu sijda mbili."** (Muttafaq).

3. Kuacha nguzo au sharuti zilizotangulia kutajwa iwapo hatoitadaraki katikati ya Swala au baada yake kidogo, kwa dalili ya kauli ya Mtume (S.A.W.) kumwambia aliyeswali vibaya: **"Rudi ukaswali tena, kwani bado hujaswali."** (Muttafaq). Alikuwa ameacha kujituliza na kuitadili nazo ni nguzo mbili.

4. Matendo mengi, kwa kutafautiana kwake na msingi wa ibada na moyo pamoja na viungo kushughulikia jambo ambalo ni nje ya Swala. Ama tendo dogo kama kurudisha salamu kwa ishara

kuitengeza nguo au kujikuna mwili kwa mkono na mfano wa hayo, haibatilishi Swala.

5. Kucheka kicheko cha "**Kwaa, kwaa.**" Wenye elimu wameafikiana juu ya jambo hilo (kuwa hubatilisha swala). Ama kutabasamu, Ulamaa wengi wamenena kuwa hakubatilishi Swala.

6. Kutovipangilia vipindi vya Swala, kama kuswali Isha kabla ya Magharibi, kwani Swala Isha itabatilika mpaka aiswali Swala ya Magharibi kwanza. Kwa sababu kupangilia baina ya vipindi vya Swala ni faradhi kwa kuwa vimepokewa kwa mpangilio wa faradhi baada ya faradhi.

7. Kusahau kuliko kubaya. Kama kuzidisha - mfano wake - katika swala, Mathalan aiswali Swala ya Isha rakaa nane. Kwa sababu tendo lake hili ni dalili ya wazi ya kutopatikaniwa khushui (unyenyekevu) ambayo ndiyo roho ya Swala.

## SIJDA YA KUSAHAU

Sijda ya kusahau ni: Sijda mbili anazosujudu mwenye kuswali ili kujaliza kasoro zilizopatikana katika Swala yake kwa sababu ya kusahau.

## SABABU YA SIJDA YA KUSAHAU

Muna sababu tatu za sijda ya kusahau:

1. Kuzidisha 2. Kupunguza 3. Kuwa na shaka

1. **Kuzidisha:**

Atakaesahau katika Swala yake akazidisha rukuu, sijda au mfano wake, basi ni juu yake asujudu sijda mbili baada ya kuitimiza Swala yake na kutoa salamu.

Imepokewa kutoka kwa Ibni Mas'uud (R.A.) kuwa Mtume (S.A.W.) aliswali adhuhuri rakaa tano. Akaulizwa: "**Swala imezidishwa?**" Akasema: "**Kwani kuna nini?**" Wakamwambia: "**Umeswali rakaa tano.**" Akasujudu sijda mbili baada ya kuwa ameshapiga Salamu.

Katika riwaya nyingine yasema: Akayakunja miguu yakę, akaelekea Qibla na akasujudu Sijda mbili kisha akatoa Salamu. (Muttafaq). Kupiga salamu kabla ya kutimiza Swala ni katika kuzidisha katika Swala. Mfano wake ni kama huu: Mwenye kuswali amezidisha Salamu katikati ya Swala. Basi atakaefanya hivyo kwa kusahau akakumbuka baada ya zama kidogo, basi ataikamilisha Swala yake, atatoa Salamu kisha atasujudu Sijda ya kusahau na atatoa Salamu.

Imepokewa kutoka kwa Abu huraira (R.A) kuwa Mtume (S.A.W.) aliwaswalisha adhuhuri au alasiri, akatoa Salamu katika rakaa ya pili, akatoka haraka katika mlango wa Msikiti. (Maswahaba wakawa) wanasema: Swala imepunguzwa. Mtume (S.A.W.) akasimama akaenda kuliegemea gogo kama kwamba amekasirika. Mtu mmoja akasimama na kuuliza: ewe Mtume wa ALLAH, umesahau ama Swala imepunguzwa? Mtume (S.A.W.) akasema: **"Sikusahau wala haikupunguzwa."** Yule mtu akasema: kwa yakini umesahau. Mtume (S.A.W.) akawauliza Maswahaba: **"Ni kweli anenayo?"** Wakasema: Ndio. Mtume (S.A.W.) akatangulia, akawaswalisha rakaa zilizobakia kisha akatoa Salamu, halafu akasujudu sijda mbili hatimae akatoa Salamu. (Muttafaq).

2. **KUPUNGUZA:**

Atakaesahau katika Swala yake, akaacha Sunna iliosisitizwa (nayo i katika hukmu ya waajib) miongoni mwa Sunna za Swala, basi atasujudu Sijda yakusahau kabla ya kutoa Salamu. Kama atakaposahau tashahudi ya kati na kati wala asikumbuke palepale au akakumbuka baada kuwa ashasimama wima, basi hatorejea (bali ataendelea na) atasujudu sijda ya kusahau kabla ya kutoa salamu.

Imepokewa kutoka kwa Abdullah bin Buhaina (R.A.) kuwa Mtume (S.A.W.) aliwaswalisha adhuhuri, akasimama katika rakaa mbili za mwanzo wala hakuketi (kitako cha tashahudi ya kwanza). Watu nao wakasimama pamoja nae. Hata alipomaliza Swala yake, watu wakawa wanangoja atoe Salamu, alipiga takbira - hali ya kuwa ameketi - akasujudu Sijda mbili kabla ya kutoa Salamu kisha akatoa Salamu. (Muttafaq).

3. **KUWA NA SHAKA:**

Nako ni kutaradadi baina ya mambo mawili, ni lipi lililotokea hasa. Shaka huwa ni katika kuzidisha na kupunguza. Kama kutia shaka kwa mwenye kuswali ameswali rakaa tatu au nne. Basi shaka hii ina hali mbili:

a. Dhana yake kuwa na nguvu juu ya moja kati ya mambo mawili, ima kuzidi au kupungua. Basi ataendelea juu ya dhana yenye nguvu na atasujudu Sijda ya kusahau baada ya Salamu.

Imepokewa kutoka kwa 'Abdullah bin Mas'uud (R.A.) kuwa Mtume (S.A.W.) amesema:

« إذا شك أحدكم في صلاته فليتحر الصواب فليتم عليه ثم ليسلم ثم ليسجد سجدتين »

**"Atakapotia shaka mmoja wenu katika Swala yake, basi ajitahidi katika usawa atimize, kisha atoe Salamu halafu asujudu Sijda mbili."** (Muttafaq).

b. Kutokuwa na nguvu kwake yeye moja kati ya mambo mawili, si katika kuzidisha wala katika kupunguza. Basi hapo atahesabu kuwa ameswali rakaa chache. Ataitimiza Swala yake kisha atasujudu Sijda mbili za kusahau kabla ya kutoa Salamu.

Imepokewa kutoka kwa Abu Said Al-Khudry (R.A.) kuwa Mtume (S.A.W.) amesema:

« إذا شك أحدكم في صلاته فلم يدر كم صلى ثلاثاً أم أربعاً ؟ فليطرح الشك وليبن على ما استيقن ثم يسجد سجدتين قبل أن يسلم ، فإن كان صلى خمساً شفعن له صلاته ، وإن كان صلى إتماماً لأربع كانتا ترغيماً للشيطان »

**"Atakapotiashaka mmoja wenu katika Swala yake, asijue ameswali rakaa ngapi, tatu ama nne? Basi aitupe shaka na aendelee juu ya (rakaa) alizoyakinisha, kisha atasujudu sijda mbili kabla ya kutoa Salamu. Akiwa ameswali rakaa tano,**

**zitamshufaiya Swala yake. Na akiwa ametimiza rakaa nne, zitamshikisha mchanga shetani."** (Muslim).

Ufupi wa yaliyotajwa ni kuwa: Sijda ya kusahau mara huwa kabla ya kutoa Salamu na mara huwa baada yake. Huwa baada ya kutoa Salamu mahali pawili.

**Pa kwanza:** Iwapo ni kuzidisha

**Pili:** Iwapo ni kwa shaka, limekuwa na nguvu moja kati ya mambo mawili.

Na - sijda ya kusahau - huwa kabla ya kutoa salamu mahala pawili:

**Pa kwanza:** Iwapo ni katika kupunguza.

**Pili:** iwapo ni kwa shaka, pana uwezekano wa moja kati ya mambo mawili kuwa na nguvu.

## FAIDA ZINAZOFUNGAMANA NA SIJDA YA KUSAHAU:

Atakapoacha mwenye kuswali Faradhi miongoni mwa Faradhi za Swala (nguzo), kikawa chenye kuachwa ni Takbira ya kuhirimia Swala, atakua hana Swala, na ni sawa sawa tu awe ameiyacha kusudi au kwa kusahau, maana Swala yake itakuwa haijafungika. Na kitakapokua chenye kuachwa si Takbira ya kuhirimia Swala, ikiwa amekiacha kusudi Swala yake itakua imebatilika. Na atakapokiacha kwa kusahau, basi atakapofika mahali pale katika rakaa ya pili yake, ile rakaa iliopita - ambamo alipoacha kitu hicho - haitohesabiwa. Bali ile rakaa iliofwatia ndio itakayosimama mahala pake. Na iwapo hatofika mahali pale katika rakaa ya pili yake, basi itampasa airudie nguzo ile aliyoiacha, aitekeleze na yalio baada yake. Katika hali zote hizo yapasa asujudu sijda ya kusahau baada ya kutoa Salamu au kabla yake.

2. Iwapo Sijda ya kusahau itakua ni baada ya kutoa Salamu, hapana budi kutoa tena Salamu mara ya pili.

3. Mwenye kuswali atakapoiacha kusudi sunna iliosisitizwa (katika hukumu ya waajib) miongoni mwa Sunna za Swala basi Swala yake imeshabatilika. Atakapoiacha kwa kusahau na akaikumbuka

kabla ya kupaacha mahali pa sunna hiyo katika Swala, basi ataitekeleza wala hana kitu cha kumlazimu. Atakapoiacha baada ya kupaacha mahala pake ilihali hajaifikilia nguzo inayofwatia, atairudia (Sunna hiyo) aitekeleze, aikamilishe Swala yake, halafu atoe Salamu, kisha asujudu Sijda ya kusahau na atoe Salamu. Atakapoikumbuka (Sunna hiyo) baada ya kuifikilia nguzo inayofwatia, basi itaanguka (Sunna hiyo) wala hatoirudia, ataendelea katika Swala yake na atasujudu Sijda ya kusahau kabla ya kutoa Salamu, kama tulivyoeleza hapo mbele katika tashahudi ya kati na kati.

## NAMNA YA KUSWALI:

1. Atasimama Muislamu kwa ajili ya Swala baada ya kuingia wakati wake, ilihali amejitwahirisha (ametawadha), amejisitiri uchi na ameelekea Qibla kwa mwili wake wote, bila ya kugeuka wala kuzunguka.

2. Kisha atanuwia - moyoni mwake - Swala anayoitaka kuiswali bila ya kuitamka niya yenyewe.

3. Kisha atapiga Takbira ya kuhirimia Swala, ilihali ya kusema:

« الله أكبر »

**"ALLAHU AKBAR".**

awe ameiyenuwa mikono yake mkabala wa mabega yake wakati wa Takbira.

4. Atauweka mkono wake wa kulia juu ya mkono wa kushoto, juu ya kifua chake au chini yake juu ya kitovu,

5. Kisha ataisoma dua ya kufungulia swala, atapiga Audhu Billahi na atasoma Bismilah. Kisha ataisoma Suratil-Faatiha, hata atakapofikia. ﴿ وَلَا الضَّالِّينَ ﴾

atasema:

﴿ آمين ﴾

**"Aamiin".**

6. Kisha atasoma sura nyingine au sehemu yoyote katika Qur'aan Tukufu.

7. Kisha ataiyenua mikono yake mkabala wa mabega yake na atarukuu hali ya kusema:

« الله أكبر »

**"ALLAH AKBAR".**

Atavituliza imara vitengele vyake katika magoti yake, ataunyosha mgongo wake. asikiinue kichwa chake wala asikiinamishe na vidole vyake aviweke mbali mbali juu ya magoti yake.

8. Atasema katika kurukuu:

« سبحان ربي العظيم »

**"Subhaana Rabbiyal-'Adhwiim".** Mara tatu au zaidi.

9. Kisha atakiinua kichwa chake kutoka katika rukuu ilihali ya kuiyenua mikono yake mkabala wa mabega yake huku akisema:

«سمع الله لمن حمده»

**"Sami'allaahu liman hamidah"**, hata atakaposimama wima katika kuitadili, atasema

« ربنا ولك الحمد حمداً كثيراً طيباً مباركاً فيه »

**"Rabbanaa walakal hamdu. Hamdan kathiiran twayyiban mubaarakanfiih".**

10. Kisha atasujudu kwa kusema:

« الله أكبر »

**"ALLAHU AKBAR."**

Atasujudu kwa viungo saba, kipaji cha uso pamoja na pua, viganja, magoti na nyayo (ncha za vidole ziingie ndani), pamoja na kuchunga kukimakinisha kipaji cha uso pamoja na uso katika ardhi. Aiyepushe mikono yake na mbavu zake. Asilaze dhiraa zake juu ya ardhi, na

azielekeze ncha za vidole vyake upande wa Qibla.

11. Aseme katika kusujudu:

« سبحان ربي الأعلى »

**"Subhaana Rabbiyal-A'laa"** mara tatu au zaid.

12. Kisha atakienua kichwa chake kutoka katika sijda kwa kusema:

« الله أكبر »

**"ALLAHU AKBAR."**

Ataketi hali ya kuulaza mguu wake wa kushoto na kuuketia na kuusimamisha mguu wa kulia hali ya kusema:

« رب اغفر لي وارحمني وعافني واهدني وارزقني »

**"Rabbighfirlii Warhamniii Wa'aafinii Wahdiinii Warzuqnii".**

13. Kisha atasujudu (tena) kama ilivyotangulia. Kisha atainuka hadi rakaa ya pili ilihali ya kupiga Takbira, atafanya kama alivyofanya katika rakaa ya kwanza, ela yeye hatosoma dua ya kufungulia Swala. Atakapokomea rakaa ya pili ataketi kwa ajili ya tashahudi. Iwapo Swala ni ya rakaa mbili kama Swala ya asubuhi ataleta tashahudi na atamswalia Mtume(S.A.W.) na atatoa salamu kwa kusema:

« السلام عليكم ورحمة الله »

**"Assalaamu 'alaykum Warahmatullaah"** atageuka upande wa kulia. Hatimaye vivyo hivyo atatoa Salamu upande wa kushoto.

14. Iwapo swala si ya rakaa mbili atasimama mwisho wa tashahudi ya kwanza, napo ni:

« أشهد أن لا إله إلا الله وأشهد أن محمداً عبده ورسوله »

**"Ash-hadu anlaa ilaaha illallahu wa ash-hadu anna Muhammadan 'Abduhuu warasuuluh".** Kisha atainuka hali ya kusimama huku akipiga Takbira kwa kuinua mikono yake mkabala wa mabega yake. Ataswali swala yake iliobakia kwa mfano uliotangulia.

Isipokuwa tu atasoma Suratul-Faatihah peke yake.

15. Kisha ataketi kitako cha tawaruk. Atausimamisha unyayo wake wa kulia, atautoa unyayo wake wa kushoto chini ya mwundi wake wa kulia, atayamakinisha makalio yake juu ya ardhi, ataiweka mikono yake juu ya mapaja yake kisha atasoma tashahudi na atamswalia Mtume (S.A.W.), atajilinda kwa ALLAH kutokana na adhabu ya Jahannam na adhabu ya Kaburini na kutokana na fitna za maisha na mauti na kutokana na fitna za Masihi Dajjaal.

16. Kisha atatoa salamu kwa sauti, akisema:

السلام عليكم ورحمة الله

**"Assalaamu 'alaykum Warahmatullaah"**, huku akielekea upande wa kulia. Kisha atatoa salamu ya pili kwa kuelekea upande wa kushoto.

*****

# SWALA YA JAMAA

## HUKMU YAKE:

Swala ya jamaa ni waajib juu ya kila Muumini. Hairuhusiwi kuiwacha ela kwa udhuru. Hadithi zinazoonyesha hukmu hiyo ni nyingi, miongoni mwazo:

1. Abu Huraira (R.A.) amesema: Mtu mmoja kipofu alimjia Mtume (S.A.W.) akasema: Ewe Mtume wa ALLAH, mimi sina kiongozi wa kuniongoza kuja Msikitini. Akamwomba Mtume (S.A.W.) amruhusu ili aswali nyumbani mwake, (Mtume) akamruhusu. Alipokua akiendazake, alimwita na akamwuliza: **"Je, wausikia Muadhini unaoita watu kuja kuswali?"** Akajibu: Ndio. Akasema (Mtume): **"Basi ujibu".** (Muslim).

2. Abu Haraira (R.A.) amesema: Mtume (S.A.W.) amesema:

« أثقل الصلاة

على المنافقين صلاة العشاء وصلاة الفجر ولو يعلمون ما فيها لأتوهما ولو حبواً ، ولقد هممت أن آمر بالصلاة فتقام ثم آمر رجلاً فيصلي بالناس ثم أنطلق معي برجال معهم حزم من حطب إلى قوم لا يشهدون الصلاة فأحرق عليهم بيوتهم بالنار»

**"Swala iliyo nzito kwa wanafiki ni Swala ya Isha na Swala ya Alfajiri. Lau wangalijua yaliyomo ndani yake wangaliziendea hata kwa kusota. Hakika nilikuwa nimetia hamu kuamrisha Swala isimamishwe, kisha nimuamuru mtu aswalishe watu, halafu niondoke pamoja na watu walio na matita ya kuni, niwaendee wale wasioshuhudia Swala nizichome nyumba zao."** (Muttafaq).

3. Abu Dardai (R.A.) amesema:
Nilimsikia Mtume (S.A.W.) akisema:

« ما من ثلاثة في قرية ولا بدو لا تقام فيهم الصلاة إلا قد استحوذ عليهم الشيطان ، فعليكم بالجماعة فإنما يأكل الذئب من الغنم القاصية »

**"Hakutapatikaniwa watu watatu katika kijiji au mashamba halafu isisimamishwe Swala miongoni mwao ela huwa shetani ameshawaghilibu. Basi shikamaneni na jamaa, hakika mbwa mwitu humla mbuzi alie mbali (peke yake)."** (Ahmad, Abu Daud, Nasai na wengineo).

4. Imepokewa kutoka kwa Ibni Abbas (R.A) kuwa Mtume (S.A.W.) amesema:

« من سمع النداء فلم يأته فلا صلاة له إلا من عذر »

**"Atakaeusikia Muadhini wala asiuwendee basi hana Swala ela kwa udhuru."** (Abu Daud, Ibnu Maajah na wengineo).

5. Ibnu Mas'uud (R.A) amesema:

« من سره أن يلقى الله تعالى غداً مسلماً فليحافظ على هؤلاء الصلوات حيث ينادى بهن ، فإن الله شرع لنبيكم ﷺ سنن الهدى ، وإنهن من سنن الهدى ولو أنكم صليتم في بيوتكم كما يصلي هذا المتخلف في بيته لتركتم سنة نبيكم ، ولو تركتم سنة نبيكم لضللتم ، ولقد رأيتنا وما يتخلف عنها إلا منافق معلوم النفاق ، ولقد كان الرجل يؤتى به يتهادى بين الرجلين حتى يقام في الصف » وفي رواية له قال : « إن رسول الله ﷺ علمنا سنن الهدى : الصلاة في المسجد الذي يؤذن فيه »

**"Anaependezewa akutane na ALLAH Mtukufu kesho (siku ya Qiyama) hali ya kuwa ni Muislamu basi azihifadhi hizi Swala wakati zinaponadiwa. Hakika ALLAH amemwekea Mtume wenu nyendo za uongofu, na hizo (Swala) ni miongoni mwa nyendo za uongofu. Lau nyinyi mtaswali majumbani mwenu kama anavyoswali huyu anaebakia nyuma nyumbani mwake mtakuwa mumeiwacha sunna ya Mtume wenu. Na lau mtawacha Sunna ya Mtume wenu mtapotea. Tulikua tukiona hakuna anaeiwacha Swala ya jamaa ela mnafiki ajulikaniwae unafiki wake. Alikuwa mtu akiletwa ilihali amewaegemea watu wawili hata asimamishwe katika safu."**

Na katika riwaya nyingine amesema:
**"Hakika Mtume (S.A.W.) ametufundisha mienendo ya uongofu: Swala katika Msikiti ambao huadhiniwa ndani yake."** (Muslim).

## FADHILA YA SWALA YA JAMAA:

Swala ya jamaa fadhila zake ni kubwa na ujira wake ni adhimu. Zimekuja Hadithi nyingi zijulishazo jambo hilo miongoni mwazo ni:

1. Imepokewa kutoka kwa Ibnu Umar (R.A.) kuwa Mtume (S.A.W.) amesema:

« صلاة الجماعة أفضل من صلاة الفذ بسبع وعشرين درجة »

**"Swala ya jamaa ni bora kuliko Swala ya upweke kwa daraja ishirini na saba."** (Muttafaq).

2. Abu Huraira (R.A.) amesema: Mtume (S.A.W.) amesema:

« صلاة

الرجل في جماعة تزيد عن صلاته في بيته ، وصلاته في سوقه(٤) بضعاً وعشرين درجة ، وذلك أن أحدهم إذا توضأ فأحسن الوضوء ثم أتى المسجد لا ينهزه(٥) إلا الصلاة . لا يريد إلا

الصلاة ، فلم يخط خطوة إلا رفع له بها درجة وحط عنه بها خطيئة حتى يدخل المسجد ، فإذا دخل المسجد كان في الصلاة ما كانت الصلاة هي تحبسه والملائكة يصلون على أحدكم ما دام في مجلسه الذي صلى فيه يقولون : اللهم ارحمه اللهم اغفر له اللهم تب عليه . ما لم يؤذ فيه ما لم يحدث فيه »

**"Mtu kuswali kwa jamaa (ujira wake) huzidia kuswali nyumbani kwake na kuswali sokoni kwake kwa daraja zaidi ya ishirini. Nako ni kuwa mmoja wao anapotawadha kwa uzuri kisha akaenda Msikitini, hakuna lililomuinua ela ni Swala tu, hakusudii ela Swala, basi (atakua) hakuinua hatua ispokua atainuliwa daraja kwa hatua hiyo na ataondolewa dhambi kwa hatua hiyo mpaka aingie Msikitini. Atakapoingia Msikitini atakua angali yu katika Swala maadamu Swala ndio inayomzuilia. Na Malaika humwombea Rehema mmoja kati yenu maadamu yuko katika kikao chake alichoswalia, wanasema":**

اللهم ارحمه اللهم اغفرله اللهم تب عليه

**"Ewe Mola mrehemu, ewe Mola msamehe, ewe Mola mkubalie toba yake." (Hali inaendelea namna hiyo) maadamu hajaudhi wala hajapatwa na hadathi."** (Muttafaq).

## KUSWIHI JAMAA KWA MMOJA PAMOJA NA IMAMU:

**Swala ya jamaa huswihi kwa mtu mmoja pamoja na Imamu, awe (huyo Maamuma) ni mtoto au mwanamke. Na kila idadi inapozidi kuwa nyingi katika Swala ya jamaa inapendeza zaidi mbele ya ALLAH Mtukufu.**

**- Ibnu 'Abbas (R.A.) amesema: "Nililala kwa khalati yangu**

**Maimuna. Mtume (S.A.W.) akasimama kuswali Swala ya usiku nami nikasimama kuswali pamoja nae. Nikasimama kushotoni mwake akakishika kichwa changu na akanisimamisha kuliani mwake."** (Muttafaq).

- Abu Said Al-Khudry na Abu Huraira (R.A.) wamesema: Mtume (S.A.W.) amesema:

« من استيقظ من الليل وأيقظ أهله فصليا ركعتين جميعاً كتبا من الذاكرين الله كثيراً والذاكرات »

**"Atakaeinuka usiku na akamwamsha ahli yake, wakaswali rakaa mbili wote wawili, wataandikiwa miongoni mwa wenye kumtaja ALLAH kwa wingi katika wanaume na wanawake."** (Abudaud na Haakim).

- Imepokewa kutoka kwa Abu Said Al-khudry (R.A.) kuwa, mtu mmoja aliingia Msikitini na Mtume (S.A.W.) ameshawaswalisha Maswahaba zake. Mtume (S.A.W.) akasema: **"Na nani atakaemtolea huyu sadaka aswali pamoja naye?"** Akainuka mtu katika watu na akaswali pamoja naye.(Ahmad, Abu Daud na Tirmidhy).

- Ubayyi bin Ka'bi (R.A.) amesema:
Mtume (S.A.W.) amesema:

« ... صلاة الرجل مع الرجل أزكى(١) من صلاته وحده وصلاته مع الرجلين أزكى من صلاته مع الرجل وما كان أكثر فهو أحب إلى الله تعالى »

**"......Swala ya mtu kuswali pamoja na mtu ina ujira mkubwa zaidi kuliko kuswali peke yake. Na mtu kuswali pamoja na watu wawili ina ujira mkubwa zaidi kuliko kuswali pamoja na mtu mmoja. Na Swala inayokuwa na watu wengi ndiyo inayopendeza zaidi mbele ya ALLAH Mtukufu."** (Ahmad, Abu Daud na Nasai).

## WANAWAKE KUHUDHURIA MISIKITINI NA UBORA WA SWALA ZAO MAJUMBANI MWAO:

Yafaa kwa wanawake kwenda Misikitini na kushuhudia Swala za jamaa, kwa sharti wajiepushe na yatakayo sababisha shahawa (matamanio) na yanayopelekea katika fitna kutokana na mapambo na manukato.

Mtume (S.A.W.) amesema:

لا تمنعوا إماء الله مساجد الله وليخرجن تفلات

**"Msiwakataze wajakazi wa ALLAH (kuenda katika) Misikiti ya ALLAH. Na watoke bila ya kujitia manukato."** (Ahmad na AbuDaud).

Pia akasema:

« أيما امرأة أصابت بخوراً فلا تشهد معنا العشاء الآخرة »

**"Mwanamke yeyote atakaejifukiza, asishuhudie pamoja nasi isha ya mwisho."** (Muslim).

Pia akasema:

« أيما امرأة تطيبت ثم خرجت إلى المسجد لم تقبل لها صلاة حتى تغتسل »

**"Mwanamke yeyote atakaejitia manukato kisha akatoka akaenda Msikitini Swala yake haitokubaliwa mpaka aoge."** (Ibnu Maajah).

Na akasema tena:

« لا تمنعوا نساءكم المساجد وبيوتهن خير لهن »

**"Msiwazuie wanawake wenu kuenda Misikini. Na nyumba zao ni bora kwao."** (Ahmad, Abu Daud na Haakim).

Pia akasema:

« خير مساجد النساء قعر بيوتهن »

**"Bora ya Misikiti ya wanawake ni ndani ya majumba yao."** (Ahmad na Bayhaqy)

# SWALA YA IJUMAA

Hukumu yake:

Swala ya Ijumaa ni waajib kwa wanaume, nayo ni rakaa mbili.

Dalili zake ni:

1. Kauli yake ALLAH:

﴿ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا إِذَا نُودِيَ لِلصَّلَاةِ مِنْ يَوْمِ الْجُمُعَةِ فَاسْعَوْا إِلَىٰ ذِكْرِ اللَّهِ وَذَرُوا الْبَيْعَ ذَٰلِكُمْ خَيْرٌ لَكُمْ إِنْ كُنْتُمْ تَعْلَمُونَ ﴾

**"Enyi mlioamini! Ikiadhiniwa Swala siku ya Ijumaa nendeniupesi kwenye dhikri ya ALLAH, na wacheni biashara. Hayo ni bora kwenu lau kama mnajua."** (62:9).

2. Kauli yake Mtume (S.A.W.):

« لينتهين أقوام عن ودعهم الجمعات أو ليختمن الله على قلوبهم ثم ليكونن من الغافلين »

**"Watu watakoma kuacha kwao Swala za Ijumaa, au ALLAH Atapiga muhuri juu ya nyoyo zao, halafu watakua katika walioghafilika."** (Muslim).

3. Kauli yake Mtume (S.A.W.):

« لقد هممت أن آمر رجلاً يصلي بالناس ثم أحرق على رجال يتخلفون عن الجمعة بيوتهم »

**"Hakika nilikuwa na hamu nimwamuru mtu awaswalishe watu kisha niwachome wanaume wanaokaa majumbani mwao wakiiwacha Swala ya Ijumaa."** (Muslim).

4. Kauli yake Mtume (S.A.W.):

« الجمعة حق واجب على كل مسلم في جماعة إلا أربعة : عبد مملوك أو امرأة أو صبي أو مريض »

**"Swala ya Ijumaa ni wajibu juu ya kila Muislamu kwa jamaa. Ela kwa watu wanne: Mtumwa aliemilikiwa, mwanamke, mtoto au mgojwa."** (Abu Dau na Hakim).

5. Ijmai. Wameafikiana Muaulamaa wote kuwa Swala ya Ijumaa ni waajib.

## UBORA WA SIKU YA IJUMAA:

Siku ya Ijumaa ni siku yenye Baraka yenye cheo kikubwa, bwana wa masiku na ni bora zaidi.

Kuhusu siku hiyo, amesema mkweli mwenye kusadikiwa (S.A.W.):

« خير يوم طلعت فيه الشمس يوم الجمعة فيه خُلق آدم ، وفيه أهبط ، وفيه تيب عليه ، وفيه مات ، وفيه تقوم الساعة ، . . . وفيه ساعة لا يصادفها عبد مسلم يصلي يسأل الله حاجة إلا أعطاه إياها »

**"Siku bora iliyotokewa na juwa ni siku ya Ijumaa, katika siku hiyo aliumbwa Aadam, katika siku hiyo akakubaliwa toba yake katika siku hiyo alikufa, katika siku hiyo Qiyama kitasimama .... na katika siku hiyo muna saa ambayo, hakuna mja yoyote Muislamu atakayeisadifu akawa yuwaswali akimwomba ALLAH haja yeyote, ela ALLAH atamtekelezea haja hiyo."** (Abu Daud, Tirmidhy, Nasai na wengineo).

## YANAYOPENDEKEZWA NA ADABU ZA SIKU YA IJUMAA:

1. Kuoga, kujipamba, kujitia manukato na kupiga msuwaki. Mtume (S.A.W.) amesema:

«غسل الجمعة واجب على كل محتلم»

**"Kuoga siku ya Ijumaa ni wajibu kwa kila aliebaleghe."** (Muttafaq).

Na akasema:

« غسل يوم الجمعة على كل محتلم وسواك ويمس من الطيب ما قدر عليه »

**"Kuoga siku ya Ijumaa ni kwa kila aliebaleghe, na kupiga msuwaki. Na ajipake manukato kiasi awezacho."** (Abu Daud na Ibnu Maajah Muttafaq)

Pia akasema:

« ما على أحدكم أن وجد سعة أن يتخذ ثوبين ليوم

الجمعة سوى ثوبي مهنته »

**"Mmoja wenu atakapokua na wasaa basi avae nguo mbili (makhsusi) kwa ajili ya siku ya Ijumaa zisizokuwa zile nguo za kazi yake."** (Al-Bazzaar, Abu Daud na Ibnu Maajah).

Katika shani ya siku ya Ijumaa Mtume (S.A.W.) amesema:

« حق كل مسلم السواك

وغسل يوم الجمعة وأن يمس من طيب أهله إن كان »

**"Ni haki kwa kila Muislamu kupiga msuwaki na kuoga siku ya Ijumaa. Na ajipake mafuta ya ahli yake (mkewe) yakipatikana."** (Al-Bazzaar).

2. Kuenda Msikitini mapema kwa ajili ya kuhudhuria Swala ya Ijumaa, aende kabla ya kuingia wakati wa Swala.

Mtume (S.A.W.) amesema:

« من اغتسل يوم

الجمعة غسل الجنابة ثم راح في الساعة الأولى فكأنما قرب بدنة ،
ومن راح في الساعة الثانية فكأنما قرب بقرة ، ومن راح في الساعة
الثالثة ، فكأنما قرب كبشاً أقرن ، ومن راح في الساعة الرابعة
فكأنما قرب دجاجة ، ومن راح في الساعة الخامسة فكأنما قرب
بيضة ، فإذا خرج الإمام حضرت الملائكة يستمعون
الذكر »

**"Atakaeoga siku ya Ijumaa - kama anavyooga janaba - kisha**

**akaenda (Msikitini) katika saa ya kwanza, basi ni kama aliekurubisha ngamia. Atakaeenda saa ya pili atakuwa ni kama aliekurubisha ng'ombe. Atakaeenda saa ya tatu atakuwa ni kama aliekurubisha kondoo mwenye pembe. Atakaeenda saa ya nne atakuwa ni kama aliekurubisha kuku, na atakaeenda katika saa ya tano, atakuwa ni kama aliekurubisha yai. Imamu atakapotoka (kupanda juu ya mimbar) Malaika huhudhuria ili kusikiliza dhikri (khutba)."** (Muttafaq).

3. Kuswali Sunna kabla ya Swala ya Ijumaa, katika Msikiti maadamu Imamu hajatoka. Ispokua tahiyyatulmasjid, kwani utaiswali hata kama Imamu yuwatoa khutba, pamoja na kuzikhafifisha.

Mtume (S.A.W.) amesema:

« لا يغتسل رجل يوم الجمعة ويتطهر بما استطاع من طهر ويدهن من دهنه أو يمس من طيب بيته ثم يروح إلى المسجد ولا يفرق بين اثنين ثم يصلي ما كتب له ثم ينصت للإمام إذا تكلم إلا غفر له من الجمعة إلى الجمعة الأخرى ما لم يغش الكبائر »

**"Mtu hataoga siku ya Ijumaa, akajitwahirisha kiasi anavyoweza kujitwahirisha kutokana na utwahara, akajipaka mafuta yake au akajitia manukato ya nyumbani mwake, halafu akaswali rakaa mbili alizojaaliwa kisha akanyamaza kumsikiliza Imamu anapozungumza isipokuwa atasemehewa kuanzia Ijumaa mpaka Ijumaa nyingine maadamu hajayaendea madhambi makubwa."** (Bukhari).

Na kauli yake Mtume (S.A.W.):

« إذا جاء أحدكم يوم الجمعة والإمام يخطب فليصل ركعتين وليتجوز فيهما »

**"Atakapokuja mmoja wenu siku ya Ijumaa na Imamu yuwakhutubu basi aswali rakaa mbili na azifupishe."** (Muttafaq).

4. Ni makruhu kuwaruka shingo walioketi, na kuwafarikisha. Kwa dalili ya kauli yake Mtume (S.A.W.) - kumwambia yule aliemuona akiruka shingo za walioketi: **"Keti, hakika umeshaudhi na umechelewa."** (Ahmad, Abu Daud na Nasai).

Na kauli yake Mtume (S.A.W.) - katika Hadithi iliotangulia: **"....Wala asifarikishe baina ya watu wawili .... isipokuwa atasamehewa kuanzia Ijumaa mpaka Ijumaa nyingine."**

5. Kukata mazungumzo, kucheza na tasubihi na mfano wake, wakati Imamu atakapotoka.

Mtume (S.A.W.) amesema:

« إذا قلت لصاحبك يوم الجمعة والإمام يخطب

أنصت فقد لغوت »

**"Utakapomwambia mwenzako siku ya Ijumaa na Imamu yuwakhutubu "nyamaza" utakuwa umefanya upuzi."** (Muttafaq).

Na kauli yake (S.A.W.):

« من توضأ فأحسن الوضوء ثم أتى الجمعة

فاستمع وأنصت غفر له ما بينه وبين الجمعة وزيادة ثلاثة أيام ،

ومن مس الحصى فقد لغى »

**"Atakae tawadha kwa uzuri kisha akaiyendea (Swala ya) Ijumaa, akanyamaza na akapulika, atasamehewa baina yake na baina ya Ijumaa (nyingine) na ziada ya siku tatu. Na atakaegusa vijiwe atakuwa amefanya upuzi."**

6. Kuharamishwa kuuza na kununua wakati wa kuadhiniwa. Kwa dalili ya kauli yake ALLAH Aliyetakasika: ﴿ ياايها الذين

آمَنُوا إِذَا نُودِيَ لِلصَّلَاةِ مِنْ يَوْمِ الْجُمُعَةِ فَاسْعَوْا إِلَىٰ ذِكْرِ اللَّهِ

وَذَرُوا الْبَيْعَ ﴾

**"Enyi mlioamini Ikiadhiniwa Swala siku ya Ijumaa nendeni upesi**

**kwenye dhikri ALLAH, na wacheni biashara."** (62:9).

7. Kukithirisha kumswalia Mtume (S.A.W.) usiku wa kuamkia Ijumaa na mchana wake.

Mtume (S.A.W.) amesema:

« أكثروا الصلاة علي في يوم
الجمعة فإنه ليس يصلى على أحد يوم الجمعة إلا عرضت علي
صلاته »

**"Kithirisheni kuniswalia siku ya Ijumaa na usiku wa kuamkia Ijumaa. Kwani hakuna yeyote atakaeniswalia siku ya Ijumaa ispokuwa yake hupitishwa kwangu."** (Al-Haakim na Bayhaqy).

**Pia akasema:**

« أكثروا الصلاة علي يوم الجمعة وليلة
الجمعة فمن صلى علي صلاة صلى الله عليه عشراً »

**"Niswalieni kwa wingi siku ya Ijumaa na usiku wa kuamkia Ijumaa. Atakaeniswalia mara moja, ALLAH Atamswalia mara kumi."** (Bayhaqy).

8. Kupendekezwa kusoma Suratul-Kahfi.

Mtume (S.A.W.) amesema:

« من قرأ سورة
الكهف في يوم الجمعة أضاء له من النور ما بين الجمعتين »

**"Atakaesoma Suratul-Kahfi siku ya Ijumaa, itamn'garia nuru baina ya Ijumaa mbili."** (Al-Haakim na Bayhaqy)

9. Kujitahidi katika dua kwa ajili ya kuitafuta saa ya ijaba.

Mtume (S.A.W.) amesema:

« إن في

الجمعة لساعة لا يوافقها عبد مسلم وهو قائم يصلي يسأل الله فيها

خيراً إلا أعطاه إياه »

**"Hakika katika Ijumaa muna saa ambayo, haiyafiki (saa hiyo) mja Muislamu ilihali amesimama yuwaswali, anamwomba ALLAH kheri katika saa hiyo ispokuwa ALLAH Atampa."** (Muslim).

Na saa hiyo ni ya mwisho katika siku ya Ijumaa. Kwa dalili ya kauli yake Mtume (S.A.W.):

« يوم الجمعة ثنتا عشرة ساعة ،

منها ساعة لا يوجد عبد مسلم يسأل الله فيها شيئاً إلا آتاه إياه ،

فالتمسوها آخر ساعة بعد العصر»

**"Siku ya Ijumaa ina masaa kumi na mbili, katika masaa hayo muna saa ambayo hatapatikaniwa mja Muislamu anamwomba ALLAH - katika saa hiyo - kitu chochote ispokuwa ALLAH Atampa. Basi itafuteni wakati wa mwisho baada ya alasiri."** (Abu Daud, Nasai na Haakim).

10. Abu Hureira (R.A.) amesema: Mtume (S.A.W.) amesema:

« خير

يوم طلعت فيه الشمس يوم الجمعة : فيه خُلق آدم ، وفيه

أهبط ، وفيه تيب عليه ، وفيه مات ، وفيه تقوم الساعة ، وما

من دابة إلا وهي مسيخة[٢] يوم الجمعة من حين تصبح حتى

تطلع الشمس شفقاً من الساعة إلا الجن والإنس ، وفيه ساعة لا يصادفها عبد مسلم وهو يصلي يسأل الله حاجة إلا أعطاه إياها »

**"Siku bora inayotokewa na juwa ni siku ya Ijumaa. Ndani ya siku hiyo Aadam ameumbwa, ndani yake akateremshwa, ndani yake akakubaliwa toba, ndani yake akafa, na ndani yake kitasimama Qiyama. Wala hakuna chochote chenye kutambaa ispokuwa ni chenye kusikiliza (kwa kungojea Qiyama) siku ya Ijumaa kuanzia kupambazukiwa hadi jua kuchomoza (siku ya pili) kwa ajili ya kukiogopa Qiyama, ela majini na wanaadamu. Ndani yake muna saa ambayo, hakuna mja Muislamu atakeisadifu saa hiyo naye yuwaswali anamwomba ALLAH haja ispokuwa ALLAH Atamtekelezea haja hiyo."** Ka'bi akauliza hivyo nikila mwaka siku moja? Nikasema (Abu Hureira) bali ni kila Ijumaa. Ka'bi akasoma Taurati, akasema: Amesema kweli Mtume (S.A.W.).

Abu Hureira akasema: Kisha nikakutana na 'Abdullah bin Salaam nikamhadithia mazungumzo yangu niliyozungumza na Ka'bi. Abdullah bin Salaam akasema: Je, umeijua ni saa gani hiyo? Nikasema: Niambie. Akasema: Ni saa ya mwisho katika siku ya Ijumaa. Nikasema: Vipi itakuwa ni saa ya mwisho katika siku ya Ijumaa, ilihali Mtume (S.A.W.) amesema: **"...hatoisadifu mja Muislamu ilihali amesimama yuwaswali"** na wakati huo hauswaliwi? Abdullah bin Salaam akasema: Je, Mtume (S.A.W.) hakusema: **"Anaeketi kwenye majilisi kungojea Swala, basi mtu huyo yuko katika Swala mpaka atakaposwali?" Nikasema: Bali amesema. Akasema: Ni hivyo."** (Abu Daud, Tirmidhy na Nasai).

Pia kumesemwa kuwa saa hiyo (ya ijaaba) ni baina ya Imamu kuketi juu ya mimbari hadi Swala itakapokwisha.

## SHARUTI ZA KUPASA IJUMAA:

Swala ya Ijumaa yapasa kwa kila Muislamu aliyehuru, aliyebaleghe, mzima na ni mwenyeji.

Mtume (S.A.W.) amesema:

« الجمعة حق واجب على كل مسلم في جماعة إلا الأربعة عبد مملوك أو امرأة أو صبي أو مريض »

**"(Swala ya) Ijumaa ni haki iliyopasa kwa kila Muislamu, kwa jamaa ela kwa watu wanne, mtumwa aliyemilikiwa, au mwanamke, au mtoto (ambae hajabaleghe) au mgonjwa."** (Abu Daud na Hakim).

Kwa msafiri, haimpasi Swala ya Ijumaa, kwa sababu Mtume (S.A.W.) alisafiri kwenda Hajj na Jihadi na wala haikunakiliwa kuwa aliswali Swala ya Ijumaa.

Imekuja katika athari kuwa Sayyidna 'Umar bin Al-Khattab (R.A.) alimwona mtu mwenye kipambo cha safari, akamsikia akisema: Lau kama leo si siku ya Ijumaa ningetoka. Sayyidna 'Umar akamwambia: **"Toka, kwani Ijumaa haimzuwii mtu kusafiri."** (Ash-Shaafi, kutoka Musnad yake).

UZINDUSHI: Baadhi ya Ulamaa wanaonelea kuwa, Swala ya Ijumaa inapasa kwa msafiri anapokuwa mwenyeji katika mji.

## SHARUTI ZA KUSWIHI IJUMAA:

Sharuti za kuswihi Swala ya Ijumaa ni:

1. Iswaliwe katika kitongoji au mjini, kwa sababu haikuswaliwa - wakati wa Mtume (S.A.W.) - ela katika miji na vitongoji, wala Mtume (S.A.W.) hakuamuru watu wa mashambani kuiswali Swala ya Ijumaa. Bali haikunakiliwa kutoka kwake - kama tulivyoeleza - kuwa aliiswali safarini.

2. Ikusanye khutba mbili, kama alivofanya Mtume (S.A.W.) na kudumisha. Na kwa kuwa khutba ni miongoni mwa

faida kubwa za Ijumaa, kwa kuwa imekusanya kumtaja ALLAH Aliyetukuka pamoja na kuwaedhea Waislamu, kadhalika kuwanasihi.

## NAMNA YA KUISWALI SWALA YA IJUMAA:

Namna ya kuiswali Swala ya Ijumaa ni imamu atoke baada ya jua kupondoka, apande mimbari na awatolee watu Salamu hata atakapoketi, mwadhini ataadhini kama anavyoadhini adhana ya adhuhuri. Atakapomaliza kuadhini imamu atasimama akhutubu. Ataifungua khutba yake kwa kumhimidi ALLAH na kumsifu, na kumwombea Rehma na Amani mja wake na Mtume wake, ayakataze yaliokatazwa na wao, awavute watu na kuwaogopesha waadi (wa ALLAH) na makemeo (Yake). Halafu ataketi kitako khafifu. Kisha atasimama na kuanza tena khutba, amhimidi na kumsifu ALLAH. Ataendelea na khutba yake kwa mtindo ule ule

(wa kwanza) na kwa sauti ile ile inayofanana na sauti ya mwenye kukhofisha jeshi, hata atakapomaliza pasina kuirefusha. Ataterèmka na mwadhini atakimu Swala. Atawaswalisha watu rakaa mbili, katika rakaa hizo atasoma kwa sauti, yapendekezwa katika rakaa ya kwanza - baada ya kusoma Suratul-Faatiha - asome Surtul-A'laa na katika rakaa ya pili Surtul-Ghaashiyah. Au katika rakaa ya kwanza atasoma Suratul-Jumuah na katika rakaa ya pili Suratul Munaafiquun. Na hapana ubaya ikiwa atasoma sura nyingine zisizokuwa hizo.

## KUSWALI SUNNA KABLA NA BAADA YA IJUMAA:

Imesuniwa mtu kuswali sunna kabla ya Swala ya Ijumaa kiasi itakavyowezekana hadi Imamu atakapo panda juu ya mimbari, wakati huo si sharia kuswali ela Tahiyalul-Masjid kwa atakaeingia Msikitini. Ataziswali ilihali Imamu yuwakhutubu pamoja na kuzikhafifisha - kama tulivyotangulia kueleza pamoja na kutaja dalili zake.

Ama baada ya Swala ya Ijumaa, imesuniwa kuswali rakaa nne au mbili.

Mtume (S.A.W.) amesema:

« مـن كان منكم مصلياً بعد الجمعة فليصل أربعاً »

**"Atakapokua mmoja wenu ni mwenye kuswali baada ya Ijumaa basi na aswali rakaa nne."** (Muslim).

Imepokewa kutoka kwa Ibni 'Umar (R.A.) kuwa:

« أن النبي ﷺ كان يصلي يوم الجمعة ركعتين في بيته »

**"Alikua Mtume (S.A.W.) akiswali rakaa mbili nyumbani mwake siku ya Ijumaa."** (Muttafaq).

Baadhi ya ulamaa wamenena - kulingana na Hadithi hizi - kuwa Muislamu atakae kuswali sunna baada ya Swala ya Ijumaa katika Msikiti basi ataswali rakaa nne, na atakaposwali nyumbani mwake ataswali rakaa mbili.

# SUNNA ZA SWALA ZA RATIBA:

Swala ya sunna imewekwa kwa ajili ya hekima kubwa na siri nyingi, kama vile kuzidishiwa mema, kuinuliwa daraja, kadhalika sunna hizo huziba pengo lililopatikaniwa na kasoro zilizotokea katika Swala za Faradhi. Vile vile katika Swala muna fadhila adhimu na daraja kubwa ambazo hazipatikaniwi katika Ibada nyenginezo.

فعن ربيعة بن كعب الأسلمي خادم رسول الله ﷺ ، قال : كنت أبيت مع رسـول الله ﷺ فآتيه بوضوئه وحاجته فقال : « سلني » فقلت أسـألك مرافقتك في الجنة فقال : « أو غير ذلك » قلت : هو ذاك . قال : « فأعني على نفسك بكثرة السجود »

Rubaiah bin Ka'bi Al-Aslamy mtumishi wa Mtume (S.A.W.) amesema: Nilikuwa nikilala pamoja na mtume (S.A.W.), nikamletea chombo chenye maji ya kutawadhia na kukidhi haja yake. Akasema: **"Niombe."** Nikamwambia: Nakuomba kufwatana nawe Peponi. Akaniuliza: **"Je, una lingine?"** Nikamjibu: Ni hilo tu. Akaniambia: **"Basi nisaidie juu ya nafsi yako kusujudu kwa wingi."** (Muslim).

وعن أبي هريرة رضي الله عنه قال : قال رسول الله ﷺ : « ان أول ما يحاسب به العبد يوم القيامة من عمله صلاته فإن صلحت فقد أفلح وأنجح وإن فسدت فقد خاب وخسر فإن انتقص من فريضته شيئا قال الرب عز وجل : « انظروا هل لعبدي من تطوع فيكمل بها ما انتقص من الفريضة ثم تكون سائر أعماله على هذا »

Abu Huraira (R.A.) amesema: Mtume (S.A.W.) amesema: **"Hakika jambo la kwanza litakalohisabiwa kwa mja katika amali yake ni Swala yake. Itakapotengea basi amenali saada na amefaulu, na ikiharibika basi amepita patupu na amekhasirika. Kikipungua kitu katika Faradhi yake, Mola Aliyeshinda na kutukuka atasema: "Tazameni, ikiwa mja wangu ana sunna**

**ajaziwe palipopunguka katika Faradhi."** Halafu amali zake zote zitakuwa kama hii. (Abu Daud, Tirmidhy na wengineo).

## VIGAWANYO VYA SUNNA:

Sunna imegawanyika katika Mutlaq na Muqayad. Mutlaq inatosha kutia niya ya Swala tu. Muqayad inagawanyika sehemu zilizoekwa katika sharia, kufwata Faradhi, pia huitwa 'Sunna za Ratiba', nazo hukusanya Sunna ya Alfajiri, Adhuhuri, Alasiri, Magharibi na Isha. Tutazizungumzia katika misitari hii.

## MLANGO: FADHILA ZA SUNNA ZA RATIBA PAMOJA NA FARADHI:

عن أم حبيبة رضي الله عنها قالت : سمعت رسول الله ﷺ
يقول : ما من عبد مسلم يصلي لله تعالى كل يوم إثنتي عشرة ركعة تطوعاً
غير الفريضة إلا بنى الله له بيتاً في الجنة »

Ummu Habiba (R.A.) amesema: Nilimsikia Mtume (S.A.W.) akisema: **"Hakuna mja yeyote Muislamu, atakaeswali - kwa ajili ya ALLAH Aliyetukuka - kila siku rakaa kumi na mbili za Sunna - zisizo za Faradhi - isipokuwa ALLAH Atamjengea nyumba Peponi."** (Muslim).

## KUBAINISHA SUNNA ZA RATIBA NA KUBAINI UCHACHE NA UKAMILIFU WAKE NA WASTANI

1.

عن أم حبيبة رضي الله عنها قالت : سمعت رسول الله ﷺ
قول : « من صلى في يوم وليلة اثنتي عشرة ركعة بُني له بيت في
الجنة : أربعاً قبل الظهر ، وركعتين بعدها ، وركعتين بعد
المغرب ، وركعتين بعد العشاء ، وركعتين قبل صلاة
الفجر »

Ummu Habiba (R.A.) amesema: Nilimsikia Mtume (S.A.W.) akisema: "**Mwenye kuswali Mchana na Usiku rakaa kumi na mbili, atajengewa nyumba Peponi: Rakaa nne kabla (Swala ya) adhuhuri, rakaa mbili baadae, rakaa mbili baada ya magharibi, rakaa mbili baada ya isha,. na rakaa mbili kabla ya alfajiri.**" (Tirmidhy).

Katika riwaya hii yabainisha na kupambanuwa rakaa kumi na mbili zilizotajwa kwa ujumla katika riwaya ya Muslim iliotangulia.

2.

عن ابن عمر رضي الله عنهما قال : صليت مع رسول الله ﷺ ركعتين قبل الظهر وركعتين بعدها وركعتين بعد الجمعة ، وركعتين بعد المغرب وركعتين بعد العشاء

Ibnu 'Umar (R.A.) amesema: "**Niliswali pamoja na Mtume (S.A.W.) rakaa mbili kabla adhuhuri, rakaa mbili baadae, rakaa mbili baada (ya Swala ya) Ijumaa, rakaa mbili baada magharibi na rakaa mbili baada ya isha.**" (Muttafaq).

3.

وعن عبد الله بن مغفل رضي الله عنه قال : قال رسول ﷺ : « بين كل أذانين صلاة ، بين كل أذانين صلاة ، بين كل أذانين صلاة » قال في الثالثة : « لمن شاء »

'Abdullah bin Mughaffal (R.A.) amesema: Mtume (S.A.W.) amesema : "**Baina ya kila adhana mbili (yaani adhana na iqama) muna Swala baina ya kila adhana mbili muna Swala**" katika mara ya tatu akasema: "**kwa anaetaka.**" (Muttafaq).

4.

وعن أم حبيبة رضي الله عنها قالت : قال رسول الله ﷺ : « من حافظ على أربع ركعات قبل الظهر وأربع ركعات بعدها حرمه الله على النار »

Ummu Habiba (R.A.) amesema: Mtume (S.A.W.) amesema: "**Atakaezihifadhi (kudumu nazo) rakaa nne kabla adhuhuri na**

**rakaa nne baadae, ALLAH Atamharamisha kuingia mtoni."** (Abu Daud na tirmidhy).

5. وعن ابن عمر رضي الله عنهما

عن النبي ﷺ قال : « رحم الله أمرأً صلى قبل العصر أربعاً »

Imepokewa kutoka kwa Ibni 'Umar (R.A.) nae kutoka kwa Mtume (S.A.W.) amesema: **"ALLAH Amrehemu mtu atakaeswali rakaa nne kabla alasiri."** (Abu Dau na Tirmidhy).

## JEDWALI YA IDADI YA RAKAA ZA SWALA

| SWALA | SUNNA ZA KABLIYA | FARADHI | SUNNA ZA BAADIYA |
|---|---|---|---|
| Asubuhi | 2 | 2 | 0 |
| Adhuhuri | 2+2 | 4 | 2 +2 |
| Alasiri | 2+2 | 4 | 0 |
| Magharibi | 2 | 3 | 2 |
| Isha | 2 | 4 | 2 |

**Tazama:** Sunna za ratiba za kabliya na baadiya zilizotajwa katika jedwali hii, zimechujwa kutoka katika mkusanyiko wa Hadithi Swahihi zilizotajwa katika mlango huu.

## WITRI

Zilizotangulia ni Sunna za ratiba zilizosisitizwa kuziswali. Pia muna sunna nyingine ambazo ni Sunna kuziswali, katika hizo ni Witri, nayo ni sunna iliyosisitizwa, haifai kwa Muislamu kuiwacha kwa hali yoyote ile.

Yatakiwa kwa Muislamu aiswali mwisho wa Swala ya Isha. Ataswali rakaa moja inayoitwa Witri.

Mtume (S.A.W.) amesema:

« صلاة الليل مثنى مثنى فإذا خشي أحدكم الصبح صلى ركعة واحدة توتر له ما قد صلى »

**"Swala ya usiku ni rakaa mbili mbili, atakapochelea mmoja wenu kutokeza asubuhi, ataswali rakaa moja, atafanya Witri katika (rakaa) alizoswali."** (Bukhari).

## YANAYOSUNIWA KABLA YA WITRI:

Katika Sunna ni mtu aswali - kabla ya witri - rakaa mbili na zaidi, hadi rakaa kumi, mbili mbili. Hatimaye ataswali witri rakaa moja, kama alivyofanya Mtume(S.A.W.).

Ishaq bin Ibrahim (R.A.) amesema: **"Maana iliyopokewa kuwa 'Mtume (S.A.W.) alikuwa akiswali witri rakaa kumi na tatu", ni kuwa, alikiswali rakaa kumi na tatu usiku pamoja na witri. Yaani jumla ya rakaa zote ni witri, ndio Swala ya usiku ikanasibishwa katika witri."**

Rakaa hizi kumi na tatu, inafaa kuziswali mbili mbili, atapiga salamu kila mwisho wa rakaa mbili, hatimaye rakaa moja kwa tahiyatu na salamu (moja). Kama inavyojuzu kuswali zote kwa tahiyatu mbili na salamu (moja), akaziunga rakaa zote bila ya tahiyatu ela katika rakaa ambayo ni kabla ya rakaa ya mwisho, ataketi tahiyatu kisha asimame katika rakaa ya mwisho aiswali, akae tahiyatu na atoe salamu. Pia yajuzu kuziswali rakaa zote (13) kwa tahiyatu moja na salamu katika rakaa ya mwisho. Njia zote hizo (tatu) zinajuzu na zimepokewa kutoka kwa Mtume (S.A.W.).

Njia ilio bora zaidi ni kutoa salamu katika kila rakaa mbili. Yamkinika kuziswali zote kwa salamu moja iwapo ni kwa udhuru wa uajizi, uzee na mfano wake.

## WAKATI WA WITRI

Ni kuanzia wakati wa Swala ya isha hadi kabla ya alfajiri. Mwisho wa usiku ni bora zaidi kuliko mwanzowe kwa atakaeweza kufanya hivyo. Atakapochelea kutoinuka usiku basi ataiswali kabla ya kulala.

## SWALA YA MGONJWA:

1. Yapasa kwa mgonjwa kuswali Swala ya Faradhi kwa

kusimama, hata kwa kuinama au kuuegemea ukuta, kiguzo au fimbo.

2. Atakapokuwa hawezi kuswali kwa kusimama ataswali kwa kuketi. Na bora zaidi awe ameketi kitako mahali pa kisimamo na rukuu, na aketi kitako cha iftirashi mahala pa kusujudu.

3. Atakapokuwa hawezi kuswali kwa kuketi ataswali kwa ubavu ilihali ya kuelekea Qibla, ubavu wa kulia ni bora kuliko ubavu wa kushoto. Isipomkinika kuelekea Qibla ataswali popote atakapoelekea, wala hatorudisha Swala.

4. Asipoweza kuswali kwa ubavu, ataswali akiwa chali (kwa kishogo), miguu yake ameiyelekeza Qibla. Na bora zaidi akiinue kichwa chake ili aelekee Qibla (kwa uso wake). Asipoweza kuiyelekeza Qibla miguu yake ataswali vyovyote itakavyokuwa, wala hatorudisha Swala.

5. Yapasa kwa mgonjwa arukuu na asujudu. Asipoweza ataashiria kwa kichwa chake kurukuu na kusujudu. Atajaalia sijda iwe ni kuinama zaidi kuliko kurukuu. Akiweza kurukuu bila ya kusujudu, atarukuu wakati wa kusujudu na ataashiria kusujudu, na akiweza kusujudu bila ya kurukuu atasujudu wakati wa kusujudu na ataashiria kurukuu.

6. Atakapokuwa hawezi kuashiria kwa kichwa chake katika kurukuu na kusujudu, ataashiria kwa jicho lake, atalifumba kidogo wakati wa kurukuu na atalifumba zaidi wakati wa kusujudu.

Ama kuashiria kwa kidole - kama wafanyavyo baadhi ya wagonjwa - Sio sahihi, wala sijui asili yake yatoka wapi, si katika Qur'aan na Hadithi wala katika kauli za wenye elimu.

7. Ikiwa ataweza kuashiria kwa kichwa wala hawezi kuashiria kwa jicho, ataswali kwa moyo wake, atanuwia rukuu, sijda, kusimama na kuketi. **"Na kila mtu atapata ujira kiasi alivyonuwiya".**

8. Yapasa kwa kila mgonjwa aiswali kila Swala kwa wakati wake, kiasi awezavyo - kama ulivyotangulia upambanuzi wake. Haifai kuichelewesha Swala kuitoa katika wakati wake. Akiwa ni katika wanaotawadha kwa mashaka, itamjuzia kukusanya kama

msafiri (lakini hatopunguza, fahamu!).

9. Atakapoona thakili kuiswali kila Swala kwa wakati wake, atakusanya baina ya adhuhuri na alasiri na baina ya magharibi na isha. Atakusanya kutanguliza au kuakhirisha (kucheleweslia) kulingana na atakavyosahilikiwa. Akitaka ataitanguliza adhuhuri na alasiri katika wakati wa adhuhuri, au ataziakhirisha katika wakati wa alasiri.

Na akitaka ataitanguliza magharibi na isha katika wakati wa magharibi au ataziakhirisha katika wakati wa isha.

Ama Swala ya alfajiri, haikusanywi na Swala ya kabla yake wala baada yake, kwa sababu wakati wake u pekee.

ALLAH Aliyetukuka amenena:

﴿ أَقِمِ الصَّلَاةَ لِدُلُوكِ الشَّمْسِ إِلَىٰ غَسَقِ اللَّيْلِ وَقُرْآنَ الْفَجْرِ إِنَّ قُرْآنَ الْفَجْرِ كَانَ مَشْهُودًا ﴾

**"Simamisha Swala jua linapopinduka(likienda magharibi) mpaka giza la usiku, na (msiache) Qur'aan ya (Swala ya) alfajiri. Hakika (kusoma) Qur'aan katika (kusali Swala ya) alfajiri kunahudhuriwa (na Malaika)."** (17:78).

*******

# NGUZO YA TATU

# ZAKA

# ZAKA

**Taarifa yake:**

Kilugha ni: usafi, ziada na baraka.

Kiistilahi ni: kiwango kilichopasa kutolewa kwa wenye kustahiki katika mali yalofikilia kiwango maalum kwa sharuti makhsusi.

**Hukmu yake:**

Ni Faradhi kwa kila Muislamu aliemiliki kiwango fulani cha mali kwa sharuti zake. Nayo ni nguzo ya tatu katika Nguzo za Uislamu. Imetajwa pamoja na Swala katika Aya thamanini na mbili (82).

Ufaradhi wake umethubutu katika Qur'aan, Hadithi na ijimai ya Umma.

Katika Qur'aan, ALLAH Amesema:

﴿ خُذْ مِنْ أَمْوَالِهِمْ صَدَقَةً تُطَهِّرُهُمْ وَتُزَكِّيهِم بِهَا ﴾

**"Chukua sadaka (Zaka) katika mali yao, uwasafishe kwa ajili ya hizo (Sadaka zao) na kuwataja kwa vizuri."** (9:103).

Akasema tena:

﴿ وَأَقِيمُوا الصَّلَاةَ وَآتُوا الزَّكَاةَ ﴾

**"Na simamisheni Swala na toeni Zaka."** (2:110).

Ama katika sunna toharifu, ni kauli yake Mtume (S.A.W.):

« بني الإسلام على خمس :

شهادة أن لا إله إلا الله وأن محمداً رسول الله ، وإقام الصلاة وإيتاء الزكاة وحج البيت وصوم رمضان »

**"Uislamu umejengwa juu ya nguzo tano: Kushudia kuwa hapana Mola anayestahiki kuabudiwa kwa haki ispokuwa AL-LAH, na kwamba Muhammad ni Mtume wa ALLAH, kusimamisha Swala, kutoa Zaka, Kuhiji Al-Kaaba na kufunga**

**mwezi wa Ramadhani."** (Muttafaq).

Pia kauli yake Mtume (S.A.W.) katika kumuusia Mu'adh bin Jabal alipompeleka Yemen:

« إنك تأتي قوماً أهل كتاب فادعهم إلى
شهادة أن لا إله إلا الله وأني رسول الله ، فإن هم أطاعوك لذلك
فأعلمهم أن الله عز وجل قد افترض عليهم خمس صلوات في كل يوم
وليلة ، فإن هم أطاعوك فأعلمهم أنه قد افترض عليهم صدقة في
أموالهم تؤخذ من أغنيائهم وترد إلى فقرائهم ، فإن هم أطاعوك لذلك
فإياك وكرائم أموالهم واتق دعوة المظلوم ، فإنه ليس بينها وبين الله
حجاب »

**"Kwa hakika unawaendea watu ambao ni Ahlul-Kitab. Basi waite katika kushuhudia kuwa hakuna Mola anaestahiki kuabudiwa kwa haki ispokuwa ALLAH, na kwamba mimi ni Mtume wa ALLAH. Wakikutii katika jambo hilo, wajulishe kuwa ALLAH Aliyeshinda na kutukuka Amewafaradhia Swala tano katika kila mchana na usiku. Wakikutii katika hilo, wajulishe kuwa Yeye (ALLAH) Amewafaradhia Zaka katika mali yao, inachukuliwa kutoka kwa matajiri wao na kurudishiwa maskini wao. Wakikutii katika hilo, basi tahadhari na utukufu wa mali yao, na uyaogope maapizo ya aliyedhulumiwa, kwani hakuna pazia baina yake na baina ya ALLAH."** (Muttafaq).

## HUKMU YA MWENYE KUZUWIA ZAKA:

Anaekataa kutoa Zaka kwa sababu ya kukanusha ufaradhi wake, basi mtu huyo ni kafiri ametoka katika Uislamu na atauliwa kwa ukafiri. Na anaekataa kuitoa kwa sababu ya ubakhili pamoja na kukubali kuwa ni waajib, basi mtu huyo atapata madhambi kwa kuzuwia, jambo hilo halitamtoa katika Uislamu, lakini itachukuliwa kwa nguvu pamoja na kuaziriwa. Atakapopigana - mbele ya Zaka

- atapigwa hadi atakapoinyenyekea Amri ya ALLAH na kutoa Zaka.

Dalili ya jambo hilo, ni kauli Yake ALLAH: **"Kama wakitubu na wakasimamisha Swala na wakatoa Zaka basi ni ndugu zenu katika Dini."** (9:11).

Na kauli yake Mtume (S.A.W.):

« أُمرت أن أقاتل الناس حتى يشهدوا أن لا إله إلا الله وأن محمداً رسول الله ، ويقيموا الصلاة ، ويؤتوا الزكاة ، فإذا فعلوا ذلك عصموا مني دماءهم وأموالهم إلا بحق الإسلام وحسابهم على الله »

**"Nimeamrishwa kupigana na watu mpaka watakaposhuhudia kuwa hakuna Mola anaestahiki kuabudiwa kwa haki ispokuwa ALLAH, na kwamba Muhammad ni Mtume wa ALLAH, wasimamishe Swala na watoe Zaka. Watakapofanya hivyo, damu zao na mali yao yatahifadhika kutokana nami ela kwa haki ya Uislamu, na hisabu yao iko kwa ALLAH."** (Muttafaq).

Na kwa dalili ya kauli ya Khalifa muongofu Sayyidna Abubakar As-Siddiq katika kupigana na waliokataa kutoa Zaka: **"Wallahi! Lau wangalininyima koo la mbuzi waliokuwa wakimtoa kwa Mtume (S.A.W.), ningaliwapiga vita kwa ajili yake."** (Muttafaq).

## HIKMA YA KUEKWA ZAKA:

Zaka imefanywa kuwa ni Sharia kwa hekima tukufu na malengo makubwa yasiyohesabika kwa wingi. Kama:

1. Kuyasafisha mali, kuyakuza na kuyakinga na maafa kwa baraka ya kumtii ALLAH na kuitukuza Amri Yake.

2. Kuitwahirisha nafsi ya kiuwanadamu kutokana na uduni wa ubakhili, pupa, uroho na tamaa.

3. Kuwasaidia mafukara, kuziba pengo kwa wahitaji na waliokosa.

Kauli yake Mtume (S.A.W.):

« من آتاه الله مالاً فلم يؤد زكاته مثل له يوم القيامة شجاعاً أقرع له زبيبتان يطوقه يوم القيامة ثم يأخذ بلهزمتيه ( يعني شدقيه ) ثم يقول أنا مالك[٢] ، أنا كنزك ثم تلا ﴿ وَلَا يَحْسَبَنَّ الَّذِينَ يَبْخَلُونَ بِمَا آتَاهُمُ اللَّهُ مِنْ فَضْلِهِ هُوَ خَيْرًا لَهُمْ بَلْ هُوَ شَرٌّ لَهُمْ سَيُطَوَّقُونَ مَا بَخِلُوا بِهِ يَوْمَ الْقِيَامَةِ ﴾

**"Atakaepewa mali na ALLAH asitekeleze Zaka yake, siku ya Qiyama atavalishwa nyoka shingoni mwake mwenye upaa na pembe mbili. Nyoka huyo atamuuma kwenye taya zake huku akimwambia: Mimi ndio yale mali yako, mimi ndio ile kanzi yako."** Kisha Mtume akasoma: **"Wala wasione wale ambao wanafanya ubakhili katika yale aliyowapa ALLAH katika fadhila zake kuwa ni bora kwao (kufanya ubakhili huo). La, ni vibaya kwao. Watafungwa kongwa (madude ya kunasa shingoni) za yale waliyoyafanyia ubakhili - siku ya Qiyama."** (3:180).

Kauli yake Mtume (S.A.W.):

« ما من صاحب كنز لا يؤدي زكاته إلا أحمي عليه في نار جهنم فيجعل صفائح فيكوى بها جنباه وجبينه حتى يحكم الله بين عباده في يوم كان مقداره خمسين ألف سنة ثم يرى سبيله إما إلى الجنة وإما إلى النار »

**"Hakuna yeyote mwenye kanzi, akawa haitekelezei Zaka yake ela (kanzi hiyo) itatiwa katika moto wa Jahannam, ifanywe mashata, achomwe nayo katika mbavu zake na kipaji chake, hata ALLAH Atakapohukumu baina ya waja wake katika siku ambayo urefu wake ni miaka elfu hamsini (ya hapa duniani). Hatimaye itaangaliwa njia yake, ima aende Peponi wa ima aende motoni."** (Muslim).

Kauli yake Mtume (S.A.W.):

« يا معشر المهاجرين ! خصال خمس إذا ابتليتم
بهن . وأعوذ بالله أن تدركوهن : لم تظهر الفاحشة في قوم قط
حتى يعلنـوا بها إلا فشـا فيهم الطاعون والأوجاع التي لم تكن
مضت في أسلافهم الذين مضوا ولم ينقصوا المكيال والميزان إلا
أخذوا بالسنين وشدة المؤنة وجور السلطان عليهم ولم يمنعوا زكاة
أموالهم إلا منعوا القطر من السماء ولولا البهائم لم يمطروا ، ولم
ينقضوا عهد الله وعهد رسوله إلا سلط الله عليهم عدواً من
غيرهم فـأخـــذوه بعض مـا كـــان في أيديهـم ، ومـا لم تحـكـم
أئمتهم بكتاب الله عز وجل ويتحروا فيما أنزل الله إلا جعل الله
بأسهم بينهم »

**"Enyi kongamano la Muhajirina! Mambo matano mkionjwa nayo - na najilinda kwa ALLAH kukutana nayo. Hautodhihiri katu uchafu miongoni mwa watu mpaka waudhihirishe ela itaenea miongoni mwao tauni na magonjwa ambayo hayakuwepo katika zama za waliowatangulia. Wala hawatapunguza vipimo na mizani ela watapatwa na ukame, gharama kubwa na ujeuri wa Sultani (Mtawala). Wala hawatazuia Zaka za mali yao ela watanyimwa tone kutoka mbinguni na lau si wanyama wasingalinyeshewa na mvua. Wala hawatatangua ahadi ya ALLAH na ahadi ya Mtume wake ela ALLAH Atasalitisha juu yao adui kutoka sehemu nyingine, wavichukue baadhi ya vile vilivyomo mikononi mwao na wasipohukumu viongozi wao kwa kitabu cha ALLAH Aliyeshinda na Kutukuka na wakayachagua Aliyoteremsha ALLAH, ALLAH Atajaalia ubaya baina yao."** (Ibnu Maajah na **Hakim).**

## ZAKA INAPASA JUU YA NANI?

Zaka inapasa kwa aliyekamilisha sharuti hizi zifwatazo:

1. Uislamu.
2. Kuwa huru.
3. Kumiliki kiwango. Kiwango hicho kiwe kimetoshelezea haja za dharura ambazo hazina budi kwa kila mtu, kama chakula, nguo, maskani, kipando na vifaa vya kazi.
4. Mali kupitiwa na mwaka mzima. Yaani mali yaliofikia kiwango cha Zaka, ispokuwa makulima na matunda, hayasharutishwi kupitiwa na mwaka. Kwa dalili ya kauli Yake ALLAH:

﴿ وَآتُوا حَقَّهُ يَوْمَ حَصَادِهِ ﴾

**"...Na toeni haki yake siku ya kuvunwa kwake."** (6:141).

5. Mali ya Zaka kutoshelezea deni lote au sehemu kubwa anayodaiwa, na pasiwepo baadae mtu atakaemdai.

## SAMPULI ZA MALI YANAYOPASA KUTOLEWA ZAKA NA MENGINEYO:

1. Fedha na dhahabu na mfano wake katika mali ya biashara na yanayokutanishwa na hayo kutokana na madini, mali ya dafina na mfano wake kutokana na karatasi za mali. Kwa kauli Yake ALLAH:

﴿ وَالَّذِينَ يَكْنِزُونَ الذَّهَبَ وَالْفِضَّةَ وَلَا يُنْفِقُونَهَا فِي سَبِيلِ اللَّهِ فَبَشِّرْهُمْ بِعَذَابٍ أَلِيمٍ ﴾

**"Na wale wakusanyao dhahabu na fedha wala hawazitoi katika njia ya ALLAH wape habari za adhabu inayoumiza (inayowangoja)."** (9:34).

Na kauli ya Mtume (S.A.W.):

« ليس فيما دون خمس أواق صدقة »

**"Hakuna Zaka chini ya wakia tano."** (Muttafaq).

Kadhalika kauli yake Mtume (S.A.W.):

وفي الركاز الخمس

**"...Na katika mali ya dafina muna *khumsi* ".** (Muttafaq).

2. Wanyama - nao ni ngamia, n'gombe na mbuzi. Kwa dalili ya kauli yake Mtume (S.A.W.): **"Hakuna mwenye ngamia, n'gombe wala mbuzi, akawa hatoi Zaka zao ela watakuja siku ya Qiyama hali ya kuwa ni wakubwa na ni wanene zaidi ya walivyokuwa, wawe wakimdunga kwa pembe zao na wakimkanyaga kwa kwato zao. Kila wanapomalizika wa mwisho, hurudia tena wa mwanzo, mpaka watu watakapohukumiwa."** (Muttafaq).

3. Matunda na nafaka, kila nafaka inayoekeka, kama vile shayiri, mtama, maharagwe, adesi, mahindi na mfano wake.

Kwa upande wa matunda ni kama tende, zetuni na zabibu. Kwa ushahidi wa kauli Yake ALLAH:

﴿ يَاأَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا أَنْفِقُوا مِن
طَيِّبَاتِ مَا كَسَبْتُمْ وَمِمَّا أَخْرَجْنَا لَكُمْ مِنَ الْأَرْضِ ﴾

**"Enyi mlioamini! Toeni katika vile vizuri mlivyovichuma, na katika vile tulivyowatolea katika ardhi."** (2:267).

Na kauli Yake ALLAH:

﴿ وَآتُوا حَقَّهُ يَوْمَ حَصَادِهِ ﴾

**".... Na toeni haki yake siku ya kuvunwa kwake."** (6:141).

Na kauli ya Mtume (S.A.W.):

« فيما سقت السماء والعيون أو كان عثريا العشر وفيما سقي بالنضح
نصف العشر »

**"Katika (Mazao) yaliyonoshelezwa kwa mvua na mito au yaliyojinwesha yenyewe (kwa mizizi yake), (Zaka yake ni:) fungu la kumi. Na yaliyonoshelezwa kwa kunyunyiziwa (Zaka yake ni:) nusu ya fungu la kumi."** (Muttafaq).

Na kauli yake Mtume (S.A.W.): **"Hakuna Zaka chini ya makapu matano."** (Muttafaq).

## MALI YASOPASA ZAKA:

1. Matunda na mboga, kwani haikuthubutu dalili ya kisharia iliyopasisha Zake yake. Ispokuwa tu, imependekezeshwa kutoa sehemu kuwapa masikini na majirani, kama ilivyoelezwa na ALLAH:

﴿ يَاأَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا أَنْفِقُوا مِنْ طَيِّبَاتِ مَا كَسَبْتُمْ وَمِمَّا أَخْرَجْنَا لَكُمْ مِنَ الأَرْضِ ﴾

**"Enyi mlioamini! Toeni katika vile vizuri mlivyovichuma na katika vile tulivyowatolea katika ardhi."** (2:267).

2. Watumwa, farasi, nyumbu na punda.

Mtume (S.A.W.) amesema:

« ليس على العبد في فرسه وغلامه صدقة »

**"Hapana Zaka juu ya farasi wa mtu na mtumwa wake".** (Muttafaq).

Wala haikupokewa kuwa Mtume (S.A.W.) alichukua Zaka juu ya nyumbu na punda.

3. Mali yasiyofikilia kiwango cha kutolea Zaka. Labuda mtu atoe kama Sadaka. Kwani Mtume (S.A.W.) amesema:

« ليس فيما دون خمسة أوسق صدقة ، وليس فيما دون خمس أواق من الورق صدقة ، وليس فيما دون خمس ذود من الإبل صدقة »

**"Hapana Zaka chini ya makapu matano, Hapana Zaka chini ya wakia tano za fedha na hapana Zaka chini ya ngamia watano."** (Muttafaq).

4. Mali ya kutundika ambayo sio ya biashara kama magodoro na mfanowe. Kadhalika majumba, viwanda na magari.

5. Majohari ya ali kama zumaridi, yakuti, lulu na johari nyenginezo, ispokuwa yatakapokuwa ni ya biashara, hapo Zaka itapasa katika kima chake kama mali ya biashara.

6. Mapambo ya wanawake, iwapo hayakukusudiwa

ispokuwa urembo. Yatakapokusudiwa (kununuliwa) kwa ajili ya urembo na kuweka akiba wakati wa haja, hapo Zaka itapasa. Pamoja na hivyo, ujue kwamba, kutoka katika shaka ni kuyatolea Zaka mapambo ya wanawake kwa kila hali. Kwa dalili ya Hadithi iliyopokewa na Bibi 'Aisha (R.A.) - na Hadithi nyenginezo zenyekinyumechake pia. (Kwa sababu dinari ni dhahabu, sarafu (chenji) kuingia katika maana ya Hadithi hii - alisema:

دخل رسول الله ﷺ فرأى في يدي فتخات من ورق فقال : « ما هذا يا عائشة ؟ » فقلت : صنعتهن أتزين لك يا رسول الله ، قال : « أتؤدين زكاتهن ؟ » قلت : لا أو ما شاء الله ، قال : « هو حسبك من النار»

Mtume (S.A.W.) aliingia, akaziona pete za fedha mkononi mwangu. Akauliza: **"Ni kitu gani hiki ewe 'Aisha?"** Nikanena: Nimezitengeza ili nikupambie, ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu. Akauliza: **"Je, wazitolea Zaka?"** Nikajibu: La, au huzitolea pale apendapo ALLAH. Akasema: **"Yatosha kukuingiza Motoni".** (Abu Daud, Daraqutany na Bayhaqy).

## SHARUTI ZA MALI YANAYOPASA ZAKA NA KUBAINISHA KIWANGO KILICHOPASA NDANI YAKE:

Fedha, dhahabu na mfano wake:

1. Dhahabu: na sharuti yake ni kufikia kiwango cha kutolewa Zaka. Kiwango chake ni dinari ishirini (ni sawa na gramu 85) na kupitiwa na mwaka. Wajibu wa kutoa Zaka ni robo ya fungu la kumi. Yaani katika kila dinari ishirini muna nusu dinari ya Zaka, na kila kinachozidi kitapigiwa hisabu yake.

2. Fedha. Sharuti ya Zaka yake ni kufikia kiwango cha wakia tano (ni sawa na gramu 595) na ipitiwe na mwaka. Wajibu katika fedha hiyo ni kutolewa robo ya fungu la kumi, kama katika dhahabu.

3. Kumiliki fedha na dhahabu: Anaemiliki kiwango kidogo cha dhahabu kisichoweza kufikia kiwango cha kutolewa Zaka na akamiliki fedha vivyo hivyo, atazikusanya pamoja. Zikifikia kiwango cha kutolewa Zaka, atazitolea zote kwa pamoja, kila mojawapo kwa hisabu yake. Kama vile inavyotosheleza kutoa moja ya madini hizo kwa nyingine. Mathalan, anaepaswa kutoa dinari moja, inamjuzuia kutoa dirhamu kumi za fedha, na kinyume chake pia. (Kwa sababu dinari ni dhahabu, sarafu (chenji) ya dinari moja ni dirhamu kumi za fedha).

4. Karatasi za noti: Anaemiliki karatasi za noti kiasi kinacholingana na dhahabu au fedha, zikapitiwa na mwaka, basi atalazimika kutolea Zaka, nayo ni robo ya fungu la kumi. Yaani: (% 2, 5).

5. Mali ya biashara: Anaemiliki mali ya biashara kiasi kinachofikia kutolewa Zaka, yakapitiwa na mwaka, atapiga hisabu mwisho wa mwaka, na atayatolea Zaka yake, nayo ni robo ya fungu la kumi katika kima anachomiliki.

Na kiwango kitolewacho Zaka katika mali ya biashara ni kile kile cha dhahabu na fedha. Kwa hivyo ni juu ya mfanyi biashara kukadiria kiwango cha Zaka kwa mojawapo ya dhahabu na fedha.

6. Madeni: Anayemdai mtu deni analoweza kulipata wakati wowote atakapolidai, analazimika kulijumlisha deni hilo pamoja na mali aliyonayo - pesa taslimu au mali - halafu atoe Zaka mwaka ukifika.

Iwapo hana pesa taslimu ispokua ni lile lile deni tu, deni hilo likawa lafikia kiwango, basi atalitolea Zaka.

Na endapo mtu anamdai mtu mwenye hali nzito, wala hawezi kulipata deni lake wakati wowote autakao, basi Zaka yake atalitolea siku ile atakapolikabidhi. Atalitolea Zaka za mwaka mmoja tu, hata kama lilipitiwa na miaka mingi.

7. Mali ya dafina: Mali ya dafina ni yale yaliokuwa yakizikwa wakati wa jahiliya. Atakaepata katika ardhi yake au nyumba yake mali yaliyozikwa zama za ujahiliya, yampasia kuyatolea Zaka za khumsi kuwapa mafukara, masikini na miradi ya Kheri. Kwa dalili ya kauli yake Mtume (S.A.W.): **"... Na katika mali ya dafina muna khumsi."**

(Muttafaq).

8. Madini: Yanapokuwa madini ni ya dhahabu au fedha, yatatolewa Zaka - ikiwa yamefikiwa kiwango cha kutolewa Zaka. Wala haizingatiwi kupitiwa na mwaka, bali Zaka yake hutolewa pale pale wakati wa kupatikana kwake - mfano wa mavuno - na kiwango chake ni kile kile kiwango cha fedha na dhahabu.

Je, (madini hayo) atayatolea Zaka ya robo ya fungu la kumi au khumsi kama mali ya dafina?

Anaesema kuwa madini Zaka yake ni khumsi, atakuwa ameyakisia kwa mali ya dafina. Na anaesema kuwa Zaka yake ni robo ya fungu la kumi, atakuwa amechukwa katika Hadithi isemayo: **"Hakuna Zaka chini ya wakia tano."** (Muttafaq).

Basi kauli yake: **"..Wakia tano"**, imekusanya madini na vyengine.

Kwa hivyo katika jambo hili muna wasaa, walillahil-hamdu!

Amma madini yatolewayo yakiwa ni chuma, shaba, petroli au kibiriti basi hupendekezwa kutolea Zaka katika kima chake kwa mnasaba ule ule wa robo ya fungu la kumi. Kwa sababu haikupokewa nasi Sarahा katika kupasa Zaka ndani yake, wala vitu hivyo si katika dhahabu na fedha hata vikawajibika kutolewa Zaka.

9. Mali yanayopatikaniwa faida ndani yake: Iwapo mali yanayoleta faida ni faida ya biashara au ni tija ya wanyama, mwenyewe atayatolea Zaka katika Zaka ya asili yake. Wala haingojewi kupitiwa na mwaka. Ambae katika mali yake ya biashara au wanyama, kunafikilia kiwango cha kutolea Zaka, mali yakaleta faida na wanyama wakazaana katikati ya mwaka, itapasa kwa wote kutoa Zaka.

Amma mali inayoleta faida yakiwa si katika faida ya biashara au tija ya wanyama, atangojea mwaka mzima kisha ayatolee Zaka.

Na atakaefaidi mali kwa kupewa bure au kwa mirathi, **hatatoa Zaka mpaka yapitiwe na mwaka.**

## b. WANYAMA NAO NI:

1. **Ngamia:** Kupasa Zaka zake ni sharti kufikia kiwango. Kiwango chake ni ngamia watano na kuendelea.

Mtume (S.A.W.) amesema: **"Hakuna Zaka chini ya ngamia watano."** (Muttafaq).

Kiwango kinachopasa katika ngamia watano ni mbuzi jadhaa, aliyekamilisha (umri wa) mwaka akaingia mwaka wa pili, awe ni kondoo au mbuzi.

Katika ngamia kumi, Zaka yake ni mbuzi wawili, katika ngamia kumi na tano Zaka yake ni mbuzi watatu na katika ngamia ishirini Zaka yake ni mbuzi wanne.

Katika ngamia ishirini na tano, Zaka yake ni ngamia bintimakhadhi, naye ni aliyekamilisha mwaka na kuingia mwaka wa pili. Asipopatikana (ngamia bintimakhadhi) basi binlabuni atatosheleza, naye ni (fahali la ngamia) aliyekamilisha miaka miwili na kuingia mwaka wa tatu.

Wakifikia ngamia 36, Zaka yake ni ngamia bintilabuni (koo la ngamia aliyekamilisha umri wa miaka miwili na kuingia watatu).

Wakifikia ngamia 46, Zaka yake ni hikka, naye ni ngamia aliyekamilisha miaka mitatu na kuingia mwaka wa nne.

Wakifikia ngamia 61 Zaka yake ni jadhaa, aliyekamilisha miaka minne na kuingia mwaka wa tano.

Wakifikia ngamia 76, Zaka yake ni bintilabuni wawili.

Wakifikia ngamia 91 hadi 120, Zaka yake ni hikka wawili.

Watakapozidi ngamia 120, basi katika kila ngamia arubaini atatoa bintilabuni mmoja, na katika kila hamsini atatoa hikka mmoja.

2. **N'gombe:**

Sharuti yake ni kama ya ngamia, kufikia kiwango cha kutolewa Zaka, kupitiwa na mwaka na wawe wanachungwa.

Kiwango cha n'gombe ni kufikia vichwa thalathini, Zaka yake ni ndamatabii au ndamatabia mwenye mwaka mmoja. (Ndamatabii na ndamatabia ni fahali au koo la n'gombe mwenye mwaka mmoja).

Wakifikia n'gombe arubaini Zaka yake ni Musinna, koo la

ng'ombe aliyekamilisha miaka sita.

Wakifikia n'gombe sitiini, Zaka yake ni ndamatabii au ndamatabia wawili.

Watakapozidi, basi katika kila n'gombe 40, Zaka yake ni Musinna. Na katika kila n'gombe 30, Zaka yake ni ndamatabii. Na katika n'gombe sabiini: Musinna na ndamatabii, na n'gombe 80, Zaka yake ni Musinna wawili. Na n'gombe 90, Zaka yake ni ndamatabii watatu. Na katika n'gombe 100, Zaka yake ni Musinna mmoja na ndamatabia wawili ... na kuendelea. Kwa dalili ya Hadithi ya Mu'adh(R.A.) aliposema:

« بعثني رسول الله ﷺ أصدق أهل اليمن فأمرني أن آخذ من البقر من كل ثلاثين تبيعاً ومن كل أربعين مسنة »

**"Mtume (S.A.W.) alinituma kuchukua Zaka za watu wa Yemen. Akaniamuru nichukue ndamatabii katika kila n'gombe 30, na nichukue Musinna katika kila n'gombe 40."** (Ahmad, Abu Daud, Tirmidhy na wengineo).

2. Mbuzi na kondoo: Sharuti yake ni kupitiwa na mwaka, kuchungwa na kufikia kiwango cha kutoa Zaka. Kiwango chake ni vichwa 40, Zaka yake ni mbuzi jadhaa. Wakififika 121, Zaka yakeni mbuzi wawili. Wakififikia 201 na kuendelea, Zaka yake ni mbuzi watatu. Wakizidi 300, katika kila mia muna mbuzi mmoja. Kwa dalili ya Hadithi ya Sayyidna Abubakar (R.A.): **"...Na katika mbuzi wanaochungwa, wanapokuwa 40, Zaka yake ni mbuzi (mmoja) ... Watakapozidi 300, basi katika kila mia muna mbuzi mmoja mmoja."** (Ahmad, Abu Daud na wengineo).

## c. MAZAO YA NAFAKA NA MATUNDA:

Zaka inapasa katika mazao yanapokua tayari. Na inapasa katika matunda yanapoanza kutengea, kwa namna yanavyoweza kuwa ni matunda yanayowezekana kuliwa. Kutengea kwa kila kitu kuna aina yake ya kujulikana, kwa mfano, kutengea tende aina ya balah ni

# JEDWALI

## ZAKA ZA WANYAMA WANAOCHUNGWA WENYE MIGUU MINNE

| N'GOMBE | | |
|---|---|---|
| Kiwango | | Zaka yake |
| kuanzia | Hadi | Zaka yake |
| 30 | 39 | Ndamatabii au Ndamatabia |
| 40 | 59 | Musinna |
| 60 | | Ndamatabia wawili |

Kisha katika kila n'gome 30 : ndamatabii mmoja. Na katika kila n'gombe 40:Musinna mmoja.

| NGAMIA | | |
|---|---|---|
| Kiwango | | Zaka yake |
| kuanzia | Hadi | Zaka yake |
| 5 | 9 | Mbuzi |
| 10 | 14 | Mbuzi wawili |
| 15 | 19 | Mbuzi watatu |
| 20 | 24 | Mbuzi wanne |
| 25 | 35 | Bintimakhadhi |
| 36 | 45 | Bintilabuni |
| 46 | 60 | Hikka |
| 61 | 75 | Jadhaa |
| 76 | 90 | Bintilabuni 2 |
| 91 | 120 | Hikka 2 |
| 121 | | Bintilabuni 3 |

Halafu katika kila Ngamia 40: bintilabuni mmoja. Na katika kila ngamia 50: Hikka mmoja

| MBUZI | | |
|---|---|---|
| Kiwango | | Zaka yake |
| Kuanzia | Hadi | Zaka yake |
| 40 | 120 | Mbuzi |
| 121 | 200 | Mbuzi 2 |
| 201 | | Mbuzi 3 |

Kisha, katika kila Mbuzi 100: Mbuzi mmoja

kuwa nyekundu au manjano, kutengea zabibu ni kuchuruzika utamu wake na kuendelea.

Dalili ya kupasa Zaka za hayo tuliyoyataja ni kauli Yake ALLAH:

﴿ وَآتُوا حَقَّهُ يَوْمَ حَصَادِهِ ﴾

**"…. Na toeni haki yake siku ya kuvunwa kwake…".** (6:141).

Kiwango cha kutolewa Zaka katika nafaka na matunda ni kuanzia Makapu matano. Kapu moja ina pishi sitiini. Na pishi ni vibaba vinne, kwa ushahidi wa kauli ya Mtume (S.A.W.): **"Hakuna Zaka chini ya makapu matano."** (Muttafaq). Hivyo basi, kiwango cha Zaka katika tende, zabibu, kunde, mchele, shayiri na mfano wake ni pishi 300 kwa pishi ya Mtume (S.A.W.), nayo ni mateko manne yalojaa katika mikono ya mtu aliyekamilika kimaumbile.

Wajibu katika nafaka na matunda ikiwa yananyunyiziwa maji bila ya gharama - kama kumea yenyewe au kwa maji ya mito na chemchemi - ni kutolewa fungu la kumi, yaani katika makapu matano atoe nusu kapu. Na ikiwa yananyunyiziwa maji kwa gharama - kama kunyunyiziwa kwa ndoo na vibarua na mfano wake (kwa kutumia ndege au helikopta) - Zaka yake ni nusu ya fungu la kumi, yaani katika makapu matano atatoa nusu kapu. Na kila kitakachozidi kitapigiwa hisabu. Kwa maneno ya Mtume (S.A.W.):

« فيما سقت السماء والأنهار والعيون أو كان عثرياً العشر وفيما سقي بالسواني أو النضح نصف العشر »

**"Katika (mazao) yalonoshelezwa kwa mvua, mito na chemchemi au yakamea yenyewe (Zaka yake ni) fungu la kumi. Na katika yalonoshelezwa kwa ngamia au kwa kunyunyiziwa (Zaka yake ni) nusu ya fungu la kumi."** (Muttafaq).

## MASURUFU YA ZAKA:

Zaka hutolewa kwa watu sampuli nane katika kauli ya ALLAH:

﴿ إِنَّمَا الصَّدَقَاتُ لِلْفُقَرَاءِ وَالْمَسَاكِينِ وَالْعَامِلِينَ عَلَيْهَا وَالْمُؤَلَّفَةِ قُلُوبُهُمْ وَفِي الرِّقَابِ وَالْغَارِمِينَ وَفِي سَبِيلِ اللَّهِ وَابْنِ السَّبِيلِ فَرِيضَةً مِنَ اللَّهِ وَاللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ ﴾

**"Sadaka (Zaka) hupewa: Mafakiri, masikini, wanaozitumikia, wanaotiwa nguvu nyoyo zao (juu ya Uislamu), katika kuwapa Uungwana watumwa, kuwasaidia wenye deni, katika (kutengeneza) mambo aliyoamrisha ALLAH na katika (kupewa) wasafiri (walioharibikiwa). Ni Faradhi inayotoka kwa ALLAH, na ALLAH ni Mjuzi (na) Mwenye hikima".** (9:60).

Katika hali ya kuyaweka wazi makundi hayo, ni kama ifwatavyo:

1. Fakiri: ni mtu asiyemiliki mali ya kukidhi haja zake na haja ya anaowalisha kutokana na chakula, kinywaji, mavazi na maskani. Asiwe ni mwenye kupata kitu, au pato lake liwe dogo kuliko nusu ya gharama zake.

2. Masikini: hwenda akawa ana afadhali kuliko fakiri, ispokuwa hukumu zao ni moja. Maskini ni muhitaji katika kila hali. Kama mwenye shillingi mia moja akawa anahitajia shillingi mia mbili.

3. Wanaozitumikia: nao ni ambao, kiongozi au naibu wake amewapa jukumu la kusimamia kazi miongoni mwa kazi za Zaka, kukusanya, au kuhifadhi, au kuzigawa. Kama vile wale wanaozunguka kuzikusanya, wawekahazina, wahasibu, walinzi, wenye kusimamia kuzipeleka huku na kule na kuzigawa na mfano wa hayo. Basi kila mmoja katika hawa ikiwa hapewi mshahara kutoka Baitulmal hupewa Zaka kama ujira wa kazi yake, hata kama ni tajiri.

4. Wanaotiwa nguvu nyoyo zao: anaetiwa nguvu moyo wake, ni Muislamu mwenye Imani dhaifu, na pengine ana kauli kwa jamaa zake, basi hapo hupewa Zaka ili moyo wake uwe na nguvu katika

Uislamu kwa kutarajia manufaa yake kuenea au kuizuwia shari yake. Au pengine mtu yule ni kafiri, yatumainiwa kuwa na Imani au watu wake kuingiwa na Imani, hapo atapewa sehemu katika Zaka ili kumpendekezeshea Uislamu.

5. Kuwapa uungwana watumwa: Muradi katika masurufu haya ya Zaka, ni kumkuta Muislamu ni mtumwa, akanunuliwa kwa mali ya Zaka na kuachwa huru. Au awe ameandikiana (kuwa akitoa kitu fulani atakuwa huru) hapo atapewa Zaka kiasi ya kuziba sehemu ya mkataba wake, ili baadaye awe huru.

**Faida:** Mtumwa ni aliyetekwa katika vita vya kidini baina ya Waislamu na makafiri, basi hapo yeye na wanawe watakuwa watumwa wa mwenye kuwamiliki. Watumwa katika wanawake huitwa vijakazi.

Wala mtumwa sio mtu mweusi, kama baadhi ya watu wanavyofahamu kimakosa. Uislamu umeeka mikakati ya kumwokoa Binadamu kutoka minyororo ya utumwa wa asiekuwa ALLAH. Hivyo tunaona namna unavyojaribu kwa njia zote kuhakikisha jambo hilo. Umefanya kuacha mtumwa huru kuwa na masurufu yake katika Zaka na ukasisitiza mno kuacha watumwa huru.

6. Wenye madeni: Mwenye deni ni yule aliyechukua mzigo wa deni kwa njia isiyokuwa ya kumuasi ALLAH. Awe amekopesha kwa ajili ya nafsi yake katika jambo linalofaa au amekopesha kwa ajili ya jambo lingine kama vile kusuluhisha waliofarikiana. Basi mtu huyu atapewa Zaka kiasi cha kuziba deni lake.

7. Njia ya ALLAH: **"Njia ya ALLAH"** ni njia inayofikisha katika Radhi Zake. Ulamaa wengi wamesema muradi wake hapa ni vita. Watapewa waliojitolea kwenda vitani (katika Jihad), ambao hawana mshahara katika Serikali, wawe ni matajiri au mafukara.

8. Mpita njia: naye ni msafiri aliye mbali na mji wake, akapatwa na mkasa uliomsababishia kuwa fakiri safarini mwake, asiweze kufika katika mji wake. Hapo atapewa Zaka kiasi cha kumsaidia pale ugenini na kumfikisha mjini mwake, hata kama ni tajiri huko kwao. Atapewa Zaka ikiwa hakupata wa kumkopesha

Amma akipata mwenye kumkopesha, atawajibika kukopa.

## FAIDA NA UZINDUSHI:

1. Haifai kuigurisha Zaka katika mji mwingine umbali wa masafa ya kukusuru Swala na zaidi. Kwa dalili ya kauli yake Mtume (S.A.W.) kumwambia Mu'adh alipomtuma kwenda Yemen:

» . . . فإن هم أطاعوك فأعلمهم أنه قد افترض عليهم صدقة في أموالهم تؤخذ من أغنيائهم وترد إلى فقرائهم «

**"....Wakikutii basi wajulishe kuwa wamefaradhiwa Zaka katika mali yao, zinachukuliwa kutoka kwa matajiri wao na kurudishiwa mafukara wao".** (Muttafaq).

2. Yatosheleza kumpa Zaka yeyote katika wale watu sampuli nane. Mali yatakapokuwa mengi basi ni aula kuigawa katika sampuli zote. Na yatakapo kuwa kidogo, basi hutosha kumpa mmoja, pamoja na kumtanguliza aliye muhimu zaidi na mwenye matatizo mengi.

3. Zaka si halali kwa ukoo wa Mtume (S.A.W.) kwa sababu ya sharafu (tashrifa) yao. Nao ni: Bani Hashim yaani ukoo wa 'Ali, 'Aqil, Ja'far, Al-'Abbas na Al-Harith.

Mtume (S.A.W.) amesema:

» إن الصدقة لا تنبغي لآل محمد ﷺ ، وإنما هي أوساخ الناس «

**"Hakika sadaka haiwafai watu wa Muhammad (S.A.W.), kwani ni uchafu wa watu".** (Muslim).

Lakini baadhi ya Ulamaa wameijuzisha iwapo watakuwa wanamatatizo wala hawakupewa fungu la **'Wenye ukuruba'.**

4. Haifai kumpa Zaka ambae chakula chake kimewajibika kwa Muislamu, kama wazazi wawili, watoto na kuteremka., kadhalika mke.

Inajuzu kwa mke kumpa Zaka mumewe masikini. Kwa dalili ya Hadithi ya Abu Said Al-Khudry (R.A.) kuwa:

أن زينب إمرأة

عبد الله بن مسعود قالت : يا نبي الله إنك أمرت اليوم بالصدقة وكـان عنـدي حلي فأردت أن أتصدق به فزعم ابن مسعود أنه وولده أحق من تصدقت عليهم . فقال النبي ﷺ : « صدق ابن مسعود زوجك وولدك أحق من تصدقت به عليهم »

**"Zainab mke wa Abdallah bin Mas'uud alisema: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, leo umeamuru watu watoe sadaka, nami nilikuwa nina mapambo ya dhahabu, nikataka kuyatoa sadaka. Ibnu Mas'uud akadai kuwa yeye na mwanawe wana haki zaidi niwape sadaka. Mtume (S.A.W.) akasema: "Amesema kweli Ibnu Mas'uud. Mumeo na mwanao wana haki zaidi uwape sadaka."** (Bukhari).

5. Zaka haipewi makafiri, mafasiki k.v. wenye kuacha Swala na wenye kuzifanyia stihizai Sharia za Uislamu. Kwa sababu Mtume (S.A.W.) amesema:

« تؤخذ من أغنيائهم وترد إلى فقرائهم »

**"Zinachukuliwa kutoka kwa matajiri wao na kurudishiwa mafukara wao."** (Muttafaq).

Makusudio ni Matajiri na Mafukara wa Waislamu tu. Ispokuwa wenye kutiwa nguvu nyoyo zao.

Kadhalika tajiri na mtu mwenye afiya anaeweza kufanya kazi, hawapewi Zaka.

Mtume (S.A.W.) amesema:

« لاحظ فيها لغني ولا لقوي مكتسب »

**"Hana fungu - katika hiyo Zaka - tajiri wala mwenye nguvu anaefanya kazi".** (Ahmad, Abu Daud na Nasai).

6. Kutoa Zaka ni Ibada miongoni mwa Ibada. Yasharutishwa - katika kuswihi kwake - kutia niya. Mwenye kutoa Zaka atie niya wakati wa kuitoa kuwa ni kwa ajili ya

ALLAH tu, na kutaraji thawabu. Kadhalika anuwie kwa dhati ya moyo wake kuwa akitowacho ni Zaka iliyofaradhiwa juu yake.

Mtume (S.A.W.) amesema:

« إنما الأعمال بالنيات »

**"Hakika kuswihi kwa amali huzingatiwa niya."**

## ZAKA YA FITRI

Ni Zaka inayopasa kwa kufungua mwezi wa Ramadhani.

**Hukmu yake:**

Ni waajib kwa kila mtu kati ya Waislamu, mdogo kwa mkubwa, mume kwa mke, huru kwa mtumwa.

Ibnu 'Umar (R.A.) amesema:

« فرض رسول الله ﷺ

زكاة الفطر من رمضان صاعاً من تمر أو صاعاً من شعير على العبد والحر والذكر والأنثى والصغير والكبير من المسلمين »

**"Mtume (S.A.W.) aliifaradhisha Zaka ya fitri katika mwezi wa Ramadhani. Pishi ya tende au pishi ya shayiri, kwa kila aliye mtumwa, huru, mume, mke, mdogo na mkubwa miongoni mwa Waislamu."** (Muttafaq).

**Hekima yake:**

Miongoni mwa hekima ya Zaka ya fitri ni:

1. Humtwahirisha aliyefunga kutokana na yale ambayo ameyatenda katika Saumu yake, kama kusema na kutenda upuzi na kutamka maneno machafu.

2. Zaka ya fitri huwasaidia mafukara na masikini wasiombe siku ya Idi.

Ibnu 'Abbas (R.A.) amesma:

« فرض رسول الله ﷺ زكاة الفطر

طهرة(١) للصائم من اللغو والرفث وطعمة(٢) للمساكين »

**"Mtume (S.A.W.) ameifaradhisha Zaka ya fitri ili iwe ni utwahirisho wa mwenye kufunga kutokana na upuzi na maneno machafu na ili iwe ni chakula kwa masikini."** (Abu Daud, Ibnu Majah na wengineo).

## INAPASA JUU YA NANI?

Zaka ya fitri inapasa kwa kila Muislamu aliyemiliki kadiri ya pishi inayozidia chakula chake na chakula cha watoto wake, mchana na usiku.

## KIWANGO NA SAMPULI YA CHAKULA KINACHOTOLEWA:

Kiwango cha Zaka ya fitri ni pishi moja. Na pishi ni vibaba vinne. Na kibaba ni teko moja lililojazwa katika viganja vya mtu mwenye viganja vya kawaida.

Zaka hiyo hutolewa kutokana na aghlabu ya chakula wanachokula watu wa mji ule. Ima iwe ni mtama, shayiri, tende, mchele, mahindi, zabibu au maziwa yaliogandishwa.

Abu Said Al-Khudry (R.A.) amesema:

« كنا إذ كان فينا رسول الله ﷺ نخرج زكاة
الفطر عن كل صغير وكبير حر أو مملوك صاعاً من طعام أو صاعاً من
أقط أو صاعاً من شعير أو صاعاً من تمر أو صاعاً من زبيب »

**"Tulikuwa - wakati Mtume (S.A.W.) angali hai - tukimtolea Zaka ya fitri kila aliye mdogo na mkubwa, aliye huru au mtamalakiwa. (Tukitoa) pishi ya chakula, au pishi ya maziwa yalogandishwa, au pishi ya shayiri, au pishi ya tende, au pishi ya zabibu".** (Muttafaq).

## NI LINI YAPASA NA LINI ITOLEWE?

Zaka ya fitri Yapasa kutolewa kuanzia kuzama jua usiku wa kuamkia Idi. Kwa sababu, huo ndio wakati wa fitri ya mwezi wa Ramadhani.

Ama wakati wa kutoa, muna nyakati mbili. Wakati wa kujuzu na wakati wa kutoa wenye fadhila.

Ama wakati wa kujuzu, ni kuitoa kabla ya Idi kwa siku moja au mbili, kwa sababu Ibnu 'Umar na wengineo katika Maswahaba ndivyo walivyofanya.

Na wakati wa kutoa wenye fadhila ni kuanzia kutokeza alfajiri ya siku ya Idi mpaka kabla kidogo ya Swala (ya Idi).

Ibnu 'Umar (R.A.) amesema:

أمرنا رسول الله ﷺ بزكاة الفطر أن تؤدى قبل خروج الناس إلى الصلاة »

**"Mtume (S.A.W.) ametuamuru Zaka ya fitri kutolewa kabla ya watu kutoka kuenda kusali."**

Naafi amesema: **"Ibnu 'Umar alikuwa akiitoa kabla ya Idi kwa siku moja au mbili".**

Katika lafdhi nyingine ya Naafi yasema: **"Alikuwa Ibnu 'Umar akiitoa kwa anayeikubali. Walikuwa wakitoa kabla ya (Idul) fitri kwa siku moja au mbili."** (Muttafaq).

Kadhalika kauli ya Ibnu 'Abbas (R.A.):

« فرض رسول الله ﷺ زكاة الفطر طهرة للصائم من اللغو والرفث وطعمة للمساكين ، من أداها قبل الصلاة فهي زكاة مقبولة ومن أداها بعد الصلاة فهي صدقة من الصدقات

**"Mtume (S.A.W.) amefaradhisha Zaka ya fitri iwe ni utwahirisho wa mwenye kufunga kutokana na upuzi na maneno machafu, na iwe ni chakula kwa masikini. Mwenye kuitoa kabla ya Swala, itakuwa ni Zaka yenye kukubaliwa. Na mwenye kuitoa baada ya Swala basi ni Sadaka (tu) miongoni mwa Sadaka."** (Abu Daud, Ibnu Majah na wengineo).

## MASURUFU YAKE:

Wanaopewa Zaka ya fitri ni wale wapewao Zaka nyingine.

Yaani hugawanywa kwa makundi manane yalotajwa katika kauli yake ALLAH:

﴿ إِنَّمَا الصَّدَقَاتُ لِلْفُقَرَاءِ وَالْمَسَاكِينِ ..... ﴾ الآية ،

**"Sadaka hupewa mafakiri na masikini......"** mpaka mwisho wa Aya. (9:60).

Mafukara na masikini ndio makundi ya muhimu zaidi, kwa ushahidi wa Hadithi iliotangulia: **"Mtume (S.A.W.) amefaradhisha Zaka ya fitri iwe ni utwahirisho wa mwenye kufunga kutokana na upuzi na maneno machafu, na iwe ni chakula kwa masikini."**

*******

# NGUZO YA NNE

# SAUMU

# SAUMU (KUFUNGA)

**Taarifa ya Saumu:**

Saumu, kilugha ni: Kujizuwia.

Kisharia ni: Kujizuwia kula, kunywa, kuingilia wanawake na mengine katika yenye kufunguza. Kuanzia kutokeza alfajiri mpaka kuzama jua, kwa niya ya kujikaribisha kwa ALLAH Mtukufu.

**Fadhila ya Kufunga:**

Linalojulisha fadhila ya kufunga ni Hadithi zifwatazo:

1. Kauli ya Mtume (S.A.W.):

« من صام يوماً في سبيل الله بعد الله وجهه عن النار سبعين خريفاً »

**"Atakaefunga siku moja katika njia ya ALLAH, ALLAH Atauwepusha uso wake na moto miaka sabiini".** (Muttafaq).

2.

« إن في الجنة باباً يقال له الريان يدخل منه الصائمون يوم القيامة لا يدخل منه أحد غيرهم ، فإذا دخلوا أغلق فلم يدخل منه أحد »

**"Hakika Peponi muna mlango uitwao Rayyaan. Wenye kufunga wataingia katika mlango huo siku ya Qiyama, hataingia mlango huo ela ni wao peke yao. Watakapoingia mlango utafungwa, hakuna yeyote atakaengia".** (Muttafaq).

3.

« الصيام جنة(٣) من النار كجنة أحدكم من القتال »

**"Kufunga ni kinga ya motoni, kama vile kinga ya mmoja katika vita".** (Ahmad, Nasai na wengineo).

## HUKUMU YA SAUMU YA RAMADHANI

Saumu ya mwezi wa Ramadhani ni waajib (lazima) kwa ushahidi wa Qur'aan, Hadithi na ijimai.

Ama katika Qur'aan, ni kauli Yake ALLAH:

﴿ شَهْرُ رَمَضَانَ الَّذِي أُنْزِلَ فِيهِ الْقُرْآنُ هُدًى لِلنَّاسِ وَبَيِّنَاتٍ مِنَ الْهُدَىٰ وَالْفُرْقَانِ فَمَنْ شَهِدَ مِنْكُمُ الشَّهْرَ فَلْيَصُمْهُ ﴾

**"(Mwezi huo mlioambiwa mufunge ni) Mwezi wa Ramadhani ambao imeteremshwa katika (mwezi) huo hii Qur'aani ili iwe uwongozi kwa watu, na hoja zilizowazi wa uwongozi na upambanuzi (wa baina ya haki na batili). Atakayekuwa katika mji katika huu mwezi (wa Ramadhani) afunge....".** (2:185).

Katika sunna ni kauli ya Mtume (S.A.W.):

« بني الإسلام على خمس شهادة أن لا إله إلا الله وأن محمداً رسول الله وإقام الصلاة وإيتاء الزكاة وحج البيت وصوم رمضان »

**"Uislamu umejengwa juu ya nguzo tano, kukiri kwa moyo na kubaini kwa ulimi kuwa hapana Mola Anaestahiki kuabudiwa kwa haki ispokuwa ALLAH, na kwamba Muhammad ni Mtume wa ALLAH, kusimamisha Swala, kutoa Zaka, kuhiji Al-Kaaba na kufunga mwezi wa Ramadhani".** (Muttafaq).

Na ama ijmai ni kuwa, Umma wote umeafikiana kuwa Saumu ya mwezi wa Ramadhani ni Faradhi, na ni mojawapo katika Nguzo za Uislamu. Na mwenye kuikanusha ni kafiri ametoka katika Uislamu.

Saumu ya Ramadhani imefaradhiwa mwezi wa Shaabani mwaka wa pili Hijriya.

## FADHILA YA MWEZI WA RAMADHANI:

Mwezi wa Ramadhani una fadhila kubwa zisizopatikana katika miezi mengine. Na Hadithi zifwatazo, zathibitisha jambo hilo.

1. Kauli yake Mtume (S.A.W.):

« الصلوات الخمس والجمعة إلى الجمعة ورمضان إلى

«رمضان مكفرات لما بينهن إذا اجتنبت الكبائر»

**"Swala tano, Swala ya Ijumaa hadi Ijumaa na Ramadhani hadi Ramadhani (yote hayo) ni yenye kufuta dhambi zilizo baina yake,maadamu madhambi makubwa yataepukwa."** (Muslim).

2.

« من صام رمضان إيماناً واحتساباً غفر له ما تقدم من ذنبه »

**"Atakaefunga Ramadhani hali ya kuamini na kutaraji thawabu, atasamehewa dhambi zake zilizotangulia."** (Muttafaq).

## UBORA WA AMALI NJEMA KATIKA MWEZI WA RAMADHANI:

Thawabu za amali njema huongezwa kwa sababu nyingi. Miongoni mwazo ni utukufu na ubora wa zama, kama mwezi wa Ramadhani.

Na zifwatazo ni baadhi tu ya amali njema zinazoongezewa thawabu katika mwezi wa Ramadhani:

1. Kusimama usiku (kwa Ibada). Mtume (S.A.W.) amesema:

« من قام رمضان إيماناً واحتساباً غفر الله له ما تقدم من ذنبه »

**"Atakaesimama Ramadhani ilihali ya kuamini na kutaraji thawabu, ALLAH Atamsamehe dhambi zake zilotangulia."** (Muttafaq).

2. Kufanya 'Umara. Mtume (S.A.W.) amesema:

« عمرة في رمضان تعدل حجة »

**"'Umra katika mwezi wa Ramadhani hulingana na Hija".** (Bukhari).

Kwa jambo gani huthubutu mwezi wa Ramadhani?

Mwezi wa Ramadhani huthubutu kwa mojawapo kati ya mambo mawili:

1. Kuuwona mwezi usiku wa kuamkia tarehe 30 ya mwezi wa Shaabani. Mwezi utakapoonekana, Saumu imeshapasa.

Mtume (S.A.W.) amesema:

« إذا رأيتم الهلال فصوموا ، وإذا رأيتموه فأفطروا »

**"Mkiuwona mwezi fungeni na mkiuwona funguweni".** (Muttafaq).

Mtu mmoja muadilifu hutosheleza kuthibitisha kuonekana mwezi wa Ramadhani.

Ama mwezi wa Shawwal (Mfungo Mosi) hauthubutu ela kwa watu wawili waadilifu.

2. Kuukamilisha mwezi wa Shaabani siku thalathini (30). Itakapotimia siku ya thalathini ya Shaabani, basi siku ya 31 ni mwanzo wa Ramadhani bila matatizo.

Mtume (S.A.W.) amesema (kuikamilisha Hadithi iliotangulia):

« ... فإن غم عليكم فأكملوا العدة ثلاثين يوماً » .

**"...Mtakapoghumiwa (Msiuwone mwezi) kamilisheni hesabu ya siku 30."**

## SHARUTI ZA SAUMU:

Katika sharuti ya kuswihi Saumu ni mtu awe Muislamu, mwenye akili na aliyebaleghe.

Mtume (S.A.W.) amesema:

« رفع القلم عن ثلاثة ، عن النائم حتى يستيقظ وعن الصبي
حتى يحتلم وعن المجنون حتى يعقل »

**"Kalamu imeinuliwa kwa watu watatu: aliyelala mpaka atakapoamka, mtoto hadi atakapobaleghe na mwendawazimu hata atakapokuwa na akili."** (Abu Daud na wengineo).

Na awe Muislamu ni mzima sio mgonjwa, aliye mjini sio msafiri na ni muweza kufunga bila mashaka yenye kupita kiasi.

Na kwa mwanamke, yapasa awe twahara kutokana na hedhi na nifasi.

Mtume (S.A.W.) amesema - katika kubainisha upungufu wa dini ya mwanamke- :

« أليست إذا حاضت لم تصل ولم تصم »

**"Je hakuwa atokwapo na hedhi, haswali wala hafungi?"** (Bukhari).

## WANAORUHUSIWA KULA NA KUPASWA KULIPA:

1. Mgonjwa anaetarajiwa kupoa. Anaruhusiwa kula kisha alipe zile siku alizokula. Na mgonjwa atakapoweza kufunga bila mashaka, atafunga.

ALLAH Amesema:

﴿ وَمَنْ كَانَ مِنْكُمْ مَرِيضًا أَوْ عَلَىٰ سَفَرٍ فَعِدَّةٌ مِنْ أَيَّامٍ أُخَرَ ﴾

**"Na atakaekuwa mgonjwa katika nyinyi au katika safari (akafunga baadhi ya siku), basi (atimize) hisabu katika siku nyingine."** (2:184).

2. Msafiri. Anaposafiri Muislamu masafa ya kukusuru (1) Swala (kupunguza) anaruhusiwa kula na kulipa zile siku alizokula.

Itakapokuwa kufunga safarini hakumpi mashaka na akafunga basi itakuwa ni vizuri. Na atakapoona uzito na akala pia itakuwa ni vizuri.

Abu Sa'id Al-Khudry (R.A.) amesema:

« كنا نغزو مع رسول الله ﷺ في رمضان فمنا الصائم ومنا المفطر فلا يجد(1) الصائم على المفطر ولا المفطر على الصائم ، يرون أن من وجد قوة فصام فإن ذلك حسن ، ويرون أن من وجد ضعفاً فأفطر فإن ذلك حسن »

**"Tulikuwa tukienda vitani pamoja na Mtume (S.A.W.) katika Ramadhani. Basi miongoni mwetu muna wenye kufunga na wenye kula. Wenye kufunga hawawakasirikii wenye kula wala wenye kula hawawakasirikii waliofunga. Walikiona kuwa mwenye kuwa na nguvu akafunga amefanya vizuri na anaepata udhaifu akala pia amefanya vizuri."** (Muslim).

---

(1). Masahaba wengi na Tabiina wameafikiana kuwa masafa ya kukusuru ni burad nne (yaani maili 48). Kadhalika hiyo ndio kauli ya Imam Malik, Shafi, Ahmad na watu wao, kadhalika na Al-Laith bin Sa'd, Al-Awaza'iy, Mafaqihi wa Hadithi na wengineo.

# HUKUMU YA MJAMZITO NA MWENYE KUNYONYESHA:

Imehalalishwa kwa mwanamke Muislamu ale iwapo ni mjamzito au yuwanyonyesha, ikiwa wote hao wanaziogopea nafsi zao tu, au wanawachelea wana wao tu, au wakawa wanazikhofia nafsi zao na watoto wao.

Mtume (S.A.W.) amesema:

« إن الله وضع عن المسافر الصوم وشطر الصلاة وعن الحبلى والمرضع الصوم »

**"Hakika ALLAH Amemwondoshea msafiri Saumu na nusu ya Swala, na Amemwondoshea Saumu mjamzito na mnyonyeshaji."** (Ahmad).

Udhuru utakapoondoka, basi mjamzito au mnyonyeshaji atalipa zile siku alizokula katika hali zote tatu. Na atazidisha - pamoja na kulipa-kutoa fidia katika hali ya pili, nayo ni atakapokua anamkhofia mtoto tu.

Fidia ni kutoa Sadaka ya kibaba cha mtama katika kila siku anayolipa kufunga. Kufanya hivyo inakua ni ukamilifu na kupata ujira mkubwa.

Na hupasa kutoa fidia (ya chakula) pamoja na kufunga iwapo huyo mjamzito na mnyonyeshaji wanawakhofia watoto tu. Hiyo ndiyo Fatwa ya Ibnu 'Abbas na Ibnu 'Umar (R.A.). Kadhalika ndiyo kauli iliyoshikiliwa na Imam Shafi na Imam Ahmad.

Imam Abu Hanifa (R.A.) anaona kuwa, anapaswa kulipa pekee bila ya kutoa chakula.

ALLAH ndiye ajuwae zaidi.

# WANAORUHUSIWA KULA NA KUPASWA KUTOA FIDIA PEKEE:

Wanaoruhusiwa kula ni mtu mzima mume na mke (wasioweza kufunga), mgonjwa asiyetarajiwa kupoa na kila alie katika hukumu ya watu hawa, ambao wanataabishwa mno na Saumu na kupata mashaka mengi katika kipindi chote cha mwaka. Basi wataruhusiwa

kula na walishe kibaba kila siku (ya kufunga) kumpa maskini, wala hawatalipa.

Ibnu Abbas (R.A.) amesema:

« رخص للشيخ الكبير أن يطعم عن كل يوم مسكيناً ولا قضاء عليه ».

**"Imeruhusiwa kwa mzee alishe maskini kwa kila siku, wala hatalipa".** (Daraqutany na Haakim).

## NGUZO ZA SAUMU:

1. Imsaak, nako ni kujizuwia na yote yenye kufunguza, kama kula, kunywa, kujamiiyana na mengineyo.

2. Niya, nayo ni moyo kuazimia kufunga kwa kufwata Amri ya ALLAH Mtukufu au kujikaribisha Kwake.

Mtume (S.A.W.) amesema:

« إنما الأعمال بالنيات »

**"Hakika kuswihi kwa amali huzingatiwa niya."** (Muttafaq).

Ikiwa Saumu ni Faradhi, basi niya inapasa tangu usiku kabla alfajiri.

Mtume (S.A.W.) amesema:

« من لم يجمع الصيام من الليل فلا صيام له »

**"Ambae hakuazimu kufunga tangu usiku, hana Saumu."** (Abu Daud, Tirmidhy na wengineo).

Na iwapo Saumu ni ya sunna, niya itaswihi hata kama ni baada ya kutokeza alfajiri na mchana kupanda, kwa sharti asiwe amekula kitu.

Nana 'Aisha (R.A.) amenena:

دخل علي رسول الله
ﷺ ذات يوم فقال : « هل عندكم شيء ؟ » قلنا : لا ، قال :
« فإني صائم »

**"Siku moja Mtume (S.A.W.) alinijilia, akasema: "Muna kitu?"**

Tukasema: "**Hatuna.**" Akasema: "**Basi nimefunga.**" (Muslim).

3. Zama. Nazo ni: Mchana wa mwezi wa Ramadhani kwanzia kutokeza alfajiri hadi kuzama jua. Kwa dalili ya kauli Yake ALLAH:

﴿ وَكُلُوا وَاشْرَبُوا حَتَّى يَتَبَيَّنَ لَكُمُ الْخَيْطُ الْأَبْيَضُ مِنَ الْخَيْطِ الْأَسْوَدِ مِنَ الْفَجْرِ ثُمَّ أَتِمُّوا الصِّيَامَ إِلَى اللَّيْلِ ﴾

"**Na kuleni na kunyweni mpaka ubainike kwenu weupe wa alfajiri katika weusi wa usiku. Kisha timizeni Saumu mpaka usiku".** (2:187).

## SUNNA ZA SAUMU:

1. Daku. Ni kula na kunywa wakati wa usiku mwingi, mwisho wa usiku kwa niya ya kufunga.

Mtume (S.A.W.) amesema:

« تسحروا فإن في السحور بركة. »

"**Kuleni daku, hakika katika daku muna Baraka.**" (Muttafaq).

2. Kuichelewesha daku hadi sehemu ya mwisho wa usiku maadamu hatachelea kutokeza alfajiri.

Mtume (S.A.W.) amesema:

« لا تزال أمتي بخير ما عجلوا الفطر وأخروا السحور »

"**Umma wangu hautoacha kuwa na kheri maadamu wanaharakisha kufuturu na wanaakhirisha kula daku.**" (Ahmad).

3. Kuharakisha kufuturu atakapohakikisha kuzama jua.

Mtume (S.A.W.) amesema:

« لا يزال الناس بخير ما عجلوا الفطر »

"**Watu hawataacha kuwa katika kheri mwida wakiharakisha kufuturu.**" (Muttafaq).

4. Futari iwe ni tende-tosa au tende (ya kawaida) au maji. Vitu hivyo vimepangwa kwa mpango huo kulingana na ubora wake.

Anas bin Malik (R.A.) amesema:

« كان رسول الله ﷺ يفطر

على رطبات قبل أن يصلي ، فإن لم تكن رطبات فتمرات ، فإن

لم تكن تمرات حسا حسوات من ماء »

**"Mtume (S.A.W.) alikuwa akifuturu kwa tende-tosa kabla kuswali, asipopata tende-tosa akifuturu kwa tende asipopata tende akinywa maji."** (Ahmad, Abu Daud na Tirmidhy).

5. Kuomba dua katika hali ya kufunga, hasa wakati wa kufuturu.

Mtume (S.A.W.) amesema:

« ثلاث

دعوات مستجابات ، دعوة الصائم ودعوة المظلوم ودعوة

المسافر» . ولقول عبد الله بن عمرو بن العاص : قال رسول

الله ﷺ : « إن للصائم عند فطره لدعوة ما ترد » وكان عبد الله

يقول إذا أفطر : اللهم إني أسألك برحمتك التي وسعت كل شيء

أن تغفر لي

**"Dua tatu ni zenye kujibiwa, dua ya mwenye kufunga, dua ya aliyedhulumiwa na dua ya msafiri."** (Baihaqy katika 'Shu'abil-Iman').

Na kauli ya 'Abdallah bin 'Amri bin 'Aas akisema: Mtume (S.A.W.) amesema: **"Hakika Wallahi! Mwenye kufunga wakati wa kufuturi kwake ana dua isorudishwa".**

Na 'Abdallah alikuwa akinena wakati akifuturu: **"Ewe Mola! Hakika nakuomba - kwa Rehema Yako iliyotoshelza kila kitu unisamehe."** (Ibnu Maajah).

## MAKURUHU YA KUFUNGA:

Yakirihishwa kwa mwenye kufunga kufanya mambo yanayopelekea kufisadi Saumu yake. Ingawa mambo hayo hasaa

hayafunguzi Saumu. Nayo ni:

1. Kuendelea sana kusukutua na kupandisha maji puwani wakati wa kutawadha.

Mtume (S.A.W.) amesema:

« وبالغ في الاستنشاق إلا أن تكون صائما »

**"Na upandishe sana maji puwani, ispokua utapokuwa umefunga".** (Abu Daud, Tirmidhy, Nasai na wengineo).

Ili kukhofia maji yasije yakateleza hadi ndani, Saumu ikaharibika.

2. Kubusu (kupiga kiss) kwa awezae kuidhibiti nafsi yake, kadhalika kushikana na kuvaana mwili na mke.

3. Kudumu kumtazama mkeo kwa shahawa, na kufikiri mambo ya kujamiiyana.

4. Kuonja chakula au kinywaji bila udhuru.

5. Kutafuna ubani ili kuhofia isije sehemu fulani ikaponyoka na kwenda ndani.

## YABATILISHAYO SAUMU:

Muna yabatilishayo saumu na ikapasa kulipa peke yake, na muna yabatilishayo saumu kulipa kutoa kafara.

a. Yabatilishayo saumu ikapasa kulipa pekee:

1. Kula na kunywa kwa kukusudia. Ama atakapokuwa amesahau au ametenzwa nguvu hatolipa.

Mtume (S.A.W.) amesema:

« من نسي وهو صائم فأكل أو شرب فليتم صومه فإنما أطعمه الله وسقاه »

**"Atakaesahau naye amefunga akala au akanywa, basi aitimize saumu yake, kwani ni ALLAH ndiye aliyemlisha na kumnywesha."** (Muttafaq).

2. Mwenye kula, au kunywa, au kujimai kwa kudhania kuwa juwa limekuchwa kisha ikambainikia kinyume chake. yaani bado mchana upo.

3. Chochote kilichofika ndani (ya mwili) kwa sababu ya kuendelea sana kusukutua na kupandisha maji puwani ilihali yuwajua kuwa amefunga. Kadhalika kupenyeza chakula hadi ndani kwa kutumia sindano ya chakula inayochangamsha mwili.

4. Kuingiza kisicholiwa kupitia tundu zilizozoeleka - kama mdomo - hadi ndani, mfano wa chumvi nyingi.

5. Kuteremsha manii kwa kujivuta, au kuvaana (na mke au mume) au kubusu au kutazama na mfano wake, kwa hiyari yake.

Ama kutokwa na manii kwa kuota haifunguzi saumu, kwa sababu si kwa hiyari ya mwenye kufunga.

6. Kujitapisha kusudi. Ama aliezidiwa na matapishi akatapika bila ya hiyari yake, Saumu yake haibatiliki.

Mtume (S.A.W.) amesema:

« من ذرعه القيء وهو صائم فليس عليه

قضاء ، ومن استقاء فليقض »

**"Atakaeghilibiwa na matapishi ilihali amefunga hatolipa. Na atakaejitapisha alipe."** (Abu Daud, Tirmidhy, Nasai na wenginco).

7. Kuitangua na kuikataa niya ya kufunga. Atakaenuwiya kula naye amefunga, saumu yake ishabatilika ingawa hakula.

8. Kutoka katika Uislamu halafu akarudia Uislamu.

ALLAH Amesema:

﴿ لَئِنْ أَشْرَكْتَ لَيَحْبَطَنَّ عَمَلُكَ ﴾

**"Ukimshirikisha (ALLAH) bila shaka amali zako zitaruka patupu, (hutazipatia thawabu ijapo ni amali njema)."** (39:65).

b. Yabatilishayo saumu ikapasa kulipa na kutoa kafara:

1. Kujamiiyana kusudi bila ya kutenzwa nguvu.

لحديث أبي هريرة رضي الله عنه :

جاء رجل إلى النبي ﷺ فقال : هلكت يا رسول الله قال : « ما

أهلكك ؟ » قال : وقعت على امرأتي في رمضان ، فقال : « هل

تجد ما تعتق رقبة ؟ » قال : لا ، قال : « فهل تستطيع أن تصوم شهرين متتابعين ؟ » قال : لا ، قال : « فهل تجد ما تطعم ستين مسكيناً ؟ » قال : لا . ثم جلس فأتي النبي ﷺ بعرق[٢] فيه تمر فقال : « خذ تصدق بهذا » قال : فهل على أفقر منا ؟ فوالله ما بين لابتيها[٣] أهل بيت أحوج إليه منا ، فضحك النبي ﷺ حتى بدت نواجذه وقال : « اذهب فأطعمه أهلك »

Abu Hureira (R.A.) amesema: Alikuja mtu kwa Mtume (S.A.W.) akasema: Nimeangamia ewe Mtume wa ALLAH! (Mtume (S.A.W.) akamsaili: **"Ni lipi lililokuangamiza?"** Akajibu: Nimemuingilia mke wangu katika Ramadhani. Akamwuliza: **"Je, unacho cha kumtolea mtumwa awe huru?"**

Akajibu: Laa.

Akamwuliza: **"Je waweza kufunga miezi miwili kufwatana?"**

Akajibu: Laa.

Akamwuliza: **"Je, unaweza kupata utakachowalishia masikini sitiini?"** Akajibu: Laa.

Kisha akaketi. Mtume (S.A.W.) akaletewa chombo (kinachoweza kuingia pishi 15) ndani yake muna tende. Akamwambia: **"Chukua, itolee sadaka".** Akauliza: **"Kwani kuna mafukara kutuzidi? Wallahi katika Madina hakuna wa nyumba yoyote wanayoihitajia kutuliko." Mtume (S.A.W.) akacheka hata meno yake ya mwisho yakaonekana. Akasema: "Nenda ukawalishe watu wako."** (Muttafaq).

Kafara ni: Kuacha huru mtumwa Muislamu. Akishindwa atafunga miezi miwili kufwatana. Akishindwa atawalisha masikini 60 chakula kizuri anachowalisha jamaa zake. Kafara itatolewa kwa mpangilio huo uliotajwa. Haiswihi kugura kutoka hali hadi hali

nyingine ela atakaposhindwa na hali iliotangulia. Kulisha (kafara hiyo) inakuwa kila maskini apate kibaba cha mahindi, au shayiri, au tende, kulingana na uwezo. Kafara huwa nyingi kadiri uhalifu unavyozidi. Anaejamiiyana makusudi halafu asitoe kafara kisha ajamiiyane tena siku nyingine katika mwezi ule wa Ramadhani basi atatoa kafara mbili.

## YALOHALALISHWA KATIKA SAUMU:

Mwenye kufunga amehalalishiwa:

1. Kuingia katika maji na kuzama na kujibaridisha kwa maji hayo kutokana na harara nyingi.

Nana 'Aisha (R.A.) amenena kuwa:

« أن النبي ﷺ كان يصبح جنباً وهو صائم ثم يغتسل »

**"Alikuwa Mtume (S.A.W.) akipambazukiwa ana janaba naye amefunga kisha akioga".** (Muttafaq).

Na pia Mtume (S.A.W.) alikuwa **"Akijimiminia maji kichwani mwake naye amefunga, (akifanya hivyo) kutokana na kiu au joto".** (Ahmad, Abu Daud na wengineo).

2. Amehalalishiwa kupambazuka hali ya kuwa ana janaba, kwa dalili ya Hadithi ya Nana 'Aisha ilotangulia. Na hivyo ilikuwa katika Saumu ya Ramadhani.

3. Kula, kunywa na kujimai usiku mpaka atakapohakikisha kutokeza alfajiri.

Mtume (S.A.W.) amesema:

« إن بلالاً يؤذن بليل فكلوا واشربوا حتى يؤذن ابن أم مكتوم »

**"Hakika Bilal huadhini usiku. Kuleni na munywe hata atapoadhini" Ibni Ummu Maktum."** (Muttafaq).

4. Wenye hedhi na nifasi, damu zao zitakapokatika usiku, inawajuzia kuahirisha kuoga hadi asubuhi, waamke wamefunga kisha wajitwahirishe kwa Swala.

5. Kupiga mswaki mwanzo na mwisho wa mchana, nayo ndio madhehebu ya Maimamu wengi na watu wao. Kwa sababu ya kuenea dalili katika kupendekezeshwa kupiga mswaki na kutokhusishwa nyakati maalumu.

Ama Hadithi zilizopokewa zioneshazo ukaraha wa kupiga mswaki kwa aliefunga baada ya zawaal, Ulamaa wamezihukumia kuwa ni dhaifu.

6. Kusafiri safari halali, ingawaje safari hiyo itampelekea kula.

7. Kujitibu kwa dawa yoyote halali isiofika ndani (tumboni), kama kutumia sindano isio na lishe.

8. Kutafuna na kuonja chakula kwa sharuti kisipenye chochote kile hadi tumboni

9. Kutumia manukato, kujifukiza na kunusa harufu mzuri.

## SAUMU YA SUNNA:

Mtume (S.A.W.) amependekeza na kusisitiza kufunga siku zifwatazo:

1. Siku sita za Shawwal, kwa kauli yake:

« من صام رمضان وأتبعه ستاً من شوال كان كصيام الدهر »

**"Atakaefunga Ramadhani akaiandamizia siku sita za Shawwal atakuwa ni kama aliefunga mwaka."** (Muslim).

2. Siku ya jumatatu na alkhamisi.

Abu Hureira (R.A.) amesema kuwa:

« أن

النبي ﷺ كان أكثر ما يصوم الإثنين والخميس فقيل له(٢) فقال :

إن الأعمال تعرض كل اثنين وخميس فيغفر الله لكل مسلم أو لكل

مؤمن إلا المتهاجرين فيقول : أخروهما »

**"Mtume (S.A.W.) alikuwa zaidi akifunga Jumatatu na Alkhamisi. Akasailiwa, akasema: "Hakika amali hupitishwa kila jumatatu na Alkhamisi. ALLAH Akamsamehe kila Muislamu au kila Muumini, ela waliogurana (walioteta), akisema: Wacheleweshеeni."** (Ahmad).

3. Siku tatu kila mwezi.

Mtume (S.A.W.) amesema:

« صيام ثلاثة أيام من كل شهر : صيام الدهر ، وهي أيام البيض : صبيحة ثلاثة عشر وأربع عشرة وخمس عشرة »

**"Kufunga siku tatu katika kila mwezi ni kufunga mwaka.** Nazo **ndizo siku nyeupe. asubuhi ya 13, 14 na 15."** (Nasai na wengineo).

4. Kufunga siku tisa za mwanzo wa Dhul Hajj (Mfungo tatu).

Mtume (S.A.W.) amesema:

« ما من أيام العمل الصالح فيها أحب إلى الله عز وجل من هذه الأيام - يعني العشر الأول من الحجة - قالوا : يا رسول الله ولا الجهاد في سبيل الله ؟ قال : ولا الجهاد في سبيل الله إلا رجل خرج بنفسه وماله ثم لم يرجع من ذلك بشيء »(٢) . وآكد هذه الأيام صوم يوم عرفة وهو اليوم التاسع لغير الحاج لقوله ﷺ : « صوم يوم عرفة يكفر ذنوب سنتين ماضية ومستقبلة »

**"Hakuna siku yoyote ile, amali njema hupendekeza zaidi mbele ya ALLAH kuliko siku hizi (yaani kumi la kwanza la Dhul Hajj)."**

Wakauliza: Ewe Mtume wa ALLAH, wala Jihad katika njia ya ALLAH? Akajibu: **"Wala Jihad katika njia ya ALLAH. Ispokuwa mtu alietoka kwa nafsi yake na mali yake, kisha asirudi na chochote katika hivyo."** (Bukhari). Na siku iliosisitizwa zaidi katika siku hizi ni siku ya 'Arafa. Nayo ni siku ya tisa, kwa asiehiji.

Mtume (S.A.W.) amesema: **"Kufunga siku ya 'Arafa hufuta**

**madhambi ya miaka miwili iliopita na itakayokuja".** (Muslim).

5. Mwezi wa ALLAH, Muharram (Mfungo nne).

Mtume (S.A.W.) alisema alipoulizwa: أي الصيام أفضل بعد رمضان

« شهر الله الذي تدعونه المحرم »

**"Ni Saumu gani bora baada ya Ramadhani? Alijibu: "Mwezi wa ALLAH, munaouwita Muharram".** (Muslim).

6. Siku ya 'Ashura, nayo ni siku ya kumi katika mwezi wa Muharram.

Mtume (S.A.W.) amesema:

« صوم يوم عاشوراء يكفر سنة ماضية »

**"Kufunga siku ya 'Ashura hufuta (dhambi za) mwaka ulopita."** (Muslim).

Imependekezwa mtu kufunga siku ya tisa na ya kumi ili kuwakhalifu Mayahudi na Manasara. Kwa sababu Mtume (S.A.W.) alipoambiwa kuhusu siku ya kumi kuwa ni siku itukuzwayo na Mayahudi na Manasara. Alisema:

« إذا كان العام المقبل إن شاء الله صمنا

اليوم التاسع . فلم يأت العام المقبل حتى توفي رسول الله ﷺ »

**"Utapokuja mwaka unaokuja tutafunga siku ya tisa inshaallah".** Lakini mwaka ule ulipokuja Mtume (S.A.W.) alikuwa ameshakufa. (Muslim).

## SIKU ZINAZOHARAMISHWA KUFUNGA:

1. Siku ya Idil-Fitri na Idil-Adh-ha.

Sayyidua 'Umar bin Al-Khattab (R.A.) amesema:

« إن هذين يومان نهى رسول الله ﷺ

عن صيامهما ، يوم فطركم من صيامكم ، والآخر يوم تأكلون فيه

من نسككم »

**"Hakika siku hizi mbili ni siku alizokataza Mtume (S.A.W.) mtu kuzifunga, siku ya kula kutoka katika saumu yenu, na siku nyingine mnakula kutoka katika Ibada zenu."** (Muslim).

2. Siku tatu za tashriq, nazo ni 11, 12 na 13 katika mwezi wa Dhul-Hajj (Mfungo tatu).

Mtume (S.A.W.) alimtuma 'Abdallah bin Hudhafa (R.A.) awe akitufu (akizunguka) Mina akisema: **"Msifunge hizi siku, kwani ni siku za kula, kunywa na kumtaja ALLAH Aliyeshinda na Kutukuka."** (Ahmad na wengineo).

Katika makatazo haya, ametolewa anaehiji anaefanya tamatui au qiran asipopata mnyama wa kuchinja.

3. Siku za hedhi na nifasi.

Mtume (S.A.W.) amesema katika haki ya mwanamke:

« أليست إذا حاضت لم تصل ولم تصم ؟ فذلك من نقصان دينها »

**"Je, hakuwa atokwapo hedhi haswali wala hafungi? Basi hiyo ndio alama ya kupungua Dini yake."** (Bukhari).

Na ni itifaki ya Waislamu wote kuwa mwenye hedhi na nifasi saumu zao haziswihi.

4. Mwanamke kufunga na mumewe akawa yupo hadhiri ispokuwa kwa idhini yake.

Mtume (S.A.W.) amesema:

« لا تصم المرأة وبعلها شاهد إلا بإذنه غير رمضان »

**"Asifunge mwanamke na mumewe yupo ela kwa idhini yake. Ispokuwa Ramadhani."** (Muttafaq).

## SIKU AMBAZO NI MAKRUHU KUFUNGA:

1. Kufunga siku ya 'Arafa kwa anaehiji, amesimama hapo 'Arafa.

Mtume (S.A.W.) amesema:

« يوم عرفة ويوم النحر وأيام التشريق عيدنا أهل الإسلام وهي أيام أكل وشرب »

**"Siku ya 'Arafa, siku ya kuchinja na siku za tashriq ni Idi yetu sisi watu wa Uislamu, nazo ni siku za kula na kunywa."** (1). (Abu Daud, Tirmidhy na wengineo).

2. Kufunga Ijumaa peke yake.

Mtume (S.A.W.) amesema:

« لا تصوموا يوم الجمعة إلا وقبله يوم أو بعده يوم »

**"Msifunge Ijumaa ela pamoja na siku kabla yake au siku baada yake."** (Muttafaq).

3. Jumamosi peke yake

Mtume (S.A.W.) amesema:

« لا تصوموا يوم السبت إلا فيما افترض عليكم وإن لم يجد أحدكم إلا لحاء(٢) عنب أو عود شجرة فليمضغه »

**"Msifunge siku ya Jumamosi ela katika muliofaradhiwa. Asipopata mmoja wenu ela ganda la zabibu au kigongo cha mti basi akitafune."** (Ahmad, Abu Daud na Tirmidhy).

4. Kufunga mwaka mzima bila kula.

Mtume (S.A.W.) amesema:

« لا صام من صام الأبد »

**"Hakufunga anaefunge daima."** (Muttafaq). Pia akasema:

« من صام الأبد فلا صام ولا أفطر »

**"Anaefunga daima basi (ajue kuwa) hakufunga wala hakula."** (Ahmad, Nasai na wengineo).

5. Kuunga saumu ya siku mbili mfululizo au zaidi kwa makusudi, nayo huitwa **'Wiswal'**.

Mtume (S.A.W.) amesema:

---

(1) Ulamaa wamesema kuwa, siku ya 'Arafa ni Idi kwa waliosimama hapo 'Arafa, kinyume na watu wa miji mingine, Idi yao ni siku ile ya kuchinja.

**"Nawatahadharisha na Wiswal."** (Muttafaq).

Pia kauli yake:

« لا تواصلوا فأيكم أراد أن يواصل فليواصل حتى السحر »

**"Msiunge (Saumu kwa mfululizo). Yeyote kati yenu anaetaka kuunga, basi aunge hadi usiku."** (Bukhari).

6. Kufunga siku ya shaka, nayo ni siku ya 30 katika mwezi wa Shaabani.

'Ammar bin Yasir (R.A.) amesema:**"Anaefunga siku inayoshakiwa, ameshamuasi Abal-Qaasim (S.A.W.)."** (Abu Daud, Tirmidhy na wengineo).

Mtume (S.A.W.) amesema: « لا تقدموا رمضان بصوم قبله بيوم أو بيومين إلا أن يكون رجل كان يصوم صوماً فليصمه »

**"Msiitangulize Ramadhani kwa kufunga siku moja au mbili kabla yake, ela mtu awe alikuwa akifunga, basi afunge."** (Muslim).

******

# NGUZO YA TANO

# HAJJ

# AL-HAJJ

## Taarifa yake:

Kilugha, Hajj maana yake ni "**Kukusudia.**" Pia maana yake ni "**Kufanya tendo mara baada ingine.**"

Ama ki-Sharia, ni kuikusudia Nyumba Tukufu ya ALLAH kwa ajili ya kufanya vitendo makhsusi vilivyonasiwa katika Kitabu cha ALLAH na kubainishwa katika sunna toharifu, kama zitakavyokuja mbeleni.

## Hukumu yake:

Hajj ni Faradhi kwa kila Muislamu mume na mke, kwa anaeweza kwenda. Umeshathubutu ufaradhi wake katika Qur'aan, Hadithi na Ijimai.

Ama katika Qur'aan, ALLAH Amesema:

﴿ وَلِلَّهِ عَلَى النَّاسِ حِجُّ الْبَيْتِ مَنِ اسْتَطَاعَ إِلَيْهِ سَبِيلًا
وَمَنْ كَفَرَ فَإِنَّ اللَّهَ غَنِيٌّ عَنِ الْعَالَمِينَ ﴾

**"Na ALLAH Amewajibishia watu wafanye Hija katika Nyumba hiyo, yule awezaye kufunga safari kwenda huko. Na atakaekanusha (asende hali ana uwezo) basi ALLAH si mhitaji kuwahitajia walimwengu."** (3:97).

Mtume (S.A.W.) amesema:

« بني الإسلام على خمس : شهادة أن لا إله إلا الله وأن محمداً رسول الله ، وإقام الصلاة ، وإيتاء الزكاة ، وحج البيت ، وصوم رمضان »

**"Uislamu umejengwa juu ya Nguzo tano: Kushuhudia kuwa hakuna Mola anaestahiki kuabudiwa kwa haki ela ALLAH, na kwamba Muhammad ni Mtume wa ALLAH, kusimamisha Swala, kutoa Zaka, kuhiji Nyumba (ya Al-Kaaba) na kufunga Ramadhani."** (Muttafaq).

Waislamu wote wameafikiana kupasa kwake, na kwamba Hajj

ni mojawapo katika Nguzo za Uislamu, na ni dharura katika Dini jambo hilo kujulikaniwa, na anaekanusha kupasa kwake, ameshakufuru na kutoka katika Uislamu.

Ulamaa wameafikiana kuwa Hajj haipasi katika umri wa mtu ela mara moja - ela Muislamu atakapoeka nadhiri, hapo itapasa kutekeleza nadhiri - na ikizidi itakuwa ni tatawu (kujizidishia Thawabu).

Abu Hureira amesema:

خطبنا رسول الله ﷺ فقال :

« ياأيها الناس إن الله كتب عليكم الحج فحجوا » فقال رجل : أكل عام يا رسول الله ؟ فسكت حتى قالها ثلاثاً ، ثم قال ﷺ : « لو قلت نعم لوجبت ولما استطعتم » ثم قال : « ذروني ما تركتكم فإنما أهلك من كان قبلكم كثرة سؤالهم واختلافهم على أنبيائهم ، فإذا أمرتكم بشيء فأتوا منه ما استطعتم ، وإذا نهيتكم عن شيء فدعوه »

Mtume (S.A.W.) alitukhutubia, akanena: **"Enyi watu, kwa yakini ALLAH Amewafaradhia Hajj, basi nendeni mukahiji."** Mtu mmoja akasaili: Je, ni kila mwaka ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu? Akanyamaa (Mtume), hata aliposaili mara tatu, Mtume (S.A.W.) alimjibu: **"Niacheni maadamu nimewaacha. Hakika limewaangamiza walokuwa kabla yenu kuuliza kwao sana na kukhitilafiana kwao na Manabii wao. Ninapowaamuru jambo, lifanyeni kadiri muwezavyo, na ninapowakataza kitu basi kiwacheni."** (Muslim).

Ibnu Abbas (R.A.) amenena:

خطبنا رسول الله ﷺ فقال :

« ياأيها الناس كتب عليكم الحج » فقام الأقرع بن حابس فقال : أفي كل عام يا رسول الله ؟ فقال : « لو قلتها لوجبت ولو وجبت لم تعملوا بها ولم تستطيعوا ، الحج مرة فمن زاد فهو تطوع »

Mtume (S.A.W.) alitukhutubia, akasema: **"Enyi watu, mmefaradhiwa Hajj." Akasimama Al-Aqra bin Haabis akasaili: Katika kila mwaka ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu? Akasema: "Lau ningalisema ni hivyo ingaliwajibika. Na lau ingaliwajibika msingalifanya wala msingaliweza. Hajj ni mara moja, awezae afanye tatawui (azidishe)."** (Ahmad, Abu Daud, Nasai na wengineo).

## FADHILA ZA HAJJ:

Sharia imesisitiza mtu kutekeleza Faradhi ya Hajj na ikabainisha Thawabu adhimu na ujira mkubwa juu ya jambo hilo.

Tazama Hadithi zifwatazo:

1. Kauli yake Mtume (S.A.W.):

« من حج فلم يرفث(٣) ولم يفسق رجع من ذنوبه كيوم ولدته أمه »

**"Atakaehiji wala asijamii wala asifanye ufuska, atarudi kutokana na dhambi zake kama siku aliyozawa na mama yake".** (Muttafaq).

2.

« العمرة إلى العمرة كفارة لما بينهما والحج المبرور ليس له جزاء إلا الجنة »

**" 'Umra mpaka 'Umra ni kafara baina yake. Na Hajj iliokubaliwa haina malipo ela Pepo."** (Muttafaq).

3. قوله ﷺ - وقد سئل عن أفضل الأعمال - فقال : « إيمان بالله ورسوله » قيل : ثم ماذا ؟ قال : « ثم جهاد في سبيل الله » قيل : ثم ماذا ؟ قال : « ثم حج مبرور »

Alipoulizwa kuhusu amali bora zaidi, alijibu: **"Ni kumwamini ALLAH na Mtume wake".** Akaulizwa: Kisha ni nini? Akajibu: **"Kisha ni Jihad katika Njia ya ALLAH".** Akaulizwa: Kisha ni nini? Akajibu: **"Hajj iliokubaliwa".** (Muttafaq).

4.

« تابعوا بين الحج والعمرة فإنهما ينفيان الفقر والذنوب كما ينفي الكير خبث الحديد والذهب والفضة وليس للحجة

المبرورة ثواب إلا الجنة »

**"Fwatilisheni baina ya Hajj na 'Umra, kwani mambo hayo huondowa ufukara na madhambi kama vile mfua-vyuma anavyoondoa uchafu wa chuma, dhahabu na fedha. Hajj iliokubaliwa haina malipo ela ni Pepo."** (Ahmad, Tirmidhy na Nasai).

Na muna Hadithi nyingine nyingi zielezazo jambo hilo.

## SHARUTI ZA KUPASA HAJJ:

Inasharutishwa katika kupasa Hajj sharuti zifwatazo:

1. Uislamu
2. Kubaleghe
3. Kuwa na akili
4. Kuwa na uhuru.

Dalili zake tumeshazitaja katika **"Swala"** na **"Saumu."**

5. Uweza.

ALLAH Amesema:

﴿ وَلِلَّهِ عَلَى النَّاسِ حِجُّ الْبَيْتِ مَنِ اسْتَطَاعَ إِلَيْهِ سَبِيلاً ﴾

**"Na ALLAH Amewajibishia watu wafanye Hija katika nyumba hiyo, yule awezaye kufunga safari kwenda huko."** (3:97).

## NGUZO ZA HAJJ:

Nguzo za Hajj ni nne: Kuhirimia, kusimama 'Arafa, kutufu na kusaayi. Nguzo moja kati ya hizo ikikosekaniwa Hajj itabatilika.

## NGUZO YA KWANZA: KUHIRIMIA:

1. Kuhirimia ni kutia niya ya kuingia katika ibada (ya Hajj na 'Umra) ilihali ya kukutanisha na kuvua nguo na kuleta Talbiya. Na kuhirimia ni sampuli tatu: Tamatui, kiraan na ifraad.

**Maana ya tamatui**: Ni Muislamu ahirimie 'Umra pekee katika miezi ya Hajj. Atapofika Makka atatufu na kusaayi kwa 'Umra, atanyoa au atapunguza. Itapofika siku ya tarwiya - nayo ni siku ya nane katika mwezi wa Dhul Hajj - atahirimia Hajj pekee, na atafanya amali zote za Hajj na atatoa fidia (atachinja mnyama, mbuzi

au kondoo) ya tamatui akiwa sio katika walohudhuria Msikiti Mtukufu.

**Kiraan ni**: Kuhirimia 'Umra na Hajj pamoja katika Miiqaat, au ahirimie 'Umra kwanza kisha aingize Hajj juu yake kabla ya kuanza kutufu, na atabakia katika ihraam yake mpaka ataporusha mawe siku ya Idi na kunyoa kichwa chake, na itampasa fidia, kama yule aliefanya tamatui.

**Ifraad:** Ni kuhirimia Hajj pekee, na abakie katika ihraam yake mpaka ataporusha mawe siku ya Idi na kunyoa kichwa chake wala hana fidia.

Katika kuhirimia muna wajibati, sunna na yaloharamishwa:

a. Wajibati: Ni amali ambazo lau ataacha moja katika amali hizo ingemlazimu mwenye kuacha kumwaya damu au kufunga siku kumi ashindwapo kumwaya damu (yaani kuchinja). Na wajibati za ihramu ni kumi:

1. Kuhirimia Miiqati. Mtume (S.A.W.) aliweka mipaka katika sehemu fulani, haifai kwa anaepita sehemu hizo nae anakusudia Hajj au 'Umra kuziuka na kuingia Makka ela awe ni mwenye kuhirimia. Sehemu zenyewe ni kama zifwatazo:

a. Dhulhulaifa, kwa sasa panaitwa Abyar 'Ali. Nayo ndio miqati ya watu wa Madina na anaekuja kupitia njia hiyo, angani au nchikavu.

b. Al-Juhfa: Ni kitongoji cha zamani juu ya njia ya Sahil. Badala yake kwa sasa watu wanahirimia Raabigh. Nayo ndio miqati ya watu wa Misri, Shamu na wanaopitia njia hiyo kwa anga, nchikavu au kwa bahari.

c. Yalamlam: Ni jabali, kwa sasa panaitwa Sa'diya. Nayo ni Miiqati ya watu wa Yemen na wanaopitia njia hiyo.

d. Qarnul-Manaazil, pia huitwa Sail. Ndio miqati ya watu wa Najdi na wanaokuja kupitia njia hiyo kwa anga au nchikavu.

e. Dhatu'irqi. Nayo ni miqati ya watu wa Iraq na wanaokuja kupitia njia hiyo kwa anga au nchikavu.

f. Ambae nyumba yake i mbele ya miqati hizi basi atahirimia Hajj au 'Umra nyumbani mwake, ela ambae nyumba yake iko

Makka, atatoka aende kujifungua na kuhirimia kwa 'Umra, ama Hajj ataihirimia Makka.

Dalili ya hayo, ni Hadithi ya Ibni 'Abbas (R.A.), amesema:

« وقت رسول الله ﷺ لأهل المدينة ذا الحليفة ، ولأهل الشام الجحفة ، ولأهل نجد قرن المنازل ، ولأهل اليمن يلملم ، قال : فهن لهن ولمن أتى عليهن من غير أهلهن لمن كان يريد الحج والعمرة ، فمن كان دونهن فمن أهله ، وكذلك حتى أهل مكة يهلون منها »

**"Mtume (S.A.W.) aliwaekea miqati watu wa Madina hapo Dhul-hulaifa, na watu wa Sham hapo Juhfa. Watu wa Najdi hapo Qarnul-Manaazil. Watu wa Yemen hapo yalamlam. Akanena: Miqati hizo ni za sehemu hizo na wanaozipita kutoka sehemu nyingine kwa anaekusudia Hajj na 'Umra. Atakaekua mbele ya hizo basi (atafanya miqati kwa) jamaa zake. Kadhalika ndivyo ilivyo. Hata watu wa Makka miqati yao ni Makka."** (Muttafaq).

**FAIDA:** Zilizopita ni miqati za mahala. Na Hajj ina miqat nyingine ambayo ni ya zama.

**MIQATI YA ZAMA:** Ni miezi iliotajwa na ALLAH katika Qur'aan:

﴿ الْحَجُّ أَشْهُرٌ مَعْلُومَاتٌ ﴾

**"Hijja ni miezi maalumu."** (2:197). Nayo ni Shawwal, Dhul-Qada na siku kumi za Dhul-Hijja. Lau mtu atahirimia Hajj kabla ya miezi hii, kuhirimia kwake hakutaswihi, wakati ambapo lau atahirimia na akasimama 'Arafa kabla ya kutokeza alfajiri usiku wa kuamkia tarehe kumi katika mwezi wa Dhul-Hijja, Hajj yake ni Swahihi.

2. Kujiepusha na nguo. Aliehirimia havai nguo (ya mzunguko) wala kanzu, wala burnusi, wala havai kilemba, wala hakifiniki kicwa chake kwa chochote, wala havai viatu vya kufunika miguu, wala soksi, wala havai nguo ilioingia zafarani au warisi (aina fulani ya mmea wenye harufu nzuri).

Mtume (S.A.W.) amesema:

« لا يلبس المحرم
القميص ولا العمامة ولا السراويل ولا البرنس ولا ثوباً مسه ورس
ولا زعفران ولا الخفين إلا أن لا يجد نعلين فليلبس الخفين
وليقطعهما حتى يكونا أسفل من الكعبين »

**"Aliehirimia asivae kanzu, kilemba, suruali, burunsi, nguo iliogusa warisi na zafarani, wala viatu vya kufunika miguu. Ela asipopata champali atavaa viatu vya kufunika na atavikata mpaka viwe chini ya macho ya miguu."** (Muttafaq).

Ama mwanamke mwenye kuhirimia, atavua vilivyo juu ya uso wake, kama nikabu, na ataondoa kufazi zilizo mikononi mwake. Wala hapana ubaya kueka mtandio usoni mwake wakati wa kupita wanaume wasio maharimu wanaopita karibu naye.

Mtume (S.A.W.) amesema:

« لا تنتقب المرأة ولا تلبس القفازين »

**"Mwanamke asivae nikabu wala kufazi".** (Bukhari). (Nikabu ni kitambaa wavaacho wanawake usoni. Na kufazi wanavaa mikononi).

## SUNNA ZA KUHIRIMIA

1. Kuoga kwa kuhirimia, japo ni kwa mwenye hedhi au nifasi.

Mtume (S.A.W.) amesema:

« إن النفساء
والحائض تغتسل[1] وتقضي المناسك كلها غير أنها لا تطوف
بالبيت حتى تطهر »

**"Hakika wenye nifasi na wenye hedhi wataoga na watafanya ibada zote ispokuwa hawatatufu Al-Kaaba mpaka watwahirike."** (Ahmad, Abu Daud na Tirmidhy).

2. Kuvaa kikoi na shuka nyeupe zilosafi.

Ibni 'Abbas (R.A.) amesema:

« انطلق رسول الله ﷺ من المدينة بعدما ترجل وادهن

ولبس إزاره ورداءه هو وأصحابه »

**"Mtume (S.A.W.) aliondoka Madina baada ya kujitana, kujipaka mafuta, kuvaa kikoi na shuka yake, yeye na maswahaba wake."** (Bukhari).

3. Kukata kucha, kupunguza masharubu, kusumua nywele za makapwa na kunyoa nywele za kinena (sehemu ya siri). Kwani Mtume (S.A.W.) alifanya hayo. Na pia ni kwa sababu muda wa kuhirimia ni mrefu aghalabu, hivyo basi apate udhia kwa nywele kuwa ndefu ilihali amekatazwa kuziondoa (wakati huo).

4. Kutia niya ya ihram (kuhirimia) baada ya Swala ya Faradhi au sunna.

5. Kuleta Talbia baada ya niya. Nayo ni:

لبيك اللهم لبيك . لبيك لا شريك

لك لبيك . إن الحمد والنعمة لك والملك لا شريك لك ،

**"Nakuitika Ewe Mola, nakuitika. Nakuitika huna mshirika, nakuitika. Hakika Sifa zote na neema ni Zako, na Ufalme. Huna mshirika."**

Mwanamume atainua sauti yake kwa Talbia hiyo, mwanamke ataisoma kiasi ya kusikia aliekaribu nae. Imependekezwa kuikariri Talbia na kuisoma kwa wingi mno. Na pia aombe na kumswalia Mtume (S.A.W.) baada yake.

## YALOHARAMISHWA KATIKA IHRAM:

Nazo ni amali zimzuwiazo aliehirimia Hajj au 'Umra, kwa

sababu ya ihram. Nazo ni:

1. Kuondoa nywele kichwani kwa kuzinyoa au kwa njia nyingine, kadhalika katika mwili wote.
2. Kukata kucha za mikono na miguuni.
3. Kufunika kichwa kwa pazia aina yoyote ile.
4. Kuvaa nguo ya mshono, kama vile juba na mfanowe.
5. Kutumia manukato baada ya kunuwiya ihram, katika nguo, mwili au mahala pengine.

Basi atakaefanya mojawapo ya mambo haya matano, itamlazimu fidia, nayo ni kufunga siku tatu au kulisha masikini sita, kila masikini kibaba cha mahindi, au kuchinja mbuzi.

ALLAH Mtukufu Amenena:

﴿ فَمَن كَانَ مِنكُم مَّرِيضًا أَوْ بِهِ أَذًى مِّن رَّأْسِهِ فَفِدْيَةٌ مِّن صِيَامٍ أَوْ صَدَقَةٍ أَوْ نُسُكٍ ﴾

**"Na atakaekuwa mgonjwa katika nyinyi au ana vya kumuudhi kicwani mwake (akafanya yalokatazwa, k.v. kunyoa), basi atoe fidia kwa kufunga au (kwa kutoa) Sadaka au kuchinja wanyama."** (2:196).

6. Kuuwa kiwinda. nae ni mnyama halali wa bara. ALLAH Amesema:

﴿ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تَقْتُلُوا الصَّيْدَ وَأَنتُمْ حُرُمٌ ﴾

**"Enyi mlioamini! Msiue mawindo na hali (ya kuwa) mumo katika Hija au 'Umra."** (5:95).

Atakaemuua makusudi, basi ni juu yake kutoa mfano wake.

ALLAH Amesema:

﴿ وَمَن قَتَلَهُ مِنكُم مُّتَعَمِّدًا فَجَزَاءٌ مِّثْلُ مَا قَتَلَ مِنَ النَّعَمِ ﴾

**"Na miongoni mwenu atakaemwua kwa kusudi, basi malipo yake yatakuwa kwa (kuchinja) kilicho sawa na alichokiua, katika wanyama wanaofugwa."** (5:95).

Au atatoa kiasi kitakachokua sawa na kima cha mfano wake, ima iwe ni chakula atakachogawia masikini, au afunge badala ya

chakula cha kila siku kwa masikini. Hali hii ni wakati panapopatikaniwa mfano wa kiwinda aliyeuwawa. Iwapo kiwinda huyo hatakuwa na mfano atampigia kima kwa darahimu na atatoa chakula kinachokuwa sawa nae atakigawa kwa masikini. Au atafunga badala ya kulisha masikini, kila siku masikini mmoja.

7. Vitangulizi vya jimai, kama kubusu na mfano wake.

ALLAH Amesema:

﴿ الْحَجُّ أَشْهُرٌ مَعْلُومَاتٌ فَمَنْ فَرَضَ فِيهِنَّ الْحَجَّ فَلَا رَفَثَ وَلَا فُسُوقَ وَلَا جِدَالَ فِي الْحَجِّ ﴾

**"Hija ni miezi maalumu. Na anaekusudia kufanya Hija katika (miezi) hiyo, basi asiseme maneno machafu wala asitende vitendo vichafu wala asibishane katika hiyo Hija."** (2: 197).

Ama kujimai, hubatilisha Hajj. Yapasa kwa aliehirimia aliefanya jimai katika kule kuharibu kwake mpaka atimize, na inampasia kutoa ngamia, na ailipe (Hajj) mwaka mwingine.

Sayyidna 'Umar bin Al-Khattab, 'Ali bin Abi Twalib na Abuhureira, waliulizwa kuhusu mtu aliejamiiyana na mkewe naye amehirimia Hajj. Wakajibu:

« ينفذان يمضيان لوجههما حتى يقضيا حجهما ثم عليهما حج قابل والهدي »

**"Watapitisha na wataendea katika njia yao hata watapomaliza Hija zao, kisha itawapasa Hija nyingine mwakani na kuchinja".** (Imam Malik).

## NGUZO YA PILI : TAWAFU (KUTUFU):

Kutufu ni kuizunguka Alkaaba Tukufu mara saba.

## SAMPULI ZA KUTUFU:

1. Tawaful - qudum.
2. Tawaful - ifadha, nayo ni nguzo katika nguzo za Hajj, anayeiwacha, Hija yake imebatilika.
3. Tawaful - wadaai. Ndio ya mwisho anayoifanya mwenye

kuhiji wakati anapotaka kusafiri kutoka Makka. Nayo ni waajib miongoni mwa wajibati za Hajj. Anayeiwacha itamlazimu kuchinja mnyama.

4. Tawafu - ttatawwu.

Katika kutufu muna sharuti, mienendo na adabu zake. Tazama ubainifu wake:

## SHARUTI ZA KUTUFU:

1. Kutia niya. Nayo ni moyo kuazimu kutufu kwa ajili ya kumtii ALLAH Mtukufu na kutafuta Radhi Zake.

2. Kujitwahirisha kutokana na hadathi ndogo, kubwa na najisi.

Mtume (S.A.W.) amesema:

« الطواف بالبيت صلاة إلا أن الله تعالى أباح فيه الكلام »

**"Kutufu Alkaaba ni kuswali, ispokuwa tu, ALLAH Alietukuka Amehalalisha mazungumzo ndani yake."** (Tirmidhy, Haakim na wengineo).

3. Kusitiri uchi, kwa dalili ya Hadithi iliotangulia. Kadhalika Mtume (S.A.W.) amesema:

« لا يحج بعد العام مشرك ولا يطوف بالبيت عريان »

**"Asihiji baada ya mwaka huu ambae ni Mushrik wala asitufu Alkaaba aliyeuchi."** (Muttafaq).

4. Iwe ni mizunguko saba kamili. Ataanzia kwenye Hajarul-aswad (jiwe leusi) na atakomea papo hapo.

Jabir (R.A.) amesema:

« لما قدم رسول الله ﷺ مكة أتى الحجر الأسود

فاستلمه ثم مشى عن يمينه فرمل ثلاثاً(٣) ومشى أربعاً »

**"Mtume (S.A.W.) alipoingia Makka, aliliendea jiwe leusi akalisalimu, kisha akatembea upande wa kuliani mwake, akaenda kwa haraka mara tatu na akatembea (kama kawaida) mara moja".** (Muslim).

5. Alkaaba iwe kushotoni mwa anaetufu.

6. Iwe kutufu Alkaaba ni ndani ya Msikiti, japokuwa Alkaaba itakuwa mbali naye.

7. Iwe kutufu ni nje ya Alkaaba. Lau atatufu ndani ya Hijri (uwa uliopo mbele ya Kaaba penye Hijri Ismail) basi tawafu yake haitasihi. Kwani Hijri na Shadharuani (jengo lililoshikana na msingi wa Alkaaba) ni sehemu ya Alkaaba.

8. Kufwatanisha baina ya kule kuzunguka, lakini lau atapambanua kwa udhuru, basi haidhurishi.

## SUNNA ZA KUTUFU:

1. Kulielekea jiwe leusi wakati wa kuanza kutufu na kulibusu ikiwezekana, isipowezekana ataligusa kwa mkono wake au fimbo na aubusu mkono au fimbo hiyo, au ataliashiria. Kwani Mtume (S.A.W.) alifanya hivyo.

2. Kujifunga idhtibai kuanzia mwanzo wa kutufu hadi mwishowe. Kujifunga idhtibai ni: Kuijaalia katikati ya shuka yake iwe chini ya kapwa lake la kulia, na ncha zake ziwe juu ya bega lake la kushoto. Atakapomaliza kutufu atairudisha shuka yake katika hali ile ilokuwa kabla ya kutufu.

3. Kutembea haraka kwa kuvuta hatua za karibu karibu, kwa wanaume wawezao, - lakini sio kwa wanawake - na iwe ni katika ile mizunguko mitatu ya kwanza. Ama mizunguko minne ilobakia, hatoenda haraka, bali atatembea kama ada yake.

Kujifunga idhtibai na kutembea haraka kumethubutu kwa Mtume (S.A.W.).

4. Kuigusa Ruknuyamani kwa mkono kwa kila mzunguko, wala hataibusu. Isipowezekana hatoisongamania. Na asipoweza kuigusa kwa mkono hatoiashiria.

5. Baina ya Rukniyamani na jiwe leusi atasema:

« ربنا آتنا في الدنيا حسنة وفي الآخرة حسنة وقنا عذاب النار »

6. Kuomba dua hapo Multazam. Multazam ni mahala baina ya mlango wa Al-Kaab na jiwe leusi.

7. Amalizapo kutufu mara saba ataenda Maqamu Ibrahim. Atasoma:

﴿ وَاتَّخِذُوا مِنْ مَقَامِ إِبْرَاهِيمَ مُصَلًّى ﴾

**"Na mahali alipokuwa akisimama Ibrahimu pafanyeni pawe pa kuswalia".** (2:125).

Maqam itakuwa kati yake na Al-Kaaba. Ataswali rakaa mbili nyuma yake. Katika rakaa ya kwanza atasoma Al-Hamdu na Qul ya Ayyuhal-Kaafiruun. Na rakaa ya pili Al-Hamdu na Qul-Huwallahu Ahad.

8. Kunywa maji ya zamzam baada ya kumaliza kuswali Rakaa mbili.

9. Kurudi na kuligusa jiwe leusi kabla ya kwenda kusaayi, itakapowezekana.

## ADABU ZA KUTUFU:

1. Iwe kutufu ni katika hali ya unyenyekevu, moyo kuwa hadhiri, kuhisi Ukubwa wa ALLAH Mtukufu, kumwogopa na kutarajia Rehema zilizo Kwake.

2. Kutozungumza ela kwa haja. Na azungumzapo basi atamke kheri.

Mtume (S.A.W.) amesema:

« الطواف بالبيت صلاة إلا أن الله تعالى أباح فيه الكلام ، فمن تكلم فلا يتكلم إلا بخير»

**"Kutufu Al-Kaaba ni kuswali. Ispokuwa tu, ALLAH Mtukufu Ameruhusu mazungumzo ndani yake. Basi atakaezungumza asizungumze ela kwa kheri."** (Twabrany).

Pia Mtume (S.A.W.) amesema: **"Kutufu ni kuswali. Punguzeni mazungumzo ndani yake."** (Ahmad).

4. Kukithirisha dhikri na dua.

5. Kutomuudhi Muislamu kwa neno au kwa tendo.

# NGUZO YA TATU: KUSAAYI:

Kusaayi ni kutembea baina ya Swafaa na Marwa kuenda na kurudi, kwa niya ya kuabudu, nayo ni nguzo katika Hajj na Umra.

ALLAH Amesema: ﴿ إِنَّ الصَّفَا وَالْمَرْوَةَ مِن شَعَائِرِ اللَّهِ ﴾

**"Hakika Swafaa na Marwa ni katika alama za kuadhimisha Dini ya ALLAH."** (2:158).

Mtume (S.A.W.) amesema:

« إسعوا فإن الله كتب عليكم السعي »

**"Fanyeni Saayi. ALLAH Amewaandikia Saayi."** (Ahmad na wengineo).

## SHARUTI ZA KUSAAYI:

1. Kutia niya. Mtume (S.A.W.) amesema: **"Hakika kuswihi kwa amali huzingatiwa niya"**. Basi Muislamu atanuwiya kwa hiyo Saayi kumtii ALLAH na kufwata Amri Yake.
2. Iwe ni baada ya kutufu. Saayi haitangulizwi mbele ya tawafu.
3. Kuanzia Swafaa na kumalizia Marwa.
4. Iwe ni kuzunguka mara saba kwa ukamilifu.5. Saayi iwe ni mahala maarufu.

## SUNNA ZA KUSAAYI:

1. Iungane na kutufu, ela kwa udhuru.
2. Kupanda hadi juu ya Swafa na Marwa, kuleta Tahlili. Takbiir na kumwomba ALLAH apendavyo.
3. Kuenda haraka - kadiri itavyowezekana - baina ya bendera mbili za kijani, na kutembea kiada sehemu zisokuwa hizo.

Watakaoenda haraka ni waume sio wanawake.

Na ataleta dhikri hii katika huko kusaayi:

« لا إله إلا الله

وحده لا شريك له له الملك وله الحمد وهو على كل شيء قدير .

لا إلـه إلا الله وحـده أنجـز وعـده ونصر عبده وهزم الأحزاب وحده ، كان يكرر ثلاث مرات ويدعوا بين ذلك »

## ADABU ZA KUSAAYI:

1. Kuiyendea Saayi kwa kupitia mlango wa Swafaa huku akisoma.

﴿ إِنَّ الصَّفَا وَالْمَرْوَةَ مِن شَعَائِرِ اللَّهِ فَمَنْ حَجَّ الْبَيْتَ أَوِ اعْتَمَرَ فَلَا جُنَاحَ عَلَيْهِ أَن يَطَّوَّفَ بِهِمَا وَمَن تَطَوَّعَ خَيْرًا فَإِنَّ اللَّهَ شَاكِرٌ عَلِيمٌ ﴾

2. Mwenye kusaayi awe twahara.
3. Kutembea katika hali ya kusaayi itapowezekana bila ya mashaka.
4. Kukithirisha dhikri na dua.
5. Kuwafanyia upole Waislamu na kutowaudhi kwa neno au kwa tendo.
6. Mwenye kusaayi ahudhurishe moyoni mwake unyonge na kumhitajia kwake ALLAH katika kuuwongoza moyo wake, kuitakasa nafsi yake na kumtengezea mambo yake.

## NGUZO YA NNE: KUSIMAMA 'ARAFA:

Mtume (S.A.W.) amesema: « الحج عرفة »
**"Hajj ni 'Arafa."**

Muradi wa kusimama 'Arafa, ni kuhudhuria hapo uwanja wa Arafa, kwa muda mchache na zaidi kwa niya ya kusimama. Kuanzia baada ya adhuhuri ya siku ya tisa mwezi wa Dhul-Hijja mpaka kutokeza alfajiri ya siku ya Idi, nayo ni siku ya kumi, mwezi wa Dhul-Hijja. Atakaetokezewa na alfajiri siku ya Idi wala hakusimama 'Arafa, ameshaikosa Hajj.

## WAJIBATI ZA HAJJ:

Wajibati za hajj ni saba nazo ni:

1. Kuhirimia katika miqati.
2. Kusimama Arafa mpaka kuzama jua.
3. Kupitiwa na usiku hapo Muzdalifa.
4. Kupitiwa na usiku hapo Mina katika masiku ya siku za tashriq.
5. Kurusha mawe.
6. Kunyoa au kupunguza.
7. Tawafu ya kuaga.

# FAIDA:

## NGUZO ZA 'UMRA:

Nguzo za 'Umra ni tatu: Kuhirimia, kutufu na kusaayi.

## WAJIBATI ZA 'UMRA:

1. Kuhirimia
2. Kunyoa au kupunguza.

Atakaewacha nguzo yoyote miongoni mwa nguzo zilotangulia katika Hajj au 'Umra basi ibada yake ya Hajj au 'Umar haitatimia ela kwa nguzo hiyo. Na atakaewacha wajibu wowote katika Hajj au 'Umra, atalazimika kutoa fidia. Atamchinja akiwa Makka na atawapa masikini wa Haram. Wala hatokula chochote katika fidia hiyo.

## FAIDA MUHIMU KUJULIKANA:

1. Inapokuwa siku ya tarwiya, nayo ni siku ya nane mwezi wa Dhul-Hijja, atahirimia yule aliefanya tamatui - aliejifungua kutoka katika 'Umra na akahirimia Hajj - wakati wa dhuha (kati ya saa mbili asubuhi hadi saa tano), na wakati wa kuhirimia kwake Hajj atafanya kama alivyofanya wakati wa kuhirimia 'Umra, atajinadhifisha, ataoga, atajitia manukato na atavaa kikoi na shuka. Atanuwiya kuhirimia Hajj kwa kusema: « لبيك اللهم حجاً »

**"Labbaikallaahumma Hajja."** (Aliefanya tamatui katika 'Umra atasema: لبيك اللهم عمرة )

Naye aweza kumwekea sharuti Mola wake kwa kuchelea kutokea jambo k.v. ugonjwa. Atasema: Nitakapofungizika kwa jambo lolote, basi kujifungua kwangu ni pale nilipofungizika. (Basi atakapopatikaniwa na udhuru aweza kujifungua kutoka katika ihramu yake, wala hatowajibika kwa chochote kile. Lakini asipoweka sharuti hiyo na akapata udhuru wa kujifungua kutoka katika ihramu, atawajibika kuchinja na kuhiji tena mwakani). Hatimaye ataendelea na Talbiya.

(Talbiya katika 'Umra ni kuanzia kuhirimia mpaka atapoanza kutufu. Na katika Hajj ni kuanzia kuhirimia mpaka atapoanza kurusha vijiwe Jamratul-'aqaba siku ya Idi).

Mwenye kufanya tamatui atahirimia mahala alipoteremka, hata watu wa Makka watahirimia Makka. Haya yote ni kwa anaefanya tamatui. Ama mwenye kufanya kiran na ifrad hawataacha kuwa katika ihram zao kuanzia Miiqaat.

2. Mahujaji wote wataenda Mina, wataswali huko adhuhuri, alasiri, magharibi, isha na alfajiri, watapunguza bila kujumuisha. Watalala Mina usiku huko, nao ni usiku wa kuamkia siku ya tisa. Kulala Mina usiku huo ni sunna. Mwenye kuhiji asipolala halazimiki kutoa fidia yoyote ile.

## YANAYOFANYWA SIKU YA 'ARAFA:

1. Juwa litapochomoza siku ya 'Arafa - nayo ni siku ya tisa - mahujaji wataenda kutoka Mina hadi 'Arafa kwa upole, taratibu na kuleta Talbiya. Wakifika watahakikisha mipaka yake sawasawa na watateremka pale patakapowasahilikia.

2. Juwa likipinduka, wataswali adhuhuri na alasiri - pamoja na Imamu ikiwezekana - jam'u takdim pamoja na kukusuru (kupunguza). Kwa muadhini mmoja na kukimu mara mbili.

3. Baada ya hapo, atakaa faragha na kufanya Dhikri,

kuomba dua na kumnyenyekea ALLAH pamoja na kuuhudhurisha moyo, kuinyanyau mikono wakati wa kuomba na kuelekea Qibla.

Basi Mahujaji hawataacha kuwa katika hali hiyo, wakileta Dhikri na Talbiya na wakiomba mpaka juwa litapozama, baada ya kuzama juwa wataenda Muzdalifa kwa upole na utulivu, huku wakishughulika na Dhikri, istighfaar na kuleta Talbiya.

4. Haifai kwa aliesimama 'Arafa nae ni mwenye kuhiji kutoka katika mipaka yake hadi machweo ya juwa siku hiyo ya 'Arafa. Kwa sababu Mtume (S.A.W.) alisimama hadi machweo, akanena:

« لتأخذوا عني مناسككم »

**"Muchukue kutoka kwangu ibada zenu (za Hajj)."** (Muslim).

Na atakaeondoka kabla machweo na akatoka 'Arafa, atawajibika kurudi hapo na kubakia hadi machweo ya juwa. Asiporudi atapata dhambi na atawajibika kutoa fidia.

5. Ambae hakufika 'Arafa ela baada ya kuzama juwa, basi inamtosha kusimama mda mchache, hata kama ni kupita tu. Wakati wa kusimama 'Arafa unaendelea mpaka kutokeza alfajiri siku ya Idi. Atakaetokezewa na alfajiri siku ya Idi wala hakusimama 'Arafa, basi Hajj imempita. Lakini atapokuwa ameeka sharuti tangu mwanzo wa kuhirimia akasema: **"Nitapofungizika kwa jambo lolote, basi kujifungua kwangu ni pale nilipofungizika"**, atajifingua kutoka katika ihram yake, wala hana kitu juu yake. Na atapokuwa hakuweka sharuti na akapitwa kusimama 'Arafa, basi atajifungua kwa 'Umra, ataenda kwenye Alkaaba, atatufu, atasaayi na atanyoa, akiwa ana mnyama atamchinja. Utakapokuja mwaka wa pili atailipa Hajj iliyompita na atachinja mnyama. Asipopata mnyama atafunga siku kumi, siku tatu katika Hajj na siku saba ataporejea kwa watu wake.

## YANAYOFANYWA MUZDALIFA:

1. Mahujaji watapofika Muzdalifa wataswali magharibi na isha kwa kujumuisha kwa mwadhini mmoja na kukimu mara mbili pamoja na kuikusuru Swala ya isha rakaa mbili, kisha watateremka

na watalala hapo.

2. Itapofika katikati ya usiku, inafaa kwa watu madhaifu kama vile wanawake, watoto, wazee na mfano wao na wanaowahitajia katika watu wenye nguvu ili kuwatumikia, inafaa kwa wote hao kuondoka Muzdalifa kwenda Mina. Watapofika Mina watarusha vijiwe Jamratul-aqaba.

Ama wale wenye nguvu waliosuhubiana na wenye nyudhuru hawatarusha mawe ela baada ya kuchomoza juwa.

3. Ama wale wenye nguvu zao lakini hawana watu madhaifu, watakamilisha kulala Mina mpaka alfajiri na wataiswali Swala ya alfajiri hapo Muzdalifa mwanzo wa wakati wake. Kisha ikiwezekana wataenda Al-Mash'aril-Haram, watashughulika na Dhikri, dua na kumnyenyekea ALLAH mpaka karibu na kuchomoza juwa.

4. Mahujaji wataenda Mina kabla ya kuchomoza juwa.

5. Haijuzu kuondoka Muzdalifa kabla ya katikati ya usiku. Atakaeondoka kabla ya hapo atapata dhambi na atalazimika kutoa fidia asiporudi. Kwa sababu kulala hapo (muzdalifa) ni waajib miongoni mwa wajibati za Hajj, na uchache wake ni mpaka katikati ya usiku.

6. Anaefika Muzdalifa baada ya nusu ya usiku inamtosha kuwa hapo wakati mchache, hata kama ni kupita.

7. Ambae hakufika Muzdalifa ela baada ya kutokeza alfajiri ya usiku wa Idi na akaidiriki Swala na akawa ameshasimama 'Arafa kabla ya alfajiri, Hija yake ni Sahihi. Kwa sababu Mtume (S.A.W.) amesema:

« من شهد صلاتنا هذه - يعني الفجر بمزدلفة - ووقف معنا حتى ندفع وقد وقف بعرفة قبل ذلك ليلاً أو نهاراً فقد تم حجه وقضى تفثه »

**"Atakaeshuhudia Swala yetu hii - yaani ya alfajiri, Muzdalifa - na akasimama pamoja nasi mpaka tukaondoka na akawa ameshasimama 'Arafa kabla ya hapo usiku au mchana, basi Hija**

(a). Kurusha vijiwe Jamratul-'aqaba.
(b). Kuchinja mnyama ikiwa anaye.
(c). Kunyoa au kupunguza.
(d). Kutufu tawafu ya ifadha na kusaayi baadaye iwapo katika haki yake amebakisha kusaayi.

Kisharia na ubora zaidi ni kutekeleza kwa mpangilio huu. Na iwapo amali nyingine atazitanguliza mbele ya nyingine inajuzu wala hapana ubaya. Kwa sababu, Mtume (S.A.W.) alipoulizwa siku hiyo - siku ya Idi - kuhusu kila amali ilotangulizwa au kuakhirishwa alinena:

« إفعل ولا حرج »

**"Fanya wala hapana ubaya."** (Muttafaq).

2. Kujifungua mara ya kwanza - nako ni kujifungua kunakomhalalishia kila kitu mwenye kuhirimia ispokuwa kuingiliana na wakeze - hupatikaniwa kwa kufanya mambo mawili katika jumla ya mambo matatu: Kurusha vijiwe Jamratul-'aqaba, kunyoa au kupunguza na kutufu tawafu ya ifadha, na kusaayi kwa aliebakisha kusaayi. Basi atakapolifanya jambo hilo la tatu atakuwa ameshafunguka mara ya pili, na ni halali kwake kila kitu, hata wakeze.

3. Haitoshelezi katika kuchinja fidia ela mnyama anaefaa kuchinjwa katika udh-hiya. Awe ameshafikia umri unaozingatiwa kisharia, nao ni miezi sita kwa kondoo, mwaka kwa mbuzi, miaka miwili kwa ng'ombe na miaka mitano kwa ngamia. Awe ameepukana na aibu, k.v. ugonjwa, uzee, ukondefu uchongo, upofu, kiwete na kukosekaniwa chochote katika viungo vyake.

4. Kiasi cha mnyama wa kuchinja aliepasa kwa aliefanya tamatui na qiran ni mbuzi mmoja, naye (mbuzi huyo) hutosha kwa mtu mmoja pekee. Au sehemu ya saba katika ngamia, au sehemu ya saba katika ng'ombe.

(Yaani watu saba washirikiane kununua ngamia au ng'ombe halafu wamchinje).

5. Ambae hakupata mnyama wa kuchinja atawajibika kufunga siku tatu akiwa Hajj na siku saba ataporejea kwa watu wake. Inajuzu siku tatu hizo azifunge katika siku za tashriq, nazo ni

tarehe 11, 12 na 13 katika mwezi wa Dhul-Hajj (Mfungo Tatu).

Nana 'Aisha na Ibni 'Umar (R.A.) wamenena:

« لم يرخص في أيام التشريق أن يصمن إلا لمن لم يجد الهدي »

**"Siku za tashriq hazikuruhusiwa kufungwa ela kwa ambae hakupata mnyama wa kuchinja."** (Bukhari).

Aydha, inajuzu kufunga siku hizo kabla ya hapo (siku za tashriq), baada ya kuhirimia 'Umra. Lakini hatozifunga siku ya Idi wala siku ya 'Arafa kwa sababu:

« النبي ﷺ نهى عن صوم العيدين ونهى عن صوم يوم عرفة بعرفة »

**"Mtume (S.A.W.) amekataza mtu kufunga Idi mbili. Na akakataza mtu kufunga siku ya 'Arafa ilihali naye yupo hapo 'Arafa."**

(Tazama katika mlango wa Saumu, katika siku ambazo ni haramu na ni makruhu mtu kufunga.)

## YANAYOFANYWA SIKU ZA TASHRIQ:

Kama ilivyotangulia, siku za tashriq ni tarehe 11, 12 na 13 katika mwezi wa Dhul-Hajj (Mfungo Tatu).

Yanayofanywa katika siku hizo ni mambo mawili, nayo ni:

1. Kulala Mina masiku ya siku zake, na kulala Mina masiku ya siku za tashriq ni waajib miongoni mwa wajibati za Hajj. Ambae hakulala sehemu hiyo bila ya kuwa ana udhuru, basi atawajibika kuchinja. Kiasi kinachotosha kulala sehemu hiyo ni kuketi na kuwepo hapo Mina katika usiku mrefu zaidi kiasi kitakachowezekana, iwe ni mwanzo wa usiku au mwishowe. Lau atateremka Makka mwanzo wa usiku kisha akarejea kabla ya nusu ya usiku, au akaondoka Mina baada ya nusu ya usiku basi hapana ubaya wowote, kwani ameshatekeleza wajibu.

2. Kurusha vijiwe sehemu tatu katika siku hizo. Wakati wa kurusha ni baada ya kupinduka juwa.

* Atarusha vijiwe hapo Jamratussughra, sehemu hiyo ni

mbali zaidi ya Makka kuliko zile Jamra nyingine. Atarusha vijiwe saba kufwatana kimoja baada kingine. Kila arushapo atapiga Takbira. Kisha ataenda mbele kidogo na ataomba dua yoyote aipendayo katika kheri za dunia na Akhera kiasi awezavyo.

* Kisha atarusha vijiwe hapo Jamratulwusta, vijiwe saba kufwatana. Kila anaporusha kijiwe atapiga Takbira. Halafu ataelekea upande wa kushoto, atasimama hali ameelekea Qibla, ataomba dua anavyopenda.

* Kisha atarusha vijiwe hapo Jamratulkubra, vijiwe saba kufwatana, atapiga Takbira kila arushapo kijiwe, kisha ataondoka bila ya kuomba dua.

Utaratibu huu katika kurusha vijiwe sehemu hizo ni waajib kuufuata. Ataanzia Jamratussughra, kisha Jamratulwusta, hatimae Jamratul'aqaba.

* Swala tano zitaswaliwa kwa wakati wake siku za Tashriq bila ya kujumuishwa. Lakini Swala yenye rakaa nne itakusuriwa hadi rakaa mbili.

3. Al-Hajj atapomaliza kurusha vijiwe siku ya tarehe 12 akitaka ataharakisha atoke Mina na akitaka ataakhirisha alale hapo usiku wa kuamkia 13.

Kurusha mawe sehemu hizo tatu ni baada ya kupinduka siku ya 13.

Kuakhirisha ni bora zaidi kuliko kuharakisha. Al-Hajj ana hiari baina ya mambo hayo mawili. Haimpasi kuakhirisha ela katika hali ya juwa kuzama na ilihali Al-Hajj yupo Mina.

## TAWAFU YA KUAGA:

Yapasa kwa Al-Hajj atapomaliza amali zake za Hajj na akataka kuondoka Makka atufu tawafu ya kuaga. Atazunguka mizunguko saba bila ya kusaayi.

Mtume (S.A.W.) amesema:

« لا ينفر أحدكم حتى يكون آخر عهده بالبيت »

**"Asiondoke mmoja wenu mpaka iwe mwisho wa wakati wake**

**(ibada zake) ni kutufu Al-Kaaba."** (Muslim).Kwa mwanamke mwenye hedhi au nifasi atasafiri bila kuaga, ispokua atapotwahirika kabla ya kufarikiana na majengo ya Makka, hapo itamlazimu tawafu ya kuaga.

## UFUPISHO WA KUFANYA 'UMRA:

1. Ihramu: Baada ya kuvuwa nguo (za kawaida) na kufanya yanayotakiwa kuyafanya wakati wa ihramu - kama ilivyotangulia - mwenye kufanya 'Umra atavaa nguo ya ihramu na atanuiliya ibada ya 'Umra - hapo Miqati - kwa kusema:

لبيك اللهم عمرة

kisha ataendelea kuleta Talbiya kwa kuinua sauti:

لبيك اللهم لبيك . لبيك لا شريك لك . . . .

2. Kutufu: Atapofika Makka ataenda Haram na ataitufu Al-Kaaba mizunguko saba, ataanzia penye jiwe leusi na atamalizikia papo hapo. Atapomaliza kutufu ataswali rakaa mbili nyuma ya Maqamu ya Nabii Ibrahim (A.S.).

3. Kusaayi: Ataenda katika Kusaayi, atapanda juu ya jabali la Swafaa na ataelekea Qibla ilihali ya kuiyenua mikono yake huku akinena:

إن الصفا والمروة من شعائر الله نبدأ بما بدأ الله به

**"Hakika Swafaa na Marwa ni katika alama za kuadhimisha Dini ya ALLAH. Twaanza kwa alipoanzia ALLAH."**

Kisha atanena:

لا إله إلا الله وحده لا شريك له له الملك وله الحمد وهو
على كل شيء قدير ، لا إله إلا الله وحده أنجز وعده ونصر عبده
وهزم الأحزاب وحده ،

Atakariri mara tatu na ataomba dua. Na atafanya kama hivyo

atapokua Marwa, ataendelea kuomba dua kila atapopanda juu ya jabali la Swafaa au Marwa. Atapofika baina ya zile alama mbili za kijani ataenda kwa haraka zaidi. Kusaayi ni mara saba, kuenda ni mara moja na kurudi ni mara ya pili hadi mwisho.

4. Kunyoa au kupunguza: Atazinyoa nywele zake zote (za kichwani) au atazipunguza. Na kwa kunyoa huko au kupunguza, atakua ameshamaliza 'Umra yake. Atafungua ihramu yake.

## UFUPISHO WA KUFANYA HAJJ:

1. Al-Hajj atavaa ihramu yake siku ya 8 mwezi wa Dhul-Hajj (Mfungo tatu) hapo Makka, na atanuwiya Hajj kwa kunena:

لبيك اللهم بحجة

Ataenda Mina, atalala huko na ataswali adhuhuri, alasiri, magharibi, isha na alfajiri, kila Swala kwa wakati wake bila ya kujumuisha, pamoja na kuikusuru Swala ya rakaa nne kuifanya rakaa mbili.

2. Ataenda hadi 'Arafa siku ya 9 baada ya kuchomoza juwa. Ataswali adhuhuri na alasiri kwa kujumuisha na kukusuru na kwa muadhini mmoja na kukimu mara mbili, pamoja na kuhakikisha kuwa anapatikaniwa ndani ya mipaka ya 'Arafa.

3. Baada ya juwa kuzama, ataondoka 'Arafa kwa utaratibu na kuelekea Muzdalifa. Ataswali magharibi na isha kwa kujumuisha na kwa muadhini mmoja na kukimu mara mbili, pamoja na kuikusuru Swala ya isha kuifanya rakaa mbili. Na atalala hapo Muzdalifa, ataswali alfajiri hapo na atamtaja ALLAH hapo Mash'aril-Haraam. Inajuzu kwa wenye nyudhuru kuondoka hapo baada ya nusu ya usiku.

4. Ataondoka Muzdalifa kabla kuchomoza juwa, ataelekea Mina. Siku hii ni siku ya Idi. Atarusha vijiwe hapo Jamratul - Kubra, vijiwe vyenyewe ni saba. Kila anaporusha atapiga Takbira.

5. Atachinja mnyama wake Mina au Makka siku ya Idi na kuendelea siku tatu baadae, atakula na atatoa Sadaka (mnyama huyo). Akiwa hamiliki thamani ya kuchinja mnyama, atafunga siku tatu akiwa Hajj na siku saba ataporudi kwao.

6. Atanyoa au kupunguza nywele zake. Na kwa amali hiyo (ya kunyoa au kupunguza) atajifungua kwa mara ya kwanza, kila kitu kitakuwa halali kwake ispokuwa mkewe.

7. Ataelekea Makka atufu tawafu ya ifadha na asaayi baada yake ikiwa ni mwenye kufanya tamatui au la na wala hakuwa amesaayi pamoja na tawaful-qudum. Na kwa amali hii atakuwa amejifungua kwa mara ya pili, kila kitu kitakua halali kwake hata wakeze.

8. Kisha atarejea Mina, atalala huko masiku ya tashriq pamoja na kurusha vijiwe kwenye Jamra zote tatu: Sughra, Wusta na Kubra katika siku hizo.

9. Atakapotaka kutoka Makka, atatufu tawafu ya kuaga bila ya kusaayi na atasafiri moja kwa moja.

## KUUZURU MSIKITI MTUKUFU WA MTUME (S.A.W.):

Kuuzuru Msikiti Mtukufu wa Mtume (S.A.W.) ni sunna iliothibiti ilopendekezeshwa, wala haina wakati maalumu katika mwaka na wala haina mafungamano yoyote na Hajj. Atakaehiji na asipate nafasi ya kuuzuru Msikiti wa Mtume (S.A.W.), Hajj yake itakuwa imetimia na ni Swahihi.

Katika kuuzuru Msikiti wa Mtume (S.A.W.) muna adabu, kwa ufupi ni kama zifwatazo:

1. Anaenuwiya kwenda Madina, atanuwiliya kuuzuru Msikiti wa Mtume (S.A.W.), kadhalika kulizuru kaburi lake itakuwa pia ishaingia.

2. Atapoingia Msikitini atautanguliza mguu wake wa kulia na atasema:

« بسم الله والصلاة والسلام على رسول الله ، اللهم اغفر لي ذنوبي وافتح لي أبواب رحمتك » .

**"Kwa Jina la ALLAH. Rehma na Amani imwendee Mtume wa ALLAH. Ewe Mola nisamehe dhambi zangu na unifungulie milango ya Rehma Zako."**

3. Ataswali rakaa mbili za Tahiyyatul-Masjid. Na ubora zaidi ni aziswali hapo Raudha, napo ni baina ya Mimbari ya Mtume (S.A.W.) na chumba chake.

4. Atasimama kwa kulielekea Kaburi la Mtume (S.A.W.), awe na adabu na utulivu. Atasema:

السلام عليك يا رسول الله ، السلام عليك يا نبي الله ، السلام عليك يا خيرة خلق الله ، السلام عليك أيها النبي ورحمة الله وبركاته ، اللهم صل على محمد وعلى آل محمد كما صليت على إبراهيم وعلى آل إبراهيم ، وبارك على محمد وعلى آل محمد كما باركت على إبراهيم وعلى آل إبراهيم إنك حميد مجيد ، أشهد أنك عبد الله ورسوله ، وأنك بلغت الرسالة وأديت الأمانة ، ونصحت الأمة ، وجاهدت في الله حق جهاده ، فجزاك الله عن أمتك أفضل ما جزى نبياً عن أمته .

**"Amani iwe juu yako ewe Mtume wa ALLAH. Amani iwe juu yako ewe Nabii wa ALLAH. Amani iwe juu yako ewe Mbora wa viumbe vya ALLAH. Amani iwe juu yako ewe Nabii, na Rehema za ALLAH na Baraka Zake."**

**"Ewe Mola, mrehemu Muhammad na Aali wa Muhammad kama ulivyomrehemu (Nabii) Ibrahimu na Aali wa Ibrahimu. Na umbariki Muhammad na Aali wa Muhammad kama ulivyombariki Ibrahimu na Aali wa Ibrahimu. Hakika Wewe ni Mwenye kuhimidiwa, Mwenye kutukuzwa."**

**"Nashuhudia kuwa wewe (Muhammad) ni mja wa ALLAH na ni Mtume Wake, na kwamba wewe umeufikisha ujumbe, ukaitekeleza amana, ukaunasihi Umma na ukapigania katika njia ya ALLAH haki ya kupigana."**

**"ALLAH Akujazi - kutoka kwa Umma wako - majaza mema zaidi kuliko alivyomjazi Nabii yeyote kutoka kwa Umma**

**wake."**

5. Kisha atavuta hatua kidogo upande wa kulia, atamsalimia Sayyidna Abubakar Assiddiq na kumwombea radhi, atanena:

السلام عليك أبا بكر الصديق صفي رسول الله

وصاحبه في الغار ، جزاك الله عن أمة رسول الله ﷺ خيراً ،

**"Amani iwe juu yake ewe Abubakar Assiddiq rafiki mukhlis wa Mtume wa Mwenyezi Mngu na ni swahiba yake katika pango. ALLAH Akujazi kutoka kwa Umma wa Mtume wa Mwenyezi Mngu (S.A.W.) majazi mema."**

Kisha atavuta tena hatua kidogo upande wa kulia, atamsalimia Sayyidna 'Umar bin Al-Khattab na kumwombea radhi, atanena: السلام عليك يا عمر الفاروق ورحمة الله وبركاته ،

جزاك الله عن أمة رسول الله ﷺ خيراً

**"Amani iwe juu yako-ewe 'Umar Alfaaruuq - na Rehma za ALLAH na Baraka Zake. ALLAH Akujazi kutoka kwa Umma wa Mtume wa Mwenyezi Mngu majaza mema."**

Hatimaye ataondoka.

6. Atakapotaka kumuomba ALLAH, atakaa mbali na kaburi, aelekee Qibla na hapo amwombe ALLAH namna anavyotaka.

Hapo itakuwa ndio mwisho wa ziara.

7. Kadhalika yapendekezwa kwa mwenye kuzuru aswali Msikiti wa Qubaa, azuru Baqii na mashahidi wa vita vya Uhud.

## ILIVYOKUA HAJJ YA MTUME (S.A.W.):

Jabir bin 'Abdulla (R.A.) amesema:

عن جابر بن عبد الله رضي الله عنهما قال : « أن رسول الله ﷺ مكث تسع سنين(1) لم يحج ، ثم أذن في الناس في العاشرة أن رسول الله ﷺ حاج . فقدم المدينة بشر كثير كلهم يلتمس أن يأتم برسول الله ﷺ ، ويعمل مثل عمله ، فخرجنا معه حتى أتينا ذا الحليفة ،

فولدت أسماء بنت عميس محمد بن أبي بكر . فأرسلت إلى رسول الله ﷺ : كيف أصنع ؟ قال « اغتسلي واستثفري[٢] بثوب وأحرمي » فصلى رسول الله ﷺ في المسجد . ثم ركب القصواء[٣] حتى إذا استوت به ناقته على البيداء نظرت إلى مد بصري بين يديه من راكب وماش وعن يمينه مثل ذلك وعن يساره مثل ذلك ومن خلفه مثل ذلك ، ورسول الله ﷺ بين أظهرنا وعليه ينزل القرآن وهو يعرف تأويله وما عمل به من شيء عملنا به . فأهل بالتوحيد[٤] « لبيك اللهم لبيك ، لبيك لا شريك لك لبيك ، إن الحمد والنعمة لك والملك لا شريك لك » ، وأهل الناس بهذا الذي يهلون به فلم يرد رسول الله ﷺ عليهم شيئاً منه ولزم رسول الله ﷺ تلبيته . قال جابر رضي الله عنه : لسنا ننوي إلا الحج ، لسنا نعرف العمرة حتى إذا أتينا البيت معه استلم الركن فرمل ثلاثاً ومشى أربعاً ثم نفذ إلى مقام إبراهيم عليه السلام فقرأ : ﴿ وَاتَّخِذُوا مِنْ مَقَامِ إِبْرَاهِيمَ مُصَلًّى ﴾ فجعل المقام بينه وبين البيت . فكان أبي يقول : « ولا أعلمه ذكره إلا عن النبي ﷺ » : كان يقرأ في الركعتين « قل هو الله أحد ، وقل يا أيها الكافرون » . ثم رجع إلى الركن فاستلمه . ثم خرج من الباب[١] إلى الصفا ، فلما دنا من الصفا قرأ ﴿ إِنَّ الصَّفَا وَالْمَرْوَةَ مِنْ شَعَائِرِ اللَّهِ ﴾ أبدأ بما بدأ الله به ، فبدأ بالصفا فرقى عليه حتى رأى البيت فاستقبل القبلة فوحد الله وكبره وقال : لا إله إلا الله وحده لا شريك له . له الملك وله الحمد وهو على كل شيء قدير لا إله إلا الله وحده أنجز وعده ونصر عبده وهزم الأحزاب وحده ، ثم دعا بين ذلك ، قال مثل هذا ثلاث مرات .

ثم نزل إلى المروة حتى إذا انصبت[٢] قدماه في بطن الوادي سعى

حتى إذا صعدتا[٣] مشي حتى أتى المروة ففعل على المروة كما فعل على الصفا ، حتى إذا كان آخر طوافه على المروة فقال : لو أني استقبلت من أمري ما استدبرت لم أسق الهدي وجعلتها عمرة ، فمن كان منكم ليس معه هدي فليحل وليجعلها عمرة . فقام سراقة بن مالك بن جعشم فقال : يا رسول الله ! ألعامنا هذا أم لأبد ؟ فشبك رسول الله ﷺ أصابعه واحدة في الأخرى وقال : « دخلت العمرة في الحج مرتين ، لا بل لأبد أبد » .

وقدم عليٌّ من اليمن ببدن[١] النبي ﷺ فوجد فاطمة رضي الله عنها ممن حل ولبست ثياباً صبيغاً واكتحلت ، فأنكر ذلك عليها . فقالت : إن أبي أمرني بهذا . قال : فكان علي يقول بالعراق : فذهبت إلى رسول الله ﷺ محرِّشاً[٢] على فاطمة للذي صنعت مستفتياً لرسول الله ﷺ فيما ذكرت عنه فأخْبَرْتُه أني أنكرتُ ذلك عليها . فقال : صَدقتْ صدَقتْ . ماذا قلتَ حين فرضتَ الحج ؟ قال : قلت : اللهم إني أهل بما أهل به رسولك . قال : فإن معي الهدي فلا تحل . قال : فكان جماعة الهدي الذي قدم به علي من اليمن والذي أتى به النبي ﷺ مائة . قال : فحل الناس كلهم وقصروا إلا النبي ﷺ ومن كان معه هدي . فلما كان يوم التروية توجهوا إلى منى فأهلوا بالحج وركب رسول الله ﷺ فصلى بها الظهر والعصر والمغرب والعشاء والفجر . ثم مكث قليلاً حتى طلعت الشمس وأمر بقبة من شعر تضرب له بنمرة[٣] فسار رسول الله ﷺ ولا تشك قريش إلا أنه واقف عند المشعر الحرام[٤] ، كما كانت قريش تصنع في الجاهلية

فأجاز[١] رسول الله ﷺ حتى أتى عرفة . فوجد القبة قد ضربت له بنمرة . فنزل بها . حتى إذا زاغت الشمس أمر بالقصواء فرحلت[٢] له . فأتى بطن الوادي[٣] فخطب الناس وقال : « . . . إن دماءكم وأموالكم حرام عليكم كحرمة يومكم هذا في شهركم هذا في بلدكم هذا ألا كل شيء من أمر الجاهلية تحت قدمي موضوع ودماء الجاهلية موضوعة ، وإن أول دم أضع من دمائنا دم ابن ربيعة بن الحارث ، كان مسترضعاً في بني سعد فقتلته هذيل ، وربا الجاهلية موضوع ، وأول ربا أضع ربانا ربا عباس بن عبد المطلب ، فإنه موضوع كله . فاتقوا الله في النساء فإنكم أخذتموهن بأمان الله واستحللتم فروجهن بكلمة الله ولكم عليهن ألا يوطئن فرشكم أحداً تكرهونه . فإن فعلن ذلك فاضربوهن ضرباً غير مبرح ولهن عليكم رزقهن وكسوتهن بالمعروف ، وقد تركت فيكم ما لن تضلوا بعده إن اعتصمتم به . كتاب الله وأنتم تسألون عني فما أنتم قائلون ؟ قالوا : نشهد أنك قد بلغت وأديت ونصحت . فقال بأصبعه السبابة يرفعها إلى السماء وينكتها إلى الناس : اللهم اشهد ، اللهم اشهد ، ثلاث مرات . ثم أذن ثم أقام فصلى الظهر ، ثم أقام فصلى العصر ولم يصل بينهما شيئاً . ثم ركب رسول الله ﷺ حتى أتى الموقف فجعل بطن ناقته القصواء إلى الصخرات[١] ، وجعل جبل المشاة[٢] بين يديه واستقبل القبلة ، فلم يزل واقفاً حتى غربت الشمس وذهبت الصفرة قليلاً حتى غاب القرص وأردف أسامة خلفه ودفع رسول الله ﷺ وقد شنق[٣] للقصواء الزمام حتى إن رأسها ليصيب مورك[٤] رحله ويقول بيده اليمنى : أيها الناس السكينة السكينة . كلما أتى حبلاً من الحبال أرخى لها قليلاً حتى تصعد حتى أتى المزدلفة فصلى بها المغرب والعشاء بأذان واحد وإقامتين ولم يسبح بينهما شيئاً ، ثم اضطجع رسول الله ﷺ حتى طلع

الفجر وصلى الفجر حين تبين له الصبح بأذان وإقامة ثم ركب القصواء حتى أتى المشعر الحرام فاستقبل القبلة فدعاه وكبره وهلله ووحده فلم يزل واقفاً حتى أسفر جداً فدفع قبل أن تطلع الشمس وأردف الفضل بن عباس وكان رجلاً حسن الشعر أبيض وسيماً فلما دفع رسول الله ﷺ مرت به ظعن[٥] يجرين فطفق الفضل ينظر إليهن فوضع رسول الله ﷺ يده على وجه الفضل فحول الفضل وجهه إلى الشق الآخر ينظر فحول رسول الله ﷺ يده من الشق الآخر على وجه الفضل يصرف وجهه من الشق الآخر ينظر حتى أتى بطن محسر فحرك قليلاً ثم سلك الطريق الوسطى التي تخرج على الجمرة الكبرى حتى أتى الجمرة عند الشجرة فرماها بسبع حصيات يكبر مع كل حصاة منها ـ حصى الخذف ـ رمى من بطن الوادي ثم انصرف إلى المنحر فنحر ثلاثاً وستين بيده ثم أعطى علياً فنحر ما غبر[١] وأشركه في هديه ثم أمر من كل بدنة ببضعة[٢] ، فجعلت في قدر فطبخت فأكلا من لحمها وشربا من مرقها ثم ركب رسول الله ﷺ فأفاض إلى البيت[٣] ، فصلى بمكة الظهر فأتى بني عبد المطلب يسقون على زمزم فقال : انزعوا[٤] بني عبد المطلب ! فلولا أن يغلبكم الناس[٥] على بسقايتكم لنزعت معكم . فناولوه دلواً فشرب منه »[٦]

**"Mtume (S.A.W.) aliketi miaka tisa bila kuhiji. Kisha katika mwaka wa kumi watu wakatangaziwa kuwa Mtume (S.A.W.) ameazimu kuhiji. Watu wengi wakafika Madina, kila mmoja anataka kumfuata Mtume (S.A.W.) na afanye kama afanyavyo. Basi tukatoka naye hata tukafika Dhalhulaifa. Asmaa binti 'Umays akamzaa Muhammad bin Abubakar, akampelekea salamu Mtume (S.A.W.) kuwa: nifanyeje?"** (Mtume S.A.W.)

akamwambia: **"Jioshe ujifunge nguo (sehemu za chini) na uhirimie."** Mtume (S.A.W.) akaswali Msikitini. Halafu akampanda ngamia wake aitwae Al-qaswaa, hata ngamia wake alipolingana sawia katika jangwa, nikatazama upeo wa kuona kwangu, mbele yake (Mtume S.A.W.) kulikuweko waliokua wamepanda juu ya vipando na wanaotembea, kuliani kwake vivyo hivyo, kushotoni kwake vivyo hivyo na nyuma yake ni vivyo hivyo. Mtume (S.A.W.) alikua nasi huku Qur'ani ikimteremkia, nae akiijua taawili yake. Chochote anachokifanya nasi twakifanya.

Akaiyenua sauti yake kwa Talbiya: « لبيك اللهم لبيك ،

لبيك لا شريك لك لبيك ، إن الحمد والنعمة لك والملك لا شريك لك »

Watu nao wakanyanyua sauti zao kwa Talbiya hii wanayoitoa, wala Mtume (S.A.W.) hakuwarudi kwa chochote, bali aliendelea na Talbiya yake.

Jabir (R.A.) anasema: Tulikua hatunuwii ispokua Hajj, tulikua hatujui 'Umra mpaka tukafika katika Al-Kaaba pamoja nae, akaipangusa nguzo, akatembea mwendo wa haraka mara tatu na akatemba kiada mara nne, kisha akaenda katika Maqamu Ibrahim (A.S.) akasoma:

﴿ وَاتَّخِذُوا مِنْ مَقَامِ إِبْرَاهِيمَ مُصَلًّى ﴾

Maqamu ikawa iko baina yake na Al-Kaaba. Baba yangu akawa akisema: Sijui alietaja jambo hilo ispokuwa latoka kwa Mtume (S.A.W.). Alikua katika rakaa mbili akisoma Qul-Huwallahu Ahad na Qul-yaa ayyuhal-kaafiroon, kisha akarudi katika nguzo na akaipangusa. Halafu akatoka katika mlango mpaka Swafaa. Alipokaribia Swafaa alisoma:

﴿ إِنَّ الصَّفَا وَالْمَرْوَةَ مِنْ شَعَائِرِ اللَّهِ ﴾ أبدأ بما بدأ الله به ،.

Akaanzia Swafaa akapanda juu hata akawa anaiyona Al-Kaaba. Akaelekea Qibla, akampwekesha ALLAH, akamtukuza na akasema:

لا إله إلا الله وحده لا شريك له .

له الملك وله الحمد وهو على كل شيء قدير لا إله إلا الله وحده أنجز وعده ونصر عبده وهزم الأحزاب وحده ،

Kisha akaomba dua. Akasema kama hivi mara tatu.

Halafu akateremka akaenda Marwa, hata nyayo zake zilipoteremka katikati ya uwanja akasaayi, hata nyayo zake zikainuka, akatembea hata akaja Marwa. Hapo Marwa akafanya kama alivyofanya Swafaa. Ilipofikia mwisho wa kutufu kwake hapo Marwa, alisema: **"Lau ningalidhihirikiwa hapo mwanzoni, na yale niliodhihirikiwa nayo mwishoni, nisingalichukuwa mnyama wa kuchinja. Basi ambae miongoni mwenu hana mnyama wa kuchinja na ajifungue kisha ajaalie (Hajj yake) kuwa ni 'Umra."** Suraqa bin Maalik bin Ju'sham akauliza: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, ni kwa ajili ya mwaka wetu huu au hata milele? Mtume (S.A.W.) akaviingiza vidole vya mkono wake kwenye vidole vya mkono mwingine na akasema: "'Umra imeingia katika Hajj." Mara mbili, **"bali ni milele, milele."**

Sayyidna 'Ali akaja kutoka Yemen na ngamia wa Mtume (S.A.W.). Akamkuta Fatima (R.A.) miongoni mwa waliofungua ihramu zao, amevaa nguo ya rangi na amejipaka wanja. Akamkataza kufanya hivyo. (Fatima) akasema: Baba yangu ameniamuru kufanya hivi.

Sayyidna 'Ali anasema: Nikamwendea Mtume (S.A.W.) nikimlalamikia alivyofanya Fatima. Nikawa nataka fatwa kwa Mtume (S.A.W.), nikamweleza kuwa jambo hilo (la kufungua ihramu) nilimkataza Fatima. Mtume (S.A.W.) akasema: **"Amesadiki, amesadiki. Ulisema nini ulipofaradhia Hajj?"** Akasema: Nilisema: **"Ewe Mola, mimi nahirimia kwa ihramu aliyoihirimia Mtume wako."** **(Mtume) akasema: "Basi mimi nnae mnyama wa kuchinja, usifungue ihramu."**

Likawa lile kundi la wanyama wa kuchinja alilokuja nalo Sayyidna 'Ali kutoka Yemen na alilokuja nalo Mtume (S.A.W.) lafika mia (100).

Wengi wao wakajifunuga na wakapunguza, ispokuwa Mtume (S.A.W.) na aliyekuwa ana mnyama wa kuchinja.

Ilipofika siku ya tarwiya, walielekea Mina na wakahirimia Hajj. Mtume (S.A.W.) akapanda (Mnyama wake). Akaswali adhuhuri, alasiri, magharibi, isha na alfajiri mahala hapo. Kisha akaketi kidogo mpaka juwa likachomoza. Akaamuru afanyiwe kuba la nywele. Mtume (S.A.W.) akaenda, na Makureshi walikuwa hawatii shaka kuwa Mtume (S.A.W.) atasimama hapo Mash'aril-Haraam, kama walivyokuwa Makureshi wakifanya zama za ujahiliya. Mtume (S.A.W.) akapapita mahala hapo akaenda karibu na 'Arafa.

Akaona kuwa ashaekewa kuba hapo Namira, akateremka.

Juwa lilipopondoka, aliamuru aletewe (ngamia wake) Al-qaswa, akabebeshwa mizigo. Akaenda katikati ya wangwa (wa 'Urana). Akawakhutubia watu, akasema:

**"....Hakika damu zenu na mali yenu ni vitu vitukufu juu yenu, kama utukufu wa siku yenu hii, katika mwezi wenu huu, katika mji wenu huu."**

**"Jueni na kutanabahi, kila kitu kilichokuwa katika ujahiliya, kiko chini ya mguu wangu kimebatilishwa, na damu (zote) za ujahiliya zimebatilishwa. Damu ya kwanza nitakayoibatilisha ni damu yetu ya Ibni Rabi'a bin Al-Harith. Alikuwa akinyonya katika (Kabila la) Bani Sa'di akauliwa na (Kabila la) Hudhail. Na riba ya ujahiliya imebatilishwa. Riba ya kwanza nitakayoibatilisha ni riba yetu, riba ya 'Abbas bin 'Abdulmuttalib, imeshabatilishwa yote."**

**"Mcheni ALLAH katika wanawake. Hakika mumewachukua kwa amana ya ALLAH. Mumezihalalisha tupu zao kwa neno la ALLAH. Haki zenu juu yao ni wasimruhusu yeyote mnaemchukia kuingia majumbani mwenu. Watakapofanya hivyo (kumruhusu mnaemchukia) wapigeni pigo lisilokuwa la tashididi (la kuwaumiza)."**

**"Na haki zao juu yenu ni kuwalisha na kuwavisha kwa wema."**

**"Nimewaachia ambacho, lau mtashikamana nacho,**

**hamtapotea baadae. (Nacho ni:) Kitabu cha ALLAH."**

**"Nanyi mtaulizwa kuhusu mimi Mutasemaje?"**

Maswahaba wakasema: Twashuhudia kuwa umebalighisha, umetekeleza na umenasihi.

Akaashiria kwa kidole chake akikinyanyua mbinguni na akiwaashiria watu (huku akisema): **"Ewe Mola shuhudia, Ewe Mola shuhudia"**, mara tatu.

Kukaadhiniwa kisha kukakimiwa, akaswali adhuhuri. Kisha kukakimiwa akaswali alasiri, wala hakuswali (Sunna) baina ya Swala hizo. Akapanda mnyama wake, hata alipofika mahala pa kusimama ('Arafa). Tumbo la ngamia wake Al-qaswa likawa juu ya mawe. Mahali pa kujumuika wanaotembea kwa miguu pakawa pako mbele yake. Akaelekea Qibla. Basi hakuacha kuwa amesimama mpaka juwa likazama, umanjano ukawa umepotea kidogo, mpaka likazama kabasa. Akampandisha Usama nyuma ya ngamia wake, Akaondoka ... akawa anaashiria kwa mkono wake wa kulia: **"Enyi watu kuweni wataratibu, kuweni wataratibu."** Akawa kila anapofika juu ya kilima akiilegeza kidogo hatamu ya ngamia, mpaka alipofika Muzdalifa. Akaswali hapo magharibi na isha kwa muadhini mmoja na kukimiwa mara mbili, wala hakuswali Swala ya ziada baina ya Swala mbili hizo. Kisha akalala mpaka kutokeza alfajiri. Akaswali alfajiri wakati ilipombainikia asubuhi. Kukaadhiniwa na kukakimiwa. Kisha akampanda ngamia wake Al-qaswaa mpaka Mash'aril-Haraam; akaelekea Qibla akaomba dua kwa ALLAH, akamtukuza, akamtakasa na akampwekesha. Basi hakuacha kuwa amesimama mpaka kulipokua kumepambazuka mno. Akaondoka kabla kuchomoza juwa. Akampandisha Al-Fadhlu bin Abbaas nyuma ya ngamia wake. Na alikuwa (huyo Al-Fadhlu) ni mwenye nywele mzuri, mweupe wa kutakata na jamali ya umbo. Mtume (S.A.W.) alipoondoka, palipita msafara wa wanawake karibu naye. Al-Fadhlu akawa anawatazama. Mtume (S.A.W.) akauweka mkono wake katika uso wa Al-Fadhlu, naye Al-Fadhlu akaugeuza uso wake upande mwingine akiwatazama. Mtume (S.A.W.) akaugeuza uso wa Al-Fadhlu kutoka upande ule hadi upande mwingine hata

walipofika uwanja wa Muhassir, Mtume (S.A.W.) alienda haraka kidogo, halafu akafwata njia ya Al-Wusta inayotokezea Al-Jamratulkubra. Alipofika hapo Al-Jamra mbele ya mti alirusha vijiwe saba. Akipiga Takbira kila anaporusha kijiwe. Alirusha katikati ya uwanja. Kisha akaondoka akaenda mahala pa kuchinja. Akachinja ngamia 63 kwa mkono wake. Kisha akmwachia Sayyidna 'Ali akachinja walobakia, na akamshirikisha katika mnyama wake wa kuchinja. Hatimaye akachukua kinofu cha nyama katika kila ngamia, vikatiwa katika chungu na vikapikwa. Wakala katika nyama hizo na wakanywa mchuzi wake. Halafu, Mtume (S.A.W.) akapanda ngamia wake, akaenda akatufu Tawafu ya ifadha katika Alkaaba. Akaswali adhuhuri hapo Makka. Akawaendea Bani 'Abdul-Muttalib wakiteka maji ya zamzam wakiyamimina kwenye mahodhi n.k. Akasema:
**"Enyi Bani 'Abdul-Muttalib! Tekeni kwa ndoo na muyavute kwa kamba. Lau sikhofii watu kuitakidi kuwa kufanya hivyo ni katika ibada za Hajj, halafu wakaja kusongamana nanyi mpaka wakawaghilibu katika kuteka kwenu, basi ningaliteka pamoja nanyi."** Wakampa ndoo, akanywa maji kutokana na ndoo hiyo. (Muslim).

* * * * * *

# MWISHO

# FAHARISI

NGUZO YA KWANZA: 7
KUSHUHUDIA KUWA HAPANA MOLA ANAYESTA-
HIKI KUABUDIWA KWA HAKI ISIPOKUWA ALLAH
NA KUWA MUHAMMAD NI MJUMBE WA ALLAH. 8

UKAMILISHO KUHUSU KUSHUHUDIA KUWA
MUHAMMAD (S.A.W.) NI MTUME WA ALLAH 35

NGUZO YA PILI (SWALA): 40
UTANGULIZI WA UTWAHARA 41
TAARIFA UTWAHARA NA HUKUMU YAKE 41
SAMPULI ZA UTWAHARA 41
UTWAHARA UNAFANYIKA KWA KITU GANI? 42
FAIDA: VIGAWANYO VYA MAJI 43
SAMPULI ZA NAJISI 44
ADABU ZA KUKIDHI HAJA 44
ADABU ZA KUTAMBA NA ISTIJMARI 46
UDHU 47
DALILI YA KUFANYWA KUWA NI SHARIA 47
FADHILA ZA UDHU 48
FARADHI ZA UDHU 49
SUNNA ZA UDHU 50
MAKRUHU YA UDHU 53
NAMNA YA KUTAWADHA 53
YENYE KUTANGUA UDHU 54
YANAYOPASISHA KUTAWADHA 56
UDHU WA MWENYE UDHURU 57
NAMNA YA UTWAHARA WA MGONJWA 58

KUOGA 59
KUEKWA SHARIA YA KUOGA 59
YENYE KUPASA KUOGA 59
MAMBO AMBAYO NI MUSTAHABU KUOGA
KWA AJILI YAKE 61
FARADHI ZA KUOGA 62
SUNNA ZA KUOGA 62
MUKRUHU KATIKA KUOGA 62
NAMNA YA KUOGA 63
AMBAYO NI HARAMU KWA MWENYE JANABA 64

SWALA 66
HUKUMU YA SWALA 66
FADHILA YA SWALA 67
KUTAHADHARI KUACHA SWALA 68
SHARUTI ZA SWALA 69
SHARUTI YA KWANZA 69
SHARUTI YA PILI 70
SHARUTI YA TATU 70
SHARUTI YA NNE 70
SHARUTI YA TANO 71
SHARUTI YA SITA 71
SHARUTI YA SABA 72
SHARUTI YA NANE 72
SHARUTI YA TISA 72
NGUZO ZA SWALA 72
WAJIBATI ZA SWALA 77
SUNNA ZA SWALA 78

KINACHOTOLEWA 148
NI LINI YAPASA NA LINI ITOLEWE? 148
MASURAFU YAKE 149

NGUZO YA NNE (SAUMU) 151
SAUMU (KUFUNGA) 152
HUKUMU YA SAUMU YA RAMADHANI 152
FADHILA YA MWEZI WA RAMADHANI 153
UBORA WA AMALI NJEMA KATIKA MWEZI WA
RAMADHANI 154
SHARUTI ZA SAUMU 155
WANAORUHUSIWA KULA NA KUPASWA KULIPA 156
HUKUMU YA MJAMZITO NA MWENYE
KUNYONYESHA 157
WANAORUHUSIWA KULA NA KUPASWA KUTOA
FIDIA PEKEE 157
NGUZO ZA SAUMU 158
SUNNA ZA SAUMU 159
MAKURUHU YA KUFUNGA 160
YABATILISHAYO SAUMU 161
YALOHALALISHWA KATIKA SAUMU 164
SAUMU YA SUNNA 165
SIKU ZINAZOHARAMISHWA KUFUNGA 167
SIKU AMBAZO NI MAKRUHU KUFUNGA 168

NGUZO YA TANO (HAJJ) 171
AL-HAJJ 172
FADHILA ZA HAJJ 174
SHARUTI ZA KUPASA HAJJ 175

| | |
|---|---|
| NGUZO ZA HAJJ | 175 |
| NGUZO YA KWANZA: KUHIRIMIA | 175 |
| SUNNA ZA KUHIRIMIA | 178 |
| YALOHARAMISHWA KATIKA IHRAM | 179 |
| NGUZO YA PILI: TAWAFU (KUTUFU) | 181 |
| SAMPULI ZA KUTUFU | 181 |
| SHARUTI ZA KUTUFU | 182 |
| SUNNA ZA KUTUFU | 183 |
| ADABU ZA KUTUFU | 184 |
| NGUZO YA TATU: KUSAAYI | 185 |
| SHARUTI ZA KUSAAYI | 185 |
| SUNNA ZA KUSAAYI | 185 |
| ADABU ZA KUSAAYI | 187 |
| NGUZO YA NNE: KUSIMAMA 'ARAFA | 187 |
| WAJIBATI ZA HAJJ | 187 |
| FAIDA: NGUZO ZA 'UMRA | 187 |
| WAJIBATI ZA 'UMRA | 187 |
| FAIDA MUHIMU KUJULIKANA | 187 |
| YANAYOFANYWA SIKU YA 'ARAFA | 188 |
| YANAYOFANYWA MUZDALIFA | 189 |
| YANAYOFANYWA SIKU YA IDI | 191 |
| UZINDUSHI KATIKA AMALI ZA SIKU YA IDI | 192 |
| YANAYOFANYWA SIKU ZA TASHRIQ | 194 |
| TAWAFU YA KUAGA | 195 |
| UFUPISHO WA KUFANYA 'UMRA | 196 |
| UFUPISHO WA KUFANYA HAJJ | 197 |
| KUUZURU MSKITI MTUKUFU WA MTUME (S.A.W.) | 198 |
| ILIVYOKUA HAJJ YA MTUME (S.A.W.) | 200 |